## *TANZANIA OSAKA ALUMNI*

# Kitabu cha

# Mbinu Bora 7

**Ofisi ya Rais,**
**Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa,**
**S.L.P. 1923,**
**Dodoma.**

**AGOSTI, 2019**

# KITABU CHA MBINU BORA 7 (2019)

**Kimeandaliwa kwa ajili ya Tanzania Osaka Alumni (TOA) na:**

| | | |
|---|---|---|
| **Paulo Faty** | - | **Mhadhiri, Chuo Kikuu Mzumbe** |
| **Ahmed Nassoro** | - | **Mhadhiri Msaidizi, Chuo cha Serikali za Mitaa** |
| **Michiyuki Shimoda** | - | **Mshauri Mwandamizi, TAMISEMI** |

**Na kuhaririwa na:**

| | | |
|---|---|---|
| **Liana A. Hassan** | - | **Mshauri** |
| **Stella M. Paschal** | - | **Afisa Serikali za Mitaa Mkuu, OR-TAMISEMI** |
| **Honorina Ng'omba** | - | **Mtaalam wa Kitaifa, OR-TAMISEMI** |

# Yaliyomo


| Mada | Kurasa |
|---|---|
| Vifupisho | i |
| Dibaji | iii |
| Utangulizi (TOA) | iv |
| Utangulizi (JICA) | v |
| SURA YA KWANZA: UTANGULIZI; MASUALA YALIYOIGWA KUTOKANA NA UZOEFU WA JAPANI | 1 |
| SURA YA PILI: JITIHADA ZA JAMII KATIKA KUBORESHA UTOAJI WA HUDUMA | 19 |
| Halmashauri Ya Wilaya Ya Ludewa; Jitihada Za Jamii Katika Ujenzi Wa Miundombinu Ya Maji Safi Na Salama | 22 |
| Halmashauri Ya Mji Wa Mbulu; Jitihada Za Jamii Ya Kata Ya Nambis Katika Ujenzi Wa Shule Ya Sekondari Ya Hhaynu | 29 |
| Halmashauri Ya Wilaya Ya Msalala; Jitihada Za Jamii Katika Uanzishaji wa Shule Ya Sekondari Ya Segese | 36 |
| Halmashauri Ya Jiji La Dodoma; Jitihada Ya Wafanyabiashara Wa Kata Ya Chang'ombe Katika Ujenzi Wa Soko | 41 |
| Halmashauri Ya Wilaya Ya Mpwapwa; Jitihada Za Jamii Katika Kuanzisha Shule Shikizi Ya Matuli | 47 |
| SURA YA TATU: USHIRIKISHAJI JAMII KATIKA UTOAJI WA HUDUMA | 53 |
| Halmashauri Ya Mji Wa Njombe; Udhibiti Shirikishi Wa Taka Ngumu Na Usafi Wa Mazingira | 57 |
| Halmashauri Ya Wilaya Ya Njombe; Uanzishaji Shirikishi Wa Soko La Mbao La Matembwe | 67 |
| Halmashauri Ya Mji Wa Makambako; Upimaji Shirikishi Wa Makazi Yasiyo Rasmi | 75 |
| Halmashauri Ya Wilaya Ya Kiteto; Uwezeshi Wa Watoto Kutoka Jamii Za Wafugaji Kupata Elimu Ya Msingi | 82 |
| Halmashauri Ya Manispaa Ya Singida; Uboreshaji Wa Kituo Kikuu Cha Mabasi Cha Misuna Kwa Huduma Bora | 89 |
| Halmashauri Ya Wilaya Ya Iramba; Uboreshaji Wa Huduma Za Afya Kwa Wajawazito | 96 |
| Sekretarieti Ya Mkoa Wa Shinyanga; Upunguzaji Wa Vifo Vya Wajawazito Na Watoto | 101 |
| Halmashauri Ya Mji Kondoa; Udhibiti Shirikishi Wa Taka Ngumu | 107 |
| SURA YA NNE: MAENDELEO YA JAMII KIUCHUMI | 113 |
| Halmashauri Ya Wilaya Ya Kiteto; Uzalishaji Na Uongezaji Wa Thamani Ya Maziwa | 115 |
| Halmashauri Ya Wilaya Ya Simanjiro; Uongezaji Wa Thamani Ya Ngozi Na Uboreshaji Wa Maisha | 122 |
| Halmashauri Ya Wilaya Ya Mbulu; Uzalishaji Na Uongezaji Thamani Wa Vitunguu Swaumu | 130 |
| Halmashauri Ya Wilaya Ya Singida; Udhibiti Wa Kideri Kuboresha Uzalishaji Wa Kuku | 137 |
| Halmashauri Ya Wilaya Ya Shinyanga; Uboreshaji Shirikishi Wa Skimu Ya Umwagiliaji Ya Nyida | 145 |
| REJEA | 156 |

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| ADF | Agency Delegated Functions |
| ALAT | Association of Local Authorities In Tanzania |
| AMCOs | Agricultural Marketing Cooperatives |
| AMREF | African Medical Research Foundation |
| AMSDP | Agricultural Marketing Systems Development Programme |
| ASDP | Agriculture Sector Development Programme |
| BRELA | Business Registration and Licencing Agency |
| CCTV | Closed-Circuit-Television |
| D by D | Decentralization by Devolution |
| DANIDA | Danish International Development Agency |
| DIDP | District Irrigation Development Programme |
| DMDD | Diocese of Mbulu Development Department |
| IFAD | International Fund for Agriculture Development |
| IRDP | Institute of Rural Development Planning |
| JICA | Japan International Cooperation Agency |
| LAT | Local Allocation Tax Grant |
| MEM | Mpango wa Elimu ya Msingi |
| MES | Mpango wa Elimu ya Sekondari |
| MILEPROMA | Mirerani Leather Processing & Product Manufacturing |
| MIVARF | Marketing Infrastructure Value Addition and Rural Financing |
| MSM | Mamlaka za Serikali za Mitaa |
| MVIWATA | Mtandao wa Vikundi vya Wakulima Tanzania |
| NMB | National Microfinance Bank |
| O&OD | Opportunities and Obstacles to Development |
| OJT | On the Job Training |
| OR - TAMISEMI | Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| OVOP | One Village One Product Movement |
| OWM - TAMISEMI | Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| POS | Point of Sale |
| RUDI | Rural and urban Development innitiative |
| SACCOs | Savings and Credit Cooperative Societies |
| SAP | Structural Adjustment Programme |
| SEMA | Sustainable Environment Management Action |
| SIDO | Small Industry Development Organization |
| SK | Serikali Kuu |
| SM | Serikali za Mitaa |
| SMEs | Small and Medium Enterprises |
| TAHA | Tanzania Horticulture Association |
| TAZARA | Tanzania Zambia Railway Authority |
| TOA | Tanzania Osaka Local Government Reform Alumni |
| UCRT | Ujamaa Community Resource Team |
| ULGSP | Urban Local Government Support Programme |
| UNFPA | United Nations Population Fund |
| USAID | United States Agency for International Development |
| UVIMASHA | Umoja wa Vikundi vya Maendeleo |
| UWAMIMA | Umoja wa Wakulima wa Miti Matembwe |
| VICOBA | Village Community Bank |

# Dibaji

Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania yamelenga katika utoaji bora wa huduma wa Serikali za Mitaa kwa kuzingatia sera za kitaifa za Serikali Kuu. Maboresho yamekaribisha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, washirika wa maendeleo na wadau wengine tangu awamu ya kwanza hadi sasa. Sera ya Ugatuaji wa Madaraka (D by D) iliwekwa dhahiri mwaka 1998 na utekelezaji wake wa maboresho ya Serikali za Mitaa ulianza mwaka 2000. Kupitia ushirikiano huu maboresho ya Serikali za Mitaa hapa Tanzania yamefanikiwa kuleta Serikali za Mitaa za kidemokrasia, matumizi bora ya rasilimali watu, kuongezeka kwa ruzuku toka hazina, kuimarika kwa utawala bora katika Serikali za Mitaa, kuongezeka kwa ushiriki wa wananchi na kwa ujumla kuongezeka kwa uhuru wa Serikali za Mitaa katika utoaji wa huduma.

Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania yametekelezwa kwa mkakati wa jumla ambao umejumuisha kujifunza jitihada za maboresho na utekelezaji wake katika nchi nyingine za Afrika na kwingineko na kuunda mkakati sahihi wa utekelezaji wake na mbinu mbadala kwa Tanzania. Tangu mwaka 2002 Serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OWM – TAMISEMI – Wakati huo) na Serikali ya Japani kupitia Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Japani (JICA) kwa pamoja wameendesha mafunzo kuhusu Ugatuaji nchini Japani kupitia mafunzo ya Osaka. Mafunzo haya yamehudhuriwa na Wakurugenzi na Watumishi wengine toka OR – TAMISEMI, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa (MSM) na wadau wengine wa maboresho ya Serikali za Mitaa. Mafunzo haya pia yalitolewa kwa Makatibu Tawala Wasaidizi, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya na Wakuu wa Idara kupitia mafunzo ya mikoa baada ya mafunzo ya Osaka.

Mafunzo ya Osaka na yale ya Mikoa yametoa fursa kwa watumishi wa Serikali Kuu na Serikali za Mitaa kujifunza uzoefu wa ugatuaji madaraka wa Kijapani, kuchagua mbinu bora za ugatuaji wa Kijapani na kutekeleza mbinu hizo katika Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa. Hili limeibua umuhimu wa kutoa taarifa za utekelezaji wa mbinu hizi bora kupitia kitabu, ili kuzifanya Sekretarieti za Mikoa na MSM kuona na kujifunza utekelezaji na siri zake humuhumu nchini.

Kitabu hiki cha Saba ni mwendelezo wa juhudi za pamoja kati ya OR – TAMISEMI na JICA kuimarisha sera ya ugatuaji wa madaraka Tanzania. Kitabu hiki kinaanza kwa kuonesha historia ya mafunzo ya Osaka na mbinu bora kama ifuatavyo; Sura ya Kwanza inaonyesha kwa ufupi Masuala mazuri yaliyoigwa toka Japani; Sura ya Pili inahusu Jitihada za Jamii katika Kuboresha Utoaji wa Huduma ikiwasilisha Mbinu Bora kutoka Hamashauri za Wilaya za Ludewa, Msalala na Mpwapwa, Halmashauri ya Mji wa Mbulu na Halmashauri ya Jiji la Dodoma. Sura ya Tatu inahusu Ushirikishwaji wa Jamii katika Utoaji wa Huduma ikiwasilisha Mbinu Bora za Halmashauri za Miji ya Njombe, Makambako na Kondoa, Halmashauri ya Manispaa ya Singida, Halmashauri za Wilaya za Njombe, Kiteto na Iramba na Sektretarieti ya Mkoa wa Shinyanga. Sura ya Nne inahusu Maendeleo ya Jamii Kiuchumi na inawasilisha Mbinu Bora kutoka Halmashauri za Wilaya za Kiteto, Simanjiro, Mbulu, Singida na Shinyanga.

OR – TAMISEMI inashauri watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na wa MSM na wadau wote wa maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania kusoma kitabu hiki, kufahamu jitihada za ndani, kujifunza siri za mafanikio na kutumia fursa zilizopo kwenye maeneo yao kuonesha utendaji mzuri katika mazingira ya ugatuaji wa madaraka.

-------------------------------------------------

**MHANDISI JOSEPH M. NYAMHANGA**
**KATIBU MKUU**
**OR-TAMISEMI**

# Utangulizi (TOA)

Kitabu cha Mbinu Bora cha Saba ni matokeo ya jitihada za pamoja za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia OR – TAMISEMI na Serikali ya Japani kupitia JICA tangu mwaka 2002 kwa kuendesha mafunzo huko Osaka na mafunzo baada ya Osaka katika kila Mkoa juu ya uzoefu wa Ugatuaji Madaraka huko Japani. Mafunzo haya yalitoa fursa kwa watumishi wa Sekretarieti za Mikoa, MSM na wadau mbalimbali wa maboresho hapa Tanzania kujifunza uzoefu wa Kijapani kuhusu Ugatuaji katika maeneo ya Utawala katika Serikali za Mitaa na Usimamizi wa Rasilimali Watu, Ugatuaji wa Masuala ya Fedha na Uboreshaji wa Mapato, Upangaji na Utoaji Huduma Shirikishi na Maendeleo ya Kiuchumi katika MSM hasa kupitia wimbi la OVOP. Masuala mazuri yaliyoigwa yametekelezwa katika Sekretariati za Mikoa na MSM nyingi kwa lengo la kuboresha utoaji huduma kwa jamii ndani ya sera ya ugatuaji, yaani “D by D”. Mbinu Bora nyingi za utekelezaji zimeonyesha mafanikio na matokeo chanya kwa jamii. Kamati ya Utendaji ya TOA imeamua kutoa Mbinu Bora ambazo zimewasilishwa kwenye toleo hili la saba. TOA itaendelea kutoa matoleo mengine ya kitabu hiki siku za mbele sambamba na utekelezaji unaondelea wa Masuala mazuri yaliyoigwa kwenye mafunzo ya Osaka na yale ya Mikoa.

Kukamilika kwa kitabu cha Mbinu Bora cha saba kumetokana na misaada kutoka taasisi na watu binafsi mbalimbali. TOA inapenda kutambua na kutoa shukrani kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na OR - TAMISEMI kwa kufikia makubaliano na Serikali ya Japani, kufadhili na kuruhusu watumishi wa Tanzania kuhudhuria mafunzo ya Ugatuaji nchini Japani toka mwaka 2002 hadi sasa. Pili, TOA inaelekeza shukrani za dhati kwa Serikali ya Japani na JICA kwa kuandaa, kusaidia na kufadhili mafunzo ya Osaka na Mafunzo ya Mikoa na uzalishaji wa kitabu hiki. TOA pia inapenda kutambua na kushukuru juhudi za Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa MSM katika utekelezaji wa masuala yaliyoigwa na utayari wao wa kuziandika Mbinu Bora kamilifu kama zinavyoonekana kwenye kitabu hiki.

Uchambuzi na uunganishi wa Mbinu Bora zilizopo kwenye kitabu hiki ulifanywa na Bwana Paulo F. Faty (Mhadhiri - Chuo Kikuu Mzumbe) na Bwana Ahmed Nassoro (Mhadhiri Msaidizi - Chuo cha Serikali za Mitaa – Hombolo). Masuala yaliyoigwa Japani yamechambuliwa na Bwana Michiyuki Shimoda (Mshauri Mwandamizi, OR – TAMISEMI). TOA inapongeza kwa dhati mchango wao na inawashukuru sana.

Mwisho, TOA inapenda kuwashukuru watumishi wote wa OR – TAMISEMI, JICA na TOA kwa kushiriki katika mikutano mbalimbali iliyoboresha na kuunda kitabu hiki. Siyo rahisi kutaja wote waliochangia katika kazi hii, hata hivyo TOA inaheshimu michango yote iliyotolewa na Taasisi na watu mbalimabali.

Mwisho kabisa, ingawa watu na Taasisi nyingi zimechangia katika kitabu hiki, TOA na timu ya uchambuaji wanawajibika kwa makosa na mapungufu yanayoweza kuhisiwa na wasomaji wa kitabu hiki.

--------------------------------------------------------

**PROF. RIZIKI SHEMDOE**
**MWENYEKITI WA TOA**

# Utangulizi (JICA)

Wasomaji Wapendwa!

Utekelezaji wa sera ya Ugatuaji wa Madaraka umechukua zaidi ya miaka 15 ukiwa na lengo la kuboresha huduma kwa kugatua shughuli, majukumu na rasilimali toka Serikali Kuu kwenda Serikali za Mitaa.

Kutokana na ukweli huu JICA imejikita katika kusaidia utekelezaji wa sera hii na kuimarisha utoaji huduma katika ngazi za msingi kwa kujenga uwezo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwa ni pamoja na maendeleo ya sekta za afya, kilimo, maji na barabara.

Tangu mwaka 2002, JICA kwa kushirikiana na OR – TAMISEMI imekuwa ikiendesha mafunzo kuhusu maboresho katika Serikali za Mitaa yanayoitwa “Mafunzo ya Osaka”. Mafunzo haya yalilenga Maofisa wa juu wa Menejimenti katika maboresho ya Serikali za Mitaa, yaani Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa MSM, Maofisa wa OR – TAMISEMI na Vyuo vya Elimu ya Juu kwa malengo ya kujifunza uzoefu wa Kijapani katika maboresho ya Serikali za Mitaa. Waliporejea nchini, waliwasilisha na kujadiliana uelewa na uzoefu walioupata kwenye warsha za mafunzo za mikoa (2003 – 2007). Kutokana na Mafunzo ya Osaka, Umoja wa Makatibu Tawala na Wakurugenzi wa MSM (TOA) ulianzishwa (2006) ili kuwa na jukwaa ambalo wajumbe wa TOA wanapata fursa ya kubadilishana uzoefu, mbinu bora na changamoto zilizopo. JICA imekuwa ikisaidia uimarishaji wa TOA.

Kutokana na utekelezaji wa Masuala yaliyoigwa kwenye mafunzo ya Osaka, mbinu bora nyingi ziliwasilishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika warsha za Mikoa zilizofanyika katika kanda sita mwaka 2011 - 2018. Baada ya uhakiki na uchambuzi wa mbinu hizi bora, “kitabu cha mbinu bora” toleo la kwanza hadi la sita na hatimaye toleo la saba limekamilika. Kitabu hiki kinathibitisha kuwa ***“tunatakiwa kujifunza siyo tu kutoka nchi nyingine bali katika jitihada nyingi zilizopo ndani ya nchi”.***

Nitafurahi kama mtajifunza vipengele muhimu kutoka kitabu hiki na kuchukua hatua ndogo lakini za uhakika ili kuboresha utendaji katika eneo husika.

JICA inapenda kuona jitihada hizi zinaendelezwa na TOA katika kutoa machapisho mengine ya Mbinu Bora zinazotekelezwa na Sekretarieti za Mikoa na MSM. Tungependa kufuatilia na kujua mbinu bora zitakazofuata zilizotokana na kitabu hiki na mafunzo yake ikiwemo uimarishaji wa jukwaa la kujifunza wenyewe kwa wenyewe katika ngazi za Msingi.

**-------------------------------------------------------------**

**NAOFUMI YAMAMURA**
**MWAKILISHI MKUU – OFISI YA JICA TANZANIA**

# Sura ya Kwanza

# Utangulizi; Masuala Yaliyoigwa Kutokana na Uzoefu wa Japani

**1.0 MAFUNZO YA OSAKA**

Kitabu hiki kimeandaliwa na TOA ambayo ni umoja wa washiriki wa mafunzo ya Osaka yanayoendeshwa na JICA nchini Japani. Mafunzo yenyewe yanaitwa “Mafunzo ya Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania”. Umoja una wanachama ambao ni Makatibu Tawala wote wa Sekretarieti za Mikoa, Maafisa Waandamizi wa OR – TAMISEMI, Wahadhiri wa vyuo rafiki na Wakurugenzi wote wa MSM nchini.

Mafunzo ya Osaka yalianza mwaka 2002. Kipindi cha miaka mitano ya mwanzo, Makatibu Tawala wote kutoka Mikoa 21 (kipindi hicho) pamoja na Wakurugenzi wa MSM wawili kutoka kila Mkoa walihudhuria. Maofisa waandamizi toka OWM – TAMISEMI (wakurugenzi na wakurugenzi wasaidizi)[1], Katibu Mkuu wa ALAT na baadhi ya wanataaluma mashuhuri walihudhuria mafunzo haya.

Kutokana na mafanikio na matokeo Dhahiri ya awamu ya kwanza (2002-2006), JICA iliamua kuendelea na mpango huu kwa miaka mingine mitano (2008-2012), kwa kupanua wigo wake kwa kuongeza nchi nyingine tatu za kiafrika ambazo zilikuwa zikipanga maboresho ya ugatuaji, yaani Kenya, Uganda na Zambia, pamoja na Tanzania. Mpaka leo zaidi ya viongozi 100 wa maboresho (wanachama wa TOA) wamefaidika moja kwa moja na mafunzo ya Osaka. Pia washiriki hawa waliporudi katika mikoa yao waliendesha warsha za ndani zijulikanazo kama “mafunzo baada ya Osaka” ili kubadilishana uzoefu na uelewa walioupata Osaka kwa kuwaalika Wakurugenzi waliobaki pamoja na wakuu wa idara wa MSM na Sekeretarieti za Mikoa. Hivyo wafaidika wa mafunzo haya waliongezeka mpaka kufikia zaidi ya 1,500, ingawa uanachama wa TOA ulibakia kuwa wa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi wa Halmashauri.

Kutoka katika Masuala mbalimbali yaliyoigwa Osaka na mafunzo baada ya Osaka, MSM zilizohudhuria ziliandaa mipangokazi ya kuboresha utendaji wao. Kukiwa na zaidi ya miaka 10 ya utendaji, imethibitishwa kuwa kuna idadi kubwa ya mbinu bora zinajitokeza katika baadhi ya MSM kwa kutekeleza mipangokazi ambayo ni vyema kuwashirikisha wengine. Kwa hiyo TOA iliamua kuhakiki na kuchambua mbinu bora na kutengeneza kitabu hiki, ili viongozi wa MSM waweze kuzirejea na kuzitumia pale wanapoona zinafaa na zina tija katika kuboresha utoaji wa huduma.

---

[1] Pamoja na Makatibu wakuu wawili wa Zamani wa OWM-TAMISEMI, yaani, MS. Tarishi M.K. na Bwana H.A. Katanga

Kabla ya kuelezea mbinu bora, ni vyema katika sura hii tukaangalia kwa nini JICA iliamua kutoa mafunzo haya kwa viongozi wa maboresho wa kitanzania, maana ya mafunzo ya Osaka kwa Tanzania na masuala gani yalijadiliwa kwenye mafunzo haya.

## 2.0 HISTORIA YA MAFUNZO YA OSAKA

Kwa nini JICA iliamua kutoa mafunzo haya na yalikuwa na maana gani kwa Tanzania?

### 2.1 Maoni ya JICA Kuhusu Msaada kwenye Ugatuaji

JICA ina maoni ya kipekee kuhusu misaada kwenye utawala ambayo yanaweza kutofautiana na maoni ya washirika wengine wa maendeleo. JICA imeshuhudia programu kubwa kubwa za maboresho zikifanywa katika nchi zinazoendelea na washirika wa maendeleo kama Programu wa kurekibisha Miundo ya Uchumi na maboresho ya utawala ikiwa ni pamoja na Ugatuaji wa madaraka. Inaweza kusemwa kuwa programu hizi na maboresho haya yaliyofanywa katika nchi zinazoendelea ni sawa kabisa na yale yanayojaribiwa sasa katika nchi zilizoendelea bila kujali tofauti iliyopo ya kihistoria na mazingira kati ya nchi hizi. Mara kwa mara inajidhihirisha kuwa maboresho haya yanatekelezwa kwa msukumo mkubwa toka kwa wafadhili, bila kuzingatia asili ya mchakato wa maendeleo na umiliki wa nchi husika.

Kutokana na machungu ya kushindwa kufikia malengo katika ushirikiano wa kimataifa wa aina hii, JICA imekuwa na msimamo ufuatao katika kusaidia ugatuaji.

(i) Hakuna mfumo wowote unaoweza kutumika katika nchi zote.
(ii) Ugatuaji wenyewe siyo lengo bali ni njia ya kufikia lengo fulani.
(iii) Kuasilisha na kukuza mfumo ndani ya nchi kupitia majadiliano ya kitaifa ni muhimu.
(iv) Jinsi gani ya kuhakikisha viwango vya chini vya kitaifa vya huduma[2] vinafikiwa ni muhimu katika kuandaa maboresho ya Ugatuaji.
(v) Maboresho ya Ugatuaji ni mchakato mrefu ambao hautakiwi kuchukuliwa kama Mradi au Programu tu.
(vi) Maboresho ya Ugatuaji ya haraka haraka yanaweza kuleta mkanganyiko. Katika kila maboresho ya Ugatuaji ni lazima kuhakikisha kuna mazingira sahihi kwa upande wa Halmashauri na wanajamii kupokea majukumu makubwa yanayogatuliwa.

### 2.0 Changamoto Kubwa Iliyogunduliwa katika Programu ya Tanzania ya Maboresho ya Serikali za Mitaa na Ujumbe wa Maandalizi ya Mafunzo wa Mwaka 2002

Baada ya maombi ya Serikali ya Tanzania kuhusu kuwepo kwa Mpango wa mafunzo wa maboresho katika Serikali za Mitaa mwaka 2001, JICA iliamua kutuma Timu ya wataalamu kwenda kuchambua hali ilivyo ili kuandaa mafunzo yenye maudhui ya kumaliza masuala muhimu. Timu ilipofika Tanzania Novemba mwaka 2002, uligundua kuwa Programu ya maboresho ya Serikali za Mitaa Tanzania ilikuwa na changamoto zifuatazo;

(i) Jedwali kubwa na lenye hatua nyingi za utekelezaji (zaidi ya kurasa 80)

[2] Viwango vya chini vya kitaifa vya huduma ni nadharia kuwa kiwango fulani cha huduma lazima kifikiwe hata kama ni katika jamii maskini vijijini sawa na kwenye miji mikubwa.

(ii) Programu ya maboresho ilikuwa ikitekelezwa kwa jedwali zuri sana lakini halikuruhusu maboresho/mabadiliko zaidi. Timu iligundua kuwepo kwa nafasi ndogo iliyoachwa ya kuweza kubadili lolote ili kuruhusu majaribio ya suala ambalo ni muhimu. Timu ilibaini programu ilikuwa imeandaliwa na wahisani na Serikali ya Tanzania kulazimika kutekeleza kama ilivyo.

(iii) Programu iliandaliwa kwa msaada mkubwa kutoka kundi la wahisani.

(iv) Wahisani wa kawaida waliopo kwenye mfuko maalumu waliunda kamati ya msukumo pamoja na Serikali. Maandalizi ya Programu na utekelezaji wake yalifanywa na wataalamu washauri kutoka nje ya nchi. Timu ya JICA ilihofia kuwa Programu ya maboresho iliandaliwa bila kupitia mchakato stahiki wa kujenga uelewa ndani ya nchi na kupata makubaliano yanayohusu mahitaji ya mabadiliko.

(v) Hatari ya kuharakisha Ugatuaji wa Madaraka.

Timu ilidhihirisha kuwa Sera ya ugatuaji iliyokuwa ikihamasishwa na Serikali ni ile ya ugatuaji wa madaraka sawa na ule wa nchi zilizoendelea. Swali likawa; Je ni kweli uwezo na mtazamo wa MSM na Wizara zote ulikuwa tayari kwa mabadiliko haya ya haraka? Timu hii iliaona changamoto zifuatazo katika hili;

- Mtazamo hasi kutoka Wizara za kisekta
- Ukosefu wa majadiliano ya kina kuhusu ugatuaji katika jamii
- Hakukuwa na uwezo kamilifu kwa upande wa MSM kuchukua majukumu yote yaliyogatuliwa

### 2.3 Uwezekano wa Umuhimu wa Uzoefu toka Japani katika Ujenzi wa Taifa na Maboresho ya Ugatuaji - Ujumbe wa Mafunzo ya Osaka kwa Watanzania

Baada ya kuona hali halisi ya Tanzania iliyoelezewa hapo juu, JICA iliamua kuwa uzoefu wa Japani kwenye ujenzi wa Taifa na Maboresho yaliyokuwa na mchakato wa muda mrefu ya Ugatuaji ungeweza kuwa unafaa na muhimu kwa viongozi wa maboresho wa Tanzania kujifunza na kupitia upya maboresho yao.

Japani ni nchi ndogo huko Bara la Asia ambayo awali haikuwa na ustaarabu wa Magharibi, ilianza ujenzi wa taifa kama nchi iliyokuwa nyuma kimaendeleo baadaye ikafikia maendeleo ya juu. Japani ina uzoefu mwingi wa aina yake wa kutumia mifano ya nje (mfano wa Magharibi) ambayo wahisani wengine hawana. Japani ilianza Ujenzi wa taifa na maendeleo, kwa kujaribu kuiga mifano ya Magharibi lakini ikashindwa mwanzoni kabisa. Tangu hapo ikawa ni mchakato mrefu wa kujaribu na kushindwa hadi Japani ilipoamua kuunda mfumo wake wa pekee unaoitwa “Nusu Japani nusu Magharibi”. Japani inaamini kuwa aina hii ya uanzishaji wa mfumo, pamoja na umiliki wake thabiti kupitia kujaribu na kushindwa mara nyingi ni muhimu sana kwa maendeleo endelevu ya nchi.

Mchakato huu ambao Japani ilitumia ili kuanzisha mfumo wake wa Serikali za Mitaa na maboresho ya Ugatuaji ni tofauti kabisa na mifano ya Ulaya ambayo nchi zinazoendelea zinajaribu kuanzisha kwa sasa. JICA ilibaini kuwa, kuwasilisha “mfumo huu tofauti” unaweza kuwa muhimu, kwani kuwa na mfano mmoja tu, inaonekana kama vile “ndio njia pekee” hakuna nyingine. Lakini kukiwa na mifano zaidi ya miwili, wanaweza wakaanza kulinganisha na

kuona ni mfano upi unafaa zaidi katika mazingira yao, na ni hatua ipi iwe ya kwanza katika kuandaa mfumo wao wenyewe.

Ifuatayo ni mifano ya vigezo vinavyoweza kuigwa toka mfumo wa kijapani kati ya mengi yaliyopo;

**(1) Mchakato wa Maboresho wa Polepole Wenye Uhakika**

Japani ilitumia miaka 110 tangu ilipoanza kuunda mfumo wa Serikali za Mitaa na Ugatuaji; ingawa tunahesabu miaka 55 ya Maboresho Makuu baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia hadi kufika ugatuaji halisi mwaka 2000. Serikali ilijaribu kuhakikisha kuwa MSM zimeshajengewa uwezo wa kutosha kabla ya kugatua majukumu, na siyo kukimbilia kurekebisha taasisi za Ugatuaji. Uzoefu huu wa Japani unaipa Tanzania fursa ya kutafakari zaidi kama mwenendo wa maboresho siyo wa kasi, na kama nchi inataka kuendelea na mwenendo uliopo, basi haina budi kuhakikisha MSM zinajengewa uwezo stahiki.

**(2) Kukasimu Majukumu**

Katika kipindi tajwa cha miaka 55, Serikali ilichagua mfumo wa kukasimu majukumu kwa wakala kama hatua ya mpito, badala ya kuharakisha kwenye ugatuaji moja kwa moja. Kwa sababu ya mfumo huu, Japani ilipingwa sana na nchi za Magharibi kwa kipindi kirefu kuwa haijafanya Ugatuaji sahihi, na mwisho Serikali ikaamua kuingia katika Ugatuaji halisi mwaka 2000 na kuondokana na mfumo wa kukasimu kwa wakala. Hata hivyo, imethibitika kuwa mfumo huo ulichangia kwa kiasi kikubwa kukua kwa mfumo mzuri wa Serikali za Mitaa na kufikiwa kwa ugatuaji halisi nchini Japani; hususan katika vipengele vifuatavyo:

- Kutokana na Mfumo wa kukasimu majukumu, MSM zilifanya kazi kwa ushirikiano wa karibu na Wizara husika, na zikaweza kujenga uwezo wao kupitia mafunzo kazini kukiwa na usaidizi wa kitaalamu wa karibu kutoka katika wizara. Kila MSM zilipopata changamoto, maafisa wa Serikali za Mitaa waliweza kuwasiliana na maafisa wa wizara husika kwa simu na maafisa ambapo walipata suluhu ya changamoto hizo kwa pamoja. Haya yote yaliwezekana kwa sababu kimsingi shughuli zote zilikuwa ni wajibu wa Wizara na zilikasimishwa tu kwa MSM. Hivyo hakukuwa na ukinzani wowote toka wizarani, zaidi ya ushirikiano ilipofikia Ugatuaji wa shughuli; tofauti na yanayotokea katika baadhi ya nchi zinazoendelea zinapotekeleza ugatuaji.
- Hoja ya msingi ilikuwa ni kuhakikisha kuwa rasilimali ambazo ni chache zilizopo ndani ya nchi zinaweza kutumika vizuri zaidi kuelekea upande mmoja yaani maendeleo ya nchi, badala ya kuzigawa na kutengeneza tofauti kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.
- Ilikuwa ni muhimu sana katika hatua za mwanzo ambapo MSM zilikuwa na uwezo dhaifu. Bila mfumo wa kukasimu kipindi hicho MSM zisingeweza kufanya vizuri shughuli zao za kuhudumia wananchi wala uwezo wao usingejengeka.
- Sababu nyingine muhimu ilikuwa mafunzo kazini. Kwa miaka 55, watumishi wote wa Serikali za Mitaa pamoja na muundo wao kwa ujumla walijenga uwezo thabiti kwa kupokea ufahamu na utaalamu kutoka wizarani, na kuwa tayari Serikali Kuu ilipoamua kugatua madaraka.

Uzoefu huu wa Japan unaleta swali moja la msingi kwa Tanzania juu ya namna gani nchi inaweza kujithibitishia uhakika na ubora wa mchakato wa kuzijengea uwezo MSM ilihali

Ugatuaji ukiendelea; kuhakikisha matumizi mazuri ya rasilimali chache zilizopo nchini na kupata ushirikiano stahiki kutoka Wizara za kisekta.

**(3) Mfumo wa Kubadilishana Watumishi kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa**

Nchini Japani, kipindi cha hatua za mwanzo za maboresho, mtindo wa kubadilishana watumishi kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa ulitumika kama mbinu bora ya (a) kujaza upungufu wa watumishi hasa wenye sifa katika Halmashauri za pembezoni na (b) kuhakikisha uhamishaji wa ujuzi na utaalamu kutoka kwa wasomi wa Wizara kwenda kwa watumishi wa Halmashauri waliokuwa na ujuzi na uzoefu mdogo ili kujenga uwezo wa Halmashauri hizo.

Serikali iliunda jopo kubwa la maofisa wataalamu katika wizara ya Serikali za Mitaa na kuwapeleka kwenda kwenye MSM zilizokuwa na uwezo mdogo ili kuzisaidia. Hatua hii ya uhamisho wa muda ilidumu kwa muda wa miaka 4 - 5 na baadaye watumishi hawa walirudishwa kwenye nafasi zao za kawaida kwenye wizara zao. Kadri walivyokuwa na uwezo wa kitaalamu kuwezesha wengine ndivyo walivyopelekwa kwenye Halmashauri za mbali na zenye udhaifu mkubwa. Pale walipofaulu na kutenda kazi vizuri katika vituo hivi vipya, waliahidiwa kupanda vyeo zaidi wanaporudi, ambayo iliwapa motisha wataalamu hawa waliobobea kwenda kwenye sehemu zisizovutia kwa hamasa. Aidha, Halmashauri nyingi zilipeleka watumishi wao kwenye wizara mbalimbali kufanya kazi katika misingi ya mafunzo kazini kwenye maeneo ambayo Halmashauri husika ilihitaji.

Baada ya kurudia mizunguko kadhaa ya kubadilishana watumishi, ujuzi na utaalamu wa kutosha ulihamishwa kikamilifu toka Wizara kwenda MSM, kitu ambacho kilisaidia sana kujenga uwezo wa MSM nchini Japani. Hivi sasa MSM zinajitegemea katika rasilimali watu bila kuitegemea Serikali Kuu.

Ni dhahiri kuwa ugatuaji wa rasilimali watu ukifanyika kwa ukamilifu wake bila kuwa na mbinu za kutatua matatizo, huleta upungufu mkubwa wa watumishi kwenye MSM zenye mazingira magumu. Ni kwa sababu hii Tanzania iliamua kurudisha masuala ya rasilimali watu Serikali Kuu kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, haina mantiki kuendeleza Ugatuaji wa madaraka bila Ugatuaji halisi wa rasilimali watu. Serikali inatakiwa kutafuta mkakati wa namna ya kugatua rasilimali watu na wakati huohuo kukwepa kutengeneza upungufu katika maeneo ya vijijini na kujiridhisha kuwa kuna mchakato wa kujenga uwezo wa baadaye wa MSM.

## 3.0 MASUALA YALIYOJITOKEZA NA KUJADILIWA WAKATI WA MAFUNZO YA OSAKA

Kutokana na upungufu wa nafasi masuala machache tu ya msingi yameweza kuwasilishwa kwenye sehemu hiyo hapo juu, kati ya mambo mengi yanayotokana na uzoefu wa Japani ambayo Tanzania imepewa. Hapa vipengele vingine vitatajwa na kuelezewa kwa kifupi.

### 3.1 Masuala ya Jumla

Masuala na Maswali yafuatayo yalijitokeza na kujadiliwa wakati wa mafunzo ya Osaka:

**(1) Umuhimu wa kukuza uwezo wa MSM kama kigezo cha mafanikio ya Ugatuaji wenyewe**

- Je hakuna hatari ya kudidimiza utoaji huduma, kugatua wajibu mkubwa kiasi hiki ndani ya muda mfupi?
- Ni namna gani ya kukabiliana na hali halisi kuwa MSM zinahitaji uwezo zaidi ili kutekeleza shughuli zilizogatuliwa?
  - Vipi kuhusu ajira? Namna gani itawezekana kupata watumishi wenye sifa katika MSM zenye mazingira magumu?
  - Ni jinsi gani ya kuziba pengo kati ya ujuzi na utaalamu katika Serikali za Mitaa na kuziendeleza? Je siyo muhimu kwanza kuweka mbinu za kuhamisha ujuzi na utaalamu, pamoja na usaidizi wa kitaalamu kutoka serikali kuu kwenda MSM? Siyo muhimu kwanza kuimarisha mahusiano ya ushirikiano kati ya Serikali Kuu na MSM badala ya kutegemea misaada toka nje?

**(2) Ugatuaji na Maendeleo**

- Ili kuweza kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi ya nchi na kwa rasilimali chache zilizopo, ni muhimu kutafuta mbinu mkakati ya kuzitumia rasilimali hizi (hivi ndivyo ambavyo Japani imekuwa ikifanya kujiletea maendeleo yake).
- Namna gani unaweza kusimamia maendeleo ya nchi na ugatuaji kwa pamoja wakati mara kadhaa hupingana? Unawezaje kujiridhisha kuwa hakutakuwa na utengano wa rasilimali na tofauti (kutokuelewana) kati ya Serikali Kuu na MSM au kati ya MSM zenyewe?

**(3) Ugatuaji na Viwango vya chini vya kitaifa**

- Jinsi gani ya kusimamia ugatuaji na kuzingatia viwango vya chini vya kitaifa? Ni jinsi gani itahakikishwa kuwa MSM zilizopo vijijini zitakuwa na uwezo wa kutosha kama zilivyo zile tajiri katika kigezo cha utoaji huduma kwa watu? (uwezo wa watumishi na fedha).

**(4) Ukweli Kuhusu Uwezo wa MSM kuweza Kutoa Huduma**

- Swali liliulizwa; Ni Maofisa Ugani wangapi waliopo katika Halmashauri ukijumuisha na wale ambao wanatumikia katika Kata na Vijiji? Swali hili liliulizwa kwa washiriki ili kuwafanya waelewe hali ilivyo mbaya ambayo Halmashauri za Tanzania zinatakiwa kukabiliana nayo. Ukichukua Mkoa mmoja kama mfano, Mkoa wa Nagano nchini Japani, ni mkoa mdogo kabisa ulioko maeneo ya vijijini lakini una maofisa ugani wa kilimo wapatao 1500. Zipo MSM 77 za ngazi za chini katika Mkoa huu ambazo kila moja inaajiri maofisa ugani kati ya 20 – 30. Maana yake kuwa wakulima katika Mkoa[3] wa Nagano wanafurahia huduma zinazotolewa na zaidi ya maofisa ugani 3,000 wa Halmshauri ikilinganishwa na wakulima wa Tanzania ambao wana maofisa ugani wasiozidi 100[4]. Aidha, nchini Japani kuna mashirika mengi ya binafsi yanayouza zana za

[3] Mkoa (prefecture) huko Japani ni karibu sawa na wilaya za Tanzania kwa ukubwa wa eneo. (Ingawa Wilaya nyingine za Tanzania ni kubwa sana kuliko Mikoa ya Kijapani).
[4] Pia si kwamba Japani ina hali nzuri katika maana hii. Kinyume chake, Japani ni nchi ambayo ina idadi ndogo kabisa ya watumishi kwa idadi ya watu waliopo ikilinganishwa na nchi zilizoendelea. Maana yake ni kuwa Uingereza, Ufaransa, Ujerumani, Italia n.k wana watumishi wengi zaidi wa serikali.

kilimo, mbolea, madawa, mbegu n.k pamoja na vyama vya ushirika vya wakulima vilivyo imara; zote hizi hutoa huduma mbalimbali za ugani na ushauri wa kitaalamu.

- Ni vyema kutambua hali ngumu iliyoelezewa hapo juu na kuanzisha mkakati mpya. Hatutakiwi kuota ndoto kwamba Tanzania inaweza kufikia kutoa huduma nzuri kama za nchi zilizoendelea kwa idadi ndogo hivi ya watumishi kwenye eneo lote hata kama Serikali Kuu itaamua kufanya kila kitu peke yake.

**(5) Umuhimu wa Juhudi za Wananchi na Ushirikiano kati ya Halmashauri na Jamii**

- Kutokana na ukweli ulioongelewa hapo juu, haikwepeki kutumia kwa kiasi kikubwa uwezo wa watu na juhudi za kujitegemea ili kutoa huduma zilizo bora.
- Ni imani ya JICA kuwa kama watu wataongozwa na kuwezeshwa vizuri, wana uwezo wa kufanya mambo mengi wenyewe, kama kujenga shule za msingi, zahanati, barabara na kuzitunza.
- Kwa Japani, kipindi cha hatua za mwanzo za Maendeleo, Serikali haikuwa na uwezo wa kujenga shule za msingi. Kwa mfano, ilikuwa ni watu katika jamii zao waliochangia kutoka mifukoni mwao na wakafanya kazi pamoja kujenga na zaidi wakatafuta watu wanaoweza kufundisha na wakawalipa mishahara. Ndiyo maana shule nyingi za kipindi hicho hazikuwa za "umma" bali "binafsi", kwa maana ya "shule zinazomilikiwa na jamii; ilikuwa ni baada ya miongo kadhaa, serikali ilipotajirika na ikaanza kuzimiliki na hatimaye kuwa shule za umma.
- Inahitaji mabadiliko ya mtazamo wa Serikali na Watu, kutoka fikra kuwa ni jukumu la Serikali kutoa huduma zote kwa watu kuelekea mtazamo kuwa watu wanaweza kufanya mengi sana kwa juhudi zao wenyewe na Serikali ikawezesha tu mchakato huo badala ya Serikali kutekeleza peke yake.

**(6) Umuhimu wa Kuainisha Ukubwa Sahihi wa Sehemu za Serikali za Mitaa; na Kuunda Mbinu Mpya za Kuzifikia Jamii kutoka makao makuu ya Halmashauri**

- Kutokana na vigezo hivyo hapo juu ni lazima kuunda mbinu imara za Halmashauri kuzifikia jamii. Hapa Tanzania, Halmashauri za Wilaya ni kubwa mno, hivyo ni muhimu kufikiria jinsi ya kujenga daraja kati ya Halmashauri na jamii.
- Kutoka kwenye wazo la kukuza mtazamo wa watu kuwa na uhuru wao, eneo la Halmashauri linatakiwa kuwa dogo sana ili watu waweze kuona kuwa sehemu hiyo kweli ni yao. Kwa upande mwingine, sehemu hii ndogo ya Serikali za Mitaa inatakiwa iwe na uimara wa kutosha kutoa huduma za kutosha ambayo inahitaji kiasi cha rasilimali fedha na watu. Haya ni mahitaji muhimu mawili yanayopingana.
- Kuweza kutoa majibu kwa swali hili hapa juu linalojipanga lenyewe, sahihisho lililopo ni kuwa na mfumo wenye ngazi nyingi kutoka Halmashauri hadi jamii. Kwa Japani mfumo huu wa ngazi nyingi unafanya kazi vizuri. Lakini Tanzania pia ina mfumo mzuri wenye Wilaya – Kata – Kijiji – Kitongoji. Hii inasaidia sana kukuza uhuru wa jamii na jitihada shirikishi za maendeleo kati ya Halmashauri na jamii. Mfumo wa Upangaji Mipango Shirikishi Jamii wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo unaweza kuwa jukwaa zuri zaidi la kuboresha mfumo huu na kuuwezesha kufanya kazi kwa ufanisi.

**3.2 Usimamizi na Ugatuaji wa Rasilimali Watu**

Kama ilivyo kwenye sehemu iliyotangulia, mafunzo ya Osaka yalitoa tahadhari kwa Viongozi wa Tanzania katika miaka michache ya mwanzo kuwa waangalifu kuhusu kutoharakisha kugatua na kupeleka madaraka katika MSM. Hata hivyo, kuhusu ugatuaji wa masuala ya rasilimali watu, ujumbe ulikuwa tofauti kidogo kwa vile ilionekana kwamba madaraka haya yalikwisha anza kurudishwa Serikali Kuu; kwani uteuzi wa Wakurugenzi na Wakuu wa Idara wa MSM unafanywa na Wizara pamoja na kuanzishwa kwa Sekretarieti ya Ajira ili kuendesha mchakato wa ajira kwa kada nyingine za watumishi wa MSM.

Nchi ya Japani haikugatua madaraka na kuyapeleka MSM kwa haraka, bali Serikali Kuu ilendelea kuhodhi baadhi ya shughuli. Kwa mantiki hii, ugatuaji nchini Japani haukuwa umekamilika kwa miaka mingi mpaka ilipofika mwaka 2000. Hata hivyo, kuhusiana na kugatua masuala ya usimamizi wa rasilimali watu, Japani ilihakikisha kwamba madaraka haya yamegatuliwa na kupelekwa MSM kikamilifu tangu mwanzo wa maboresho.

Ugatuaji wa masuala ya usimamizi wa rasilimali watu ndiyo jambo la muhimu sana na msingi wa ugatuaji. Kwa mujibu wa mfumo wa Serikali za Mitaa Japani, masuala yote huamuliwa na kutekelezwa ndani ya MSM husika bila kuingiliwa na Serikali Kuu, yaani kuajiri na kufukuza, kuendesha mafunzo, kupanga ngazi za mishahara, kufanya uhamisho, kupandisha vyeo, mpaka kustaafu. MSM Japani huajiri wahitimu wapya kutoka vyuo vikuu kila inapofika mwezi Aprili kulingana na mahitaji yao. Wahitimu walioajiriwa na Mamlaka fulani ya Serikali za Mitaa, wataitumikia Mamlaka husika kwa maisha yao yote mpaka watakapostaafu. Hakuna kanuni ya uhamisho kutoka Mamlaka moja ya Serikali za Mitaa kwenda mamlaka nyingine.

Zaidi ya hayo, Wenyeviti au Mameya ni wanasiasa na huchaguliwa na wananchi kwa njia ya kura, na ndio wakuu wa Tawi la Utawala/Utendaji sambamba na Tawi la Baraza la Madiwani la Halmashauri husika. Watendaji wanawajibika kwa Meya/Mwenyekiti na siyo kwa Madiwani, kwa hiyo masuala ya watendaji hulindwa na huwakilishwa na Meya/Mwenyekiti katika Baraza la Madiwani.

Kwenye mafunzo ya Osaka, mambo matatu yafuatayo yalitiliwa mkazo kwamba ndivyo vitu muhimu katika kufikia uwezo wa juu wa rasilimali watu katika Halmashauri:

1) Kuajiri
   Kuajiri watumishi wenye sifa kuliko wote na wanaofaa katika kufikia dhima/malengo ya mamlaka husika;
2) Mafunzo
   Baada ya kuajiri, kuwapa mafunzo yanayolenga na kuwezesha kufikiwa kwa dhima/malengo ya mamlaka husika (siyo malengo ya mtu binafsi);
3) Kujipanga
   Kuhakikisha kuwa uwezo wote wa Rasilimali watu katika Halmashauri unatumika kikamilifu ili kutimiza malengo ya mamlaka husika.

Kwa minajili hiyo, Japani iliona kuwa ni jambo lisilokwepeka kutangulia kugatua madaraka yahusuyo usimamizi wa rasilimali watu ili kila Halmashauri iweze kuchambua hali halisi,

kupanga mipango, kuajiri, kutoa mafunzo, kupanga majukumu na kudhibiti watumishi. Mtumishi wa Halmashauri lazima awe mtu anayelipenda eneo husika na watu waliopo, anayefanya kazi kwa bidii kwa ajili ya watu, anayeelewa vizuri kuhusu hali ya eneo husika, anayewafahamu watu vizuri na kuwa na uwezo wa kufanya kazi kwa karibu na wakazi wa eneo husika; hii ndiyo mantiki ya ugatuaji. Ni uzoefu wa nchi ya Japani kwamba, kwenye Halmashauri zenye mafanikio ya kuridhisha, kuna maofisa na watendaji wanaofanya kazi kwa kujituma hasa katika kuwahudumia watu, na kushirikiana na wakazi; wengi wao ni wale watendaji waliozaliwa na kukulia katika maeneo hayo na wanayapenda makazi hayo, pamoja na uongozi thabiti wa Meya/Mwenyekiti ambaye naye ni mzawa.


Jambo jingine muhimu linalozifanya MSM za Japani ziwe na nguvu ni juhudi waliyonayo katika kuwapa watumishi wao mafunzo. MSM za Japani zinawekeza sana kwa watumishi kwa kuwapeleka kwenye mafunzo pamoja na mpango wa mafunzo kazini ambao uko kimkakati kulingana na mahitaji ya kitaasisi (siyo mahitaji binafsi) na kwa mtazamo wa miaka ijayo.

Hili linawezekana kule Japani kwa sababu hakuna uhamisho wa watumishi toka MSM moja kwenda nyingine na kiwango cha kubakiza/kushikilia watumishi kazini ni kikubwa sana, hivyo MSM huwekeza bila hofu kwamba baada ya kuwasomesha watahama.

Kinyume chake, Tanzania kuna uhamisho wa mara kwa mara wa watumishi muhimu kutoka MSM moja kwenda nyingine na hivyo ni vigumu sana kuwabakiza/kuwashikilia watumishi kwenye Halmashauri moja. Katika hali kama hii, changamoto kubwa ni jinsi ya kuhakikisha kwamba matokeo yatokanayo na mafunzo ya watumishi yanabaki ili yalete maboresho katika utendaji kazi wa mamlaka husika, na kuzifanya Halmashauri ziwe na bidii katika kujenga uwezo wa watumishi licha ya uwezekano mkubwa wa kuwapoteza baada ya kuwasomesha. Swali moja liliulizwa kwenye mafunzo ya Osaka kama Tanzania inaweza kuandaa na kutekeleza mpango mkakati na thabiti wa muda mrefu wa mafunzo ya kuwajengea watumishi wake uwezo katika hali hii.

Kwa upande mwingine, mafunzo ya Osaka yaliibua suala la "kufanya kazi kama timu" ili kuweza kutumia asilimia 120 ya uwezo wa nguvukazi iliyopo na kuyafikia malengo ya kitaasisi. Kule Japani, kuna mambo kadhaa kuhusu mfumo wa usimamizi wa rasilimali watu ambayo yamefafanuliwa kwa uangalifu mkubwa kwa ajili hiyo, kama vile:

1) Ngazi za mishahara zimewekwa makusudi kwa lengo la kuondokana na rushwa na kuchochea watumishi wafanye kazi kwa bidii hadi watakapostaafu;
2) Mfumo wa kipekee wa Japani "kuchelewesha upandishaji vyeo" ili kumfanya kila mtu afanye kazi kwa bidii kwa miaka mingi kabla ya kupandishwa cheo (kutumia asilimia 120 ya uwezo wa kila mmoja);
3) Watumishi kufanya kazi kwa kuzunguka kila idara ya Halmashauri husika na mtindo wa kuweka kumbukumbu za kila mwaka za utendaji wa kila mtumishi ili kufanya tathmini kwa haki na kwa malengo na kuchagua wale wenye uwezo mkubwa na wanaostahili kupandishwa vyeo kuwa Wakurugenzi;
4) Shughuli zote zinazohusu rasilimali watu ziko chini ya Idara ya Uendelezaji Rasilimali Watu ili iwezeshe namba 3 hapo juu;




5) Mazingira ya kipekee ya Japani yanawezesha "utendaji kazi kama timu", usimamizi unaofanywa na wakuu/viongozi, na mafunzo kazini yanayoendeshwa na wasimamizi, mtindo unaojulikana kama mtindo wa "chumba kikubwa"; ofisi ya wazi ambapo mkuu wa idara hufanya kazi pamoja na wasaidizi wake kwenye chumba kimoja.

Yote yaliyoelezwa kwenye sehemu hiyo hapo juu yamewekwa na kanuni zinazotawala MSM za Japani ili kuhakikisha mambo matatu yahusuyo usimamizi wa rasilimali watu yanazingatiwa mfano 1) kuajiri; 2) mafunzo; na 3) kufanya kazi kwa bidii. Swali liliulizwa, katika mazingira ya sasa ya Halmashauri za Tanzania, ni kwa jinsi gani zinaweza kutekeleza mambo haya matatu.

### 3.3 Fedha za Serikali za Mitaa na Ugatuaji wa Masuala ya Fedha

**a) <u>Misingi ya kifedha katika Halmashauri</u>**

Michoro (1) na (2) inaonyesha japo kwa ufupi hali ya Halmashauri za Japani kuhusu masuala ya fedha.

**Mchoro (1) Uwiano wa Matumizi ya SK na SM kwa kila sekta**
Chanzo: Mwongozo wa fedha za Serikali za Mitaa, 2010
(Wizara ya Mambo ya Ndani, Japani)


Mchoro (1) unaonyesha ukubwa wa majukumu ya Halmashauri katika matumizi ya kutoa huduma ndani ya kila sekta. Ukiangalia sekta ya afya, Halmashauri hutumia 94% ya fedha iliyotengwa kwenye bajeti ya afya ya Taifa na Serikali Kuu hutumia 6% tu. Kwenye elimu uwiano kati ya Halmashauri na Serikali Kuu ni 85% kwa 15%.

Ukizingatia uhusiano wa karibu uliopo kati ya uzito wa majukumu na matumizi, Halmashauri za Japani zinafanya sehemu kubwa zaidi ya majukumu ya Serikali ya kutoa Huduma. Kwa upande mwingine, ni muhimu kutambua kwamba kiasi kikubwa cha bajeti <u>hutengwa</u> kwa ajili ya kuziwezesha Halmashauri kutekeleza majukumu mazito yaliyogatuliwa na kupelekwa kwao.


Je hali ikoje Tanzania? Ukweli ni huu, ukiangalia majukumu yote yaliyogatuliwa na kupelekwa kwenye ngazi za msingi katika MSM Tanzania, ukubwa wa majukumu ni sawa na yale ya MSM za Japani. Lakini, bajeti iliyotengwa kwa ajili ya Halmashauri Tanzania, ilikuwa pungufu ya TZS trilioni 3 ya bajeti ya taifa ya zaidi ya TZS trilioni 11 ya mwaka 2011/12.

Ulinganisho unaofanywa, ni ule unaohusu bajeti za Halmashauri zilizo na masharti au uhuru wa matumizi. Mchoro (2) unaonyesha viwango na vyanzo mbalimbali vya mapato ya Halmashauri za Japani. Kama ilivyothibitishwa na takwimu hizi, 51% ya mapato hutokana na vyanzo vya ndani (kodi, ushuru na malipo mbalimbali). Aidha, kuna ruzuku ambazo hazina masharti yoyote ya matumizi zinazoitwa "ruzuku toka Serikali Kuu kwenda MSM" (ruzuku za LAT). Ruzuku ya LAT ni fedha nyingi inayotoka Serikali Kuu kwa mara moja kwenda MSM na serikali za mikoa. Fedha hii inahamishwa toka Wizara ya Fedha kwenda kwenye akaunti kuu ya kila Halmashauri siku ya kwanza ya kila robo mwaka. Ukijumlisha mapato ya ndani na ruzuku za LAT toka Serikali Kuu, Halmashauri za Japani zina aslimia 75% ya bajeti isiyo na masharti na wanaweza kutumia kama wanavyoamua wenyewe.

Mchanganuo huu ni wa muhimu sana kwa MSM za Japani katika kufikia malengo ya mipango yao ya maendeleo, kwani wana bajeti ya kutosha na ya uhakika kila mwaka. Washiriki toka Tanzania walipochunguza hali za MSM, walithibitisha kwamba zina hali mbaya ya kifedha pia fedha nyingi wanayopokea ina masharti ya matumizi kama ilivyo kwenye Mchoro, (3).




Mchoro (3): Muundo wa vyanzo mapato ya SM za Tanzania
Chanzo: Ni hesabu zilizofanywa na mwandishi toka tovuti ya serikali ya Tanzania





Mchoro(2): Vyanzo na viwango vya mapato ya SM za Japani
Chanzo: Mwongozo wa fedha za Serikali za Mitaa, 2010 (Wizara ya Mambo ya Ndani, Japani)

Ama kwa hakika, hata kwa hali hii ingelikuwa jambo la maana kama 94% ya ruzuku wanayopokea isingelikuwa na masharti ili Halmashauri ziwe na uhuru wa kuzitumia. Bahati mbaya, kuna ruzuku mbalimbali zinazokuja zikiambatana na masharti katika matumizi. Hivyo basi, hata kama Halmashauri itaanda mipango mizuri ya maendeleo, ni vigumu sana kutekeleza miradi yao ya vipaumbele kwa sababu ya ruzuku zenye masharti, ambazo husababisha mipango ya maendeleo isitekelezeke kirahisi.

Ikumbukwe kwamba kiasi cha fedha inayotengwa kwenye bajeti za Halmashauri ni kidogo mno cha Shilingi trilioni 3 kati ya trilioni 11 za bajeti ya taifa (2011/12). Hizi Shilingi trillioni 3 ni sawa

na 94% ya bajeti nzima ya Halmashauri, na hii inathibitisha jinsi ambavyo hawana vyanzo vya ndani vya kutosha.




**Mchoro (4): Aina za Kodi kwenye Majiji/Miji**
**Chanzo: Mwongozo wa fedha za Serikali za Mitaa, 2010 (Wizara ya Mambo ya Ndani, Japani)**

Mafunzo ya Osaka yaliwataka viongozi wa Serikali ya Tanzania kutenga kiasi cha kutosha cha bajeti kutekeleza wingi wa majukumu ya Halmashauri yaliyogatuliwa na kupelekwa kwao kama kweli wameazimia kufikia ugatuaji wa madaraka. Fedha hizi zinaweza kutoka vyanzo vya ndani au katika ruzuku isiyo na masharti[5]. Kama hakuna bajeti ya kutosha inayotengwa, basi hakuna sababu ya kugatua majukumu kwenda ngazi za Halmashauri. Vinginevyo, shughuli hizo hazitatekelezwa na mwishowe jamii itateseka kwa kukosa huduma. Kama tulivyoona kwa Halmashauri za Japani, ikitokea kwamba 85% ya majukumu ya kutoa huduma za elimu yamegatuliwa na kupelekwa ngazi za Halmashauri, basi kiasi cha kutosha cha bajeti ya kutekeleza majukumu hayo hugatuliwa na kupelekwa Halmashauri ili kufikia malengo. Vinginevyo si haki hata kidogo kwa Halmashauri na hasa kwa watu wanaotegemea huduma.

**b) <u>Kodi za Ndani kwa ajili ya Uendelevu na ushamiri wa Serikali za Mitaa</u>**

Nchini Japani, kuna sababu zilizo wazi kabisa kuhusu aina zote za kodi zinazotengwa kwenye ngazi zote mbili za MSM (Mikoa ndiyo ngazi ya juu ya MSM, Miji na Majiji ndiyo ngazi za chini za SM[6]). Japokuwa Mikoa ndiyo ngazi ya juu ya MSM ya Japani, zinaweza kulinganishwa na Halmashauri za Tanzania kwa ukubwa wa eneo. Kuhusu majukumu, ngazi za chini za MSM Japani ndizo zinalinganishwa na ngazi za Halmashauri za Wilaya/Miji/Manispaa/Jiji kwa Tanzania. Hata hivyo kule Japani, huduma zote za muhimu kwa jamii hutolewa na Majiji/Miji kwa sababu ndizo ngazi za msingi zilizo karibu na watu, huku Mikoa wanahusika na maendeleo ya kiuchumi kwa vile majukumu haya yanahitaji eneo kubwa kwa ajili ya mipango na kuyatekeleza kimkakati.

Kulingana na majukumu yalivyo na wajibu wa Majiji/Miji, zifuatazo ni kodi ambazo zinaweza kutozwa na Majiji: Kama inavyoonekana katika mchoro (4), kodi za nyumba na mali zisizo hamishika ni sawa na 45.3% ya mapato yatokanayo na kodi, ambayo ni takribani nusu ya mapato yote yatokanayo na kodi. Ukijumlisha na "Kodi ya mkazi" (kodi ya Kichwa) pamoja na "kodi ya mipango miji", inakuwa ni zaidi ya 80% ya mapato yatokanayo na kodi. Kodi za nyumba

[5] Kwa hatua zilipofikia kwa sasa, bado haishauriwi kugatua madaraka ya kifedha na kuwapa SM mamlaka makubwa ya kutoza kodi. Hii ni kwa sababu hali hii itaziumiza zile SM zilizo kwenye maeneo yenye ufukara ya vijijini, kwa vile hazina vyanzo vya uhakika vya kodi, huku zile SM tajiri za mijini zitakuwa na mapato mengi kutoka vyanzo vyao vya ndani . Kwa hiyo ni busara zaidi kuendelea kutoa ruzuku kutoka chanzo kimoja, lakini SM ziwe na uhuru na maamuzi wa kuzitumia kulingana na vipaumbele vyao kwa sasa.

[6] Kuna Mikoa 47 na Manispaa 1,742 hadi kufikia Oktoba 2012. Manispaa za Japani zinajumuisha Majiji**<u>, Miji na Vijiji</u>**, na tofauti na mgawanyiko wa ngazi za MSM za Tanzania.

na kodi ya mipango miji hutozwa kwenye ardhi na majengo na hizi ni kodi ambazo hakuna awezaye kuzikwepa. Kama ardhi yote na majengo yote yamesajiliwa na kuthaminiwa vizuri, basi hivi ni vyanzo vya uhakika kwa MSM.

“Kodi ya kila mkazi wa Halmashauri za Japani” ni “kodi ya kichwa” iliyofutwa hapa Tanzania ambayo ni “kodi ya maendeleo”[7]. Chanzo hiki cha kodi pia huwa ni chanzo cha kuaminika kwa sababu wakazi wote wameandikishwa na Halmashauri inajua wanapoishi. Tukiangalia hali ya Tanzania, vyanzo vingi vya mapato ni vile vinavyohusiana na shughuli za kiuchumi, mfano ushuru wa mazao (23%), ushuru wa huduma (18%), ushuru wa nyumba za kulala wageni (3%), leseni (10%), karo na malipo mbalimbali (17%), ambazo hubadilika kulingana na mabadiliko ya hali ya uchumi wa eneo husika, na cha kushangaza ni kwamba kodi ya majengo ni 8% tu ya mapato yatokanayo na kodi.

Mafunzo ya Osaka yaliwapa viongozi wa Tanzania changamoto kwamba ili Halmashauri ziweze kutoa huduma endelevu zinazohitajika kwa wakati na viwango vinavyotegemewa, ni lazima kujenga wigo mpana na mfumo wa uhakika wa kukusanya kodi ndani ya Halmasahuri zenyewe. Uzoefu wa Japani unaonyesha kwamba bila kuweka msisitizo kwenye vyanzo vyenye uhakika vya kodi/ushuru kama vile kodi za majengo, kodi ya kichwa/kodi ya maendeleo, siyo rahisi hata kidogo kwa Halmashauri kutekeleza majukumu yake. Kwa mazingira haya, ni muhimu kuwa na mfumo wa daftari la kuandikisha ardhi na mali zisizohamishika pamoja na daftari la wakazi wote kwa kila Halmashauri. Hii itasaidia nchi nzima siyo tu kwenye masuala ya kukusanya mapato, bali kwa matumizi mengine mengi.

Kuhusu utaratibu huu, inafaa kusema kwamba tayari Tanzania kuna mifano ya kufurahisha na inayotia moyo ya Halmashauri zinazotekeleza kile kinachopendekezwa hapa. Rejea kisa mkasa cha Manispaa ya Mtwara Mikindani kwenye Sura ya Tatu ya Kitabu cha Mbinu Bora Toleo la Kwanza .

### 3.4 Maendeleo ya Kiuchumi ya Serikali za Mitaa – Uzoefu wa kufurahisha wa dhana ya ki-Japani ya “Vuguvugu la Kijiji Kimoja Zao Moja” (OVOP)

Hitaji la maendeleo ya kiuchumi ya Halmashauri limekuwa likisumbua vichwa vya Wakurugenzi wengi wa Tanzania. Kuhusiana na hili, kuna uzoefu maarufu nchini Japani wa dhana ijulikanayo kama “Vuguvugu la Kijiji Kimoja Zao Moja” maarufu kama OVOP, lililoanzia kwenye Mkoa wa Oita ambao hapo awali ulikuwa fukara kuliko yote nchini humo. Uzoefu unaotokana na dhana hii unaweza kuwa muafaka kwa Tanzania kama utatafsiriwa na kutumika inavyostahili kulingana na mazingira ya Tanzania.

---

[7] Tofauti pekee ni kwamba kodi ya kichwaTanzania hutozwa kwa kiwango sawa kwa kila mtu, kwa Japani kodi ya mkazi hutozwa kulingana na viwango vya kipato cha kaya. Kama hakuna kipato cha kiasi fulani kinachokubalika, basi wanakaya wa kaya hiyo hawana sababu ya kulipa kodi ya mkazi.

**(a) Kijiji Kimoja Zao Moja ni nini?**

Vuguvugu la "Kijiji Kimoja Zao Moja" au OVOP ni mkusanyiko wa ubunifu wa shughuli za maendeleo ya jamii zilizobuniwa na kupata msukumo wa viongozi kutoka jamii husika katika Mkoa wa Oita, ambao waliipenda jamii yao na wakahuzunishwa kutokana na hali ya ufukara uliokuwa umekithiri huko miaka ya nyuma. Japokuwa juhudi kama hizo za mtu mmoja mmoja zilikuwepo hapa na pale kwenye Mkoa wa Oita tangu miaka ya 1960, dhana yenyewe ya "Kijiji Kimoja Zao Moja" ilianzishwa rasmi mwaka 1979 na Dk. Morihiko HIRAMATSU, akiwa Gavana[8] wa Mkoa huo kwa kuanza kuzitambua baadhi ya juhudi za jamii zilizokwisha anza na kuziendeleza.

Dk. HIRAMATSU alikuwa ni msomi mwenye mafanikio makubwa akiwa mtumishi wa cheo cha juu kwenye Wizara ya Biashara za Kimataifa na Viwanda. Hii ilikuwa Wizara yenye nguvu sana, lakini aliamua kuacha kazi hiyo na kurudi kwenye Mkoa wa Oita; nyumbani kwao. Kilichomsukuma ni kwa sababu alihofia sana kuwa Mkoa wa nyumbani kwake uliendelea kubaki nyuma kimaendeleo na kuwa miongoni mwa Mikoa fukara kuliko yote nchini Japani kwa wakati huo.

Baada ya kurudi kwao, aligombea na kushinda cheo cha Ugavana wa Mkoa wa Oita. Alipoanza kazi hii jambo la kwanza alilolifanya ni kutembelea vijiji vyote kwenye Mkoa huo. Wakati akifanya matembezi haya, alikuta kuna miradi ya maendeleo na jitihada mbalimbali za watu wenyewe kujaribu kujinasua huko vijijini. Aliguswa sana na jitihada hizo za wananchi wakiongozwa na viongozi wao wenye mapenzi mema na juhudi hizi zilikuwa hazijulikani kwa serikali. Alithamini sana juhudi za jamii, akawatia moyo waendelee na jitihada za kujikwamua. Kwa wanavijiji, wengi wao walikuwa hawajawahi kutoka nje ya vijiji vyao, kwa hiyo kwao ilikuwa ni faraja kubwa kutembelewa na mtu mkubwa kama Gavana na kusifiwa kwa kile walichokuwa wanakifanya! Hawakuwahi kuwaza kwamba kile walichokuwa wanakifanya kilikuwa ni kitu cha kipekee na cha thamani machoni pa wengine. Tangu Gavana wao Dk. HIRAMATSU alipofanya ziara hizi, juhudi hizo za jamii zilipewa msukumo mkubwa na watu wakahamasika zaidi na kujisikia fahari wenyewe.

Kwa upande wake, Dk. HIRAMATSU alifikiri ni jukumu muhimu kwa Serikali ngazi ya Mkoa kuunga mkono na kuendeleza juhudi za thamani kubwa zilizoanzishwa na wananchi kutaka kuboresha maisha yao wenyewe, kuzieneza zaidi na kubadilisha uzoefu huu mzuri na viongozi kwa vijiji vingine ndani ya Mkoa wao.

Vuguvugu la "Kijiji Kimoja Zao Moja" lina mambo muhimu yanayolitofautisha na dhana nyingine kwani Vuguvugu hili husababisha kuzalisha bidhaa za kipekee (ikijumuisha utalii), ili kupata maendeleo kwa kutumia rasilimali zilizopo ndani ya jamii husika. Hata hivyo, jambo jingine la tofauti kwenye vuguvugu la "Kijiji Kimoja Zao Moja"ni kwamba: kuna uzoefu thabiti wa jamii unaopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi midogo ya maendeleo ya shughuli za kiuchumi ngazi za msingi. Wananchi husika huunganisha uwezo wao wa kujipanga na kutekeleza

[8] Cheo cha Gavana wa Mkoa ni cheo cha juu zaidi kwenye MSM za juu Japani ikilinganishwa na Meya wa kwenye MSM za Tanzania (Ona "3.2. Usimamizi wa Rasilimali Watu na Ugatuzi wa madaraka" kwa Meya.)

mustakabali wa maisha yao; jamii zimejijengea uwezo, zimeamka na zina ujasiri; Jamii zimeimarika na zimefikia uwezo wa kujitawala na kujiendesha zenyewe kama kijiji. Ukweli uliopo hapa ni kwamba wananchi wana uzoefu wa kufanikiwa na wakati mwingine kushindwa (lakini wamejijengea uwezo na tabia ya kujikwamua katika kushindwa huko), siyo tu kwamba jamii inategemea kupata mafanikio ya kiuchumi pekee, bali pia jamii inatarajia kujijengea uwezo, uzoefu na ujasiri na kupata nguvu zaidi katika mchakato huo. Ukweli huu ni muhimu ufahamike ili kulielewa vizuri vuguvugu la "Kijiji Kimoja Zao Moja". Ikumbukwe kwamba ni rahisi sana kupata mafanikio au faida ya mara moja katika biashara au mradi fulani kutokana na msaada wa mara moja kutoka nje ya jamii, lakini kama jamii hiyo itakumbana na vikwazo fulani fulani baadaye, hawataweza kuvishinda kama watakuwa hawajajijengea uwezo kupitia michakato iliyotangulia ya kutatua matatizo yao kwa nguvu na jitihada zao wenyewe.

Kwa mantiki hii, ni vyema kutambua kwamba kati ya juhudi zilizojitokeza kwenye Vuguvugu la "Kijiji Kimoja Zao Moja" kule Oita, zilipitia mchakato ufuatao:

- Kabla ya vuguvugu la "Kijiji Kimoja Zao Moja", wanavijiji wa Oita walikuwa fukara sana, walikuwa wamekata tamaa kuhusu mabadiliko, wenye kijicho na kuoneana wivu wao kwa wao; kutokana na hali hii haikuwezekana kushirikiana baina yao ili kuboresha maisha kwa pamoja. Hata hivyo, kupitia Vuguvugu la "Kijiji Kimoja Zao Moja" walianza kujitambua kwamba "Ndiyo, tunaweza kama tunataka!" Haya ni mafanikio makubwa katika mchakato wa kubadili fikra.
- Katika badiliko la fikra hapo juu, wanavijiji walianza kujijengea uzoefu wa kushirikiana kwenye shughuli mbalimbali ndani ya jamii, wakizikabili changamoto wanazokutana nazo na kuzishinda kwa pamoja. Mchakato huu uliwafanya waweze kujipanga vizuri zaidi.
- Kupitia mchakato huo, waliimarisha mahusiano na taasisi za nje zenye usaidizi ikijumuisha Halmashauri, Asasi za kiraia na mashirika yasiyo ya kiserikali.
- Pamoja na ujenzi wa uwezo wa jamii ulioelezwa hapo juu, jamii husika zilifanikiwa kupata matokeo dhahiri ya maendeleo ya kiuchumi.

**(b) DK. HIRAMATSU Alifanya Nini Akiwa Gavana wa Mkoa?**

Kwanza kabisa, ieleweke vizuri kwamba vuguvugu la "Kijiji Kimoja Zao Moja" halikuwa ni programu ya lazima ("maamrisho ya kutoka juu kwenda ngazi za msingi") iliyoandaliwa na Dk. HIRAMATSU na kwamba watu hawakuambiwa cha kufanya. Kwa bahati mbaya, baadhi ya nchi zinazoendelea ambazo zilivutiwa na Vuguvugu la "Kijiji Kimoja Zao Moja", waliuelewa vibaya ukweli huu. Walizingatia tuu zile faida za kiuchumi zinazotokana na "Kijiji Kimoja Zao Moja" na kujaribu kuendeleza vuguvugu la "Kijiji Kimoja Zao Moja" kama sera ya taifa na kutoa maamrisho kutoka juu kwamba kila kijiji kizalishe kitu ambacho kinaweza kuuzwa hapa nchini au nje ya nchi. Kinyume chake sasa, alichokifanya Dk. HIRAMATSU kwenye Mkoa wa Oita ilikuwa ni; kwanza, kutembelea vijiji vyote, kuzitambua juhudi za thamani za wananchi ambazo zilikwishaanza, kuwasifu na kuwatia moyo.

Pili, alivishirikisha vijiji vingine na viongozi wao kuhusu mambo mema yanayofaa kuigwa ili habari hii iwe kichocheo, waanze na wao kufikiri kuhusu maendeleo yao kwa kutumia rasilimali

zilizopo kwenye maeneo husika, badala ya kulalamika kutokuwa na rasilimali kwenye vijiji vyao na kukata tamaa.

Tatu, alitambua bidhaa za kipekee kwenye baadhi ya vijiji na alisaidia kutafuta soko la ndani na nje ya Mkoa wa Oita. Alitumia maarifa yake, uzoefu na mitandao ambayo alikwisha jijengea alipokuwa afisa wa ngazi za juu Wizara ya Biashara ya Kimataifa na Viwanda. Alizitangaza bidhaa hizi nchi nzima.

Nne, aliwezesha suala zima la kubadilishana uzoefu baina ya viongozi wa vijiji mbalimbali ili wajifunze na kuhamasika kutokana na kujifunza kwa watu walio kwenye ngazi moja na siyo kujifunza kwa ngazi tofauti za maendeleo. Alianzisha shule ya kuendeleza rasilimali watu[9]" iliyoitwa "*Toyonokuni*[10]. Juhudi hizi za Gavana, zilisaidia kuchochea ari ya viongozi na hii ikasaidia kuibuka kwa miradi mingi yenye sura ya "Kijiji Kimoja Zao Moja".

Kama inavyoonekana hapo juu, dhamira ya vuguvugu la "Kijiji Kimoja Zao Moja" ilikuwa ni Halmashauri kuzitambua, kuzisifia na kutia moyo juhudi za kimaendeleo zinazojitokeza kwa jamii. Jukumu la Halmashauri ni "uwezeshaji" na siyo "utekelezaji" au "uelekezaji". Dk. HIRAMATSU hakuwaambia wanavijiji jambo la kufanya katika kuendeleza vuguvugu hili, bali aliheshimu juhudi zao na umiliki wao, pamoja na nguvu zao. Mafunzo ya Osaka yanasisitiza vuguvugu la "Kijiji Kimoja Zao Moja", kwani ni dhana muafaka kwa mazingira ya Tanzania, na inaaminika kwamba tayari zipo juhudi za namna hiyo kwenye Vijiji na wapo viongozi wazuri wanaojali maendelo katika maeneo yao. Ingelikuwa ni jambo la manufaa makubwa kwa Tanzania kuunga mkono vuguvugu hili na kutoa fursa ya wazalishaji kujifunza kwa wenzao walio ngazi moja. Mafunzo ya Osaka yaliwataka viongozi wa Tanzania kutodhani hakuna chochote kwenye vijiji vyao. Kuna mambo mengi mazuri yanayostahili kuigwa lakini pengine wao ndio hawajayatambua. Ni wajibu wa viongozi wa Halmashauri kuanza kuzitambua juhudi za jamii zilizopo, kuzitia moyo, na kubadilishana uzoefu na wengine. Ingekuwa ni njia yenye tija zaidi ya wazalishaji kujifunza kutoka kwa wenzao walio kwenye ngazi moja kuliko kujifunza kutoka kwa watu wa ngazi tofauti au kutoka kwenye vitabu. Ni kutokana na mtizamo huu ndipo kitabu hiki kikaandaliwa.

### 3.5 Masuala Mengine

Kuna mengi ambayo hatukugusia hapo juu kutokana na kukosa nafasi. Lakini, yapo ambayo ni ya muhimu kugusia ambayo yanafaa kwa Tanzania kama vile kisamkasa cha Minamata na na madhila yaliyotokana na "Ugonjwa wa Minamata" na jinsi walivyoweza kuhuisha jamii kutokana na mkasa huo; Upangaji mipango shirikishi jamii; mipango miji; mipango ya matumizi bora ya ardhi na marekebisho ya ardhi, uzoefu wa Japani kuhusu maendeleo ya kiuchumi na mchango wa Halmashauri katika mkasa huo.

---

[9] Inaitwa "shule" lakini hakuna majengo. Huwa ni aina fulani ya mafunzo kwa njia ya warsha kwa ajili ya viongozi ili kuwakutanisha pamoja.

[10] "Toyonokuni" jina la kienyeji la eneo hili la Mkoa wa Oita

Kuhusu kisamkasa cha Minamata, mafunzo ya Osaka yanaweka msistizo kwenye umuhimu wake, na inaaminika kwamba nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania zina mengi ya kujifunza kutokana na kisa mkasa hiki.

## 4.0 MAENDELEO BAADA YA MAFUNZO YA OSAKA YALIYOSABABISHA KUANDALIWA KWA KITABU HIKI

Kama ilivyoelezwa kwenye sehemu ya 1 hapo juu, mafunzo ya Osaka yalikuwa yameandaliwa mahsusi kwa nchi ya Tanzania kwenye miaka mitano ya mwanzo (2002 – 2007), yaliendelea kwa miaka mingine sita lakini wigo wake ukapanuliwa na kuingiza nchi nyingine tatu (2008 – 2012). Mafanikio makubwa katika miaka hii 11 hapa Tanzania ni kule kuanzishwa kwa TOA. Huu ni mfano wa pekee Duniani kuwa na Umoja wa Wahitimu wa kozi ya aina moja ukijumuisha wadau maarufu ambao ni viongozi wa maboresho. Kuanzishwa kwa TOA ni mfano wa kipekee hata kwa JICA ambayo inaendesha maelfu ya kozi za mafunzo duniani kote lakini haijatokea kuanzishwa kwa umoja wa aina hii sehemu nyingine.

TOA imeanza kuendesha semina mbalimbali na warsha za mafunzo kama vile Mafunzo baada ya Osaka na Warsha za Mafunzo ya Kanda kwa ajili ya kubadilishana uzoefu baina ya Halmaushauri na wanachama. Fursa hizi, siyo tu kwamba zinasaidia kubadilishana maoni baina ya Halmashauri wanachama, bali zimetoa uwanja ambao ni nadra kuupata wa majadiliano kuhusu uhalisia wa Ugatuaji wa Madaraka, hususani changamoto wanazokutana nazo katika kutekeleza maboresho ya Serikali za Mitaa.

Mpaka sasa, hakuna asasi ya namna hii hapa Tanzania, inayowahusisha Watendaji wa Serikali za Mitaa na wale wa Sekretarieti za Mikoa. Jumuia ya Serikali za Mitaa (ALAT) ipo, lakini wahusika wake wakuu ni Wenyeviti wa Halmashauri, Mameya na Wabunge. Vikao vya Jumuiya hii haviwapi fursa Wakurugenzi wa Halmashauri kushiriki kikamilifu na kutoa ushauri wa kitaalamu ingawa wao ni wajumbe. Kwa mantiki hii, TOA ina uwezekano mkubwa wa kukua hadi kuwa Umoja wa Watendaji Wakuu wa Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa ambao ni wataalamu na watekelezaji wa ugatuaji wa madaraka na maboresho nchini. Hawa ndio wanaoshughulika kila siku kwenye mstari wa mbele wa maboresho. Maoni na mapendekezo yao ya pamoja yanaweza kuwa ya msingi na kuongeza ufanisi kwenye kutekeleza maboresho.

Kuhusu mambo mema yanayofaa kuigwa, tayari Tanzania imekwishajijengea uzoefu kwa zaidi ya muongo mmoja wa utekelezaji Ugatuaji wa Madaraka kwenda ngazi za msingi katika kila MSM. Lazima kutakuwepo na idadi kubwa ya mambo ya kuvutia na uzoefu mzuri kwenye Halmashauri nyingi kote nchini ambayo yanafaa kushirikisha Halmashauri nyingine. Japani inaamini kwamba aina hii ya kujifunza kwa taasisi zilizo kwenye ngazi zinazofanana inaweza kuwa muafaka zaidi kuliko kujifunza kutoka nje ya nchi; kutoka kwenye ngazi tofauti au ya juu sana. Tanzania inaweza kujifunza vizuri kutokana na uzoefu ulioko ndani, mfano shughuli za "Kijiji Kimoja Zao Moja" kama zilivyoelezwa kwenye 3.4. hapo juu. Kitabu hiki cha rejea kiliandaliwa kwa kuzingatia maelezo na msingi huo ulioelezwa hapo juu. Ni matumaini ya TOA kwamba mafunzo ya Osaka yatachangia kuboresha utendaji ndani ya MSM, kila moja ikimchochea mwenzie, na kuendeleza mambo mema yanayojitokeza ambayo yataleta ufanisi na mafanikio ya ugatuaji wa madaraka katika nchi hii.

Mwisho, inastahili kusema kwamba kutokana na matokeo chanya yaliyotokana na mafunzo ya Osaka kwa nchi ya Tanzania, ambayo yameelezwa kwenye sura hii, JICA iliamua kuendelea kutoa mafunzo ya Osaka kwa miaka mingine mitano, yaliyolenga kuwezesha shughuli za wanaumoja wa TOA na juhudi zake za ujenzi wa kitaasisi. Hii ina maana kwamba, viongozi wengine wengi wa maboresho Tanzania walifaidika kutokana na mafunzo ya Osaka na wakaweza kuchangia utekelezaji wa maboresho ya ugatuaji wa madaraka kwenda ngazi za msingi nchini.

# Sura ya Pili

## Jitihada za Jamii kwa Ajili ya Huduma Bora

Mtazamo wa Jitihada za Jamii ni mfumo mpya katika eneo la maendeleo vijijini, ambao lengo kuu ni maendeleo vijijini. Malengo Mahsusi ya mfumo huu ni kuongeza ubora wa maisha ya watu maskini, na kuboresha miuondombinu. Ni mfumo wa hiari wa kundi la watu wanojiendesha wenyewe wakiwa na tabia zinazofanana za kijamii na kiuchumi, ambao wanaungana ili kuanzisha fikra zitakazochochea maendeleo endelevu. Mtazamo wa Jitihada za Jamii kwa ajili ya Maendeleo Vijijini katika hali ya kendesha mipango ya kiuchumi huleta ajira, miondombinu ambayo jamii inaweza kujitengenezea, stadi za kazi pamoja na shughuli mchanganyiko. Mtazamo huu huleta mipango ya ustawi wa jamii ili kuboresha afya, lishe na maslahi ya jamii kwa ujumla.

Jitihada za jamii huwa na maana ya majaribio ya jamii kupambana na changamoto zinazoikabili kijamii na kiuchumi bila kusubiri miradi mikubwa kutoka serikalini. Jitihada za jamii hujumuisha maazimio ya kutatua matatizo ya jamii kupitia jamii kujipanga, kushiriki na kutekeleza. Katika haya yote, jamii yenyewe huona hitaji, hupanga namna ya kufikia hitaji, hutafuta rasilimali zilizopo zinazohitajika kufikia hitaji, hujipanga katika makundi ya utekelezaji na kutekeleza miradi.

Mara nyingi jitihada za jamii huwa na maana ya uundaji wa vyama vya hiari katika jamii, ambapo wanchama huwa na malengo yanayofanana, hujipanga na kuratibu mipango wakiwa na lengo mahsusi la kuboresha hali ya kijamii na kiuchumi katika jamii yote. Tafiti zinaonesha kuwa vikundi katika jamii kwa miaka mingi vimefanikiwa kujiendesha katika kujenga barabara, vituo vya afya, madaraja na nyumba, kulima mashamba, kufadhili masomo, na kuanzisha taasisi za viwanda.

Hapa Tanzania, Jitihada za Jamii na Ushiriki wa Jamii vimekuwa dhahiri kutokana na historia ya itikadi ya kijamii na kiuchumi ya kujitegemea. Tangu Uhuru, jamii katika vijiji vyao zilishauriwa kuishi katika jamii na kutumia mbinu za ushirika katika kutatua matatizo yao. Kati ya miaka ya 1960 na 1970 na hasa baada ya Azimio la Arusha, jamii zilianzisha miradi mbalimbali na kuitekeleza ikiwa ni pamoja na ujenzi wa shule na zahanati, kuchimba visima na mabwawa madogo, kulima barabara na kuendesha kilimo cha ushirika.

Pamoja na kuwa mbinu hizi zilipungua katika miaka ya 1990 kuelekea milenia mpya kutokana na mtazamo wa Serikali kuwa inaweza kutoa huduma zote, kuna jamii ambazo siku za karibuni zimetumia jitihada za jamii kwa kina katika ujenzi wa shule, zahanati, madarasa na majengo ya Serikali; vyote vikilenga kuboresha utoaji wa huduma.

Katika Sura hii Mbinu Bora mbalimbali zimewasilishwa kutoka Hamashauri za Wilaya za Ludewa, Msalala na Mpwapwa, Halmashauri ya Mji wa Mbulu na Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa inahusu Jitihada za Jamii Katika Ujenzi wa Miundombinu ya Maji Safi na Salama katika Kijiji cha Itundu ambacho kilikuwa na upungufu mkubwa wa maji. Wananchi walitembea umbali mrefu (hadi 5km) kwenda kwenye vyanzo vya maji na kuwafanya wanawake kutumia takribani masaa 8 kwa siku kutafuta maji. Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuongeza upatikanaji wa maji katika Kijiji cha Itundu na kutafuta vyanzo vipya vya maji ili kujenga miundombinu ya maji ya mserereko. Mbinu zilizotumika kufikia lengo hili ni pamoja na ujenzi wa uelewa, michango, uundaji wa kamati ya maji, ujenzi wa banio, ujenzi wa bomba kuu, ukarabati wa vituo vya zamani, maombi ya kibali cha kutumia maji na kupima ubora wa maji. Jitihada hii imefanikiwa kukamilisha miundombinu ya maji, huduma za maji zimeimarika, wanawake wamewezeshwa, huduma za maji majumbani zimeongezeka, magonjwa yatokanayo na maji machafu yametokomezwa na shughuli mpya za kiuchumi zimepatikana. Kamati ya Maji inaendelea kuhamasisha jamii kuunganisha maji katika makazi yao ili kuongeza mapato. Kijiji cha Itundu kimefanikiwa kutokana na uwazi na uongozi imara wa kamati ya maji. Mradi huu ulifanikiwa sana kutokana na kuwa hitaji halisi la jamii ya Kijiji cha Itundu.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Mji wa Mbulu inahusu Jitihada za Jamii ya Kata ya Nambis Katika Ujenzi Wa Shule ya Sekondari ya Hhaynu. Halmashauri ilikuwa na changamoto ya msongamano wa wanafunzi katika Shule ya Sekondari ya Murray kutokana na ufaulu wa juu wa shule zote 4 za msingi za Kata ya Nambis. Jamii ya Kata hii ililenga kupunguza msongamano wa wanafunzi kutoka 100 hadi 40 kwa mkondo mmoja katika Shule ya Sekondari ya Murray kwa kuanzisha Shule mpya ya Sekondari ya Hhaynu. Mbinu zilizotumika kufikia lengo hili ni kupitisha mapendekezo, uteuzi wa kamati ya utekelezaji, utwaaji wa ardhi, uhamasishaji wa jamii, maombi ya michoro na miongozo, uchangiaji wa fedha taslimu, uanzishaji wa sheria ndogo na utafutaji wa michango kutoka kwa wadau mbalimbali. Jamii ya Kata ya Nambis imefanikiwa kuwa na miundombinu ya shule, Shule ya Sekondari ya Hhaynu inafanya kazi, kuongezeka kwa uandikishaji na jamii yenye motisha na umoja. Ili kuwepo kwa uendelevu wa jitihada hii, jamii imepanga kuendelea na ujenzi na upandaji miti ili kuifanya shule kuwa ya kijani na inayovutia. Sababu kubwa za kufanikiwa kwa jitihada hii ni uwazi na uwajibikaji.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Wilaya ya Msalala inahusu Jitihada za Jamii katika Uanzishaji wa Shule ya Sekondari ya Segese. Kata ya Segese ilikuwa na shule moja tu ya sekondari iliyoitwa Shule ya Sekondari ya Mwalimu Nyerere ambayo ilikuwa na msongamano. H/W ya Msalala ililenga katika kuboresha ubora wa elimu kwa kuanzisha shule mpya ya sekondari ili kuwapatia nafasi zaidi wanafunzi kupata elimu bora. Mbinu zilizotumika ni pamoja na uhamasishaji wa jamii, uundaji wa kamati ya ujenzi, utafutaji wa rasilimali, ununuzi wa ardhi ili kujenga miundombinu ya shule, utafutaji wa fedha na utaalamu kutoka Halmashauri. Kata ya Segese imefanikiwa kuwa na mazingira bora ya kufundisha na kujifunza, kuongezeka kwa uandikishaji wa wanafunzi na ushirikiano imara kati ya wadau. Halmashauri inaendelea kutenga bajeti kila mwaka na kuongeza idadi ya watumishi na vifaa vya elimu. Siri ya mafanikio ya jitihada hii ni uhusiano mwema kati ya Halmashauri na uongozi wa Kata ya Segese.

Mbinu bora ya Jiji la Dodoma inahusu Jitihada ya Jamii ya Wafanyabiashara wa Chang'ombe Katika Ujenzi wa Soko. Kata ya Chang'ombe ni Kata yenye watu wengi zaidi Jijini na ilikuwa na masoko mengi yasiyo rasmi katika maeneo ya makazi. Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuanzisha soko la kisasa katika Kata likiwa na miundombinu ya kutosha ili kubeba masoko yote yasiyo rasmi. Kufikia lengo hili, Halmashauri iliendesha mikutano ya maamuzi, utwaaji wa ardhi katika eneo la Chang'ombe D, uundaji wa kamati ya kusimamia ujenzi, uhamasishaji na kukuza uelewa, uandaaji wa michoro ya soko na ujenzi wa miundombinu ya soko. Kwa sasa, Kata ya Chang'ombe ina soko jipya ambalo linadhihirisha modeli mpya ya jitihada za pamoja kati ya jamii na Serikali katika kutatua changamoto. Soko limeweza kubeba wafanyabiashara 700, vizimba 155 vya matunda na mboga na kuwezesha upatikanaji wa fursa za ajira na maisha bora. Halmashauri imejipanga kufanya ukarabati na uboreshaji wa soko wa mara kwa mara. Siri

ya mafanikio ya jitihada hii ni uongozi imara na thabiti wa Halmashauri, Mwenyekiti wa Mtaa wa Msamaria na Afisa Mtendaji wa Kata ya Chang'ombe.

Mbinu bora ya H/W ya Mpwapwa inaonesha Jitihada za Jamii Katika Kuanzisha Shule Shikizi ya Matuli. Kabla ya mwaka 2001, Kijiji cha Matuli kilikuwa na changamoto katika utoaji wa elimu ya msingi. Wanafunzi walilazimika kwenda Shule ya Msingi Manghaliza iliyopo takribani 5km kutoka Matuli. Ili kufikia lengo, Serikali ya Kijiji cha Matuli ilihamasisha wanakijiji, ilitwaa ardhi, iliunda kamati ya ujenzi, ilianzisha michango na hatimaye kujenga miundombinu ya shule. Kwa sasa, miundombinu ya shule ipo kwani jamii ikishirikiana na Halmashauri imejenga madarasa 6, vyoo 4 na nyumba ya walimu 1. Ili kuwepo na uendelevu, kuna uhamasishaji wa jamii endelevu ili kuhakikisha jamii inashiriki katika kuihudumia shule. Jitihada hii ilifanikiwa kwani ilikuwa ni hitaji halisi la jamii na hivyo kuwa na azma thabiti ya kukamilisha mradi.

# HAMLASHAURI YA WILAYA YA LUDEWA

**JITIHADA ZA JAMII KATIKA UJENZI WA MIUNDOMBINU YA MAJI SAFI NA SALAMA**





*Uzoefu wa Kijiji cha Itundu*

**1.0 UTANGULIZI**

H/W ya Ludewa ni moja kati ya Halmashauri za Mkoa wa Njombe inayopatikana kati ya Latitudo $9^0$30 na $10^0$30 Kusini na Longitudo $34^0$35 and $35^0$10 Mashariki. Halmashauri hii hupakana na H/W za Njombe, upande wa Kaskazini, Makete upande wa Kaskazini Magharibi, Songea upande wa Mashariki, Mbinga na Nyasa upande wa Kusini na Ziwa Nyasa upande wa Magharibi. H/W ya Ludewa ina eneo la 8,397$km^2$ kati ya hizo, 2,072$km^2$ ni eneo lenye maji na 6,325$km^2$ ni eneo la milima, misitu na mabonde. Eneo linalofaa kwa kilimo ni 4,650$km^2$ ambapo ni 3,444$km^2$ tu zinazolimwa. Kwa mujibu wa Sensa ya 2012, Halmashauri ina watu 133,218; wanaume (63,442) na wanawake (69,776) na ongezeko la watu la 0.8%. Halmashuri ina Tarafa 5, Kata 26, Vijiji 77 na Vitongoji 352 vyenye kaya 30,164.

Jamii kuu za wakazi ni Wapangwa, Wakisi na Wamanda. Wapangwa wanapatikana Kaskazini mwa Halmashauri na hujishughulisha na kilimo na ufugaji wakati Wamanda na Wakisi hupatikana katika fukwe za Ziwa Nyasa wakijishughulisha na uvuvi na ufugaji kama shughuli kuu za kiuchumi. Sehemu kubwa ya wakazi hutegemea mito midogo kama vyanzo vya maji ya matumizi ya nyumbani.

**2.0 TATIZO**

Maji ni rasilimali muhimu katika shughuli za maisha. Ukosefu wa maji huweza kudhoofisha ustawi wa watu kijamii na kiuchumi. Katika miaka ya 1980, DANIDA ikishirikiana na jamii ilijenga skimu ya maji kwa ajili ya Kijiji cha Itundu. Mradi huu wa DANIDA ulilenga kutoa huduma kwa wakazi 2,000 wa Kijiji cha Itundu. Kati ya mwaka 1990 na 2010 idadi ya watu iliongezeka hadi 4,471 na Kaya 1,135 ilihali mindombinu ya maji ikisalia vilevile. Matokeo yake ni kuwa, wananchi walianza kushuhudia ukosefu mkubwa wa maji.

Upungufu wa maji ulizaa matatizo mengine katika Kijiji cha Itundu. Wanakijiji walizazimika kutembea umbaliu mrefu wa hadi 5km kwenda kwenye vyanzo vya maji na kuwafanya wanawake kutumia masaa takribani 8 kwa siku kutafuta maji. Wanawake walilazimika kuamka mapema asubuhi (saa 10:00 alfajiri) kila siku; suala ambalo liliwazuia kushiriki shughuli za kiuchumi. Pamoja na hilo, matukio ya ugomvi katika kaya yalidhihirika kutokana na imani kuwa wanawake walitumia muda mwingi kutafuta maji kuliko ilivyohitajika. Ofisi ya Kijiji ilipokea malalamiko 6 ya ugomvi katika kaya yaliyoambatana na tatizo la ukosefu wa maji. Kwa upande mwingine, wanafunzi walitumia sehemu ya muda wa shule kutafuta maji hasa kabla ya kuanza vipindi. Baadhi ya kaya zilitumia gharama kubwa kutafuta maji kwa kutumia pikipiki (bodaboda) ambapo TZS 2,000 zilitumika kwa ndoo moja. Baadhi ya kaya zilitegemea maji kutoka katika mito na visima ambayo si salama na yaliongeza uwepo wa magonjwa yatokanayo na maji machafu kama homa ya matumbo na kipindupindu. Taarifa hii ilitolewa na Dk. Bosco Nyongeza, Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya cha Mlangali kilichopo kijijini Itundu.

**3.0 LENGO**

Upatikanaji wa maji safi na salama ni muhimu kwa ustawi wa binadamu na maendeleo kijamii na kiuchumi. Sera ya Taifa ya Maji ya 2002 inalenga katika kuhakikisha wanufaika wanashiriki kikamilifu katika hatua zote za uendelezaji wa rasilimali maji. Sera inatambua muungano muhimu na madhubuti kati ya maji na maendeleo kijamii na kiuchumi, pamoja na mahitaji ya mazingira. Msisitizo wa Sera ni kuwa kila kaya Tanzania ipate maji safi na salama ndani ya 1km msimu wa ukame. Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 imesisitiza upatikananaji wa maji safi na salama ndani ya 400m.

Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuongeza upatikanaji wa maji katika Kijiji cha Itundu. Mahsusi kabisa, jitihada ililenga;

(i) Kuanzisha vyanzo vipya vya maji na kujenga miundombinu ya mserereko ya maji.
(ii) Kuongeza upakikanaji wa maji kukidhi mahitaji ya watu kwa kujenga vituo vipya vya maji.

(iii) Kupunguza muda uliotumika kutafuta maji kutoka saa 6 hadi chini ya dakika 14.
(iv) Kupunguza umbali kutoka kaya hadi kituo cha maji kutoka 5km hadi 400m kama ilivyo katika Sera ya Taifa ya Maji.
(v) Kutokomzeza magonjwa yatokanayo na maji machafu.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Mwaka 2016 Halmashauri ya Kijiji ilibaini kuwa tatizo la upungufu wa maji kijijini litaongezeka na kudumu endapo hatua za haraka hazitachukuliwa. Mkutano wa Halmashauri ya Kijiji uliitishwa kujadili suala hili na kufanya maamuzi. Kupitia mkutano huu; ilikubalika kuwa tatizo lishirikishwe kwa wanakijiji wote. Mwenyekiti wa Kijiji aliitisha mkutano ili kuwepo kwa mjadala mpana, maamuzi na utekelezaji shirikishi. Kwenye mkutano wa Kijiji, wanajamii walibaini ukubwa wa tatizo na kuelewa kuwa endapo hawatachukua hatua mapema, tatizo la maji litadumu na kuwaathiri. Mkutano uliamua kuhusu chanzo cha maji na mbinu za kushirikisha wanajamii, ikiwa ni pamoja na wafanyabiashara na wazawa waishio nje ya Kijiji katika utekelezaji wa mradi. Ili kufikia malengo ya jitihada hii mbinu zifuatazo zilitumiwa.

Kukuza Uelewa; ili kukuza uelewa kuhusu tatizo na kuhamasisha wanakijiji wote, vipindi vya uhamasishaji viliandaliwa na kutekelezwa kupitia mikutano katika ngazi ya Kitongoji. Wenyeviti wa Vitongoji kwa kushirikiana na wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji walitoa elimu kwa wanajamii kuhusu umuhimu wa maji safi na salama katika kila Kitongoji Kijijini. Kijiji cha Itundu kina Vitongoji 5. Mikutano hii ya kujenga uelewa ililenga katika kuahamasisha jamii kutambua tatizo na kuamsha utayari wa kushiriki katika kulitatua. Wanakijiji walikubali kushirikiana na Halmashauri ya Kijiji katika mchakato wote wa utekelezaji wa maradi. Mihutasari ya mikutano hii iliandaliwa na kupelekwa kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya.

Kuanzisha Michango; Halmashauri ya Kijiji iliandaa Mkutano wa Kijiji ili kujadili mchakato wa shughuli za ujenzi wa miundombinu ya maji. Mkutano huu uliamua kila mwanakijiji achangie TZS 50,000 na wote ambao ni wastaafu, watumishi wa Serikali na wafanyabiashara wachangie TZS 80,000. Ili kuwatia hamasa wanakijiji kuchangia, wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na watu wote maarufu kijijini waliamua kuchangia kiasi chote siku hiyohiyo uamuzi ulipopitishwa. Mkutano huu pia, ulibariki azimio la kushirikisha wazawa waishio nje ya kijiji kuchangia shughuli za maendeleo zinazotekelezwa katika ardhi yao ya asili. Orodha ya wafanyabiashara na wazawa waishio nje ya kijiji iliandaliwa na mawasiliano kuhusu michango ya fedha na vifaa yalifanywa. Ili kuhakikisha walengwa wote wanachanga, kipindi cha miezi sita kilipitishwa kukamilisha michango kwa awamu. Kutokana na tatizo kuwa hitaji la jamii, kaya 719 kati ya 725 zilichangia ndani ya muda na kaya 6 zilizochelewa zilihimizwa kulipa.

Uundaji wa Kamati ya Maji; kamati ya wajumbe 10 ilianzishwa (2 kutoka kila Kitongoji). Kamati ilipatiwa majukumu yanayohusu ufuatiliaji wa michango, uainishaji wa gharama za mradi na uamuzi wa chanzo cha maji ambapo banio litasimikwa. Kamati hii ilipendekeza chanzo cha maji kiwe eneo la Salale katika milima ya Igongwi. Chanzo hiki kilipendekezwa kutona na uwezo wake katika kusaidia msererekо wa maji kuelekea Kijiji cha Itundu.

Ununuzi ya ardhi kwa ajili ya ujenzi wa banio katika Kijiji cha Msimbwe; kutokana na chanzo cha maji kuwa katika eneo la kijiji kingine (Msimbwe), Halmashauri ya Kijiji cha Itundu iliwasiliana na Halmashauri ya Kijiji cha Msimbwe ili kuanzisha ushirikiano wa namna ya kutumia vyanzo vya rasilimali maji kwa pamoja. Ilikubalika kuwa Halmashauri ya Kijiji cha Itundu inunue ardhi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu (banio) ya maji katika eneo la Salale kwenye milima ya Igongwi. Ardhi hii ilininuliwa kwa gharama ya TZS 1,000,000.

Ujenzi wa Banio; ujenzi wa banio ulifanywa na mafundi wenye uelewa na uzoefu wa ujenzi wa miundombinu ya maji. Katika hatua hii hakukuwa na usaidizi wa kitaalamu toka Halmashauri. Wananchi walijiongoza wenyewe katika shughuli za ujenzi kwa kukusanya vifaa vya ujenzi kama mawe, mchanga na kokoto. Vifaa vya viwandani kama saruji na nyaya zilinunuliwa na kamati ya mradi wa maji kutumia fedha zilizochangwa.



***Ujenzi wa Banio***

Ununuzi ya bomba za maji; Kamati ya Mradi wa Ujenzi ilitafiti bei na ubora wa bomba za maji katika mji wa Njombe na Jiji la Dar es Salaam. Iliamuliwa kuwa bomba zinunuliwe Dar es Salaam kutokana na bei kuwa nafuu ikilinganishwa na Njombe Mjini. Mfanyabiashara aitwaye Mendrad Chapemba anayemiliki malori alijitolea na kulipia usafirishaji wa bomba kutoka Dar es Salaam hadi kijijini Itundu. Hii inaonesha jinsi kila mdau alivyojitoa katika jijihada hii na kuthamini utekelezaji wa maradi kwa ajili ya Kijiji cha Itundu na vitongoji vyake.

Ujenzi wa bomba kuu na ukarabati wa vituo vya zamani; wanakijiji walijipanga katika ngazi za vitongoji na kushiriki katika kuchimba mfereji wa 9km kutoka chanzo cha maji hadi kijijini. Zoezi la kuchimba mfereji na kuweka bomba kutoka kwenye chanzo (9km) ulitekelezwa na wanakijiji kama ilivyokubalika katika mikutano ya kijiji na vitongoji. Wenyeviti wa vitongoji walipatiwa jukumu la kuongoza na kusimamia wakazi wa vitongoji ili washiriki kikamilifu katika shughuli za kuchimba mitaro na kulaza bomba. Utekelezaji wa mradi huu ulijumuisha ujenzi wa vituo vipya vya maji na ukarabati wa vituo vya zamani ambavyo vilijengwa enzi za mradi wa DANIDA.

Kuomba ufadhili wa Serikali; Halmashauri ya Kijiji iliamua kuandaa andiko la kitaalamu ili kuiomba Serikali kusaidia ukamilishaji wa mradi wa maji wa Itundu. Kwa bahati nzuri, katika kipindi hicho, kulikuwa na ziara ya Naibu Waziri wa Maji Mhandisi Kamwela ambayo ilitoa fursa kwa Kijiji kuwasilisha pendekezo na maombi ya ufadhili kwa Waziri. Waziri alielekeza Halmashauri ya Wilaya kutenga bajeti kusaidia jitihada ya Kijiji. Halmashauri ilitenga TZS 50,000,000 ili kusaidia mradi huu.

Kuomba kibali cha matumizi ya maji na cheti cha ubora; Halmashauri ya Kijiji iliomba kibali cha matumizi ya maji kutoka Mamlaka ya Bonde la Ziwa Nyasa ambapo Halmashauri ya Kijiji iliwasiliana na Mamlaka hii, ikaeleza uhitaji wa kutumia maji kutoka milima ya Igongwi na kupata kibali cha kutumia maji kwa mujibu wa sheria. Halmashauri ya Kijiji ilipata kibali hiki cha kutumia maji na hulipa TZS 100,000 kila mwaka ili kujihakikishia upatikanaji wa maji kisheria. Hatua nyingine muhimu ilikuwa kupima ubora wa maji. Hili lilihitaji mchakato wa kupima maji katika maabara ambapo kiasi kidogo cha maji kilipelekwa Maabara ya Taifa kwa ajili ya kupimwa ubora wake kwa matumizi ya binadamu. Mkemia Mkuu alitoa cheti cha ubora wa maji kwa ajili ya matumizi ya wanakijiji wa Itundu.

**5.0 RASILIMALI**

H/W ya Ludewa na wanakijiji wa Itundu walitumia rasilimali mbalimbali kuwezesha utekelezaji. Rasilimali watu ilitumika kwa namna mbalimbali ikijumuisha wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji ambao walianzisha na kuongoza jitihada, Mwenyekiti wa Kijiji Bw. Maiko Ang'ala ambaye alihamasisha jamii kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mradi na Bw. Athanas Mungi ambaye ni fundi kutoka Halmashauri aliandaa michoro na kuongoza ujenzi wa vituo vya maji. Mafundi wenyeji walishiriki katika ujenzi wa banio na vituo vya maji. Wanakijiji walileta na kutumia vifaa vya ujenzi kama mawe, mchanga na kokoto.

Rasilimali fedha zote zilizotumika katika kukamilisha mradi wa maji wa Itundu ni TZS 277,550,000/= na zilitoka kwa wadau mbalimbali kama inavyooneshwa katika jedwali 1 hapa chini.

**Jedwali 1: Rasilimali Fedha**

| SN | Shughuli | Kiasi (TZS) | Chanzo cha Fedha |
|---|---|---|---|
| 1 | Upimaji na michoro | 2, 384,800 | Jamii |
| 2 | Ununuzi wa bomba | 50,000,000/= | Jamii/Wizara ya maji |
| 3 | Ununuzi wa bomba | 165,000,000/= | Jamii |
| 4 | Ujenzi wa banio | 12,000,000/= | Jamii |
| 5 | Uchimbaji na ujenzi wa bomba kuu (9km) | 24,000,000/= | Jamii/Kujitolea |
| 6 | Wataalam na vibarua kwenye kutandaza bomba | 2,615,200/= | Jamii |
| 7 | Ukarabati wa vituo vya maji vya zamani | 2,000,000/= | Jamii |
| 8 | Usafiri wa vifaa | 9,000,000/= | Jamii |
| 9 | Ukusanyaji wa vifaa vya ujenzi | 11,000,000/= | Jamii |
| | **JUMLA** | **277,550,000/=** | |

**6.0 MATOKEO**

H/W ya Ludewa na Jamii ya Kijiji cha Itundu ililenga katika kuboresha upatikanaji wa maji safi na salama ya kutosha katika Kijiji na vitongoji vyake, kuboresha usafi wa mazingira katika jamii na kupata maji ya kutosha kwa matumizi ya nyumbani. Upatikanaji wa maji safi karibu na makazi huongeza muda wa kufanya kazi za uzalishaji suala ambalo linachangia katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Maboresho katika huduma za maji, usafi na mbinu za kiafya hupunguza magonjwa yatokanayo na maji machafu na hivyo kuimarisha uzalishaji wa mtu mmoja mmoja kwa kujikita zaidi katika shughuli za kiuchumi. Upatikanaji wa maji ya kutosha yenye ubora hupunguza muda uanaotumika kutafuta maji, huboresha afya na huleta uhakika wa mazingira bora kwa wanafunzi kuhudhuria shule. H/W ya Ludewa na Jamii ya Kijiji cha Itundu ilifanikiwa kupata matokeo mengi kutokana na utekelezaji wa mradi huu. Matokeo haya yameelezwa kwa kina hapa chini.

Miundombinu ya maji iliyokamilika na kufanya kazi; Kijiji kina miundombinu ya maji inayojumuisha banio na vituo 127 vya maji vilivyopo katika maeneo muhimu ya Kijiji na katika vitongoji. Pamoja na hilo, taasisi zote za huduma kama Kituo cha Afya na shule za msingi zina vituo vya maji ambavyo hutoa maji yanayohitajika kwa watu na usafi kwa wakati.



***Banio katika milima ya Igongwi***

Huduma za maji zilizoimarika; kama ilivyosisitizwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kuhusu upatikanaji wa maji safi na salama kwa wote ndani ya 400m, wakazi wa Kijiji cha Itundu sasa wanapata maji ndani ya 400m ikilinganishwa na enzi kabla ya utekelezaji wa mradi huu muhimu. Mradi huu umeokoa muda mwingi kwani wanakijiji wanatumia dakika 15 tu kufika kwenye vituo vya maji ilikilinganishwa na saa 6 hapo awali.

Kuinua wanawake kiuchumi; kama tokeo la mradi huu wanawake wamepata muda wa kutosha kujikita katika shughuli za kiuchumi jambo ambalo limeboresha vipato na hadhi zao. Jitihada ya maji imeondoa matukio yote ya migogoro katika familia iliyotokana na tatizo la maji.

Matokeo mengine ni pamoja na;

(i) Kuongezeka kwa upatikanaji wa maji katika kaya ambapo vituo 127 vimejengwa (76 katika nyumba binafsi na 51 katika maeneo ya umma).

(ii) Kutokomezwa kwa magonjwa yatokanayo na maji machafu. Hili ni tokeo la upatikanaji wa maji bora yaliyoidhinishwa na Mkemia Mkuu.

(iii) Kuongezeka kwa shughuli mpya za kipato kama uoshaji wa magari na kilimo cha mbogamboga.



***Kituo cha Maji***

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Kwa kusaidiwa na Idara ya Maji ya H/W ya Ludewa, Kijiji cha Itundu kimeanzisha Kamati madhubuti ya maji inayohakikisha kuwa kila kaya inayochota maji katika vituo vya maji hulipa TZS 4,000/= kwa mwaka na kaya ambazo zimeunganishwa na huduma ya maji hulipa TZS 4,000/= kwa mwezi. Kijiji kimeshakusanya TZS 500,000/= kama malipo ya ankara za maji na makusanyo haya hutumika kulipa mafundi na kununua bomba na vifaa vingine vya matengenezo na upanuzi wa mradi. Kamati hii inaendelea kuhamasisha wakazi kuunganisha maji katika nyumba zao ili kuongeza mapato. Gharama za uunganishaji mpya ni TZS 15,000 kama ada na TZS 4,000 za ankara ya maji kwa mwezi. Wakazi

wanaohitaji kuunganishiwa maji hununua bomba na vifaa. Mikakati hii imelenga katika kufanya mradi kuwa endelevu na kupanuka siku zijazo.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Mafanikio ya Kijiji cha Itundu yamejikita katika uwazi na uongozi imara wa kamati ya maji ya Kijiji. Wakati wa utekelezaji, kamati ilitoa taarifa za mapato na matumizi kwa jamii ili kuonesha waziwazi makusanyo na matumizi. Siri nyingine ni umoja wa wanakijiji na kujitoa kwa dhati kwa ajili ya mradi, uhamasishaji wa jamii kuhusu umuhimu wa mradi uliofanywa na viongozi wa Kijiji na uwepo wa vyanzo vya maji karibu na Kijiji. Mradi huu ulifanikiwa sana kwani ulikuwa hitaji muhimu la jamii ya Kijiji cha Itundu.

# HALMASHAURI YA MJI WA MBULU

**JITIHADA ZA JAMII YA KATA YA NAMBIS KATIKA UJENZI WA SHULE YA SEKONDARI YA HHAYNU**




***Uzoefu wa Kata ya Nambis***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Mji wa Mbulu ni moja ya Halmashauri 7 za Mkoa wa Manyara iliyoanzishwa tarehe 25 Septemba 2015. Mji huu unapatikana Kaskazini Mashariki mwa Tanzania ukipakana na H/W ya Karatu upande wa Kaskazini, H/W ya Babati upande wa Kusini na H/W ya Mbulu upande wa Magharibi. Halmashauri ina eneo la 1891km$^2$ na idadi ya watu 146,527 ambao kati yao 74,112 ni wanaume na 72,415 ni wanawake ikiwa na ongezeko la watu la 3.8%. Halmashauri ina Tarafa 3, Kata 17, Vijiji 34, Vitongoji 153 na Mitaa 58.

H/Mji wa Mbulu hutegemea zaidi uchumi wa kilimo. Takribani 85% ya wakazi wamejikita katika kilimo na ufugaji. Nje ya shughuli za kilimo na ufugaji wakazi hawa hujishughulisha na ufugaji nyuki, uvuvi, biashara na uendeshaji wa viwanda vidogo.

H/Mji wa Mbulu ina shule za msingi 57 (54 za Serikali na 3 za binafsi). Shule hizi za msingi ndio chanzo cha wanafunzi wanaotakiwa kuandikishwa katika shule 14 za sekondari ikiwa ni pamoja na Hhaynu. Kabla ya mwaka 2018 kulikuwa na shule za sekondari 13 zilizotakiwa kuchukua wanafunzi kutoka shule zote 54 za msingi. Kwa sasa Halmashauri in shule za msingi 54 na 14 za sekondari.

**2.0 TATIZO**

Kabla ya mwaka 2018, wanafunzi kutoka Kata ya Nambis walikuwa wakiandikishwa katika Shule ya Sekondari ya Murray iliyopo Kata ya Murray. Maelekezo ya kitaifa ni kuwa kila Kata inatakiwa kuwa na shule yake ya sekondari. Hali ya Kata mbili kuwa na shule moja ya sekondari lilileta matatizo kadhaa.

(i) Wanafunzi 200 kutoka Kata ya Nambis walioandikishwa katika Shule ya Sekondari ya Murray tangu 1997 hadi 2018 walilazimika kutembea umbali mrefu wa hadi 8km kila siku kwenda shule.

(ii) Uhalisia wa kijiografia na asili ya sura ya nchi vililazimu wanafunzi kubaki majumbani msimu wa mvua. Zaidi ya wanafunzi 35 waliathiriwa na mafuriko ya msimu kutokana na kukosekana kwa madaraja katika baadhi ya mito na vijito.

(iii) Msongamano wa wanafunzi katika Shule ya Sekondari ya Murray uliotokana na ufaulu wa juu (100%) katika shule zote 4 za eneo husika. Wahitimu wote wa darasa la 7 walichaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari ya Murray; matokeo yake uwiano wa darasa 1:40 haukuzingatiwa. Ililazimu darasa moja kuchukua wanafunzi kati ya 80-100 jambo ambalo liliathiri mazingira ya kujifunza na ufundishaji na kusababisha utendaji duni kitaaluma.



***Miundombinu ya Shule ya Sekondari ya Murray***

**3.0 LENGO**

Elimu ya sekondari nchini Tanzania imeandaliwa kipekee ili kuunganisha na kupanua wigo wa fikra, elimu, stadi na kanuni zinazotolewa na kuendelezwa katika elimu ya msingi. Elimu ya sekondari inapendekezwa na serikali ili kuendeleza na kuuenzi umoja wa kitaifa, kutambulika na maadili,

kujiheshimu, kuheshimu na kuwa tayari kufanya kazi, haki za binadamu, sifa za kiutamaduni na maadili, mila, desturi, majukumu na wajibu wa kijamii.

Elimu ya Sekondari huchochea kuimarika kwa uwezo wa lugha na matumizi sahihi ya stadi za mawasiliano katika Kiswahili na walau lugha nyingine moja ya kigeni, hutoa fursa ya kupata elimu, stadi, mitizamo na uelewa katika fani mojawapo inayopendekezwa. Elimu ya Sekondari humwandaa mwanafunzi kwa ajili ya elimu ya juu, ufundi na utaalamu na huingiza hisia na uwezo wa kujisomea, kujiamini na kujiendeleza katika maeneo ya sayansi na teknolojia, taaluma na ujuzi, na stadi na humwandaa mwanafunzi kujiunga na ulimwengu wa kazi. Katika mazingira haya, yeyote ambaye hupoteza nafasi hii pekee ya kupata elimu ya sekondari ambayo inafadhiliwa zaidi na Serikali, hujiondolea fursa nyingi za maendeleo binafsi. Kwa sababu hizi jamii ya Nambis iliamua kuhakikisha kuwa vijana wao wanapata elimu bora karibu na vijiji vyao.

Mwishoni mwa mwaka 2012, jamii ya Nambis ilifanya uamuzi thabiti wa kujenga shule yao ya sekondari. Jitihada hii ililenga kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunza kwa kujenga Shule ya Sekondari ya Hhaynu. Malengo mahsusi ya jitihada hii yalikuwa;

(i) Kupunguza msongamano wa wanafunzi katika Shule ya Sekondari ya Murray kutoka 100 hadi 40 kwa chumba cha darasa ifikapo 2018.
(ii) Kuongeza uandikishaji wa wanafunzi katika Shule ya Sekondari ya Hhaynu hadi kufikia uwezo wa 100%.
(iii) Kupunguza umbali wa kutembea kila siku kwenda shule kutoka 8km hadi 4km.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Kufanya maamuzi; mwaka 2012 wazo kutoka jamii ya Nambis la kujenga shule yao ya sekondari lilijadiliwa katika kamati anzilishi ya Halmashauri ambapo mjadala ulijikita katika kutenga eneo linalofaa kwa ajili ya shule. Halmashauri ilipendekeza kuwa vijiji viwili katika Kata ya Nambis vijenge shule yao ya sekondari. Suala hili lilianzishwa na H/W ya Mbulu kwani kwa kipindi hicho H/Mji wa Mbulu ilikuwa bado haijaanzishwa. Vijiji viwili ambavyo viliathirika sana kwa wanafunzi kutembea hadi 8km kwenda Shule ya Sekondari ya Murray vilikuwa Kwermusl na Amowa. Pendekezo hili lilijadiliwa kwa pamoja katika mkutano uliohusisha wenyeviti na wajumbe wa Halmashauri za vijiji vya Amowa and Kwermusl ambapo iliamuliwa kuwa pendekezo lipelekwe kama ajenda katika mikutano ya wanakijiji katika vijiji husika.

Kupitishwa na kuundwa kwa kamati ya utekelezaji; mikutano ya Halmashauri za Vijiji ilijadili na kukubaliana kujenga shule mpya katika eneo lao. Kufikia lengo hili, kamati ya ujenzi wa shule ilianzishwa ikiwa na wajumbe 14 kutoka Kijiji cha Kwermusl na 13 kutoka Kijiji cha Amowa. Kati ya wajumbe wa kamati hii ni wastaafu wenye ujuzi na uzoefu katika uundaji na utekelezaji wa mipango. Kamati ilipewa shughuli za kuainisha gharama za ujenzi wa shule ya sekondari, kutambua eneo linalofaa kujenga shule, kumiliki ardhi na kuhamasisha jamii kuhusu michango.



***Makamu Mwenyekiti wa Kamati na baadhi ya wajumbe***

Upatikanji wa ardhi; kamati ya ujenzi ilifanya majadiliano na wamiliki wa ardhi wenyeji na kukubaliana kubadilishana ardhi. Hivyo, shule imejengwa kwenye ardhi iliyopatikana kwa kubadilishana ardhi ambayo kabla ilimilikiwa na familia kadhaa ambazo zilifidiwa kwa ardhi ya kijiji iliyokuwepo katika eneo la Dawi ndani ya Kijiji cha Kwermusl. Utaratibu huu ulikuwa wa lazima kwani eneo la wamiliki hawa wenyeji lilikuwa linafaa zaidi kwa ujenzi wa shule kutokana na mahali lilipo na tambarare.

Uhamasishaji wa Jamii; jamii ilihamasishwa kupitia mikutano na majadiliano. Wanavijiji wa Amowa na Kwermusl kwa pamoja waliiitisha mkutano na kujadili mbinu na mikakati ya kuchangia kufikia lengo kwa mujibu wa mpangokazi wa utekelezaji wa mradi ulioandaliwa na kamati. Sambamba na hili, watu maarufu kama Mbunge na Mkurugenzi wa Halmashauri walialikwa katika mkutano wa vijiji wa pamoja ili kuhamasisha jamii kwa ujumla.

Maombi ya michoro na miongozo; Septemba mwaka 2014, vijiji vya Amowa and Kwermusl vilialika maofisa wa Halmashauri kutoa vipimo vinavyofaa kwa ujenzi wa shule kwa mujibu wa Miongozo ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Maofisa walioalikwa ni pamoja na Afisa Elimu wa Wilaya kwa ajili ya maelekezo ya ramani na michoro ya kisera na Mhandisi wa Wilaya ambaye anahusika na uandaaji wa msingi wa majengo, kukagua vipimo kwenye kiwanja cha jengo kwa mujibu wa michoro na vipimo, kuchimba msingi na kutoa ratiba ya usimamizi na ufuatiliaji. Mwenyekiti na Mkurugenzi wa Halmashauri pia walialikwa kwenye eneo la ujenzi ili kuongoza jitihada hii.

Michango ya fedha taslimu na awamu za ujenzi; iliamuliwa kuwa kila kaya ichangie TZS 382,000 kwa awamu 5. Katika awamu ya kwanza (2014-2015) kila kaya ilitoa TZS 150,000 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa, vyoo na nyumba za walimu, awamu ya pili TZS 32,000 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 3 vya maabara, awamu ya tatu TZS 60,000 kwa ajili ya jengo la utawala, awamu ya nne TZS 40,000 ili kukamilisha nyumba 2 za walimu na awamu ya tano TZS 100,000 ili kujenga madarasa 2 na nyumba za walimu 3.

Ushiriki wa jamii; jamii ilishiriki katika kutengeneza matofali na kukusanya mawe, kokoto na mchanga uliandaliwa kwa namna ambayo kila kaya ilitakiwa kutengeneza matofali 300 katika eneo la ujenzi. Ukusanyaji wa vifaa vingine vya ujenzi vinavyopatikana katika maeneo ya wenyeji ulifanywa na wananchi katika vitongoji vyao na kusafirishwa kwenda eneo la ujenzi. Mbinu hizi zilipunguza matumizi ya fedha taslimu kununua vifaa vinavyopatikana katika jamii.

Kuanzishwa kwa sheria ndogo; mkutano wa pamoja wa vijiji ulitunga sheria iliyotumika kudhibiti wakwepaji wa kuchangia shughuli za maendeleo. Kwa bahati nzuri sheria hii haikutumika kwani wanajamii wote walihamasika kwa kiasi kuwa hapakuwa na wakwepaji. Hii inaonesha kuwa suala la ujenzi wa shule lilikuwa hitaji halisi la jamii.

Kupanga awamu za utekelezaji; awamu ya kwanza (2014-2015) ilihusu ujenzi wa madarasa, vyoo na nyumba za walimu. Awamu ya pili (2014-2015) ilihusu ujenzi wa vyumba vya maabara 3 (hadi hatua ya lenta), awamu ya tatu ujenzi wa jengo la utawala hadi kukamilika (2017), awamu ya nne ukamilishaji wa nyumba za walimu 2 (2017-2018), kupaua nyumba ya walimu 1 (2019) na kupaua maabara 3 (2018). Awamu ya tano ilihusu ujenzi wa madarasa 2 hadi kukamilika (2018-2019), ujenzi wa nyumba za walimu 2 hadi kukamilika (2018-2019) na ujenzi wa nyumba ya walimu 1 hadi kwenye lenta. Majengo yote ya shule yanajengwa kwa mujibu wa viwango na vipimo kama inavyoelekezwa na Wizara ya Elimu. Michoro yote na makadirio ya gharama yaliandaliwa na Mhandisi wa Halmashauri.

Kuendesha harambee; mwaka 2015 baada ya kuanza kwa H/Mji wa Mbulu, jukumu la kusimamia na kufuatilia mradi lilihamia kwa menejimenti ya Mji kwa kushirikiana na kamati ya ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Hhyanu. Mkurugenzi wa Mji aliandaa tukio la Harambee ili kukusanya fedha za kupaua maabara 3. Jumla ya TZS 5,000,000 zilikusanywa.

Kutafuta michango kutoka kwa wadau mbalimbali; kamati ya ujenzi wa shule iliwaomba wadau kuchangia ili kusaidia jitihada ya wazazi. Wadau wengi walikubali ombi hili. Mbunge wa Jimbo la Mbulu Mjini alichangia mabati 100 kwa ajili ya kupaua nyumba za walimu, na rafiki mmoja wa H/Mji wa Mbulu Mama Teun Van Daig alichangia TZS 2,400,000 ili kutengeneza madawati na viti 40 na TZS 4,800,000 ili kununua vitabu.

Usajili wa Shule; mwaka 2017 Halmashauri ilianza mchakato wa kusajili Shule ya Sekondai ya Hhyanu. Tarehe 17 Decemba 2017 shule ilisajiliwa. Mara baada ya usajili Halmashauri ilipeleka walimu 4 kuanza kuendesha shule na wanafunzi 93 wa kidato cha kwanza waliandikishwa Januari 2018.

## 5.0 RASILIMALI

Kwa kushirikiana na H/Mji wa Mbulu na wadau, jamii za vijiji vya Amowa na Kwermusl zilitumia rasilimali fedha na watu kama inavyofafanuliwa katika jedwali 1 hapa chini.

**Jedwali 1: Rasilimali**

| Na | Chanzo | Kiasi | Asilimia |
|---|---|---|---|
| 1. | Jamii (fedha) | 256,300,000.00 | 61.9 |
| 2. | Nguvukazi | 101,190,000.00 | 24.4 |
| 3. | Jamii (miti na mbao toka kaya) | 56,000,000.00 | 13.5 |
| | **Jumla** | **413,490,000.00** | **100** |

## 6.0 MATOKEO

Mwaka 2012 Jamii ya Kata ya Nambis ilifanya uamuzi thabiti wa kujenga shule yao ya sekondari ili kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunza kwa kuanzisha Shule ya Sekondari ya Hhyanu. Septemba mwaka 2014 ujenzi wa majengo ya shule ulianza. Hapa chini yameelezwa matokeo yaliyokuwepo Februari 2019.

Uwepo wa miundombinu ya shule; hadi mwisho wa mwaka 2017 wanavijiji wa Amowa na Kwermusl walikuwa wamekamilisha madarasa 4, jengo la utawala, nyumba za walimu 2, vyoo vya wasichana na wavulana 20 na choo cha watumishi. Maabara 3 na nyumba ya walimu 1 zilikuwa kwenye hatua mbalimbali za ukamilishaji.



*Madarasa 4 yaliyokamilika*



***Choo cha Wavulana (matundu 10)***



***Choo cha Wasichana (matundu 10)***

Shule ya Seondari ya Hhaynu inayojiendesha; shule imesajiliwa kwa Namba 5008 na inajiendesha ikiwa na wanafunzi 85 wa kidato cha kwanza, walimu 9 na watumishi wasaidizi 4.

Kuboreshwa kwa mazingira ya kujifunza na kufundisha; ujenzi wa shule ya sekondari ya Hhyanu umeleta maboresho mengi; wanafunzi wamepata shule karibu na makazi yao, umbali wa kutembea kutoka nyumbani kwenda Shule ya Sekondari ya Murray na kurudi umepungua kutoka 8km hadi chini ya 4km, msongamano uliokuwepo katika Shule ya Sekondari ya Murray umepungua kutoka 100 hadi 40 na utoro umepungua sana. Shule ina jengo la utawala na nyumba za walimu kwa ajili ya Mkuu wa Shule na walimu wengine wawili. Majengo haya ni muhimu sana kwani yanaweka mazingira sahihi ya kazi na kuongeza ari na motisha wa walimu kufanya kazi kwa bidii na kutoa muda wao mwingi kusaidia wanafunzi ili kuwapatia elimu bora na stadi stahiki za maisha.



***Jengo la Utawala***



***Nyumba za Walimu***

Kuongezeka kwa uandikishaji; ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Hhaynu umeongeza wigo wa Halmashauri kuongeza uandikishaji wa wanafunzi kutoka vijiji vya Kwermusl, Amowa, Hhayloto na Gwaami. Inatarajiwa kuwa uandikishaji utaongezeka hadi kufikia wanafunzi 200 ifikapo mwisho wa mwaka 2019.

Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Hhaynu imekuwa mfano wa kuigwa; Kata ya Nambis ina Vijiji 4 vya Kwermusl, Amowa, Hhayloto na Gwaami. Ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Hhaynu kwa kutumia mbinu za ushiriki wa jamii na kujitegemea umechochea vijiji vya Hhayloto na Gwaami kujenga shule ya sekondari (Nambis) karibu na vijiji vyao, hivyo ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Nambis upo katika hatua za mwisho.

Jamii yenye motisha na umoja; jamii za Kata ya Nambis (vijiji viwili vya Amowa na Kwermusl) zimeunganika na zinahamasishana. Ushiriki katika ujenzi, mikutano ya mara kwa mara na shughuli za kamati ya ujenzi vimeleta hali ya umoja na imani kuwa "tunaweza".

## 7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

H/Mji wa Mbulu na jamii ya Nambis wamedhamiria kuendelea na jitihada hii hadi shule itakapokuwa na uwezo kamili wa kuchukua na kubeba wanafunzi wa kidato cha I-IV. Hivyo, vijiji vya Amowa na

Kwermusl vimejipanga kuendelea na michango ya fedha taslimu kwa kaya na kushiriki moja kwa moja katika ujenzi hadi mradi utakapokamilika.

Ujenzi unaendelea; ujenzi wa madarasa 2, nyumba za watumishi 2 na maabara za sayansi 3 (Kemia, Baolojia na Fizikia) zipo katika hatua ya kupaua na zitakamilika mwishoni mwa 2019.



***Madarasa 4 (hayajakamilika)***



***Maabara 3 (hazijakamilika)***

Kwa sababu za uendelevu, jamii ina mpango wa kupanda miti ili kuifanya shule kuwa ya kijani na inayopendeza. Baada ya miaka kadhaa miti itakuwa chanzo cha mapato yatakayotumika kwa ukarabati na maboresho ya miundombinu ya shule.

Vijiji vya Amowa na Kwermusl vimeazimia kuifanya shule hii moja ya shule bora katika kutoa elimu bora, mazingira bora ya kujifunza na inayoongoza katika ufaulu. Wanavijiji hawa wamepanga kujenga mabweni kwa ajili ya wavulana na wasichana, maktaba, ukumbi, vyumba vya kompyuta na nyumba za kutosha za walimu. Sambamba na hayo, jamii ya Amowa na Kwermusl inaendelea kutafuta wadau ambao watachochea mchakato wa kukamilika kwa uwepo wa shule ya sekondari ya kawaida na ya juu.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Uamuzi wa Jamii ya Kata ya Nambis kujenga shule ya sekondari ulilenga katika kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunza kwa kuanzisha Shule ya Sekondari ya Hhyanu. Moja ya sababu za msingi za kufanikiwa kwa mradi huu ni uwazi na uwajibikaji. Taarifa za maendeleo ya ujenzi wa shule ziliandaliwa na kuwasilishwa katika mkutano wakijiji kila miezi mitatu ya utekelezaji kwa ajili ya majadiliano na maamuzi ya awamu zifuatazo.

Kila mwanajamii wa Amowa na Kwermusl alikuwa tayari kwa mabadiliko na uchangiaji wa hiari. Vilevile, jamii ya kabila moja imekuwa ya msukumo mkuu wa mafanikio. Utamaduni wa ushirikiano ambao upo katika kabila la Wairaq umechangia sana katika kufikia lengo hili. Mwisho, ingawa si kwa umuhimu, uwepo wa misitu, mawe na mchanga umesaidia ukamilishaji wa mradi. Sababu nyingine ni uendeshaji wa harambee, utafutaji wa wadau na uwepo wa kamati imara ya utekelezaji wa mradi.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MSALALA

**JITIHADA ZA JAMII KATIKA UANZISHAJI WA SHULE YA SEKONDARI YA SEGESE**




***Uzoefu wa H/W ya Msalala***

**1. 0 UTANGULIZI**

H/W ya Msalala ni mojawapo ya Halmashauri 6 za Mkoa wa Shinyanga. Halmashauri hii ilianzishwa Julai 2013. Halmashauri ina eneo la 2,635.52km$^2$ ambazo ni sawa na 5.2% ya eneo lote la Mkoa wa Shinyanga na inapatikana kati ya Latitudo 3$^0$ 13’’ na 4$^0$ 12’’ Kusini na Longitudo 32$^0$ 13’’ na 33$^0$ Mashariki. Halmashauri ina Tarafa 2 (Msalala and Isegehe), Kata 18, Vijiji 92 na Vitongoji 389. Kwa mujibu wa sensa ya 2012, Halmashauri ina watu 331,852, kati yao 159,289 ni wanaume na 172,563 ni wanawake ikiwa na ongezeko la watu la 3.7% kwa mwaka. Idadi ya watu kwa km$^2$ ni 95. Ongezeko kubwa la watu linatokana na sababu kama uhamiaji utokanao na shughuli za uchimbaji mdogo wa madini na uwiano wa juu wa uzazi. Makabila makuu ni Wasukuma, Wasumbwa na Wanyamwezi. Makabila mengine ni Waha, Wahangaza na Wadakama.

Halmashauri ina eneo kubwa ambalo ni tambarare (80%), mabonde (13%) na milima midogo (7%). Msimu wa mvua unatenganishwa na kipindi cha wiki mbili hadi mwezi mmoja cha ukame, hasa kati ya Januari na Februari. Wastani wa mvua ni kati ya 750mm - 1030mm kwa mwaka. Hali ya joto si ya kubadilika kwa kipindi chote cha mwaka na huwa kati ya 21$^0$C - 26$^0$C. Kwa ujumla Halmashauri hupatikana katika uwanda uliopo kati ya 345m na 958m juu ya usawa wa bahari ambapo miinuko ya Chella ndiyo sehemu ya juu zaidi.

Uchumi wa H/W ya Msalala hutegemea zaidi kilimo, ufugaji, uchimbaji wa madini na biashara ndogondogo. Takribani 85% ya wananchi hutegemea kilimo na ufugaji kama shughuli kuu. Eneo linalofaa kwa kilimo (482,320ha) hutumika kwa uzalishaji wa mazao na malisho. Mashamba huwa na ukubwa tofauti wa kati 0.4 - 20ha kwa kaya. Mazao makuu ni pamoja na mahindi, mpunga, karanga, kunde na pamba. Halmashauri hii ndio mzalishaji mkubwa katika kanda ya ziwa wa mpunga ambapo 40% ya mpunga huzalishwa. Uchimbaji wa madini (mdogo na mkubwa) ni shughuli nyingine kuu ya kiuchumi.

H/W ya Msalala ina shule za msingi 43, shule za sekondari 15. Kata ya Segese ina shule za msingi 5 na shule za sekondari 2 zikiwa na madarasa 16. Idara ya Elimu ya sekondari ina jukumu la kuhakikisha elimu bora ya sekondari inatolewa kwa wanafunzi na kusimamia Elimu Shirikishi Baada ya Elimu ya Msingi kupitia uwezeshi na ufuatiliaji wa maelekezo na sera za kitaifa.

**2.0 TATIZO**

Ili kupata elimu ya sekondari iliyo bora, mazingira ya kufundisha na kujifunza lazima yawe sahihi na rafiki kuruhusu wanafunzi kushiriki kikamilifu katika mchakato wa kujifunza. Madarasa yenye msongamano, ukosefu wa madawati na vifaa vya kufundishia husababisha ufundishaji duni, utoro na ufaulu duni kwenye mitihani. Mwaka 2013 Kata ya Segese ilikuwa na shule moja tu ya sekondari iitwayo Shule ya Sekondari ya Mwalimu Nyerere. Shule hii ilikuwa na msongamano wa wanafunzi kutokana na idadi kubwa ya wanafunzi walioandikishwa kutoka shule za msingi mbalimbali katika Kata ya Segese na Kata ya Mega ambayo haikuwa na shule ya sekondari. Wanafunzi walioandikishwa ni 8,305 zaidi ya uwezo wa shule ambao ni wanafunzi 5,000.

Licha ya ongezeko kubwa la kuandikishwa wanafunzi, miundombinu ya shule ilikuwa haitoshi; madarasa yalikuwa na msongamano mkubwa uliosababisha ufundishaji kuwa duni. Uwiano wa wanafunzi kwa darasa ulikuwa 80:1, uwiano wa wanafunzi kwa tundu la choo ulikuwa 60:1 kwa wavulana na 50:1 kwa wasichana kinyume na uwiano wa matundu wa 25:1 kwa wavulana na 20:1 kwa wasichana kwa mujibu wa sera. Changamoto nyingine zilizoikumba Shule ya Sekondari ya Mwalimu Nyerere zilikuwa upungufu

wa samani (madawati na meza), bajeti finyu na ucheleweshaji wa fedha toka Serikalini ambao uliathiri utekelezaji wa shughuli. Masuala mengine yalikuwa upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi, na uelewa mdogo wa jamii kuhusu umuhimu wa elimu ambao ulisababisha uotaji duni wa michango kwa ajili ya miradi ya elimu. Changamoto hizi ziliongeza utoro na mahudhurio duni.



***Darasa lenye Msongamano katika Shule ya Sekondari ya Mwl Nyerere***

**2.0 LENGO**

Elimu ya sekondari nchini Tanzania imeandaliwa kipekee ili kuunganisha na kupanua wigo wa fikra, elimu, stadi na kanuni zinazotolewa na kuendelezwa katika elimu ya msingi. Elimu ya sekondari inapendekezwa na serikali ili kuendeleza na kuuenzi umoja wa kitaifa, kutambulika na maadili, kujiheshimu, kuheshimu na kuwa tayari kufanya kazi, haki za binadamu, sifa za kiutamaduni na maadili, mila, desturi, majukumu na wajibu wa kijamii. Kwa msingi huu, Jamii ya Segese ikishirikiana na H/W ya Msalala ililenga katika kuongeza ubora wa elimu kwa kuanzisha shule mpya ya sekondari ili kutoa nafasi zaidi kwa wanafunzi kupata elimu bora. Jamii na Halmashauri kwa ujumla zilidhamiria kuwepo kwa mazingira sahihi ya kufundisha na kujifunza kwa kujenga miundombinu kama madarasa, vyoo, maabara za masomo ya sayansi na kuinua ari ya jamii kushiriki katika kusukuma maendeleo ya elimu.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Wazo la kujenga shule ya sekondari lilianza mwaka 2013. Diwani wa Kata ya Segese Mhe. Joseph Manyara alitoa wazo hili kwenye kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kata. Wazo hili lilijadiliwa na maamuzi yaliwasilishwa Halmashauri kwa hatua zaidi. Katika ngazi ya Halmashauri ilikubalika kuwa jamii ijenge maboma ya majengo ya shule hadi hatua ya lenta na Halmashauri itasaidia kupaua na hatua za mwisho za ujenzi. Kuweza kufikia lengo hili, mbinu mbalimbali zilitumiwa kama ambavyo zimejadiliwa hapa chini.

Uhamasishaji na kukuza uelewa; uhamasishaji na ukuzaji wa uelewa kwa wanajamii ulikuwa muhimu ili kuwa na uelewa wa pamoja. Shughuli hii ilifanywa na Diwani, Mratibu wa Elimu Kata na wajumbe wa Halmashauri za Vijiji katika Mikutano ya Vijiji na Vitongoji. Katika mikutano ya vijiji wazo na pendekezo la kuanzisha Shule ya Sekondari ya Segese lilijadiliwa na kukubaliwa na wanavijiji. Maamuzi yaliyofikiwa yalijumuisha upatikanaji wa ardhi, uundaji wa kamati ya ujenzi na ukusanyaji wa rasilimali kupitia michango.

Uundaji wa kamati ya ujenzi; kamati ya wajumbe 10 iliundwa ili kuratibu shughuli zote za uanzishaji wa Shule ya Sekondari ya Segese. Wajumbe wa kamati hii waliteuliwa kutoka vijiji vyote 5 vya Kata ya Segese. Kamati ilipewa majukumu ya kuandaa rasimu ya bajeti, kuainisha idadi ya kaya, kuainisha kiasi na kukusanya michango ya fedha taslimu kutoka kwa wadau na kusimamia kazi za ujenzi. Bajeti

iliyopendekezwa ilikuwa TZS 45,448,000 na idadi ya kaya ilikuwa 3,666. Hata hivyo ni kaya 2,511 tu zilizobainika kuwa na uwezo wa kuchangia jitihada hii.

Ukusanyaji wa rasilimali; Diwani alihamasisha wanajamii kuchangia kwa fedha taslimu na kwa nguvukazi. Wanajamii wengi walikubaliana na mapendekezo ya Diwani na kupendekeza kiasi ambacho kila kaya itachangia. Kuliwekwa makundi matatu ya uchangiaji; wadau wenye hali nzuri kiuchumi walichangia TZS 200,000 kila mmoja, hawa ni wafanyabiashara wakubwa. Wakazi wenye maduka madogo katika maeneo ya kati ya vijiji waliombwa kuchangia TZS 50,000 kila mmoja na wanavijiji wengine waliombwa kuchangia TZS 8,000 kwa kila kaya. Hivyo, wafanyabiashara maarufu walichangia TZS 8,688,000, wamiliki wa maduka madogo TZS 3,000,000 na wanajamii TZS 14,151,000. Sambamba na uchangiaji wa fedha taslimu, wanajamii walichangia mchanga tani 532, mawe, mifuko ya saruji 279 na mabati 30.

Ununuzi wa ardhi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule; ardhi yenye ukubwa wa 5ha ilinunuliwa kwa bei ya TZS 3,800,000 kutokana na michango ya wanajamii. Awali, ardhi hii ilimilikiwa na mwanakijiji wa Kijiji cha Busungo ndani ya Kata ya Segese. Baada ya kupatikana kwa ardhi kazi za ujenzi zilifanywa na wanajamii kwa kutumia mafundi wenyeji.

Maombi ya fedha kutoka Halmashauri; sambamba na michango, Diwani aliomba fedha kutoka Halmashauri na kiasi cha TZS 5,200,000 kutoka katika Mfuko wa Maendelo wa Jimbo zilitolewa. Aidha, Halmashauri ilitoa TZS 53,000,000 kwa ajili ya kupaua na na TZS 29,693,000 kumalizia ujenzi.

Kupata usaidizi wa utaalamu; Halmashauri ilitoa ushauri wa kitaalamu kupitia michoro, gharama za ujenzi, usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za ujenzi. Jamii ilishiriki katika kutengeneza matofali ya saruji, kukusanya vifaa vya ujenzi na kusaidia mafundi kwenye mchakato wa ujenzi. Mwaka 2015, madarasa 4, vyoo 2 vyenye matundu 10, nyumba ya walimu 1 na maabara 3 vilikamilika na mwaka 2016 madarasa mengine 2 yalijengwa. Baada ya kukamilika kwa shughuli za ujenzi, Shule ya Sekondari ya Mwalimu Nyerere ilitoa madawati, meza na viti na Halmashauri ilinunua madawati mengine 276. Mwaka 2015, Halmashauri ilipeleka walimu 7, vifaa vya elimu na kuzindua shule hata kabla ya usajili ili kupunguza msongamano wa wanafunzi uliokuwepo katika madarasa ya Shule ya Sekondari ya Mwalimu Nyerere.

**5.0 RASILIMALI**

Shughuli ya ujenzi wa madarasa mapya ya shule ya Sekondari ya Segese ulitumia aina mbalimbali za rasilimali.

(i) Rasilimali watu; jamii ya Segese ilijitoa kikamilifu kwa kuchangia nguvukazi, mawazo, muda, vifaa vya ujenzi na fedha taslimu.
(ii) Rasilimali nyingine kama ardhi na vifaa vya ujenzi.
(iii) Rasilimali fedha; Fedha taslimu TZS 31,039,000 kutoka jamii ya Kata ya Segese na TZS 87,893,000 kutoka Halmashauri.

**6.0 MATOKEO**

Jitihada za Jamii ya Kata ya Segese katika ujenzi wa shule ya sekondari mpya zilileta mabadiliko chanya katika sekta ya elimu. Shule imeanzishwa ikiwa na miundombinu bora; madarasa 10, maabara 3, vyoo vya wanafunzi 8, vyoo vya walimu 2 na nyumba ya walimu 1. Kukamilika kwa shule hii kumeongeza idadi ya shule za sekondari ndani ya Halmashauri kutoka 14 hadi 15 na idadi ya madarasa kutoka 146 hadi 156. Picha iliyopo hapa chini inaonesha Shule ya Sekondari ya Segese, mpya.



*Shule ya Sekondari ya Segese*

Mazingira ya kufundisha na kujifunza yameboreshwa; uwiano wa wanafunzi kwa darasa umeboreshwa kutoka 80:1 had 55:1 na madarasa hayana msongamano tena. Halmashauri imeongeza walimu kutoka 7 mwaka 2015 hadi 23 mwaka 2019. Jambo hili limeongeza ari ya walimu kufanya kazi na wanafunzi kuhudhuria shule.

Kuongezeka kwa uandikishaji; shule mpya ya sekondari ya Segese imeandikisha wanafunzi 729 ambao kati yao 425 ni wavulana na 304 ni wasichana. Aidha, shule hii inapokea wanafunzi kutoka Kata nyingine za jirani za Shella na Mgani. Hali hii imeleta furaha kati ya wazazi kwani watoto wao wanatumia shule ambayo wamejenga kwa nguvu zao.

Kuimarika kwa ushirikiano; ushirikiano kati ya wanajamii kuhusu shughuli za maendeleo umeongezeka baada ya kufanikiwa kujenga miuondombinu ya shule. Wanajamii wameazimia kujenga miundombinu mingine kama madarasa, nyumba za walimu na jengo la utawala na kushiriki kikamilifu katika shughuli nyingine za maendeleo zitakazofanyika katika maeneo yao.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Jamii ya Segese ina mipango ya kuhakikisha kuwa jitihada hii ni endelevu na ina utendaji bora unaotakiwa kwa kutekeleza mikakati ifuatayo;

(i) Kuendelea kuchangia rasilimali kwa ajili madarasa mengine 4 na jengo la utawala.

(ii) Jamii imeanzisha Kamati ya Shule ambayo imepatiwa jukumu la kufuatilia mara kwa mara kuhakikisha shule inaendelea vyema.

(iii) Halmashauri inaendelea kutenga fedha za maendeleo kila mwaka na kuongeza watumishi na vifaa mbalimbali vya elimu. Maboresho haya yatapandisha uwezo wa shule hii na kufikia hadhi ya kuwa shule ya sekondari kamili na iliyosajiliwa kwani kwa sasa inaendeshwa kama sekondari shikizi ya Shule ya Sekondari ya Mwalimu Nyerere. Mchakato wa usajili wa shule hii utasaidia kukamilika kwa uanzishaji wa Shule ya Sekondari ya Segese.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Siri iliyopo katika mafanikio haya imejikita katika mahusiano mema yaliyopo kati ya H/W ya Msalala na uongozi wa Kata ya Segese. Diwani aliandaa mikutano kadhaa na kumwalika Mkurugenzi Mtendaji kujionea mafanikio ya wanavijiji. Stadi za Uongozi alizonazo Diwani na uwezo wake wa kushawishi wanajamii kutoa rasilimali kwa ajili ya maendeleo ya umma, vinabaki kuwa nguzo ya mafanikio ya jitihada hii. Bila jitihada pekee za Diwani huyu ni dhahiri kuwa ujenzi wa shule mpya ya sekondari katika Kata ya Segese usingefanikiwa.

# HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

**JITIHADA YA WAFANYABIASHARA WA KATA YA CHANG'OMBE KATIKA UJENZI WA SOKO**




***Uzoefu wa Jiji la Dodoma***

## 1.0 UTANGULIZI

Historia ya Jiji la Dodoma inafahamika hata kabla ya ukoloni ambapo eneo hili lilikuwa maarufu kwa mapito ya wanyama kutoka upande wa Kaskazini (Arusha) kwenda ukanda wa kusini (Mikumi) siku hizi pakijulikana kama Hifadhi ya Taifa ya Mikumi. Aidha, kulitokea tukio la kihistoria ambapo kundi la Tembo lilizama katika tope karibu na Shule ya Sekondari ya Mazengo. Kitendo cha kuzama katika tope hujulikana kama *idodomya* kwa lugha ya Kabila la Kigogo. Tukio hili la kihistoria ndilo limeleta chanzo cha jina Dodoma.

Halmashauri ya Jiji la Dodoma ndio Makao Makuu ya Nchi kwa mujibu wa Tamko la Rais Na.320 la mwaka 1973. Jiji hili linapatikana kwenye mwinuko wa 1,200m juu ya usawa wa bahari na katika Latitudo $6.00^0$ na $6.30^0$ Kusini na Longitudo $35.30^0$ na $36.02^0$ Mashariki. Jiji hili lipo katika eneo la kati la Tanzania katika eneo muhimu la reli ya kati na katika makutano ya barabara muhimu za kitaifa ambazo ni barabara kuu ya Mashariki kuelekea Magharibi na barabara maarufu ya kimatafa ya Kaskazini (kutoka Capetown kwenda Cairo). Jiji la Dodoma hupakana na H/W ya Bahi upande wa Magharibi na H/W ya Chamwino upande wa Kaskazini, Mashariki na Kusini. Jiji hili lina Tarafa 4, Kata 41, Mitaa 170, Vijiji 18 na Vitongoji 89. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, Jiji hili lina watu 459,350 ambapo 222,978 ni wanaume na 236,371 ni wanawake.




***Ramani ya Jiji la Dodoma***

Eneo la jiji la Dodoma ni $2{,}769km^2$ lenye kipenyo cha kati ya 30km-40km kila upande. Hii ndio Halmashauri ndogo zaidi katika Mkoa wa Dodoma ikiwa na 6.3% tu ya eneo lote la Mkoa. Hali ya hewa ni ya ukame, ikiambatana na mvua za msimu mfupi, ambapo kuna kipindi kirefu cha ukame (Aprili hadi Novemba) na kipindi kifupi cha mvua (Desemba hadi Machi) na wastani wa mvua kwa mwaka wa 550mm – 600mm. Jiji lina ardhi yenye upotevu wa unyevu wa wastani likiwa na uoto wa savanna hasa mibuyu na migunga. Wastani wa joto huwa $20^0$C msimu wa Julai na $30^0$C kipindi cha Novemba.

Kiuchumi, takribani 75% ya kipato cha wakazi wa Jiji la Dodoma hutokana na kilimo na ufugaji. 25% ya wakazi hushughulika na biashara ndogondogo za maduka, useremala na uuzaji wa vyakula. Shughuli nyingine za kiuchumi ni pamoja na viwanda vidogo na vya kati, ushauri na ujenzi. Bidhaa kuu zinazozalishwa viwandani ni mvinyo, magodoro, samani na maji. Bidhaa nyingine ni asali, nta na mazao ya misitu.

## 2.0 TATIZO

Soko ni sehemu ambapo bidhaa hununuliwa na kuuzwa kwa bei za rejareja au jumla. Hivyo, sokoni ni mahali ambapo kuna aina mbalimbali za maduka na vizimba na huuzwa aina mbalimbali za bidhaa.

Masoko mengi hutegemea wauzaji wa bidhaa na huduma wanobadili bidhaa zao kwa fedha taslimu kutoka kwa wanunuzi.

Kata ya Chang'ombe ndiyo yenye wakazi wengi zaidi katika Jiji la Dodoma ikiwa na watu 26,122 (10,020 wanaume na 16,102 wanawake) ikilinganishwa na wastani wa idadi ya watu 11,203 kwa Kata. Kwa idadi hii ya watu, kulikuwa na masoko mengi madogomadogo na yasiyo rasmi yaliyokuwa katika makazi ya watu. Masoko haya hayakuwa na huduma za msingi kama vyoo, maji safi na umeme. Kukosekana kwa dampo kulisababisha uchafu wa masoko haya kutapakaa katika makazi. Maeneo haya yalikuwa machafu na yenye msongamano yakiambatana na hatari za magonjwa na uchafu wa hewa. Milipuko ya magonjwa kama kipindupindu na homa ya matumbo lilikuwa suala kawaida hasa msimu wa mvua. Masoko haya yasiyo rasmi yalisababisha Halmashauri kushindwa kukusanya mapato (ushuru wa soko na leseni za biashara). Hali hii ililazimu Halmashauri kwa kushirikiana na jamii ya wafanyabiashara wa Chang'ombe kupanga, kuchora ramani na kujenga soko jipya lenye ukubwa sahihi ili kukidhi mahitaji ya jamii.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuanzisha soko la kisasa ndani ya Kata lenye huduma zote za msingi na za kutosha ili kubeba masoko yote madogo na yasiyo rasmi yaliyokuwa katika maeneo ya makazi. Ili kufikia azma hili, jitihada hii ililenga;

(i) Kutafuta eneo mahsusi la kujenga soko bora lenye sehemu na huduma zote za msingi kama maji, vyoo na dampo.
(ii) Kushirikisha jamii katika ujenzi na uendeshaji wa soko.
(iii) Kuboresha huduma za usafi wa mazingira.
(iv) Kuongeza idadi ya wafanyabiashara na hivyo kuongeza fursa za ajira.
(v) Kuboresha na kuongeza nafasi za kupakia na kushusha bidhaa katika soko.
(vi) Kuongeza mapato ya Halmashauri kupitia ada za soko na leseni za biashara.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Utekelezaji wa jitihada hii ulianza katika jamii yenyewe. Wanajamii waliichukia hewa chafu katika makazi yao iliyotokana na kuoza kwa uchafu utokao kwenye masoko yasiyo rasmi. Mwaka 2015 wanajamii waliwasilisha kwa Mwenyekiti wa Mtaa malalamiko kuhusu uchafu wa mazingira uliosababishwa na soko lisilorasmi la Msamaria na kuomba lifungwe au lihamishwe kwenda eneo jingine mbali na makazi yao. Mwenyekiti wa Mtaa aliwasilisha lalamiko hili katika Ofisi ya Kata ambapo wajumbe wa Kamati ya Maendelo ya Kata walilijadili na kuamua kulitolea taarifa Halmashauri kwa hatua zaidi. Halmashauri, Kata ya Chang'ombe na jamii ya wafanyabiashara kwa pamoja walitumia mikakati mbalimbali iliyochambuliwa hapa chini kufikia lengo.

Kuandaa mikutano ya maamuzi; mwaka 2015, Afisa Mtendaji wa Kata aliitisha mkutano kati ya wafanyabishara na maofisa wa Halmashauri kujadili changamoto za masoko yasiyo rasmi na kuamua kuanzisha soko jipya. Katika mkutano huu Afisa Mtendaji wa Kata alipewa jukumu la kutafuta eneo la wazi linalofaa kwa ujenzi wa soko. Wafanyabiashara waliombwa kushiriki katika ujenzi wa soko kwa mfumo wa kuchangia gharama na kuunda kamati ya pamoja ya kusimamia shughuli za ujenzi.

Upatikanaji wa Ardhi; eneo la ardhi katikati ya mtaa wa Chang'ombe D lilipendekezwa na mchakato wa kulimiliki ukatekelezwa. Halmashauri ilikubali kubadili matumizi ya eneo hili kutoka kuwa eneo la wazi na kuwa eneo la soko.

Kuundwa kwa kamati ya usimamizi ya pamoja; kamati iliundwa na ilikuwa na wajumbe kutoka Halmashauri ambao ni Mkurugenzi wa Jiji, Mwanasheria wa Jiji, Afisa Mipango Miji wa Jiji, Mhandisi wa

Jiji, Afisa Biashara wa Jiji, Afisa Mtendaji wa Kata ya Chang'ombe na Mwenyekiti wa Mtaa wa Msamaria. Kwa upande mwingine, wafanyabiashara walikuwa na wawakilishi 17 ambao ni pamoja na Mwenyekiti, Makamu Mwenyekiti, Katibu na Mweka hazina wao. Jukumu la kamati hii lilikuwa kutoa ushauri na kuhamasisha jamii kushiriki katika uanzishaji wa soko jipya.

Uhamasishaji na kujenga uelewa; zoezi hili lilifanywa kwa umma wote na jamii ya wafanyabiashara kupitia mikutano mbalimbali. Kujenga uelewa kulihusu kutoa maelezo ya umuhimu na faida za soko jipya na ushirikiano uliotakiwa ili kufanikisha jitihada. Jamii ilielezwa faida za soko jipya ikiwa ni pamoja na kuboreshwa kwa afya na usafi, kuwepo kwa vifaa vya kuondoa takataka, kujengwa kwa mifereji ya kuondoa maji ya mvua na kupatikana kwa eneo rasmi la biashara linaloaminika kwa wakopeshaji.

Kuandaa michoro ya soko; Afisa Mipango Miji wa Jiji alipima na kuainisha mipaka ya eneo la soko na kuandaa michoro ya vibanda viliyopendekezwa kuzunguka eneo la soko. Michoro hii ilikabidhiwa kwa Afisa Mtendaji; kila mfanyabiashara iliyeomba kujenga kibanda cha biashara alitakiwa kutumia michoro ambayo imeidhinishwa kutoka kwa Afisa Mtendaji. Lengo lilikuwa kuhakikisha vibanda vyote vinajengwa kwa kufanana ili kupendezesha soko na kuruhusu uwepo wa nafasi kwa ajili ya miundombinu mingine ya soko.

Ujenzi wa miundombinu ya soko; ilikubalika kuwa miundombinu inayozunguka eneo kuu la soko ijengwe na wafanyabiashara ambapo wafanyabiashara 654 walitambuliwa na kupewa viwanja kwa ajili ya ujenzi wa vibanda vya biashara. Ujenzi ulifanywa na mafundi wenyeji walioajiriwa na wamiliki wa viwanja chini ya uangalizi wa Mhandisi wa Jiji. Moja ya masharti katika makubaliano ni kuwa gharama za ujenzi hazikutakiwa kuzidi TZS 3,750,000 kwa kibanda. Baada ya kukamilika kwa shughuli za ujenzi, kila mmiliki wa vibanda alipewa hadhi ya mpangaji na alitakiwa kulipa 40% ya gharama za kupanga kwa miaka 11. 60% ya gharama ilitumika kulipa gharama za ujenzi kwa kipindi cha miaka 11; baada ya kipindi hiki wapangaji wote watakuwa wakilipa 100% ya kodi ya pango. Eneo la ndani ambalo ndio soko kuu linatumika kwa vyakula, mbogamboga na matunda, lilijengwa kwa ushirika kati ya Halmashauri na wafanyabiashara. Wauzaji wote wa bidhaa (155) walitakiwa kuchangia TZS 150,000 kila mmoja kwa ajili ya ujenzi wa jengo kuu la soko.



***Eneo la mbele la soko na vizimba vya mbogamboga***

**5.0 RASILIMALI**

Ujenzi wa Soko la Chang'ombe ulitumia aina mbalimbali za rasilimali ikiwa ni pamoja na rasilimali fedha, watu na ardhi. Rasilimali fedha zilizotumika ni TZS 45,564,800 kama zinavyooneshwa kwenye Jedwali 1 hapa chini.

**Jedwli 1: Rasilimali Fedha**

| Na. | Aina ya Mchango | Chanzo | Kiasi |
|---|---|---|---|
| **1** | Vifaa vya Ujenzi | Wafanyabiashara | 20,956,800 |
| **2** | Vifaa vya Ujenzi | Mbunge | 3,995,000 |
| **3** | Vifaa vya Ujenzi | Halmashauri ya Jiji | 1,298,000 |
| **4** | Saruji, kokoto, bati | Mbunge | 10,975,000 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **5** | Bati na mbao | Halmashauri ya Jiji | 2,320,000 |
| **6** | Umeme na maji | Halmashauri ya Jiji | 6,000,000 |
| | | **Jumla** | **45,564,800** |

Rasilimali watu zilijumuisha maofisa wa jiji, wakazi wa Mtaa wa Chang'ombe na wafanyabiashara ambao kwa pamoja walishiriki moja kwa moja kwa kuchangia na kushiriki kwenye shughuli za ujenzi. Rasilimali nyingine muhimu ni ardhi iliyotumika kuanzisha soko.

## 6.0 MATOKEO

Ujenzi wa soko jipya la Chang'ombe limeleta mabadiliko chanya kwa Halmashauri ya Jiji na wafanyabiashara. Soko hili jipya ni mfano pekee wa jitihada za pamoja kati ya jamii na serikali katika kutatua changamoto. Matokeo mengine ni;

(i) Uwepo wa miundombinu ya soko ya kutosha wafanyabiashara 700 wanaoendesha maduka na vizimba 155 vyenye wauzaji wa vyakula, matunda na mbogamboga.

(ii) Kuimarika kwa upatikanaji wa huduma muhimu katika soko. Huduma hizi ni pamoja na vyoo, maji na umeme.

(iii) Kuboreshwa kwa huduma za afya na usafi wa mazingira katika eneo la soko na hivyo kuzuia uwezekano wa kutokea kwa magonjwa ya mlipuko kama kipindupindu. Kuna mapipa makubwa ya kukusanya taka ngumu.

(iv) Halmashauri ya Jiji imeweka Afisa Afya Msaidizi wa kudumu katika eneo la soko anayesimamia masuala ya afya, mazingira na usafi.

(v) Kuimarika kwa ukusanyaji wa mapato ya Jiji kutoka kwenye ushuru wa soko na ada za leseni za biashara. Wauzaji wa matunda na mbogamboga hulipa TZS 4,000 kwa mwezi na wamiliki wa maduka hulipa TZS 50,000.

(vi) Kuongezeka kwa nafasi za ajira kutokana na kuongezeka kwa idadi ya wauzaji na watoa huduma mbalimbali hivyo kusababisha kuongezeka kwa fursa za ajira na kuimarika kwa viwango vya ubora wa maisha.

(vii) Kuanzishwa kwa stendi mpya ya mabasi yanayotoa huduma kati ya Dodoma na Wilaya za Kondoa na Chemba na hivyo kuongeza idadi ya wateja wa huduma za soko. Inakadiriwa kuwa kuna mabasi 50 yanayotoa huduma karibu na soko kila siku.

(viii) Uwepo wa soko la Chang'ombe lenye wafanyabiashara walioungana umesaidia ukusanyaji wa michango ili kukamilisha ujenzi wa maabara za masomo ya sayansi katika Shule ya Sekondari ya Chang'ombe na ujenzi wa ofisi ya Kata.

(ix) Soko la Chang'ombe sasa linatumika kama soko la mfano katika ujenzi wa masoko mengine Jijini. Kwa mfano uanzishaji wa masoko katika eneo la Kikuyu na Stendi ya Bahi ulitumia michoro na mbinu za soko la Chang'ombe.

## 7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

Jamii ya Kata ya Chang'ombe kwa kushirikiana na Halmashauri ya Jiji imeweka mikakati mbalimbali ili kufikia mafanikio ya muda mrefu na uwepo wa uendelevu wa soko bora. Mikakati hii ni pamoja na;

(i) Matengenezo ya mara kwa mara ya miundombinu ya soko.

(ii) Kuendelea kuwekeza katika kuboresha soko kwa kutumia mapato yanayokusanywa.

(iii) Mipango ya kuweka vifaa vya kung'amua moto na kutoa elimu kwa wafanyabiashara na jamii kuhusu mbinu za kukabiliana na dharura za moto katika soko.

## 8.0 SIRI YA MAFANIKIO

Siri ya mafanikio ya jitihada ya ujenzi wa soko la Kata ya Chang'ombe ni pamoja na;

(i) Uongozi bora na imara wa Halmashauri ya jiji, Mwenyekiti wa Mtaa wa Msamaria na Afisa Mtendaji wa Kata ya Chang'ombe.
(ii) Jitihada binafsi za hali ya juu za Diwani na Mbunge wa Dodoma Mjini katika kuhamasisha wanajamii kutekeleza ujenzi wa soko jipya.
(iii) Utayari wa wafanyabiashara kuchangia rasilimali fedha na vifaa vya ujenzi.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA

JITIHADA ZA JAMII KATIKA KUANZISHA SHULE SHIKIZI YA MATULI



*Uzoefu wa H/W ya Mpwapwa*

## 1.0 UTANGULIZI

H/W ya Mpwapwa ni mojawapo ya Halmashauri 8 za Mkoa wa Dodoma. Halmashauri nyingine ni H/W za Bahi, Chamwino, Kondoa, Mpwapwa, Chemba, Halmashauri ya Mji wa Kondoa na Halmashauri ya Jiji la Dodoma. H/W ya Mpwapwa hupatikana kati ya Latitudo $6^{0}00$" na $7^{0}30$'' Kusini na Longitudo $35^{0}45$" na $37^{0}00$ Mashariki. Halmashauri hii hupakana na H/W za Kilosa upande wa Mashariki, Kongwa upande wa Kaskazini, Kilolo upande wa Kusini na Chamwino upande wa Magharibi. Halmashauri ina eneo la 7,379$km^2$ ambalo ni 18.1% ya eneo lote la Mkoa wa Dodoma ikiwa na Tarafa 4, Kata 33, Vijiji 113, Vitongoji 575 na Mji mdogo 1 wenye Mitaa 18. Kwa mujibu wa sensa ya 2012 Halmashauri ina watu 324,681 ambapo 156,783 ni wanaume na 167,898 ni wanawake, na ongezeko la watu la 2.1%. Makabila makuu ni Wagogo wakifuatiwa na Wahehe, Wakaguru na Wabena.

Halmashauri ina eneo ambalo kwa ujumla ni kame likiwa na safu za milima upande wa Kusini na Magharibi inayoinuka kati 915m hadi 1,200m juu ya usawa wa bahari. Halmashauri ina hali ya savana yenye ukame ikiwa na wastani wa joto wa $27^{0}$C. Mvua hunyesha kwa kipindi kifupi kati ya Desemba na Aprili kwa wastani wa 600mm – 700mm na 1,200mm kwa mwaka katika maeneo ya milimani hasa Kiboriani, Wotta, Lufu, Mbuga na Mang'aliza.

Shughuli kuu za kiuchumi katika H/W ya Mpwapwa ni kilimo na ufugaji ambavyo huajiri 90% ya wakazi, biashara ndogondogo na za kati 7%, viwanda vidogovidogo 1% na shughuli za maofisini 2%. Mazao yanayozalishwa ni mahindi, mtama, karanga, maharagwe, mpunga, viazi vitamu, vitunguu na alizeti. Inakadiriwa kuwa sekta ya kilimo inachangia 48% ya pato lote la Halmashauri.

H/W ya Mpwapwa ina shule za awali 122, shule za msingi 115, walimu 956 na shule za sekondari za umma 24 zenye walimu 234. Kiwango cha kujua kusoma na kuandika kinakadiriwa kuwa 53% tu.

## 2.0 TATIZO

Upungufu wa idadi ya shule za msingi, umbali na vikwazo vya kijiografia kufika shuleni ni mojawapo ya changamoto kubwa katika vijiji vingi Tanzania. Itifaki ya Haki za Mtoto (1990) inaeleza kuwa "Haki ya mtoto kupata elimu ndio msingi wa Itifaki". Itifaki hii imeendelea kueleza masuala muhimu katika kupata elimu katika ngazi yoyote, kuwa mtoto hatakiwi kupata tu fursa ya kuandikishwa shule bali anatakiwa kuhitimu ngazi husika ya elimu. H/W ya Mpwapwa ilikumbwa na utoro uliokithiri, uandikishaji duni na mahudhurio hafifu katika shule za msingi. Sababu zilizochangia hali hii ni pamoja na umbali kwenda shule na jiografia ngumu ya mahali shule zilipo. Katika baadhi ya maeneo wanafunzi wa shule za msingi walipata changamoto nyingi katika kuhudhuria vipindi na kuchukia shule kwa ujumla wake kutokana na mvua, mafuriko na vitisho vya wanyama wa porini wakiwemo nyoka.

Kjiji cha Matuli katika Kata ya Manghaliza kipo 120km kutoka Mpwapwa mjini. Kabla ya mwaka 2001, Kijiji cha Matuli kilikuwa na changamoto nyingi katika huduma ya shule ya msingi. Wanafunzi walilazimika kwenda Shule ya Msingi ya Manghaliza iliyopo 5km kutoka Matuli na walitumia zaidi ya saa 2 kutembea kila siku. Umbali huu katika misitu, ukiambatana na uwepo wa wahuni katika njia na misitu waliopita wanafunzi, ulisababisha matatizo kama ubakaji na mimba za utotoni. Kati ya mwaka 1995 na 2005 kulikuwa na mimba za utotoni 5. Mwaka 1990 vifo 3 vya wanafunzi kutokana na mvua kubwa wakiwa njiani kwenda shule vilitolewa taarifa. Pamoja na ukweli kuwa elimu ya msingi ni ya lazima kwa watoto wote wenye umri wa miaka 7 na kuendelea, zaidi ya 60% ya watoto wa Kijiji cha Matuli hawakuandishwa kuingia shule ya awali au ya msingi. Kati ya 40% ambao waliandikishwa, 15% walishindwa kuendelea na shule kutokana na changamoto hizi.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunza kwa kuanzisha shule shikizi ya Matuli. Malengo mahsusi yalikuwa;

(i) Kujenga miundombinu ya shule ya msingi kama madarasa, vyoo na ofisi kwa ajili ya wanafunzi na walimu.
(ii) Kupunguza na kutokomeza utoro.
(iii) Kupunguza umbali toka nyumbani hadi shule.
(iv) Kuboresha upatikanaji wa huduma za elimu ya msingi.
(v) Kupunguza na kutokomeza hatari zilizoambatana na umbali wa kutoka nyumbani kwenda shule.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Shule za Msingi na Sekondari zilizokuwepo katika H/W ya Mpwapwa zilikuwa na upungufu mkubwa wa miundombinu. Serikali kuu kupitia Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MEM) na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (MES) imekuwa ikisaidia jitihada za jamii katika ujenzi wa miundombinu ya shule hususani madarasa, nyumba za walimu, maabara, mabweni na vyoo. Hata hivyo ujenzi wa Shule Shikizi ya Matuli ulitekelezwa bila usaidizi mkubwa wa Serikali.

Uanzishaji wa jitihada; ujenzi wa shule ya msingi si jambo rahisi kwa jamii yenye kipato cha chini hususani katika maeneo ya kijijini na pembezoni. Ujenzi wa shule shikizi ya Matuli ulikuwa tofauti kidogo. Wanajamii walihamasika sana na walikuwa na hitaji halisi la kushiriki katika ujenzi. Ndiyo sababu jitihada ya ujenzi wa shule hii ulianzishwa na wananchi wenyewe. Kwa lugha ya kigogo jitihada ya hiari ya aina hii huitwa *Wanyahusi*. Wazo la jitihada hii lilitoka kwa Bw. Mariani Munyi mwaka 2000. Alianza kujadili wazo lake hili na watu maarufu ikiwa ni pamoja na wazee wa Kijiji cha Matuli, Viongozi wa Dini, wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na majirani. Bw. Munyi alisema *"….niliamini itakuwa kweli, siku moja tutawaokoa watoto wetu katika mzigo huu mkubwa wa kutembea zaidi ya 5km kwenda shule....wengine walidhani ni ndoto, lakini kwangu….ni kama hadithi isiyokuwa na mwisho hadi tatizo lilipotatuliwa, huwezi kuamini ….mwisho tulikamilisha madarasa 6, vyoo 4 na nyumba za watumishi 2 hadi leo"*.

Ushiriki wa jamii na motisha; mbinu moja muhimu iliyotumika ni kumwalika kila mwanajamii kushiriki katika mchakato wa ujenzi wa shule bila kujali uwezo wake wa kiuchumi. Taarifa ilitumwa kwa kaya zote katika kijiji cha Matuli. Umoja huu ulileta motisha chanya na maamuzi binafsi ya kushiriki katika ujenzi. Kwa kutumia mfumo wa kujitegemea, jamii ya Kijiji cha Matuli iliibua mikakati mbalimbali kufikia lengo la kuanzisha shule ya msingi.

Uhamasishaji wa Jamii; utekelezaji wa jitihada hii ulianza mwaka 2001 kwa kufanya mikutano ya umma na watu maarufu. Viongozi wa Kijiji na Vitongoji walikuwa muhimu sana katika mchakato huu. Viongozi maarufu ikiwa ni pamoja na viongozi wa kimila walipewa jukumu la kuhamasisha jamii, kujenga uelewa na kuwatia moyo wanakijiji kushiriki kikamilifu katika utekelezaji wa mradi. Sambamba na hili, mikutano mbalimbali iliendeshwa katika ngazi za vitongoji, Halmashauri ya Kijiji na mkutano wa kijiji kujadili na kuongeza uelewa wa wanajamii na wadau ili kulitambua tatizo la ukosefu wa shule katika kijiji chao na changamoto zilizowakumba wanafunzi. Kufuatia mikutano kadhaa na kujengwa kwa uelewa, jamii ilikubali kushiriki kikamilifu katika kuchangia fedha taslimu, kutengeneza matofali na kushiriki katika shughuli zote za ujenzi.

Kumiliki Ardhi; ardhi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule ilipatikana kutoka kwa wanajamii. Mwaka 2003 Agnes Haliyake Mdede na Isdory Yotham Dama waliotambua vema uhitaji wa kuwa na

shule kwa ajili ya watoto waliamua kutoa sehemu ya ardhi yao bila kuomba fidia. Eneo lote ni ekari 7, linalokidhi mahitaji ya ujenzi wa madarasa, ofisi, vyoo, nyumba za walimu na viwanja vya michezo.

Uundaji wa kamati ya ujenzi; wanakijiji walitambua kuwa Halmashauri ya Kijiji ina majukumu mengi ya kila siku na kuwa isingekuwa fanisi katika kusimamia shughuli za ujenzi. Iliamuliwa iundwe kamati maalumu ya ujenzi ili kuondokana na ucheleweshaji usiokuwa wa msingi. Kamati yenye wajumbe 8 iliundwa ikizingatia vigezo vya jinsia na uwakilishi wa kila kitongoji cha Kijiji cha matuli. Kamati ilipewa hadidu za rejea ili kuendesha shughuli za kila siku. Baadhi ya majukumu ya kamati yalikuwa ukusanyaji wa michango kutoka kwa wanajamii, usimamizi wa fedha na kuongoza shughuli za ujenzi.

Uchangishaji; wanakijiji walikubali kuchangia TZS 10,000 kutoka katika kaya zote 300. Licha ya uchangiaji wa fedha taslimu ilikubalika kila kitongoji kitengeneze matofali 5,000. Wenyeviti wa vitongoji walipewa jukumu la kuwaongoza watu kwenye utengenezaji wa matofali ili kufikia lengo la matofali 35,000 yaliyohitajika. Utengenezaji wa matofali na ukusanyaji wa michango ya fedha taslimu vilikamilika mwaka 2003.

Ujenzi wa madarasa, vyoo na nyumba za walimu; shughuli za ujenzi zilianza mwaka 2004 na ilipofika mwaka 2010 madarasa 6, vyoo 4, nyumba ya walimu na ofisi vilikamilika na wanafunzi kuandikishwa. Wakati wa ujenzi, jamii ilishiriki kwa kukusanya vifaa vya ujenzi kama mchanga na mawe na kuteka maji. Fedha taslimu zilizokusanywa zilitumika kununua vifaa vya viwandani. Mbunge wa eneo hili alitoa bati 140 kusaidia jitihada za jamii. Hata hivyo shule hii bado haijasajiliwa na inatumika kama shule shikizi ya Shule ya Msingi Manghaliza.

**5.0 RASILIMALI**

Rasilimali zilizotumika ni pamoja na rasilimali fedha, watu na vitu. Rasilimali fedha ni TZS 50,000,000 kutoka katika michango ya wanajamii. Rasilimali nyingine muhimu ni ekari 7 za ardhi, madawati 50 yaliyotolewa na Halmashauri na bati 140 zilizochangiwa na Mbunge. Rasilimali watu zilijumuisha wanajamii, viongozi wa kijiji ambao waliwaongoza watu kukamilisha ujenzi na nguvu kazi yote ya kijiji.

**6.0 MATOKEO**

Utekelezaji wa jitihada hii ya Kijiji cha Matuli imeleta matokeo mbalimbali yaliyochambuliwa kwa kina hapa chini.

Miundombinu ya shule imekamilika; Jamii na Halmashauri zimefanikiwa kujenga madarasa 6, vyoo 4, nyumba 1 ya walimu na kutengeneza madawati 50 kama miundombinu muhimu ya Shule Shikizi ya Matuli. Uwepo wa miundombinu na samani umeboresha mazingira ya kufundisha na kujifunza na kuanzisha safari mpya ya elimu ya msingi kwa watoto wa Kijiji cha Matuli kuelekea kizazi cha wasomi.



***Miundombinu ya Shule Shikizi ya Matuli***

Kupungua kwa umbali wa kutembea kwenda shule; umbali wa kutembea kutoka nyumbani hadi shule na kurudi nyumbali umepungua kutoka 5km hadi chini ya 1km jambo ambalo limeongeza motisha kwa wanafunzi kuhudhuria shule na kupunguza utoro kutoka 60% hadi chini ya 10%. Hatari zote ambazo ziliambatana na kutembea umbali mrefu kutoka kwenda shule na kurudi nyumbani zimetokomezwa.

Kupungua kwa idadi ya wanakijiji wasiojua kusoma na kuandika; kiwango cha wasiojua kusoma na kuandika katika Kijiji cha matuli kimepungua kwani watoto wengi wenye umri wa kwenda shule wanaandikishwa na kuhudhuria shule.

Kuimarika kwa ushiriki wa jamii katika shughuli za maendeleo; jamii imebaini kuwa kupitia jitihada za jamii, inayo uwezo wa kukamilisha miradi mingine mingi ya maendeleo. Wanajaamii wamejifunza kuwa maisha na maendeleo yao yapo mikononi mwao. Picha iliyopo hapa chini inaonesha wanajamii wenye furaha wakiwa mbele ya madarasa waliyojenga kwa nguvu zao.



***Wanajamii wenye Motisha***

Wanajamii wameanzisha shamba la shule ili kuzalisha mahindi yatakayotumika kuwapa wanafunzi uji kila siku wawapo shuleni. Wazazi/walezi hushiriki katika maandalizi ya shamba, kupanda na kupalilia. Picha zilizopo hapa chini zinaonesha shamba la mahindi la shule shikizi ya Matuli.



***Shamba la mahindi la Shule Shikizi ya Matuli***

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Ushiriki wa jamii katika kuanzisha hoja za maandalizi, utekelezaji, ufuatiliaji na upimaji wa miradi umejenga uwezo wa jamii kushiriki katika shughuli za maendeleo na tabia ya umiliki vyote vikileta uendelevu wa jitihada za maendeleo. Ili kuwa na uhakika wa uendelevu wa matokeo ya jitihada hii, mikakati mbalimbali imewekwa na jamii.

(i) Kuendelea na uhamasishaji wa jamii na kujenga uelewa ili kuendelea kushiriki katika kuitegemeza shule yao.
(ii) Jamii ina mipango ya kujenga miundombinu zaidi ya shule ili kutimiza vigezo na mahitaji ya shule kusajiliwa.
(iii) Halmashauri inaendelea kutoa ushauri wa kitaalamu unaotakiwa kuhakikisha shule inakidhi vigezo vya usajili.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Jitihada hii inatokana na hitaji halisi la jamii; jamii ilitambua hatari ya kuwa kijiji cha pembezoni hivyo kuwa na nia na ari thabiti ya kufanikisha jitihada hii. Sambamba na hili, uongozi imara wa vitongoji na Kijiji katika kuwaongoza wanajamii ulisababisha utekelezaji bora wa jitihada hii. Ushirikiano bora kati ya wajumbe wa Halmashauri ya Kijiji na kujitoa kikamilifu kwa watu maarufu kijijini kuliwatia motisha wanajamii kukamilisha mradi. Moyo wa kishujaa wa mwanakijiji mmoja kushirikisha wazo lake uongozi wa kijiji na wanajamii wengine ulitumika kama chachu ya kukamilisha mradi huu.

# Sura ya Tatu

## Ushiriki wa Jamii katika Utoaji wa Huduma

Utoaji huduma ni jukumu muhimu katika mahusiano ya taasisi za Serikali na wananchi. Huduma ni mfumo au mpangilio unaokidhi mahitaji ya jamii. Helmsing (1995) anaeleza kuwa utoaji wa huduma ni uamuzi wa lazima unaofanywa na maafisa wa kuchaguliwa au kuajiriwa kutumikia au kutoa bidhaa na huduma kwa wapokeaji. Utoaji wa huduma ni wa namna ya mtazamo na mwelekeo, ukihusisha sifa na desturi za kitaifa na kimataifa.

Utoaji huduma ni mchakato endelevu na unaojirudia wa kupanga na kutoa huduma zinazozingatia mpokea huduma. Huhusu ushiriki wa mpokea huduma katika kuainisha wapokea huduma na kutambua mahitaji yao. Utoaji wa huduma pia unahitaji mchakato wa kubuni na kupanga huduma baina ya watumiaji, watoaji, wasambazaji na washirika katika kuanzisha, kubuni na kupanga huduma na kukidhi mahitaji ya watumiaji wa huduma. Hatimaye utoaji wa huduma unahusu uzalishaji, usambazaji na uwasilishaji wa huduma ambazo zinakidhi lengo na zinafaa kwa mahitaji ya watumiaji. Katika utoaji wa huduma muda wote panahitajika mfumo wa ufuatiliaji na uboreshaji wa kukusanya maoni ya watumiaji na vipimo vya utendaji ili kuwezesha ufuatiliaji na uboreshaji wa bidhaa na huduma wa mara kwa mara.

Utoaji wa huduma ni shughuli ya msingi ya Serikali. Serikali ndiyo taasisi pekee inayoweza kutoa kwa usahihi maelekezo kuhusu huduma muhimu kama usalama wa raia, ulinzi na miundombinu. Ulazima na umuhimu wa masuala haya huleta uhalali katika shughuli za Serikali. Imewekwa katika katiba na mikataba ya kimataifa kwamba Serikali inawajibika na huduma za msingi katika maeneo mengi ya kijamii ambayo ni pamoja na elimu, hifadhi ya jamii, mahitaji ya msingi, ulinzi wa kisheria na makazi. Serikali lazima iwapatie wananchi uhakika wa kuendeleza utoaji huduma; kupatikana huduma kwa wote bila kujali tofauti za kijamii na kiutamaduni na kwa bei zinazofaa. Hili lina matokeo kwa taasisi za Serikali. Uwazi, ufanisi, upatikanaji na mambo mengine, huleta ubora katika bidhaa zitolewazo na Serikali kama huduma kwa wananchi wake.

Serikali ya Mtaa ndio ngazi ya Serikali iliyo karibu zaidi na wananchi. Mfumo wa Tanzania wa Serikali za Mitaa unaonesha kuwa MSM hutoa huduma ambazo zina asili ya kijamii, kama vile afya, maji, elimu, ustawi, usimamizi wa taka, na zile zenye asili ya kiuchumi ambazo ni ardhi na makazi, muindombinu, kilimo, mazingira na maendeleo ya jamii.

Nadharia ya utoaji huduma shirikishi iliyotumika katika sura hii, ina maana ya utoaji huduma ambao huhusisha wadau wote. Kiini cha ushiriki ni jamii ambayo hufaidika na huduma zitolewazo na jamii yenyewe, MSM, Serikali Kuu, mashirika yasiyo ya kiserikali na mashirika ya kimataifa. Utoaji huduma shirikishi huweka jamii faidika kama msingi wakati wa kupanga, utoaji wa huduma na upimaji wa ubora wa huduma. Utoaji huduma shirikishi huleta uendelevu wa huduma inayotolewa.

Katika sura hii, mbinu bora 8 zimewasilishwa kutoka H/Miji ya Njombe, Makambako na Kondoa, Halmashauri ya Manispaa ya Singida, H/W za Njombe, Kiteto na Iramba na Sektretarieti ya Mkoa wa Shinyanga.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Mji wa Njombe inahusu Udhibiti Shirikishi wa Taka Ngumu na Usafi wa Mazingira. Hadi mwaka 2010, ongezeko la watu katika mji wa Njombe lilisababisha kuongezeka na kurundikana kwa kasi kwa uchafu katika Kata za mjini ilihali Halmashauri ikiwa haina fedha za kutosha kudhibiti taka zote kutokana na kutegemea fedha kutoka Serikali Kuu. Lengo kuu lilikuwa kuboresha usafi na kupunguza mrundikano wa taka ngumu. Halmashauri iliamua kuingia katika mikataba, kukarabati malori, kuandaa ratiba ya ukusanyaji wa taka ngumu mitaani, kukusanya taka kutoka maeneo zinapozalishwa, kukuza uelewa na kutekeleza sheria ndogo. Matokeo ya jitihada hii yanajumuisha kupungua kwa magonjwa yatokanayo na uchafu, kupata tuzo katika mashindano ya kila mwaka ya usafi wa mazingira, kujanisha na kupendeza kwa mji na kuongezeka kwa ukusanyaji wa ada ya uzoaji taka. Ili kuendeleza jitihada hii, Halmashauri ina mpango wa kuendelea kuhamasisha jamii kuhusu masuala ya udhibiti wa taka kwa kuchambua na kutenga taka ngumu katika eneo la uzalishaji. Jitihada hii ilifanikiwa kwa sababu ya kujitoa na ubunifu wa idara ya usafi na mazingira kuhusu usafi na udhibiti wa taka ngumu, utayari wa jamii kuchangia ada na kuona kuwa jamii ni sehemu husika ya usafi wa mji, umoja na uwezo wa Timu ya Menejimenti ya Halmashauri na utayari wa viongozi wa kisiasa kushiriki katika masuala yote ya usafi wa mji na udhibiti wa taka ngumu.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Wilaya ya Njombe inachambua Ushiriki wa Jamii Katika Uanzishaji wa Soko la Mbao la Matembwe. Jamii katika Halmashauri hii zilikuwa na changamoto ya ukosefu wa soko la mbao la uhakika na lililopo katika sehemu moja. Hivyo Halmashauri ikaamua kujenga soko ambalo litakuwa kituo cha pamoja cha kukusanyia mapato ya Halmashauri, kutoa vibali vya usafirishaji, usajili wa leseni za biashara ya mazao ya misitu na utoaji wa risiti za kieletroniki za mamlaka ya mapato Tanzania. Kufikia malengo haya, Halmashauri ilitumia mikakati mbalimbali ikiwa ni pamoja na uhamasishaji na uundaji wa Umoja wa Wakulima wa Miti (UWAMIMA), kuhamasisha upandaji wa miti na ufugaji wa nyuki, ujenzi wa barabara za mlisho, kutoa mafunzo kwa wanachama wa UWAMIMA na kuanzisha soko la mbao kama kituo kimoja cha huduma. Matokeo ya jitihada hii ni dhahiri kwani kuna umoja imara na soko linatoa huduma, fursa za ajira, kuongezeka kwa uzalishaji wa mbao na ukusanyaji wa mapato, kuongezeka kwa uchakataji wa mbao na kuimarika kwa taarifa na mawasiliano ya bei za mbao. Ili kufanya jitihada hii kuwa endelevu, UWAMIMA inatarajia kujenga kiwanda kikubwa cha kuchakata mbao na mzani wa kupima uzito wa malori ili yalipe kwa haki. Wataalamu wa Halmashauri wataendelea kujenga uwezo wa soko la mbao la UWAMIMA katika shughuli za kawaida na kutoa mafunzo kwa kamati ya soko kuhusu usimamizi, utunzaji wa kumbukumbu na ufanyaji wa maamuzi. Kwa ujumla mafanikio ya jitihada hii yanatokana na mazingira asilia, hali ya hewa na jamii zinazojituma katika kazi.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Mji wa Makambako inahusu Upimaji Shirikishi wa Makazi yasiyo rasmi katika Kata ya Maguvani. Kati ya mwaka 1969 na 2015, ukuaji wa mji ulizidi uwezo wa wataalam kudhibiti matumizi ya ardhi. Baada ya kubaini kuongezeka kwa kasi ya matumizi ya ardhi yasiyopangwa, Halmashauri ilidhamiria kupanga na kupima ardhi katika maeneo yote ya Kata ambayo hayakupimwa. Utekelezaji wake ulishirikisha wadau, kuchangia gharama za upimaji ardhi, kutumia wanafunzi wa mafunzo kwa vitendo na kupima viwanja kwa awamu. Jitihada hii imezalisha viwanja vilivyopimwa 291, kuongezeka kwa thamani ya ardhi, kutatua migogoro ya ardhi, kupata ardhi kwa ajili ya matumizi ya umma na kutoa hati kwa wamiliki wa ardhi. Halmashauri ina mpango mkakati wa kushirikiana na wadau kupanga na kupima maeneo yote ya Kata za mjini kwa kutumia Modeli ya Maguvani. Ushiriki wa jamii

katika mchakato wote na kuchangia gharama za upimaji ardhi kati ya Halmashauri na wamiliki wa ardhi ndiyo siri ya mafanikio ya jitihada hii.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto inahusu Uwezeshi wa Watoto Wenye Umri wa Kuandikishwa Shule Kutoka Jamii za Wafugaji Kupata Elimu ya Msingi katika Kata ya Partimbo. Kabla ya utekelezaji wa jitihada hii utoro wa wanafunzi ulikuwa wa juu kutokana na mimba, ndoa za utotoni na utumikaji katika uchungaji wa mifugo. Sababu nyingine zilikuwa ushiriki wa watoto katika kuchunga mifugo na kutembea umbali mrefu kutoka nyumbani kwenda shule. Hali hii iliilazimu Halmashauri kuingilia kati ili kuboresha huduma na miundombinu ya elimu kwa jamii za vijijini na wafugaji. Halmashauri, kwa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya, ilihamasisha wazazi kuandikisha watoto kwenye elimu ya msingi. Sambamba na hilo, Halmashauri iliboresha mabweni, ilinunua vitanda na magodoro, ilijenga bwalo na ilianzisha rejesta ya wazazi na wanafunzi wa bweni. Matokeo ya jitihada hii yanajumuisha kuimarika kwa uelewa wa wazazi, utoaji wa chakula shuleni, malezi bora, kuongezeka kwa uhitaji wa elimu na uwepo wa miundombinu bora ya shule. Halmashauri ilifanikiwa kutokana na uongozi bora wa Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Halmashauri ambao waliisaidia sana jitihada hii, utoaji wa chakula bora kwa wanafunzi kilichowatia motisha kubaki shuleni na kutumia wazazi kuwaeleza wanafunzi masuala ya kisasa ya kuzingatia wakiwa shuleni kwa lugha ya kimasai.

Jitihada ya Manispaa ya Singida inahusu Ujenzi wa Kituo cha Mabasi cha Misuna kwa ajili ya kuboresha utoaji wa Huduma. Kabla ya utekelezaji wa jithada hii, Halmashauri ilipitia kipindi kigumu cha ufinyu wa mapato kutokana na uhaba wa vyanzo vya mapato ya ndani na kusababisha kutokuwepo kwa ufanisi katika utoaji wa huduma. Manispaa ya Singida iliamua kujenga kituo cha mabasi cha kisasa kwa ajili ya kutoa huduma na kuboresha mapato. Halmashauri ilipata ardhi eneo la Misuna baada ya kuendesha mikutano mbalimbali na wananchi wa Misuna na kubaini uwepo wa eneo la wazi. Vilevile Halmashauri iliendesha mikutano na wafanyabiashara kujenga vibanda vya maduka, migahawa na choo kuzunguka eneo la kituo cha mabasi kwa kutumia gharama zao kwa maelewano kwamba watatumia vibanda hivyo hadi kurudisha gharama zao na hatimaye kubaki kuwa wapangaji wa Halmashauri. Vilevile Manispaa iliomba fedha kutoka Serikali Kuu kupitia Mradi wa Uendelezaji Miundombinu ya Miji (ULGSP) kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha mabasi. Matokeo ya jitihada hii ni pamoja na uwepo wa kituo cha mabasi na kuongezeka kwa mapato na fursa za ajira. Siri ya mafanikio ni pamoja na ushirikiano na Serikali Kuu, kufanya kazi kama timu na ushirikiano na ofisi ya Mkuu wa Mkoa.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Iramba inahusu uboreshaji wa huduma za afya kwa mama mjamzito. Wastani wa vifo vya wajawazito katika H/W ya Iramba vilifikia 100 kwa kila 100,000. Baada ya kubaini tatizo hili Halmashauri iliamua kuboresha huduma za afya na kuondoa kabisa vifo vya mama na mtoto. Kwa kushirikiana na wadau Halmashauri iliunda kikosi kazi cha kubaini chanzo cha tatizo na kushauri namna bora ya kutatua tatizo. Baada ya kubaini sababu, Halmashauri ilichukua hatua mbalimbali zikimwemo kutoa elimu kwa wajawazito, kuimarisha huduma za rufaa kutoka zahanati, kituo cha afya hadi hospitali ya wilaya na kukarabati jengo la mama ngojea. Matokeo ya jitihada hii ni kupungua kwa vifo, kuongezeka kwa idadi ya wajawazito katika kutumia huduma za afya na kuimarika kwa huduma ya rufaa. Siri ya mafanikio inatokana na utayari wa jamii kukubali kubadilika na Halmashauri kuwekeza fedha katika kuboresha huduma.

Jitihada ya Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga inahusu Upunguzaji wa Vifo vya Mama na Mtoto. Vifo vya wajawazito na watoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga vilikithiri kutokana na ukosefu wa damu salama na maji tiba. Sekretarieti ya Mkoa kwa kushirikiana na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa

iliweka lengo la kuimarisha huduma za afya kwa kupunguza vifo vitokanavyo na kukosa damu salama na maji tiba. Sekretarieti ya Mkoa iliandika barua kwa wadau mbalimbali kueleza tatizo na kuomba usaidizi ili kutatua tatizo. Baadhi ya wadau hao ni Umoja wa Mataifa, Touch Foundation na Saint Luke. Kutokana na juhudi hizi, Sekretarieti ya Mkoa na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa zilifanikiwa kuanzisha Benki ya damu salama, jengo la mama ngojea, kiwanda cha kutengeneza maji tiba hivyo kupunguza idadi ya vifo. Jitihada hii ilifanikiwa kutokana na ubunifu wa menejimenti ya Sekretarieti ya Mkoa na ushirikiano kati ya Sekretarieti ya Mkoa na wadau wa ndani na nje ya nchi.

Mbinu bora ya H/Mji wa Kondoa inahusu Udhibiti Shirikishi wa Taka Ngumu. Halmashauri ilishuhudia ongezeko la taka ngumu kutoka 47.45T hadi 59.22T kwa siku kutokana na ongezeko la watu. Wakazi walitupa taka ovyo katika maeneo ya makazi hivyo kusababisha uchafu wa mazingira na milipuko ya magonjwa yatokanayo na uchafu kama vile kipindupindu, homa ya matumbo na kuhara. Juni, 2017 Halmashauri iliweka lengo la kuimarisha udhibiti wa taka ngumu ili kupunguza magonjwa na kupendezesha mji. Halmashauri ilitumia mbinu mbalimbali zikiwemo uelimishaji wa jamii, ugatuaji wa shughuli za udhibiti wa taka ngumu, kuanzisha kamati za mazingira za Mitaa na usimamizi shirikishi wa sheria ndogo ya usafi wa mazingira. Matokeo ya jitihada hii ni kuimarika kwa usafi, kukua kwa uelewa usafi wa mazingira, kupungua kwa magonjwa ya mlipuko, udhibiti wa taka ngumu katika ngazi za msingi na kuongezeka kwa fursa za ajira. Mafanikio haya yametokana na kufanya kazi kama timu kwa watumishi wa Halmashauri na ofisi ya Mkuu wa Wilaya katika kusimamia usafi na utayari wa jamii kubadilika.

# HALMASHAURI YA MJI WA NJOMBE


**UDHIBITI SHIRIKISHI WA TAKA NGUMU NA USAFI WA MAZINGIRA**



***Uzoefu wa H/Mji wa Njombe***

## 1.0 UTANGULIZI

H/Mji wa Njombe ni mojawapo ya Halmashauri 6 Mkoani Njombe iliyoanzishwa mwaka 2007. Halmashauri hii inapatikana kati ya Latitudo $9^{0}10'$ na $9^{0}45'$ Kusini na Longitudo $34^{0}25'$ na $35^{0}27'$ Mashariki. H/Mji wa Njombe ni ya pili kwa udogo katika eneo la Mkoa ikiwa na eneo la 3,212$km^{2}$ sawa na 15.2% ya ardhi yote ya Mkoa. Halmashauri ina Tarafa 2, Kata 13, Mitaa 26, Vijiji 44 na Vitongoji 232. Kata za Njombe Mjini, Mjimwema na Ramadhani zipo katika eneo la mjini. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 H/Mji wa Njombe ina watu 130, 223 ambapo 61,112 ni wanaume na 69,111 ni wanawake. Uchumi wa Halmashauri unategemea biashara, kilimo, ufugaji, uvuvi, viwanda na ajira katika kampuni binafsi za mbao na sekta ya umma.




***H/Mji wa Njombe kwenye ramani ya Mkoa wa Njombe***

## 2.0 TATIZO

Kati ya miaka ya 1990 na 2000 H/Mji wa Njombe ilikumbwa na ongezeko kubwa la watu kutokana na uhamiaji wa watu kutoka sehemu mbalimbali za Tanzania kwa sababu ya kuimarika kwa shughuli za biashara. Ilipofika mwaka 2010, ongezeko la watu lilisababisha ongezeko na mrundikano mkubwa wa taka ngumu katika Kata za mjini. Licha ya kuongezeka kwa uzalishaji wa taka ngumu, mfumo wa kudhibiti taka ngumu ulibaki kuwa uleule. Hapakuwa na vifaa vya kutosha vya kukusanya taka ngumu kutoka kwenye vituo vya kukusanya taka kwenda kwenye dampo. Ingawa Halmashauri ilikodi magari kutoka kwa wamiliki binafsi, magari haya hayakutosha kukusanya taka ngumu zote zilizozalishwa kwa siku. Ni 10% tu ya tani 65 za taka ngumu zililizokusanywa kwa siku.

Halmashauri haikuwa na fedha za kutosha za kudhibiti taka ngumu kutokana na utegemezi kwa mapato ya ndani ili kulipa gharama za magari yaliyokodiwa. Ushiriki wa jamii kupitia michango ya ukusanyaji wa taka ilikuwa duni sana. Aidha, jamii haikuwa na uelewa wa uchangiaji na ushiriki unaotakiwa katika kudhibiti taka ngumu kwani iliamini kuwa shughuli hii ni jukumu la Halmashauri kwa ujumla. Hali hii ilisababisha kurundikana kwa kwa taka ngumu katika vituo vya kukusanyia taka kama sokoni na mitaa ya SIDO, Magereza, Kambarage, Posta Kati, Mgendela na National Housing. Maeneo haya yalibadilika na kuwa kero kwa kaya za jirani na kuiweka jamii katika hatari ya magonjwa.



***Mrundikano wa taka ngumu katika Kizimba***

**3.0 LENGO**

Ukusanyaji ni shughuli muhimu ya kwanza ya udhibiti wa taka ngumu. Udhibiti wa taka ngumu hujumuisha ukusanyanji wa taka kutoka maeneo mbalimbali ya makazi, biashara, taasisi, viwanda na katika bustani za umma. Mbinu kuu tatu za ukusanyaji ni zile za kuweka taka zilizofungashwa karibu na barabara, kuweka taka kwenye vifungashio na kuchukuliwa na wakusanyaji kwa utaratibu maalumu na kukusanya taka katika vizimba vidogo nyuma ya kaya. Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuboresha usafi na kupunguza kurundikana kwa taka ngumu kwa kuimarisha ukusanyaji na usafirishaji wa taka zinazozalishwa kwenda katika dampo kwa wakati. Malengo mahususi ya jitihada hii yalikuwa;

(i) Kujenga uwezo wa jamii kuhusu udhibiti wa taka ngumu.
(ii) Kuanzisha ada za ukusanyaji taka.
(iii) Kukarabati na kununua mitambo mipya ya udhibiti wa taka.
(iv) Kusimamia utekelezaji wa sheria na sheria ndogo za udhibiti wa taka.
(v) Kuzuia milipuko ya magonjwa yatokanayo na uchafu wa mazingira.
(vi) Kushirikisha wadau mbalimbali katika masuala ya afya na usafi.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Ukusanyaji wa taka ngumu ni kitendo cha kupeleka mbali uchafu unaozalishwa katika kaya na maeneo ya biashara karibu na makazi, maduka, migahawa, viwanda vidogo na masoko. Uchafu huchukuliwa katika kaya kwenda kwenye vizimba vilivyo jirani. Hii ni awamu ya kwanza ya ukusanyaji. Kutoka kwenye vizimba Halmashauri au wakala binafsi husafirisha uchafu wote kwenda kwenye dampo la Halmashauri ambapo huteketezwa. Hii ni awamu ya pili ya ukusanyaji.

Ukusanyaji wa taka ngumu ni moja ya vipaumbele vya H/Mji wa Njombe vinavyolenga kuwepo kwa mazingira safi, mazuri na yenye afya kwa wakazi. Halmashauri hii inaamini kuwa afya bora ya watu ni sehemu muhimu ya maendeleo na kuwa mazingira safi na yenye afya huzuia magonjwa na kupunguza gharama za matibabu. Ili kufikia malengo haya, Halmashauri ilibuni mikakati mbalimbali iliyochambuliwa kwa kina hapa chini.

Matumizi ya mikataba na mikutano ya jamii; mwaka 2013, H/Mji wa Njombe ilitambua hitaji la kujikita kwa kina katika masuala ya udhibiti wa taka ngumu. Mwanzoni, Halmashauri iliamua kubinafsisha ukusanyaji wa taka ngumu na ukusanyaji wa ada za taka kwa sekta binafsi, lakini mtoa huduma alishindwa kukidhi mahitaji baada ya miezi 9 tu. Hali hii ilisababisha Halmashauri kutafuta mbinu nyingine ikiwa ni pamoja na kuitisha mikutano na viongozi wa masoko ambapo kulikuwa na ugumu wa kulipa ada za taka na malalamiko mengi kuhusu kiasi cha ada ya taka inayotakiwa kulipwa. Baada ya mikutano na uhamasishaji, viongozi wa soko waliamua kusimamia masuala ya taka ngumu katika masoko na kukubali kukusanya TZS 1,000 kutoka kwa kila mfanyabiashara kwenye eneo la soko. Kiasi cha fedha zilizokusanywa kwa mwezi kutoka sokoni kilikuwa TZS 3,190,000/= ambacho hakikutosha kukusanya taka ngumu zote katika eneo la soko. Hali hii iliwafanya watumiaji wa soko kukubali kulipa ada za ukusanyaji taka kwa mujibu wa sheria ndogo za Halmashauri.

Ukusanyaji wa taka ngumu na Halmashauri yenyewe; katika mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri iliamua kukusanya na kudhibiti taka ngumu moja kwa moja bila kutumia watoa huduma binafsi. Idara ya Usafi na Mazingira ilitoa pendekezo kwa Timu ya Menejimenti ya Halmashauri la kubadili matumizi ya lori la Halmashauri kutoka shughuli nyingine za maendeleo hasa ujenzi na kutumika kwa ajili ya ukusanyaji na usafirishaji wa taka kwenda kwenye dampo. Pendekezo hili lilikubalika kwenye Timu ya Menejimenti na Kamati ya Fedha na hivyo idara ya usafi na mazingira kuanza kulitumia lori kukusanya taka toka kwenye vizimba.



***Lori la H/Mji wa Njombe la kukusanya taka***

Ukarabati wa lori za zamani; mwaka huohuo (2016/17), idara ya usafi na mazingira iltoa pendekezo lingine la kukarabati lori aina ya Isuzu ambalo lilikuwa linasubiri kupigwa mnada. Pendekezo hili lilipita katika Menejimenti, Kamati ya Fedha na kuidhinishwa na Baraza na hivyo Halmashauri kutumia TZS 13,000,000 kwa matengenezo ya lori. Lori hili liliongeza uwezo wa kusafirisha taka ngumu kwenda kwenye dampo.



***Lori aina ya Isuzu lililofanyiwa ukarabati***

Kuandaa ratiba ya ukusanyaji wa taka katika mitaa; baada ya kuwa na malori mawili Halmashauri iliandaa ratiba ya ukusanyaji wa taka mjini. Ratiba inaonesha tarehe, muda na eneo la ukusanyaji na ofisa mhusika na nasimamiwa na Maofisa Watendaji wa Mitaa. Ratiba hii imeoneshwa kwenye jedwali 1 hapa chini. Lori la pili hushughulika zaidi na maeneo ambayo yanahitaji usafi wa kila siku kama Hagafilo Polisi (barabara ya Songea), Soko Kuu, Stendi ya mabasi madogo na Stendi Kuu.

**Jedwali 1: Ratiba ya Ukusanyaji Taka**

| Ratiba hii ni ukusanyaji wa taka ngumu katika mitaa | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Lori la kwanza** | | | | |
| **S/N** | **SIKU** | **MUDA** | **ENEO** | **MHUSIKA** |
| **1** | JUMATATU | 02:00 – 04:00 | IDUNDILANGA | Afisa Usafiri, Afisa Mtendaji wa Mtaa |
| | | 05:00 - 07:00 | MPECHI | |
| | | 08:00 – 10:00 | KIBENA | |
| | | 08:00 – 10:00 | HAGAFILO | |
| | | 08:00 – 10:00 | MJIMWEMA | |
| | | 08:00 – 10:00 | NATIONAL HOUSING | |
| | | | | Bwana Afya |
| **2** | JUMANNE | 02:00 – 04:00 | KWIVAHA | Afisa Usafiri, Afisa Mtendaji wa Mtaa |
| | | 05:00 - 07:00 | KIHESA | |
| | | 07:00 - 08:00 | RAMADHANI | |
| | | 08:00 – 10:00 | KAMBARAGE | |
| | | | | Bwana Afya |
| **3** | JUMATANO | 02:00 – 04:00 | BUGURUNI | Afisa Usafiri, Afisa Mtendaji wa Mtaa |
| | | 05:00 - 07:00 | SIDO | |
| | | 08:00 - 10:00 | POSTA-MITAANI | |
| | | | | Bwana Afya |
| **4** | ALHAMISI | 02:00 – 04:00 | MGENDELA | Afisa Usafiri, Afisa Mtendaji wa Mtaa |
| | | 05:00 - 07:00 | NATIONAL HOUSING | |
| | | 07:00 - 08:00 | KIHESA | |
| | | 08:00 – 10:00 | KIBENA | |
| | | | | Bwana Afya |
| **5** | IJUMAA | 02:00 – 03:00 | MJI MWEMA | Afisa Usafiri, Afisa Mtendaji wa Mtaa |
| | | 03:00 - 05:00 | NAZARETI | |
| | | 05:00 - 07:00 | MELINZE | |
| | | 07:00 - 08:00 | MPECHI | |
| | | 08:00-04:00 | JOSHONI | |
| | | | | Bwana Afya |
| **6** | JUMAMOSI | 02:00 – 03:00 | HAGAFILO | Afisa Usafiri, Afisa Mtendaji wa Mtaa |
| | | 05:00 - 07:00 | BUGURUNI | |
| | | 07:00 - 09:00 | SIDO | |
| | | 09:00- 10:00 | POSTA MITAANI | |
| | | | | |
| | | | | |

Kuanzisha ukusanyaji wa taka ngumu kutoka kwenye chanzo; kutokana na ufanisi wa malori mawili na kuzingatiwa kwa ratiba ya ukusanyaji, Halmashauri iliamua kuacha matumizi ya vizimba ambavyo vilikuwa kero kwa wakazi wa maeneo ya kati ya mjini na kuanza kukusanya taka kutoka eneo zinapozalishwa. Wanajamii walishauriwa kukusanya taka ngumu katika kaya na sehemu za biashara na kuzileta moja kwa moja kwenye malori badala ya kuzitupa kwenye vizimba.



***Watu wakipakia taka ngumu kwenye lori***

Ukuzaji wa uelewa; Halmashauri iliendesha vipindi vya elimu ya udhibiti wa taka ngumu kwa jamii kuhusu utenganishaji wa taka, ulipaji wa ada za taka na usafi wa jumla wa mazingira yanayozunguka kaya na maeneo ya biashara walau kwa mwezi mara moja. Uhamasishaji huu ulifanyika kupitia mikutano katika kila mtaa. Mikutano iliandaliwa na kuhutubiwa na Maafisa Maaendeleo, Maafisa Mazingira na Maafisa Watendaji wa Mitaa.



***Usafi wa Mazingira (kila mwezi)***

Utekelezaji wa sheria; Halmashauri ilingia mkataba na dalali wa mahakama aitwaye *Yono Auction Mart* ili kusimamia utekelezaji wa sheria ndogo za usafi, upendezeshaji mji na ukusanyaji wa ada ya taka. Sambamba na hilo, Halmashauri iliajiri askari mgambo 5 wanaotumika kuzuia watu kufanya biashara katika maenezo yasiyoruhusiwa (jambo ambalo huchangia uchafu na msongamano wa watu mjini).

Ununuzi wa lori na trekta mpya; mwaka 2016/2017 Halmashauri ilinunua lori jingine kwa matumizi ya usafirishaji wa taka lililogarimu TZS 218,000,000. Lori hili ilimeongeza uwezo wa usafirishaji wa taka kwenda dampo kutoka tani 20 hadi 60 kwa siku. Pia, Halmashauri ilipewa zawadi ya trekta kwa ajili ya ukusanyaji wa taka ngumu kwenye mashindano ya Mazingira na Usafi kwa Halmashauri za Miji (yanayo andaliwa na Wizara ya Afya) na kuongeza zaidi uwezo wa usafirishaji wa taka kwenda dampo. Mwaka 2017/2018, Halmashauri ilinunua trekta jingine kwa gharama ya TZS 79,000,000 na kuongeza uwezo wa kusafirisha taka kwenda dampo hadi tani 65 kwa siku. Halmashauri ilishiriki tena mashindano ya Mazingira na Usafi mwaka 2017/2018 na kuzawadiwa trekta jingine.



***Wawakilishi wa H/Mji wa Njombe wakipokea trekta la mshindi wa kwanza katika Mashindano ya Mazingira na Usafi***

kuunda ushirikano na viongozi wakuu wa kisiasa; Halmashauri iliwasilisha pendekezo la jitihada hii kwa viongozi wa kisiasa (Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya). Zoezi hili liliwapatia viongozi hawa undani wa suala hili na mikakati inayotekelezwa ili kuboresha usafi wa mji. Wakuu hawa wa Mkoa na Wilaya waliafikiana na jitihada hii na kutoa maelekezo ya kuondoa biashara zote katika maeneo yasiyo rasmi.

Uanzishaji wa soko la Joshoni na Machinjioni; ili kuhamisha wafanyabiashara wadogo (*Machinga*) kutoka maeneo ambayo si rasmi kwa shughuli zao, Halmashauri ilianzisha masoko mawili katika maeneo ya Joshoni na Machinjioni kwa ajili ya wafanyabiashara na wamachinga waliotumia kingo za barabara ya Makambako – Songea kuuza bidhaa zao na kufanya mji kuwa mchafu na wenye msongamano.



***Soko la Joshoni***

Usafi wa mazingira kuwa ajenda ya kudumu; Halmashauri iliamua suala la usafi wa mazingira kuwa ajenda ya kudumu katika vikao vya ngazi zote kutoka Kamati za Maendeleo za Kata hadi Baraza ili kuleta uendelevu wa usafi katika Mji wa Njombe. Uamuzi huu umefaulu kuhakikisha kuwepo kwa majadiliano ya masuala na changamoto zote za usafi na upendezeshaji wa mji katika mikutano yote ya Baraza.

**5.0 RASILIMALI**

Ili kufikia malengo ya kuwa na Mji safi, Halmashauri ilitumia rasilimali mbalimbali kama watu, vitu na fedha. Rasilimali watu zilizotumika ni pamoja na wajumbe wa Timu ya Menejimenti ya Halmashauri, Wajumbe wa Kamati za Maendeleo za Kata, Maafisa Watendaji wa Mitaa, vibarua 35, askari mgambo 5 na madereva ambao kwa pamoja walijipanga kuhakisha Mji wa Njombe ni safi na unavutia. Halmashauri ilitumia vitendea kazi kama greda 1, malori 3, trekta 3 na pikipiki 1. Rasilimali fedha zilijumuisha TZS 627,000,000 zilizotengwa kwa miaka mitatu mfululizo (2015/2016, 2016/2017 na 2017/2018) kama inavyooneshwa kwenye jedwali 2 hapa chini.

**Jedwali 2: Rasilimali Fedha**

| 2015/2016 | 2016/2017 | 2017/2018 | Chanzo |
|---|---|---|---|
| **108,000,000/=** | 132,000,000/= | 113,000,000/= | Mapato ya Ndani |
| | 195,000,000/= | 79,000,000/= | ULGSP |



***Greda likiwa katika dampo la Maheve***

**6.0 MATOKEO**

Utekelezaji wa jitihada shirikishi ya udhibiti wa taka ngumu na usafi wa mazingira umeifanya H/Mji wa Njombe kupata matokeo makuu mbalimbali. Tokeo moja kuu ni kupungua kwa magonjwa yanayotokana na uchafu kama inavyooneshwa kwenye jedwali 3 hapa chini. Kwa mfano, hapajatokea taarifa yoyote ya ugonjwa wa kipindupindu tangu kuanza kwa jitihada hii. Mwaka 2015, kipindupindu kilienea sehemu nyingi Tanzania lakini ni Mji wa Njombe tu ambao haukuwa na mgonjwa hata mmoja.

**Jedwali 3: Matukio ya Magonjwa yatokanayo na uchafu**

| UGONJWA | MWAKA | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2014 | 2015 | 2016 | 2017 | 2018 |
| Homa ya matumbo | 3268 | 2211 | 1164 | 998 | 406 |
| Kuhara | 570 | 546 | 339 | 271 | 231 |
| Malaria | 2489 | 2317 | 2238 | 1185 | 706 |

Kupata tuzo katika Mashindano ya Mwaka ya Mazingira na Usafi; Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto huendesha mashindano ya Serikali za Mitaa kuhusu Mazingira na Usafi kila mwaka ambapo Halmashauri za Miji ni kundi mojawapo. H/Mji wa Njombe ilishinda mara tatu mfulululizo (mwaka 2016, 2017 na 2018) kwenye kundi la Halmashauri za Miji Tanzania. Halmashauri ilipata tuzo za pikipiki 1 (2016) na Trekta 2; moja mwaka 2017 na nyingine mwaka 2018.




*Tuzo ilizoshinda H/Mji wa Njombe*

Ujanishaji na upendezeshaji wa mji; H/Mji wa Njombe huwa na misimu mirefu ya mvua ikiambatana na hali ya hewa ya baridi. Hali hii huruhusu mazingira ya kijani ambayo hutoa fursa kwa Halmashauri na jamii kujishughulisha na utunzaji wa bustani na maeneo ya wazi. Katika mukhtadha huu, halmashauri imefanikiwa kubadili maeneo yaliyokuwa na vizimba vya taka ngumu kuwa bustani za mapumziko. Bustani iliyopigwa picha hapa chini ni mfano wa eneo la kizimba lililoboreshwa na kuwa eneo la mapumziko ikitumiwa na watoto, wazee na wandaa matukio mbalimbali kama wapiga picha za mnato na video.



*Bustani ya mapumziko*

Makusanyo ya ada za ukusanyaji taka yameongezeka kutoka TZS 8,843,000 mwaka 2014/2015 hadi kifika TZS 43,318,000 mwaka 2017/2018. Kutokana na kubadilika kwa mtazamo wa jamii kuhusu udhibiti wa taka ngumu, utayari wa kushiriki na kulipa ada za taka umeongezeka sana. Haya yanaonekana dhahiri katika ongezeko la mapato na usafi wa mji. Jamii inashiriki katika usafi wa jumla, kuchambua na kutenganisha taka ngumu jambo ambalo limepunguza mzigo wa Halmashauri wa mazoezi haya na kuboresha udhibiti wa taka ngumu na uendeshaji wa dampo.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

H/Mji wa Njombe imedhamiria kujikita katika usafi wa mazingira na udhibiti wa taka ngumu bila kuathiri viwango vilivyofikiwa. Kuhakikisha uendelevu wa Mji kuwa safi na udhibiti wa taka ngumu, Halmashauri imejipanga;

(i) Kuendelea kuhamasisha jamii kuhusu masuala yote yanayohusu udhibiti wa taka ikiwa ni pamoja na kuchambua, kutenganisha na kudhibiti taka katika maeneo ya uzalishaji.

(ii) Kuendelea kushirikisha viongozi wa ngazi za juu, (Mkuu wa Mkoa na Wilaya) ili waendelee kuongoza katika jitihada za usafi wa mazingira na udhibiti wa taka ngumu.

(iii) Kuendelea kununua, kukarabati na kuhudumia magari na mitambo ya udhibiti wa taka ngumu.

(iv) Kuunda vikundi vya kiuchumi hasa vya wanawake na vijana na kuvipatia mikopo nafuu itakayosaidia kukusanya, kuchakata na kutumika tena kwa taka za plastiki, karatasi na mpira.

(v) Kushirikisha mashirika ya kidini na sekta binafsi katika udhibiti wa taka ngumu. Halmashauri ipo kwenye mchakato wa kujenga kiwanda cha kuchakata taka ngumu, kwa kushirikiana na Kanisa Katoliki ili kutumia taka ngumu kama mali ghafi.

(vi) Kuhakikisha kuwa masuala ya usafi wa mazingira na udhibiti wa taka ngumu ni ajenda ya kudumu katika vikao vyote kuanzia ngazi ya Kata hadi Halmashauri ili kuleta uendelevu katika usafi wa mji.

(vii) Kuharakisha mchakato wa kuandaa mpango kabambe wa Mji na ujenzi wa stendi kuu ya mabasi na soko kuu ambavyo vitakuwa na huduma zote za udhibiti wa taka ngumu.

(viii) Kuharakisha mapitio ya sheria ndogo za ada za ukusanyaji wa taka ili kuakisi gharama halisi za shughuli za udhibiti wa taka ngumu.

## 8.0 SIRI YA MAFANIKIO

H/Mji wa Njombe imepata mafanikio haya kutokana na sababu mbalimbali za msingi. Sababu moja kubwa ni kujituma kwa bidii na ushirikiano fanisi kati ya Mkurugenzi na Mwenyekiti wa Halmashauri katika kufanya maamuzi kwa muda kuhusu rasilimali za kuendesha shughuli za usafi wa mazingira na udhibiti wa taka ngumu. Sababu nyingine ni kujituma na ubunifu katika idara ya mazingira na usafi kuhusu usafi na udhibiti wa taka, utayari wa jamii kulipa ada za taka na kukubali kuwa sehemu ya usafi wa mji. Mengine ni umoja na uwezo bora wa Timu ya Menejimenti ya Halmashauri na utayari wa viongozi wakuu wa kisiasa kujikita katika masuala yote ya usafi wa mji na udhibiti wa taka ngumu.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE

**UANZISHAJI SHIRIKISHI WA SOKO LA MBAO LA MATEMBWE**





***Uzoefu wa Kata ya Matembwe***

## 1.0 UTANGULIZI

H/W ya Njombe ni mojawapo ya Halmashauzi 6 za Mkoa wa Njombe katika Nyanda za Juu Kusini ikipakana na Mji wa Makambako na H/W ya Mufindi upande wa Kaskazini, Mkoa wa Morogoro upande wa Mashariki, Mji wa Njombe upande wa Kusini, Mkoa wa Ruvuma upande wa Kusini Magharibi na H/W ya Wangingómbe upande wa Magharibi. Halmashauri hii ipo kwenye Latitudo $08^0$.8' hadi $09^0$.8' Kusini na Longitudo $33^0$.5' hadi $35^0$.8' Mashariki. H/W ya Njombe ina eneo la 3,154km$^2$.

Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 Halmashauri ina watu 85,747 ikilinganishwa na idadi ya 89,433 ya sensa ya mwaka 2002. Kupungua kwa idadi ya watu, kulitokana na kuanzishwa kwa H/W ya Wanging'ombe kwa kuigawa H/W ya Njombe mwaka 2012. Ikilinganishwa na Halmashauri nyingine za Mkoa wa Njombe, Halmashauri hii ndio yenye idadi ndogo zaidi ya watu baada ya Mji wa Makambako, ikichangia 12.21% tu ya idadi ya watu katika Mkoa. Halmashauri in Tarafa 2, Kata 12, Vijiji 45, Vitongoji 227 na Kaya 20,341.




***Ramani ya Mkoa wa Njombe***

H/W ya Njombe ipo kwenye mwinuko ambapo zipo safu za milima ya Kipengere upande wa Kaskazini Magharibi, Milima ya Lukumburu upande wa Kusini na Milima ya Lupembe upande wa Mashariki. Hali ya hewa ya Njombe ni ya baridi ambapo joto huwa juu mwezi Novemba likiwa na wastani 18.0°C. Mwezi Julai ndio wenye baridi zaidi kukiwa na wastani wa 12.8°C. Katika mwezi Machi, mvua hufikia kilele cha wastani wa 258mm.

Kilimo ndicho chanzo kikuu cha kipato kwa wakazi wa H/W ya Njombe. Kwa mujibu wa sensa ya 2012, sekta ya kilimo iliajiri 72% ya wakazi. Pamoja na ukweli kuwa kilimo ndiyo sekta inayoongoza katika uchumi wa Halmashauri, uzalishaji umekuwa ukipungua kutokana na sababu mbalimbali kama matumizi ya zana duni, matatizo ya wadudu waharibifu na uwezo mdogo wa wakulima kutumia mbinu za kisasa za kilimo.

Upandaji miti umekuwa shughuli muhimu ya wakulima wadogo katika H/W ya Njombe. Inakadiriwa kuwa 19,538.31Ha za ardhi zina mashamba ya miti yanayomilikiwa na wakulima wadogo na 10,328.14Ha za mashamba ya miti yanayomilikiwa na umma. Misitu ya asili ina eneo la 1,225.76Ha ikijumuisha msitu wa Iditima (500Ha) ambao unamilikiwa na Serikali Kuu kupitia Wakala wa Misitu Tanzania.

**2.0 TATIZO**

H/W ya Njombe ina utajiri mkubwa wa misitu. Misitu hii hutumiwa kwa mahitaji mbalimbali ya kuni, mkaa, mbao na vifaa vya ujenzi. Jitihada kadhaa zimefanyika kuhifadhi baadhi ya misitu ili kuzuia uvunaji holela wa misitu.

Jamii za H/W ya Njombe zilikumbwa na ukosefu wa soko la uhakika la mbao kutokana na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na madalali wasio waaminifu, bei zisizo za uhakika, uvunaji wa miti michanga na changamoto za ukusanyaji mapato hasa kutokana na kutawanyika kwa vituo vya kuuza na kununua mbao. Ukosefu wa mfumo bora wa soko la mbao ulileta changamoto nyingi. Uvunaji wa miti michanga kutoka kwenye misitu isiyo na uangalizi ulikithiri na kupunguza ubora wa mbao zinazozalishwa na hivyo kuuzwa kwa bei za chini. Kwa mfano, katika Halmashauri hii mbao yenye vipimo vya 2” X 4” iliuzwa kwa kati ya TZS 800/= and TZS 1,500/=, wakati katika masoko mengine nje ya Mkoa wa Njombe bei zilikuwa kati ya TZS 4,500/= na TZS 6,000/=. Hali hii iliwaingiza wakulima wa miti katika wimbi la kudumu la umaskini. Tatizo la pili lilijikita katika barabara mbovu; jambo hili liliendelea kuwa kikwazo kwa wakulima wa miti hasa msimu wa mvua katika kusafirisha mbao kwenda kwenye masoko na kusababisha bei kuwa ndogo hivyo kipato cha wakulima kuendela kuwa duni.

Changamoto hizi zilijidhihirisha kwenye makusanyo duni ya mapato ya Halmashauri. Kwa mfano mwaka 2014, Halmashuri ilikusanya chini ya TZS 540,000/=. Madalali wengi wa mbao walikwepa kulipa ada za mazao ya misitu kama mbao na mkaa. Hii ilisababisha kuongezeka kwa gharama za ufuatiliaji na doria za kuzuia usafirishaji haramu wa mazao ya mbao. Doria iliigharimu Halmashauri TZS 670,000/= kwa siku.

Halmashauri ilikuwa na upungufu mkubwa wa rasilimali watu katika Idara ya Maliasili hivyo kusababisha utoaji duni wa huduma za ugani. Mwaka 2019 Halmashauri ilikuwa na watumishi 8 tu katika idara hii wakati sehemu kubwa ya jamii inategemea upandaji miti. Ikumbukwe kuwa zaidi ya 19,538.31Ha ni misitu inayomilikiwa na wakulima wadogo ambao huhitaji huduma za ugani kwa wakati, za kutosha na endelevu.

**3.0 LENGO**

Sera ya Misitu inasisitiza na kuhimiza upandaji miti sambamba na kuanzisha shughuli mbadala za uzalishaji wa kipato kama motisha katika kujenga uwezo wa kiuchumi kwa lengo la kupunguza umaskini katika jamii za wapanda miti. Kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo, Halmashauri iliunda vyama 5 vya wakulima wa mti katika vijiji vya Matembwe, Ikuna, Nyombo, Ikang’asi na Itambo. Wanachama wa vyama hivi waliwezeshwa vifaa na mitambo ya upandaji miti na kupatiwa mafunzo muhimu. Kati ya vyama vilivyoundwa mojawapo ni “Umoja wa Wapandaji Miti Matembwe” (UWAMIMA) ambacho kilionesha maendeleo chanya na matokeo dhahiri. Umoja huu ulianzishwa mwaka 2009 na kusajiliwa tarehe 22/09/2010 kwa namba ya usajili: S.A 17093 katika Wizara ya Mambo ya Ndani. Malengo mahsusi yalikuwa;

(i) Kuongeza faida za moja kwa moja kwa wapanda miti; wajumbe wa UWAMIMA.
(ii) Kuunda na kuboresha mnyororo wa thamani wa mazao ya misitu na mazao yatokanayo na misitu.
(iii) Kujenga soko ambalo litakuwa kituo kimoja kwa Halmashauri kukusanya mapato, kutoa vibali vya usafirishaji, usajili wa leseni za biashara za mazao ya misitu na kusimika mfumo wa kieletroniki wa risiti za Mamlaka ya Mapato Tanzania.
(iv) Kuongeza ukusanyaji wa ushuru wa Halmashauri na kuboresha utoaji wa huduma.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Mazao ya misitu kama mbao, mirunda na mkaa huchangia kwa kiasi kikubwa kwenye mapato ya Serikali Kuu na H/W ya Njombe. Mapato ya mazao ya miti hukusanywa kutoka kwenye mauzo ya mazao ya misitu, usajili wa wafanyabiashara, faini, vibali vya kisafirisha, na ada za maombi ya kufanya biashara za mazao ya miti. Kwa ujumla, mapato yanayokusanywa kutoka kwenye mbao/magogo ni 58.7% ya mapato yote ya H/W ya Njombe. Ukweli huu ulileta uhitaji wa kuchukua hatua za kuboresha mfumo wa soko la mazao ya misitu. Mikakati iliyotumiwa imejadiliwa kwa kina katika vifungu vilivyopo hapa chini.

Uhamasishaji na uanzishaji wa chama cha wakulima wa miti; mwaka 2009 Halmashauri iliendesha zoezi la uhamasishaji kuhusu uundaji wa vyama vya wakulima wa miti kwa lengo la kuboresha uoteshaji wa miti, ufugaji wa nyuki na uuzaji wa mazao ya miti. Baada ya malalamiko ya miaka mingi juu ya bei za chini za mazao ya misitu kama mbao na mkaa, wakulima wa miti walikubali kuunda vikundi chini ya uwezeshi wa maofisa wa Halmashauri. Hivyo, mwaka 2010 vyama 3 viliundwa vikijumuisha UWAMIMA, Nyombo and Ikuna. Badaye UWAMIMA ndiyo iliyoanzisha soko la mbao la Matembwe. Mwaka 2010 UWAMIMA iliandika katiba yake na kusajiliwa.

Uoteshaji wa miti na ufugaji wa nyuki; baada ya kusajiliwa wanachama wa UWAMIMA walianza shughuli rasmi. Umoja huu ambao ulikuwa na wanachama 74 (37 wanaume na 36 wanawake) uliotesha miti kwenye eneo la 30ha katika 60ha zilizokuwepo na kuanzisha shughuli za ufugaji nyuki. UWAMIMA inamiliki mizinga ya nyuki ya kisasa 250. Shughuli hizi zilihitaji rasilimali za kutosha hivyo wanachama walihamasishwa kuchangia kutoka kwenye vipato vyao duni na kufanikiwa kupata TZS 13,000,000 kwa lengo la kuimarisha umoja wao na kuanzisha soko la mbao.

Kuandaa andiko la mradi; wadau wa maendeleo mbalimbali waliombwa kusaidia uanzishaji wa soko la mbao. Wanachama wa UWAMIMA waliajiri mtaalamu mshauri aliyeandaa andiko la mradi ambalo lilitumwa kwa mashirika yenye uwezo wa kufadhili miradi ya aina hii. Kupitia mbinu hii UWAMIMA ilipata TZS 89,143,953/= kutoka Serikali ya Finland ili kujenga soko la mbao. UWAMIMA iliamua kumiliki ardhi iliyokuwa ya Kijiji, kiasi cha ekari 60 kwa kufanya majadiliano na Serikali ya Kijiji; hatimaye UWAMIMA ilipewa ardhi hii bila malipo (ardhi ambayo ina thamani ya TZS 10,000,000/=) ili kuanzisha soko la mbao.

Ujenzi wa barabara za mlisho; H/W ya Njombe ilichangia utaalamu, ikiwa ni pamoja na upimaji wa maeneo ya barabara na ujenzi wa barabara katika maeneo ya misitu kuelekea kwenye soko la mbao kwa gharama ya TZS 32,000,000/=. Barabara hizi zimeboresha sana usafirishaji wa mbao na mazao mengine ya misitu kutoka mashambani kwenda kwenye soko na hivyo kupunguza gharama kwa kiasi kikubwa.



***Barabara iliyoboreshwa kueleke soko la mbao la Matembwe***

Kutoa mafunzo kwa wanachama wa UWAMIMA; H/W ya Njombe iliwezesha safari za mafunzo ambazo ziliwapatia fursa wanachama wa UWAMIMA kushuhudia na kujifunza uendeshaji wa masoko ya mbao. Safari hizi ziliwatia motisha wakulima wa miti kuanzisha na kuendesha soko lao. Sambamba na hili, Halmashauri iliwezesha wanachama wa UWAMIMA kuhudhuria maonesho kama NaneNane na masoko mengine yaliyopo H/W ya Mafinga, H/Mji wa Mafinga, H/Mji Makambako na masoko mengine.

Uanzishaji wa soko kama kituo cha huduma mbalimbali; biashara ya mazao ya misitu huhitaji uzingatiaji wa sheria na taratibu mbalimbali za Serikali ikiwa ni pamoja na usajili wa biashara ya mazao ya misitu, vibali vya usafirishaji, mapato ya Halmashauri na kodi mbalimbali za Mamlaka ya Mapato Tanzania. Wakulima wa miti sasa wanapata huduma hizi zote kwa soko la mbao la UWAMIMA, Matembwe. Zamani ingewalazimu wakulima, wauzaji na wanunuaji kusafiri kwenda Njombe Mjini (takribani 68km) kupata vibali na nyaraka nyingine za kisheria. Uwepo wa soko la mbao umeongeza idadi ya wakulima wa miti na wafanyabiashara wa mbao katika Vijiji na Kata za jirani na soko la mbao la Matembwe.

Uundaji wa taratibu za soko; licha ya uendeshaji, soko lina mfumo unaoruhusu uingizaji, uhifadhi na utoaji wa bidhaa kwa kuzingatia taratibu mbalimbali zilizoainishwa bayana. Aidha, kuna ada mbalimbali za kutumia huduma za soko.

## 5.0 RASILIMALI

H/W ya Njombe ilitumia rasilimali mbalimbali kufikia mafanikio ya kujenga na kutumia soko la UWAMIMA, Matembwe. Jedwali 1 hapa chini linaonesha rasilimali zilizotumika kupata matokeo na jinsi zilivyopatikana ili kuanzisha soko la mbao la Matembwe.

**Jedwali 1: Rasilimali**

| Na. | Rasilimali | Melezo | Kiasi (TZS) |
|---|---|---|---|
| 01 | Fedha | – Michango ya wafadhili<br>– Michango ya wanachama wa UWAMIMA<br>– H/W ya Njombe (miundombinu)<br>– H/W Njombe (mafunzo) | 89,143,953<br>13,000,000<br>32,000,000<br>1,300,000 |
| 02 | Watu | – Wakulima wa Miti (UWAMIMA) walikuwa na Uongozi na Menejimenti imara na H/W Njombe kupitia idara ya maliasili ilitoa stadi za kitaalam zilizohitajika.<br>– Nguvukazi kutoka wanajamii wa Matembwe. | |
| 03 | Jamii | Jamii katika Kijii cha Matembwe ambapo wanachama wa UWAMIMA wanaishi ilikubali uwepo wa soko katika Kijiji chao | |
| 04 | Vitu | Ardhi ya Kijiji | 10,000,000 |
| | | **Jumla** | **145,443,953** |

## 6.0 MATOKEO

Miundombinu ya masoko hutoa fursa kwa watu waishio katika eneo hilo kununua na kuuza aina mbalimbali za bidhaa. Masoko hutoa nafasi za ajira kwa watu mbalimbali. Wazalishaji wa mashambani huuza mazao yao katika masoko haya na walaji hununua mazao ya kilimo na viwanda kwa matumizi ya nyumbani. H/W ya Njombe na wadau wote wamefanikiwa kufikia malengo ya kaunzisha soko la Mbao la Matembwe kama inavyoelezwa hapa chini.

Uwepo wa Umoja imara na Soko linalotoa huduma; UWAMIMA imekuwa ni chama chenye nguvu kuweza kudhibiti biashara ya mbao kwa kutumia jitihada, utawala na rasilimali zake. Uwepo wake unatoa nafasi sahihi kwa Halmashauri kutokomeza madalali wote wa biashara ya mbao katika Kata ya

Matembwe na kuelekeza faida zote za mazao ya misitu kwa wakulima wa miti na jamii. Soko hili la mbao limeibuka kuwa kituo cha ukusanyaji wa mbao kwa wakulima wa miti wakati uendeshaji wa shughuli za biashara katika soko zipo wazi na zenye ushindani na hivyo kusababisha uwepo wa bei za mazao ya misitu zinazotabirika na kuongezeka.



***Ofisi ya soko la UWAMIMA, Matembwe***

Kuwepo kwa fursa za ajira; kupitia uanzishaji wa soko la mbao, UWAMIMA imeunda nafasi za ajira ya kudumu 6. Kuna nafasi za ajira za muda ambapo zaidi ya watu 80 wameajiriwa katika upakiaji, ushushaji, uchakataji na usafirishaji wa mbao. Zaidi ya hilo, soko hili limeleta ajira zisizo za moja kwa moja katika huduma nyingine kama uuzaji wa vyakula, udereva wa bodaboda na uendeshaji wa maduka madogo kuzunguka eneo la soko.



***Maduka na vijana waliojiajiri katika Soko la Matembwe***

Kuongezeka kwa uzalishaji wa mbao na mapato; Kata ya Matembwe imekuwa eneo linaloongoza kwa uzalishaji wa mbao kutokana na jitihada hii ya UWAMIMA na uwezeshi ambao umeleta urahisi katika uzalishaji na uuzaji wa mbao. Soko hili limepunguza umbali ambao wakulima wa miti walizoea kusafiri kwenda kupata huduma za uuzaji wa mbao kutoka 80km hadi kati ya 5km na 9km. Halmashauri pia imeongeza mapato yake ya misitu kutoka TZS 540,000 mwaka 2014 hadi TZS 231,452,850 mwaka 2018. Mapato yote ya Halmashauri yameongezeka kutoka TZS 950,586,000 mwaka 2013 hadi TZS 1,671,823,012 mwaka 2018/2019. Uwepo wa soko la mbao la UWAMIMA umeziba mianya ya ukwepaji kodi na tozo nyingine za mazao ya misitu.



***Malori yakipakia mbao katika Soko la Matembwe***

Kuongezeka kwa uchakataji wa mbao; takwimu za mwaka 2013 zinaonesha kuwa wastani wa thamani ya mbao ambazo zinachanwa na viwanda vidogo vya kuchana mbao katika H/W ya Njombe kwa mwezi ni TZS 7,055,484,250.51 na kuleta thamani ya TZS 84,466,580,000 kwa mwaka. Ujazo wa jumla wa mbao zilizochanwa kwa mwaka ni 139,502.28m$^3$ na ujazo wa mirunda inayozalishwa kwa mwaka ni 3039.36m$^3$ ikiwa na jumla ya thamani ya TZS 1,512,828,640. Halmashauri hukusanya wastani wa jumla ya TZS 231,452,850 kwa mwaka kutoka mazao ya miti. Thamani iliyobaki ya TZS 2,897,715,258/= kutoka mazao ya miti hurudi kwa wakulima wa miti kama kipato.



***Mazao ya miti katika soko la Matembwe***

Kuimarika kwa taarifa za bei na mawasiliano; soko la UWAMIMA limerahisisha mawasiliano ya taarifa za bei ikijumuisha kutambua mahitaji na mbao zilizopo kwenye masoko mengine nje ya H/W ya Njombe. Hali hii huleta uhakika wa bei na husaidia maamuzi sahihi ya uuzaji wa mbao. Aidha, soko lina kamati kabambe ambayo hufanya maamuzi kila siku kuhusu masuala yote ya masoko. Soko la Matembwe limekuwa kituo cha kujifunza; kwa mfano wakulima wa miti kutoka H/Mji wa Makambako walitembelea soko hili kwa sababu za kujifunza. Jitihada hii imeboresha utunzaji wa mazingira na takwimu za mazao ya misitu katika H/W ya Njombe.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

H/W ya Njombe na UWAMIMA kwa pamoja zimeweka mikakati mbalimbali ya kuhakikisha jitihada hii inaendeleza faida zake na kuongeza matokeo yake kwa miaka mingi ijayo na kwa jamii pana. Mikakati hiyo ni pamoja na;

(i) Soko linaendeshwa na UWAMIMA kwa misingi ya kidemokrasia. Timu ya Menejimenti ya UWAMIMA imedhamiria kuendelea kuwatambua wanunuzi wa mbao na wakulima wa miti ili waendelee kutumia soko na kufaidika kwa ongezeko la thamani na matokeo.

(ii) UWAMIMA ina mipango ya kuwezesha na kuongeza ajira ya vibarua kwa jamii za jirani na kulifanya soko sehemu ya biashara za aina mbalimbali.

(iii) Shughuli za Menejimenti ya UWAMIMA zimelenga kulifanya Soko la Matembwe kuwa soko la mfano katika Nyanda za Juu Kusini.

(iv) UWAMIMA ina mipango ya kununua na kusimika mitambo mikubwa ya uchakataji wa mbao na mzani wa kupima uzito wa malori ili kuwa na bei za haki za ushafirishaji.

(v) Wataalamu wa H/W ya Njombe wataendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Soko la UWAMIMA katika shughuli zake za kila siku na kujenga uwezo wa kamati ya soko kuhusu menejimenti, utunzaji wa taarifa na ufanyaji wa maamuzi.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

H/W ya Njombe na UWAMIMA zimefanikiwa kupata faida za Soko la Mbao la Matembwe kutokana na sababu mbalimbali. Sababu ya kwanza ni utayari wa wanachama kujitoa kikamilifu kwa kuchanga TZS

13,000,000 ikidhihirisha kuwa wakulima hawa wa miti wana umoja na azma thabiti. Sababu ya pili ni uhakika wa Halmashauri katika kutoa huduma za ugani kwa wakulima wa miti na kwa mbinu shirikishi. Tatu, maamuzi bora ya usimamizi wa fedha ambapo fedha zinazokusanywa kutoka soko la Matembwe zinatumiwa kwa usahihi na UWAMIMA na Halmashauri hutenga 12% ya makusanyo yote na kupeleka Kata ya Matembwe kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Pamoja na sababu zote hizi, mazingira asilia, hali ya hewa na jamii yenye watu wanaojituma ndio siri kuu ya kufanikiwa kwa jitihada ya uanzishaji wa soko la mbao.

# HALMASHAURI YA MJI WA MAKAMBAKO

**UPIMAJI SHIRIKISHI WA MAKAZI YASIYO RASMI**




***Uzoefu wa Kata ya Maguvani***

**1.0 UTANGULIZI**

Halmashauri ya Mji wa Makambako ni mojawapo ya Halmashauri 6 za Mkoa wa Njombe iliyoanzishwa Julai mwaka 2012. Kabla ya mwaka 2012, Mji wa Makambako ulikuwa Tarafa mojawapo ya Wilaya za Njombe kwenye Mkoa wa Iringa. Mara baada ya kuundwa kwa Mkoa wa Njombe, Tarafa ya Makambako ilipandishwa hadhi kuwa Halmashauri ya Mji wa makambako. Mji huu upo katika makutano ya barabara za Tanzania – Zambia na Dar es Salaam - Songea. H/Mji wa Makambako ina Kata 12, Mitaa 54, Vijiji 14 na Vitongoji 67. Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, H/Mji wa Makambako ina watu 93,827 na ukuaji wa idadi ya watu ya 0.31 kwa mwaka. Halmashauri ina eneo la 883.7 Km$^2$ ambazo 60% ya eneo lote ni la Vijiji na 40% eneo la Mjini likiwa na 15% iliyopimwa.

Joto katika Mji wa Makambako huwa kati ya 17$^0$C msimu wa Juni hadi Aogosti na 22$^0$C kati ya Novemba and Desemba. Mazingira ya Mji huu yanaambatana na pepo kali zivumazo kutoka Kusini Mashariki na kuleta hali ya vumbi. Kuna msimu mmoja tu wa mvua ambazo hunyesha kuanzia Desemba hadi Machi kwa wastani wa 600mm - 1000mm kwa mwaka. Mji wa Makambako unakua kwa kasi kutokana na uwepo wa shughuli mbalimbali za kiuchumi zinazofanywa na wenyeji.




***Ramani ya H/Mji wa Makambako***

**2.0 TATIZO**

Tangu mwaka 1969 Mji wa Makambako ulikuwa umepimwa kwa kutumia mfumo wa kadastrali, hata hivyo makazi yaliyokuwa yamepimwa yalikuwa kwenye eneo dogo kulingana na idadi ya watu na uhitaji mdogo wa viwanja enzi hizo. Maeneo ya zamani yaliyokuwa yamepimwa ni Uhuru, Sokoni, Mwembetogwa na Mjimwema ambayo ndiyo yanaunda eneo la kati la kibiashara la sasa. Zoezi la kupima makazi ya zamani lilianzishwa na TAZARA kwani haingewezekana kuwekeza katika miradi mikubwa kwenye ardhi ambayo haijapimwa. Michoro ya Mipango Miji ya awali iliyoandaliwa mwaka 1969 ni ya maeneo 5 yaani Mwembetogwa, Ubena, Uhuru, Mizani na Kahawa na vipimo 4 vya Kadastrali vya Mwembetogwa, Ubena, Uhuru, Mizani na Kahawa. Kwa bahati mbaya zoezi hili halikuwa endelevu hivyo kusababisha kuchipuka kwa makazi yasiyopangwa kutokana na upimaji ardhi wa taratibu ikilinganishwa na ukuaji wa mahitaji ya viwanja.

Mwaka 1983, Mji Mdogo wa Makambako uliandaa Mpango Kabambe ambao ulitumika kama msingi wa kuendeleza mji. Mpango huu ulizingatia utarajibu wa jumla wa upangaji miji hivyo kushindwa kukidhi mahitaji ya uendelezaji mji kwani umma haukuhusishwa wala kushirikishwa katika mchakato. Hali hii ilichangia kwa kiasi kikubwa uharibifu wa haraka wa mazingira, afya na ustawi wa wakazi.

Kasi ya ukuaji wa Mji ilizidi uwezo wa maafisa, fedha na miundombinu kudhibiti maendeleo na matumizi ya ardhi. Kutokana na mapungufu haya yaliyojikita ndani ya Mpango Kabambe, kulihitajika utafiti wa mbinu mpya wa kudhibiti maendeo ya Mji. Mwaka 1992, mpango mpya wa upangaji na usimamizi wa ukuaji wa miji ulianzishwa Tanzania. Mpango huu ulileta mbinu ambayo masuala ya mazingira huainishwa kwanza na wadau kutoka sekta ya umma na binafsi ndipo kwa kuzingatia changamoto za kimazingira zilizoibuliwa mikakati na mipango kazi huandaliwa kuzitatua.

Mwaka 1999, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilibaini kuwa changamoto za udhibiti wa ukuaji wa Mji zilizoukumba mji mdogo wa Makambako ilihitajika mbinu mpya ambayo inaongozwa na wadau, inazingatia mahusiano kati ya mazingira na maendeleo na inasisitiza ushiriki wa sekta na wakala mbalimbali wa uratibu. Kuanzishwa kwa Mpango wa Maendeleo Endelevu ya Miji kulitoa fursa kwa Mji wa Makambako kutumia rasilimali, ubunifu na vitendea kazi kwa kushirikiana na wakazi wa Kata ya Maguvani kupima ardhi na kuwa na matumizi bora ya ardhi.

Utaratibu wa kawaida ni kuwa kila panapotokea upimaji wa ardhi mijini, Serikali huwapa fidia wamiliki wa asili. Kutokana na ukuaji wa kasi wa idadi ya watu na mji wa Makambako; hadi 2005 Serikali ilishindwa kutimiza jukumu la kupima maeneo na kulipa fidia. Matokeo yake mji ukawa haujapangwa, kuongezeka kwa makazi yasiyo rasmi na kuharibu sura ya mji. Ukuaji wa makazi yasiyo rasmi ulipunguza uwezekano wa serikali kujenga miundombinu ya huduma kama elimu, viwanja vya michezo, majengo ya umma, makaburi, maeneo ya wazi, nyumba za ibada na barabara. Kutopangwa kwa makazi kulileta changamoto za kiafya na viwango vya maisha masuala ambayo ni kinyume na Sheria ya Mipango Miji iliyopitiwa mwaka 2018.

Huduma za mipango miji ziliathirika sana kutokana na ukosefu wa fedha za ulipaji wa fidia, uandaaji wa michoro na upimaji wa ardhi. Sheria ya Ardhi Na. 4 ya mwaka 1999 kifungu cha 1(a) kinaeleza "kutambua kuwa ardhi yote ya Tanzania ni ya umma na imekabidhiwa kwa Rais, kama mdhamini kwa niaba ya wote". Hata hivyo, ukweli ni kuwa, hakuna ardhi ambayo haijamilikiwa. Ardhi yote ipo chini ya umiliki wa wenyeji, wengi wakimiliki kimila. Kupanga na kupima ardhi inayomilikiwa kimila ulipaji wa fidia ni lazima.

Tatizo la pili lilikuwa upungufu wa watumishi; Mji wa Makambako ulikuwa mojawapo ya Tarafa za H/W ya Njombe, hivyo usimamizi wa karibu wa shughuli za mipango miji haukuwepo kutokana na umbali (65km) kutoka makao makuu ya Wilaya. Hali hii ilizidi kuwa mbaya kutokana na idadi ndogo ya watumishi waliozidiwa na majukumu. Tatizo jingine lilikuwa ukuaji wa kasi wa mji kutokana na asili yake na mahali ulipo. Mji upo kwenye barabara kuu za Dar es Salaam, Makambako Songea, Msumbiji na Dar es Salaam, Makambako, Mbeya, Zambia na Afrika Kusini ambapo watu wengi kutoka maeneo mbalimbali huingia kwa malengo ya biashara na uwekezaji.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la H/Mji wa Makambako lilikuwa kuboresha makazi ya mjini kwa kupanga, kupima ardhi na kuongeza hadhi ya makazi yasiyo rasmi. Halmashauri ililenga kuhamasisha jamii kuhusu umuhimu wa mipango miji na ushiriki wa wadau katika kumiliki na kupima ardhi. Hatimaye jitihada hii ingeboresha matumizi ya ardhi, makazi na uwekezaji.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

H/Mji wa Makamabako ilitumia mikakati mbalimbali kupata matokeo. Mikakati hii kwa pamoja imeunda modeli ya Maguvani ya Uchoraji na Upimaji Miji. Maguvani ni moja ya Kata 12 za H/Mji wa Makambako

yenye wakazi 1,500 ambapo kuna wanaume 427, wanawake 497 na watoto 576. Umbali kutoka katikati ya Mji ni 5km. 90% ya ardhi ya Kata ya Maguvani ni ardhi iliyo wazi ikiambatana na idadi ndogo ya watu na uwekezaji. Utekelezaji wa jitihada hii ulitumia mikakati ambayo imedadavuliwa hapa chini.

Ushiriki wa wadau; shughuli za upangaji na upimaji wa miji ni za gharama sana kwa sababu ya ukweli kuwa kwa Tanzania shughuli hizi huambatana na ulipaji wa fidia. Kwa sasa hakuna ardhi ambayo haina mmiliki; kila kipande cha ardhi kinamilikiwa kimila au kwa namna nyingine nyingi. Hali hii huleta ugumu katika upimaji wa ardhi mijini kwa sababu sheria ya ardhi Na.4 ya mwaka 1999 kifungu 1(1) (f) inasema *"ichukuliwe kuwa uhitaji wowote wa ardhi una thamani yake na thamani hiyo lazima izingatiwe katika miamala ihusuyo uhitaji huo; (g) kulipa fidia yote, ya haki na ya mara moja kwa mtu yeyote ambaye haki yake ya umiliki au umiliki wa muda mrefu wa ardhi au utumiaji wa kimila wa ardhi unasitishwa au kuingiliwa na dola na kuwepo hasara kwa wamiliki chini ya sheria hii au ardhi imechukuliwa chini ya sheria ya umiliki wa ardhi".* Katika ukweli huu, kati ya mwaka 2007 na 2015 Halmashauri ilichukua ardhi kutoka kwa wenyeji ili kujenga Shule ya Sekondari ya Kata ya Maguvani na kuahidi kulipa fidia. Halmashauri haikuweza kutekeleza ahadi hii kutokana na ukosefu wa fedha. Mwaka 2016 Halmashauri iliamua kutumia mbinu shirikishi inayoruhusu kugawana gharama. Halmashauri ilichagua kushirikiana na wadau, wamiliki wa kimila wa ardhi na wanasiasa kutimiza azma ya kupima ardhi.

Mikutano ya Wadau; ilikuwa muhimu kuitisha mikutano kati ya wamiliki ardhi wa kimila (wanajamii wa Kata ya Maguvani) na watumishi wa idara ya ardhi. Madiwani walialikwa na mojawapo wa madiwani ni Mhe. Conrad Mfikwa wa Kata ya Maguvani ambaye aliongoza jitihada hii. Malengo ya mikutano hii yalikuwa kujenga uelewa na kuwapatia wenyeji elimu ya kutosha ya umuhimu wa upimaji ardhi katika maeneo ya thamani ya ardhi, maboresho ya mitaa, upatikanaji wa barabara zinazopitika na uwepo wa nafasi kwa ajili ya taasisi za huduma. Wadau wote walielezwa kwa kina kuwa kupitia umiliki wa hati za viwanja, wamiliki watakuwa na sifa za kupata mikopo kutoka taasisi za fedha.



***Mhe. Conrad Mfikwa (Diwani) na Wafaidika wa Maguvani***

Mapendekezo ya kuchangia gharama za upimaji; nadharia ya kuchangia gharama za upimaji ardhi ilibuniwa ha Halmashauri kutokana na ukweli dhahiri kuwa Halmashauri haikuwa na fedha za fidia, uchoraji ramani na upimaji wa ardhi. Hali hii ilileta uhitaji wa kutumia mbinu shirikishi ambapo jamii ingetoa ardhi, Halmashauri ingepima na hatimaye kugawana viwanja vilivyopimwa kwa wamiliki wa kimila kupata 60% na Halmashauri 40%. Kwa mfano, kama eneo la mmiliki wa kimila likitoa viwanja 10 vilivyopimwa, basi mmiliki mwenyeji atapata viwanja 6 (vyenye hati) na Halmashauri itachukua viwanja 4. Utaratibu huu unafidia ardhi ya mmiliki mwenyeji na huipatia Halmashauri ardhi kwa matumizi mengine. Baada ya mikutano hii, mihutasari na majina ya washiriki yaliandikwa kwa lengo la kuhifadhi kumbukumbu na kuthibitisha kuwa wanajamii wamekubali rasmi na utayari wao wa kuachia ardhi yao halali. Baada ya kukubalika kwa pendekezo hili Halmashauri iliendesha zoezi la ukaguzi kuainisha

ukubwa wa ardhi ya kila mmiliki. Zoezi hili lilifanyika kwa lengo la kukazia makubaliano ya kuchangia gharama kwa uwiano wa 60% na 40% wa viwanja vilivyopatikana.

Kutumia wanafunzi wa mafunzo kwa vitendo; Halmashauri iliwatumia wanafunzi wa Chuo cha Ardhi Morogoro waliokuwa kwenye mafunzo kwa vitendo kupanga na kupima ardhi katika Kata ya Maguvani. Mbinu hii ilipunguza gharama na muda. Kimsingi, upimaji wa ardhi ni zoezi la gharama kubwa kwani linahitaji mkataba na kampuni za wataalamu, taratibu ngumu za zabuni na changamoto kadhaa za ufuatiliaji. Mchakato wote wa Maguvani ulitekelezwa na wanafunzi 12 ambao walishiriki kikamilifu kwani ilikuwa sehemu muhimu ya mafunzo yao. Zoezi lote lilisimamiwa na wakufunzi 2 kutoka Chuo cha Ardhi Morogoro. Mradi ulikamilika kama ulivyopangwa na ulichukua muda mfupi.

Upimaji wa viwanja kwa awamu; Halmashauri iliamua kuugawa mradi wa upimaji viwanja kwa awamu mbili ambapo awamu ya kwanza ilikamilisha upimaji wa viwanja 291 katika eneo lenye ekari 43.14. Sababu ya kuanza na viwanja hivi 291 ilikuwa kutoa fursa kwa wamiliki wote ambao walikuwa na maeneo yaliyokamilika kuzalisha viwanja ambavyo vingeruhusu mgawanyo wa 60% kwa 40% kama ilivyo kwenye makubaliano. Awamu ya pili ilijikita kwa wale ambao walikuwa na maeneo madogo yanayotoa kiwanja kimoja au viwili na kutokuwepo uwezekano wa kugawana viwanja; hawa walitakiwa kulipia gharama za upimaji.

## 5.0 RASILIMALI

Halmashauri ililazimika kushirikiana na jamii ili kuchangia gharama za kupanga na kupima mji. Jamii ilichangia kwa nguvukazi na kwa hiari kwa kuachia 40% ya ardhi ichukuliwe na Halmashauri kwa matumizi mengine. Halmashauri ilichangia utaalamu na fedha. Jedwali lililopo hapa chini linaonesha rasmali fedha.

**Jedwali 1: Rasilimali**

| Na. | Rasilimali | Thamani TZS |
|---|---|---|
| 1 | Wanafunzi 12 na wakufunzi 2 wakitumia kifaa cha *Total Station* | 14,000,000/= |
| 2 | Vifaa vya ujenzi (saruji na nondo) | 4,000,000/= |
| 3 | Shajala | 3,000,000/= |
| 4 | Usimamizi (H/Mji wa Makambako) | |
| 5 | Ukaguzi wa Ardhi (H/Mji wa Makambako) | |
| 6 | Maandalizi ya vigingi na kuvigawa (H/M ya Makambako) | |
| | JUMLA | 21,000,000/= |

## 6.0 MATOKEO

Jitihada ya H/Mji wa Makambako ya kupanga na kupima matumizi ya ardhi kwa namna shirikishi ilifanikiwa na kuitia hamasa jamii. Jitihada hii imeleta matokeo mengi yaliyo dhahiri kama yanavyochambuliwa hapa chini.

Uzalishaji wa viwanja 291 vilivyopimwa; mradi huu umefanikiwa kupima ekari 43.14 ambazo zilikuwa zikimilikiwa na wanajamii kimila na kuzalisha viwanja 291 vilivyopimwa ikiwa ni pamoja na viwanja vya matumizi mbalimbali ya umma kwa gharama ya TZS 21,000,000 tu. Kama mradi huu usingetekelezwa kwa mbinu shirikishi, mradi ungeigharimu Halmashauri TZS 380,000,000. Viwanja vilivyopimwa vina vigingi vilivyotengenezwa kwa saruji na nondo ili kuonesha namba na alama za kiwanja. Vigingi hivi hutumika kuonesha mipaka halisi kati ya viwanja.




***Kigingi kikionesha mipaka ya Shule ya Sekondari ya Maguvani***

Kuongezeka kwa thamani ya ardhi; thamani ya ardhi imeongezeka kwa kiasi kikubwa. Kabla ya jitihada hii, thamani ya ekari moja (4,900m$^2$) ilikuwa TZS 500,000, lakini mara baada ya upimaji wa ardhi hii thamani ya kiwanja chenye 500m$^2$ imepanda hadi TZS 2,500,000. Halmashauri inajivunia mafanikio haya kwa sababu mradi huu umejenga uwezo wa wamiliki wa ardhi kumiliki kisheria viwanja vilivyopimwa na hivyo kuwapatia fursa ya kupata mikopo katika taasisi za fedha.

Kumalizika kwa ulipaji fidia na migogoro ya ardhi; Halmashauri imefanikiwa kulipa fidia kwa wanajamii walioachia maeneo yao kwa ajili ya matumizi ya umma kama ujenzi wa shule na makao makuu ya Halmashauri. Fedha za kulipa fidia zilitokana na 40% ya viwanja ilivyopata baada ya upimaji. Halmashauri iliuza viwanja hivi na kupata fedha za kulipa fidia. Pamoja na hili, kupitia jitihada hii Halmashauri imeweza kutatua migogoro ya ardhi iliyohusu viwanja kugawiwa kwa wamiliki zaidi ya mmoja. Migogoro 19 ya ardhi ilitatuliwa.

Ardhi kwa ajili ya huduma za umma; katika Kata ya Maguvani, Halmashauri imefanikiwa kumiliki ardhi kwa matumizi ya umma kama makaburi, zahanati, shule ya chekechea na sekondari. Viwanja hivi vina ukubwa wa 1896m$^2$, 1293m$^2$ na 3740m$^2$ kwa ajili ya majengo ya umma, 1479m$^2$ kwa ajili ya shule ya chekechea/msingi/sekondari, 4581m$^2$ kwa ajili ya zahanati, 2217m$^2$ eneo la wazi na 3670m$^2$ eneo la maziko.



***Makazi yaliyopangwa na kupimwa katika Kata ya Maguvani***

Uwezeshi wa kupata Hati za Viwanja; Halmashauri iliwezesha zoezi la kuwapatia hati za viwanja wamiliki wote. Hati ni muhimu kwa uhakika wa umiliki, ongezeko la thamani na kuaminika kwa wakopeshaji. Mradi huu umepandisha mapato ya Serikali kwani wamiliki wa viwanja sasa wanalipa kodi ya ardhi. Tokeo jingine kuu ni kuwepo kwa makazi rasmi na yaliyopangwa katika Kata ya Maguvani ambayo imekuwa ya mfano kwa Kata nyingine ambazo hazijapimwa katika Mji wa Makambako. Kwa upande wa

makundi maalumu, wanawake na vijana wamefaidika kumiliki viwanja vyenye hati hivyo kuongeza hadhi yao na uhuru wa kiuchumi.



***Wafaidika wa Kata ya Maguvani (wanawake na vijana)***

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

H/Mji wa Makambako imebuni mikakati mbalimbali ya kuleta uendelevu katika sekta ya mipango miji. Halmashauri ina mpango mkakati wa kushirikiana na wadau wengine kupanga na kupima Kata zote za mjini kwa kutumia Modeli ya Maguvani. Wakati jitihada hii ikihakikiwa, Halmashauri ilikuwa kwenye hatua za mwisho za kutumia Modeli ya Maguvani katika Kata za Mlowa na Majengo. Mkakati wa Halmashauri ni kushirikiana na wadau wa Kata ambazo hazijapimwa na kutumia mbinu ya Maguvani.

Ili kupata fedha zaidi za kuendesha mazoezi ya mipango miji na upimaji, Halmashauri ina mpango wa kujenga soko la kimataifa. Eneo la soko limetengwa na wamiliki wa ardhi kupatiwa fidia. Inatarajiwa kuwa wawekezaji kutoka nchi mbalimbali watavutiwa na kuungana na wawekezaji wa ndani katika soko la Mji wa Makambako.

Halmashauri ina lengo la kupima ardhi yote na imeelekeza ujenzi wote mpya ufanyike baada ya kuwa na mpango wa kiwanja, michoro na kibali cha ujenzi. Uamuzi huu unalenga kutokomeza kupanuka kwa makazi yasiyo rasmi. Pamoja na hili, Halmashauri imejipanga kuboresha makazi yote yasiyo rasmi kwa kupima, kuweka vigingi na kufungua barabara za mitaa.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Kufanikiwa kwa jitihada hii kumetokana na siri na ubunifu kadhaa. Ushiriki wa jamii katika mchakato mzima na uchangiaji wa gharama kati ya Halmashauri na Jamii ni siri mojawapo. Hata hivyo, hii ilitokana na uhamasishaji fanisi pamoja na utoaji wa elimu kuhusu mipango miji na upimaji shirikishi. Siri nyingine ya kipekee ni uongozi na utawala wenye kutia hamasa wa Mkurugenzi wa Mji (Bw. Paulo Malala), uelewa wa Mwenyekiti wa Halmashauri (Mhe. Conrad H. Mfikwa) na kujituma kwa dhati kwa watumishi wa Idara ya Ardhi ya Halmashauri.

Siri nyingine ni kuingia katika mikataba kati ya Halmashauri na wamiliki wa ardhi ili kugawana viwanja vilivyopimwa, matumizi ya wanafunzi wa masomo kwa vitendo kutoka Chuo cha Ardhi Morogoro na kuwapatia hati wamiliki wa viwanja vilivyopimwa.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO

## UWEZESHI WA WATOTO KUTOKA JAMII ZA WAFUGAJI KUPATA ELIMU YA MSINGI



*Uzoefu wa Shule ya Msingi Partimbo*

**1.0 UTANGULIZI**

H/W ya Kiteto ni mojawapo ya Halmashauri 8 za Mkoa wa Manyara, iliyoanzishwa mwaka 1984 ikiwa 220km kutoka makao makuu ya Mkoa wa Manyara - Babati. Halmashauri hii inapakana H/W za Simanjiro upande wa Kaskazini, Kilindi upande wa Mashariki, Gairo na Kongwa upande wa Kusini na Chamwino na Chemba upande wa Magharibi. Halmashauri ipo kwenye Latitudo $40^{0}31'$ na $60^{0}3'$ Kusini na Longitudo $36^{0}15'$ na $37^{0}25'$ Mashariki ikiwa na eneo la 16,685$km^2$ ambalo 3,800$km^2$ hutumika kwa shughuli za kilimo, 12,322$km^2$ kwa mifugo na wanyama wa porini, 560$km^2$ ni misitu na 203$km^2$ maji.

Halmashauri ina eneo lenye ukame wa wastani. Hali ya joto ina wastani wa 22°C huwa na joto miezi ya Julai, Agosti, Septemba, Oktoba na Novemba na baridi miezi ya Machi, Aprili, Mei na Juni. Pamoja na kuwepo kwa mabadiliko katika unyevu wa hewa, Halmashauri hupata wastani wa mvua kati 350mm - 700mm kwa mwaka. Kuna msimu mmoja tu wa mvua ambao huanza Januari hadi Mei.

Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, H/W ya Kiteto ina watu 244,669, kati yao 120,233 ni wanaume na 124,436 ni wanawake na ongezeko la 3.2% kwa mwaka. Makabila makuu ni Wamasai (32%), Wagogo (27%), Warangi (18%) na Wanguu (2.6%). Makabila mengine yanaunda 20.4% ya watu wote. Halmashauri imegawanyika katika Tarafa 7, Kata 23 na Vijiji 63.

Shughuli kuu za kiuchumi ni kilimo na ufugaji. Takribani 90% ya wakazi hushughulika na ufugaji na 10% hufanya shughuli nyingine za kiuchumi kama biashara, viwanda vidogo na ufugaji nyuki. H/W ya Kiteto ndiyo yenye mifugo mingi zaidi mkoani Manyara.

H/W ya Kiteto ina shule 90 za msingi na 18 za sekondari. Kati ya shule 90 za msingi, 87 ni za serikali na 3 ni za binafsi. Idadi ya walimu wanaotakiwa ni 1,160, hata hivyo kwa sasa kuna walimu 695 (406 wanaume na 289 wanawake), ikiashiria upungufu wa 40.08%. Halmashauri ina madarasa 467, madawati 14,423 na nyumba za walimu 211.

Tangu kuanzishwa kwa mpango wa elimu bure mwaka 2016, kumekuwa na ongezeko kubwa la wanafunzi wanoandikishwa shule katika Halmashauri hii. Katika shule za msingi, wanafunzi walioandikishwa waliongezeka kutoka 39,655 (wavulana 19,906 na wasichana 19749) mwaka 2016 hadi 46,410 (wasichana 23,516 na wavulana 22,894) mwaka 2017; ongezeko la 14.6%. Takwimu za Novemba mwaka 2018 zinaonesha wanafunzi walioandikishwa shule za msingi walikuwa 51,049 ikilinganishwa na idadi ya wanafunzi 46,410 mwaka 2017.

Shule ya Msingi Partimbo ni mojawapo ya shule maalumu katika Halmashauri ikiwa na wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia. Pia, shule ina mpango maalumu wa kufundisha wanafunzi ambao walinyimwa fursa na wazazi ya kuhudhuria shule kutoka katika jamii za wafugaji. Mwanzoni, shule hii ilijengwa kama shule ya bweni ya wasichana kwa msaada wa Serikali ya Japani. Hata hivyo, tangu mwaka 2017 shule ilianza kupokea wavulana na wasichana kama wanafunzi wa bweni kufuatia jitihada ya Halmashauri na Mkuu wa Wilaya ya kuwezesha watoto wote wenye umri wa kwenda shule kutoka katika kaya za wafugaji kuandikishwa ili kupata elimu ya msingi.




***Shule ya Msingi Partimbo ilifadhiliwa na Serikali za Tanzania/Japani***

## 2.0 TATIZO

Shule ya Msingi Partimbo ipo katika Kata ya Partimbo ambayo ina shule za msingi 8 katika Vijiji 4. Kata hii ina wanfunzi wa shule za msingi wapatao 4,580 na ndio Kata yenye idadi kubwa ya wanafunzi. Shule ya Msingi Partimbo ni ya tatu kwa uandikishaji katika Kata. Tangu mwaka 2015 kumekuwa na ongezeko katika uandikishaji kutoka wanafunzi 110 hadi 651 Novemba 2018.

Pamoja na kuongezeka kwa uandikishaji katika kipindi cha miaka 4, kumekuwa na utoro kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo mimba na shughuli za nyumbani. Utoro kutokana na kazi za nyumbani ulifikia wanafunzi 226 (wavulana 171 na wasichana 95) mwaka 2016, 397 (wavulana 224 na wasichana 173) mwaka 2017 na 690 (wavulana 203 na wasichana 487) mwaka 2018. Kwa upande mwingine, utoro kutokana na mimba ulifikia wasichana 22 (2016), 8 (2017) na 10 (2018).

**Jedwali 1: Takwimu za Mimba Shule za Msingi na Sekondari**

| Mwaka | Shule za Msingi | | | | Shule za Sekondari | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jumla | Mahakama | Uchunguzi wa Polisi | Hukumu | Jumla | Mahakama | Uchunguzi wa Polisi | Hukumu |
| 2016 | 22 | 2 | 12 | 8 | 85 | - | 61 | 24 |
| 2017 | 8 | 4 | 3 | 1 | 50 | 12 | 28 | 10 |
| 2018 | 10 | 3 | 5 | 2 | 66 | 20 | 28 | 6 |

Kuwatumia kuchunga mifugo ni mojawapo ya sababu za utoro kwa wanafunzi wengi, hasa wavulana. Kwa familia za kimasai uchungaji wa mifugo ni shughuli ya watoto wenye umri wa miaka 5 na kuendelea ambao pia ndio umri wa kupata elimu ya msingi. Kata ya Partimbo ni mojawapo ya Kata zenye eneo kubwa na huwa na changamoto kwa watoto kwani hulazimika kutembea umbali mrefu kutoka nyumbani kwenda shule. Kwa mfano, watoto wanoishi Vitongoji vya Napilukunya na Porikwapori walilazimika kutembea zaidi ya 20km (kwenda na kurudi ni 40km) kwenda shule za msingi za Kimana na Mbigiri. Umbali huu mrefu uliwakatisha tamaa watoto kuhudhuria masomo hasa msimu wa masika.

## 3.0 LENGO

Lengo kuu la H/W ya Kiteto lilikuwa kuboresha huduma na miundombinu ya elimu katika jamii za vijijini hasa jamii za wafugaji. Malengo mahususi yalikuwa;

(i) Kuongeza uandikishaji wa watoto wenye umri wa kwenda shule.
(ii) Kutoa fursa kwa watoto kutoka familia za wafugaji kuandikishwa, kupata elimu bora na kuhitimu elimu ya msingi.
(iii) Kuweka mazingira bora ya kujifunza kwa ajili ya wanafunzi wa shule za msingi kwa kujenga madarasa na mabweni na kuwapatia vitanda na magodoro.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Mwaka 2016, Mkuu wa Wilaya alitembelea Shule ya Msingi Partimbo na kubaini kuwa kulikuwa na mabweni ambayo hayakuwa yanatumika na yalikuwa na uwezo wa kuchukua wanafunzi wengi zaidi. Mkuu wa Wilaya alikuwa anafahamu vizuri tatizo la watoto wengi wenye umri wa kwenda shule katika maeneo mbalimbali Wilayani kutokwenda shule kutokana na kukosekana kwa shule karibu na vijiji vyao, ndoa za utotoni na kutumika kwa watoto kama wachungaji wa mifugo. Alipendekeza shule ya msingi Partimbo itumike kwa ajili ya watoto waliopo katika vijiji vya mbali.

Mkuu wa Wilaya akishirikiana na Maafisa Maendeleo ya Jamii alichukua jukumu la kuongoza kampeni ya kuongeza uelewa wa wazazi katika Kata zote 23 ili wawaandikishe watoto wao katika elimu ya msingi. Jamii za wamasai zilishirikishwa kikamilifu kwani wanajamii walifahamu kaya ambazo zinawaficha watoto wenye umri wa kwenda shule. Kwenye hatua za awali Polisi walitumika kuwachukua watoto wenye umri wa shule kwa nguvu na kuwahamishia kwenye shule za msingi za bweni.

Afisa Elimu wa Wilaya (Elimu ya Msingi) na Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Partimbo walishiriki kikamilifu katika mpango huu na walihusika na taratibu za kupokea na kuwalea watoto walioletwa toka vijiji mbalimbali. Viongozi wa Kikabila (*Laigwanan)* na wajumbe wa mabaraza ya vijiji walishirikishwa katika hatua za awali za mpango huu mwaka 2016 ili kupata ridhaa yao na kufanya mchakato wa kuchukua watoto wenye umri wa kwenda shule uwe mwepesi. Halmashauri ilichukua jukumu muhimu la kutoa fedha za kununua magodoro 84 na kukarabati mabweni ya wasichana na wavulana ili kukabiliana na ongezeko la uandikishaji.

Baraza la Madiwani lilipitisha TZS 2,500,000 zitumike katika kuboresha mabweni, ununuzi wa vitanda na magodoro na ujenzi wa bwalo. Mganga wa Wilaya alisaidia kusajili wanafunzi wote katika skimu ya bima ya afya ili kuweza kuwapatia kwa urahisi huduma za afya. Mratibu wa Elimu Kata alisimama imara kuhakikisha walimu wanawapatia wanafunzi elimu stahiki na bora.

Halmashauri ilitumia mikakati mbalimbali kubadili mitazamo ya familia za Wamasai hadi kuwaruhusu watoto wao kuachana na shughuli za uchungaji wa mifugo na kuhamia katika mabweni ya Shule ya Msingi Partimbo.

(i) Kushirikisha na kukubaliana na viongozi wa vijiji wa kikabila (*Laigwanan*) katika jamii za Wamasai.
(ii) Kuainisha kaya zenye watoto wenye umri wa kwenda shule kwa kutumia wanajamii wenye taarifa za kaya/familia zinazoficha watoto. Jumla ya watoto 167 waligundulika na kupelekwa shule.
(iii) Kutembelea nyumba hadi nyumba na kuwasaka watoto wenye umri wa kwenda shule kwa kutumia taarifa zilizotolewa na viongozi wa vijiji na *Laigwanan*.
(iv) Kugawa sare kwa wanafunzi ambao hawakuwa na sare kati ya wale 167 walioletwa shule mwanzoni mwa mpango.
(v) Kuanzisha rejesta ya wazazi na wanafunzi hasa wanafunzi wa bweni ili kurahisisha mawasiliano kati ya utawala wa shule na wazazi endapo kuna dharura.
(vi) Kuingiza wanafunzi wote wa bweni katika huduma za bima ya afya, hasa Mfuko wa Afya Jamii.
(vii) Ukarabati wa mabweni ili kuongeza idadi ya wanafunzi. Ukarabati ulifanywa na Halmashauri.
(viii) Kushirikisha wadau tangu mwanzo wa mpango mwaka 2016. Wadau hawa ni pamoja na KINNAPA ambaye alijenga tanki la kuvuna maji ya mvua na UCRT ambaye alichangia fedha na usafiri kipindi cha kampeni za kujenga uelewa kwa jamii za wafugaji ili wawapeleke watoto wao shule na ununuzi ya vitanda 25 na magodoro 84.

**5.0 RASILIMALI**

Utekelezaji wa jitihada hii ulitumia rasmali mbalimbali zikiwemo vitu, fedha na watu. Rasilimali watu zilijumuisha Mkuu wa Wilaya, Mkurugenzi wa Halmashauri, watumishi wa Halmashauri, Polisi na walimu. Jedwali Na. 2 linaonesha kwa muhtasari rasilimali fedha na vitu zilizotumika kwenye utekelezaji wa mpango.

**Jedwali 2: Rasilimali Fedha**

| Na. | Matumizi | Idadi | Kiasi TZS | Jumla TZS |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Posho | 15 | 60,000 | 600,000 |
| 2 | Dizeli | 200 | 2,500 | 500,000 |
| 3 | Magodoro | 70 | 85,000 | 2,125,000 |
| 4 | Gari la kukodi | 1 | - | 3,225,000 |
| 5 | JUMLA | | | 6,550,000 |

**6.0 MATOKEO**

H/W ya Kiteto imepata mafanikio mengi tangu kuanza kwa jitihada hii. Mafanikio haya yameainishwa hapa chini.

Kuongezeka kwa uelewa; kwa ujumla kumekuwa na maboresho katika kiasi cha uelewa kati ya wazazi kuhusu umuhimu wa kuandikisha watoto wenye umri wa kwenda shule. Kwa ufasaha zaidi, jitihada hii imeleta fursa kwa watoto 250 kuhudhuria elimu ya msingi, watoto hawa wameandikishwa katika shule mbalimbali kulingana na ukaribu wa shule na mahali makazi ya watoto yalipo. Shule ya Msingi Partimbo siyo tu imerahisisha mazingira ya watoto kujifunza bali inatoa mazingira ambayo ni mazuri na yenye hamasa kwa watoto kujifunza.



***Watoto wenye ulemavu wa kusikia wakiimba wimbo wa taifa kwa kutumia lugha ya alama***

Uwepo wa huduma za chakula na malezi; Shule ya Msingi Partimbo huwapa chakula wanafunzi kwa kutumia ruzuku ya elimu na michango ya wazazi. Kamati ya wazazi inahusika kikamilifu na malezi hasa katika kubadili wanafunzi kuwa na tabia za mchanganyiko bila kupoteza tabia za asili. Kutokana na nyama ya ng'ombe kuwa chakula kikuu cha wamasai, shule huwapa wanafunzi nyama ya ng'ombe mara kwa mara kama mkakati wa kuwafanya wajisikie nyumbani.



***Wanafunzi wakijiandaa kupata chakula***

Miundombinu bora ya shule; mabweni 2 yamekarabatiwa ili kuongeza wanafunzi wa bweni kutoka jamii za vijijini na ukarabati wa vitanda 70 kati ya 180 vilivyopo. Madawati 25 yalitengenezwa na Serikali ya Kijiji cha Partimbo na kukabidhiwa shuleni, ikiwa ni pamoja na usimikaji wa mfumo wa kuvuna maji ya mvua na ununuzi ya vifaa mbalimbali vya wanafunzi wenye ulemavu.



***Bweni lililokarabatiwa    na mfumo wa uvunaji maji ya mvua***

Kuongezeka kwa uhitaji wa elimu; kuongezeka kwa uelewa katika jamii za wamasai kunadhihirshwa na idadi kubwa ya wazazi wanaoomba kuandikisha watoto wao katika shule hii. Mwalimu Mkuu amekuwa akipokea maombi zaidi ya 20 kwa ajili ya wanafunzi wa bweni kila mwaka. Idadi ya wanafunzi imeongezeka kutoka 110 mwaka 2016 hadi 651 mwaka 2018; kati yao wanafunzi 250 waliandikishwa kupitia jitihada hii.

Watumishi wenye motisha; kutokana na uwepo wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, miuondombinu bora, taratibu za bima ya afya ya wanafunzi na uongozi bora, walimu wa Shule ya Msingi Partimbo wana motisha na wanafanya kazi kwa kujituma ili kuwapatia elimu bora wanafunzi kutoka jamii za wafugaji.



***Watumishi wenye motisha***

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

H/W ya Kiteto huwa na changamoto ya watoto wenye umri wa kwenda shule kutoandikishwa kutokana na uwepo wa jamii za vijijini hasa jamii za wafugaji. Hata hivyo, Halmashauri inaendelea kuweka

mikakati ya kuhakikisha watoto wote wenye umri wa kwenda shule wanaandikishwa. Ili kuleta uendelevu Halmashauri imedhamiria kujikita katika mikakati ifuatayo.

i. Kuendelea na mahusiano bora ya kazi kati ya utawala wa shule, Halmashauri na Kamati ya Shule hasa mwenyekiti ambaye amechukua jukumu muhimu la kuwasiliana na wanafunzi kwa lugha ya kimasai.
ii. Kuanzisha uhusiano wa karibu na wazazi. Kanzidata imeendaliwa ambayo ina taarifa za wazazi wote wenye wanafunzi wa bweni katika Shule ya Msingi Partimbo.
iii. Kuendelea kutumia wazee wa kimasai kuwaeleza wanafunzi wa kimasai kuhusu changamoto mbalimbali na kuzitatua kwa pamoja.
iv. Kuendelea na kampeni za kukuza uelewa kuhusu umuhimu wa elimu katika jamii za wafugaji kwa kutumia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya na Halmashauri.
v. Kuzingatia na kutekeleza sheria ya elimu (Sura 353 ya 2002) ambayo huonesha hatua za kisheria na adhabu za wazazi ambao huwanyima watoto wao fursa ya kupata elimu ya msingi.
vi. Kuendelea kuhamasisha wazazi kuchangia gharama za kulea watoto wao wakiwa bweni na kuendelea kutenga fedha katika bajeti ya Halmashauri.
vii. Kuendelea kujenga uelewa wa wazazi ili waendelee kutoa ada kwa ajili ya malezi ya watoto wao na kushawishi wanajamii wengine wa jamii za wafugaji kuandikisha watoto wao katika elimu ya msingi.

## 8.0 SIRI YA MAFANIKIO

Mafanikio ya H/W ya Kiteto katika kutekeleza mpango huu yametokana na sababu mbalimbali ambazo zililelata umoja na hivyo kasi ya utekelezaji. Sababu hizi ni;

i. Uongozi bora wa Mkuu wa Wilaya na Mkurugenzi wa Halmashauri ukisaidiwa na timu thabiti ya elimu ya msingi, jeshi la polisi shupavu, kamati ya shule ya msingi Partimbo na walimu wenye motisha.
ii. Kuwapatia wanafunzi chakula wanachopenda, hasa nyama kwani wengi wao ni wamasai. Hii inasaidia kuwapa wanafunzi chakula chenye ladha sawa na vyakula vya nyumbani.
iii. Kuwatumia wazazi kuwaelewesha wanafunzi masuala ya kisasa ambayo wanatakiwa kuyazingatia wakiwa shuleni kwa kutumia lugha ya kimasai.
iv. Uwepo wa mtandao wa simu wa kampuni ya Halotel (ambayo mtandao wake unapatikana katika maeneo yote ya Halmashauri) umerahisisha mawasiliano kati ya wazazi na utawala wa shule.
v. Matumizi ya akaunti maalumu (*force account)*, mbinu ya manunuzi ambayo husaidia kununua chakula kwa gharama nafuu. Fedha zinazookolewa hutumika katika mahitaji mengine muhimu.

# HALMASHAURI YA MANISPAA YA SINGIDA

**UBORESHAJI WA KITUO KIKUU CHA MABASI CHA MISUNA KWA HUDUMA BORA**



*Uzoefu wa H/Manispaa ya Singida*

## 1.0 UTANGULIZI

H/Manispaa ya Singida ni moja kati ya Halmashauri 7 za Mkoa wa Singida. Halmashauri hii imezungukwa na H/W ya Singida. Inapatikana kati ya Latitudo $4^{o}\ 40^{'}$ hadi $5^{o}0^{'}$ Kusini na Longitudo $30^{0}30^{'}$ hadi $34^{o}53^{'}$ Mashariki. H/Manispaa ya Singida ina eneo la $754km^2$, Tarafa 2, Kata 19, Mitaa 37 na Vitongoji 115. Kwa Mujibu wa Sensa ya 2012, Manispaa hii ina watu 150,379; Wanaume 73,484 na Wanawake 76,895. Wastani wa ongezeko la watu kwa mwaka ni 4.9% na wastani wa watu katika kaya ni 5.

Hali ya hewa ya Manispaa ya Singida ina vipindi vya kiangazi kati ya mwezi Mei hadi Novemba na vipindi vya mvua kati ya Desemba hadi Aprili ambapo wastani wa mvua kwa mwaka ni 660mm. Hali ya joto ni kati ya $24^{o}$ C na $31^{o}$ C. Hakuna mito ya kudumu ndani ya eneo la Halmashauri lakini kuna Maziwa ya maji chumvi; Singidani na Kindai ambapo moja lipo upande wa Kaskazini na jingine Kusini mwa Mji. Kuna upepo mkali ambao unaweza kutumika katika uzalishaji wa umeme.

Ardhi ina miamba ambayo husababisha udongo wenye asili ya kichanga wakati miti na misitu huchukua sehemu ndogo ya eneo la mji. Mimea ni pamoja na misitu ya asili na misitu iliyopandwa ambayo husaidia kukinga na kupunguza kasi ya upepo. Manispaa ya Singida imebarikiwa katika uzalishaji wa mafuta ya alizeti. Shughuli kuu za kiuchumi ni pamoja na kilimo, ufugaji, kilimo cha mbogamboga, biashara, ajira katika sekta za umma na viwanda vidogovidogo. Wastani wa pato ni TZS 350,294. Singida ni kitovu cha barabara za kwenda Dodoma, Arusha, Kigoma na Mwanza zinazounganisha kanda ya kaskazini, kanda ya ziwa na kanda ya kati.

## 2.0 TATIZO

Tangu mwaka 2010, Halmashauri imekuwa ikikabiliwa na upungufu wa fedha kutokana na ukusanyaji duni wa mapato kutoka vyanzo vya ndani ambapo wastani wa mapato ulikuwa TZS 0.7 billioni. Hali hii ilisababisha Halmashauri kushindwa kuendesha shughuli za kawaida na za maendeleo kama ujenzi wa shule, zahanati na barabara bora. Hii ilisababisha utoaji duni wa huduma za kijamii na kiuchumi ambapo ilithibitishwa na barabara mbovu, huduma duni katika vituo vya afya, uhaba wa madawati na madarasa na maji safi na salama katika maeneo ya pembezoni. Halmashauri kwa kiasi kikubwa ilitegemea fedha za ruzuku kutoka Serikali Kuu kuendesha shughuli za kiuchumi na za kijamii. Hata hivyo, fedha za ruzuku hazikutosheleza mahitaji yote na mara nyingi zilitolewa kwa kuchelewa.

Vyanzo vya mapato ya Halmashauri vilitokana na kodi za majengo ambazo zilichangia 35% ya mapato yote ya ndani, ushuru wa huduma 15%, soko kuu 9% mabango 11% kodi ya ardhi 8%, minada ya vijijini 5% na vyanzo vingine ikiwa ni pamoja na kituo cha mabasi 17%. Kutokana na mapato hafifu yaliyopatikana, Halmashauri ililazimika kusubiri ruzuku ya Serikali Kuu na fedha za wahisani kutekeleza miradi ya maendeleo. Suala hili liliilazimu Halmashauri kubuni namna ya kuboresha vyanzo vya mapato ilikuweza kukidhi utoaji wa huduma za kijamii na kiuchumi.

Kabla ya kuboresha kituo cha mabasi cha Misuna, makusanyo yalikuwa duni. Wastani wa ukusanyaji ulikuwa TZS 350,000 kwa siku. Hali hii ilisababishwa na miundombinu mibovu, kukosekana kwa eneo la maegesho na miundombinu kama vyoo na maduka. Vilevile mifumo iliyotumika katika ukusanyaji wa mapato ilikuwa duni. Kituo cha mabasi cha awali hakikuwa kimeboreshwa kwa kiwango cha lami hivyo kutapakaa kwa vumbi na tope. Hali kadhalika, hapakuwa na uzio wa kuzunguka kituo hivyo ukusanyaji wa ushuru kutoka kwa watumiaji ulikuwa mgumu.



*Kituo cha mabasi cha zamani*

## 3.0 LENGO

Kituo cha mabasi ni muhimu katika mfumo wa usafirishaji. Hutumika kama sehemu ya kusafirisha na kupokea abiria pamoja na mizigo. Vituo vya mabasi katika maeneo ya miji hutoa huduma mbalimbali kama sehemu za kusubiria wasafiri, huduma za jamii na biashara ndogo ndogo. Vile vile kituo cha basi ni sehemu ya kuhifadhi taarifa za wasafiri kupitia tiketi za mabasi. Tofauti na nchi nyingie, Vituo vya mabasi kwa Tanzania hutumika kama chanzo cha mapato katika maeneo ya miji. Vituo hivi huwa ni sehemu ya biashara kama maduka na migahawa hivyo huvutia watu wengi.

Kwa kuzingatia umuhimu wa kituo cha mabasi, Manispaa ya Singida ilimua kuboresha eneo la Misuna kuwa kituo kipya cha mabasi cha kisasa. Lengo kuu la jitihada hii ni kujenga kituo cha mabasi cha kisasa ili kutoa huduma bora pamoja kukusanya mapato kwa ajili ya kuiwezesha Manispaa kutoa huduma mbalimbali. Jitihada hii ilienga, kuimarisha na kuanzisha chanzo kipya cha mapato kwa kujenga kituo cha mabasi cha kisasa chenye huduma bora kwa wasafiri na wakazi wa Manispaa.

### 4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI

Kote ulimwenguni, Kituo cha mabasi ni moja ya huduma muhimu katika mfumo wa usafirishaji. Kituo cha mabasi inahitaji ardhi kubwa ya kutosha na katika eneo muhimu ndani ya mji. Kituo cha mabasi ambacho kimepengwa na kuendeshwa vyema huwa kichocheo cha maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika maeneo jirani. Hata hivyo, kituo cha mabasi ambacho hakijapangwa vyema kinaweza kusababisha matatizo ya msongamano na kuwa kero kwa watumiaji na watu maeneo jirani. Katika kuhakikisha faida za kituo zinafikiwa, Manispaa ya Singida ilitekeleza mikakati ifuatayo;

Kutafuta ardhi katika eneo la Misuna; Katika jitihada ya uboreshaji wa kituo cha mabasi, Halimashauri ilitafuta eneo jipya lenye nafasi ya kutosha kuhimili kutoa huduma zote muhimu za kituo. Mchakato ulianza kwa kuandaa mikutano mbalimbali katika ngazi za Kata na kujadili namna ya kupata eneo jipya la ujenzi wa kituo. Katika mkutano na wananchi wa Kata ya Misuna ilibainika kuwepo kwa eneo la wazi ambalo Halmashauri inaweza kulichukua na kuliendeleza kuwa kituo kipya cha mabasi. Wananchi wa Misuna walikubali kuachia baadhi ya maeneo yao ili kuongeza eneo la ujenzi wa kituo. Katika makabidhiano ya eneo hilo, wananchi wa Kata ya Misuna walihakikishiwa kupewa nafasi za upendeleo katika kuendesha shughuli za kiuchumi ndani ya kituo kama maduka, migahawa na ajira za muda kipindi cha ujenzi.

Kufanya mikutano na wafanyabiashara; baada ya kupata ardhi ya ujenzi wa kituo cha mabasi, Halmashauri iliandaa mkutano na wafanyabiashara katika kituo cha mabasi cha zamani ili washiriki katika ujenzi wa vibanda vya maduka, migahawa na vyoo kuzunguka kituo cha mabasi cha Misuna kwa kutumia fedha zao na hatikamaye kuendesha biashara ili kuendeleza kituo kiuchumi. Wafanyabiashara walishiriki katika ujenzi kwa mkataba wa jenga-tumia–rejesha. Jumla ya vibanda 20 vya maduka

vilijengwa chini ya usimamizi wa Halmashauri kwa kutumia michoro iliyokubaliwa na hutumiwa kama ofisi za kuuza tiketi za mabasi, migahawa na huduma nyinginezo.



***Vibanda vilivyojengwa eneo la kituo***

Usaidizi kutoka Serikali Kuu; Serikali Kuu kupitia Programu ya Uimarishaji Serikali za Mitaa katika Mamlaka za Miji, iliingia makubaliano na Benki ya Dunia kuimarisha miundombinu ya Majiji na Manispaa 18 ikiwemo Manispaa ya Singida (Nyingine ni Manispaa za Morogoro, Shinyanga, Musoma, Tabora, Bukoba, Moshi, Lindi, Songea, Iringa na Sumbawanga na Halmashauri za Miji ya Geita, Bariadi, Babati, Korogwe, Kibaha, Njombe na Mpanda). Programu hii ililenga kuimarisha na kuboresha mifumo ya mipango miji pamoja na kuongeza vyanzo vya mapato kwa Halmashauri hizo. Singida ilitumia fursa hii kuboresha kituo cha mabasi cha Misuna. Serikali Kuu ilitoa TZS 8 billion ambapo TZS 2.7 billion zilitengwa kuendeleza kituo cha mabasi (kusawazisha eneo la kituo, kujenga sehemu za waenda kwa miguu, vyoo, maegesho ya magari, miavuli, vizimba vya kukusanyia mapato, uzio wa kituo na taa zinazotumia nishati ya jua).

Mchakato wa zabuni; Mchakato wa kupata mkandarasi ulifuata taratibu za zabuni.. Halmashauri ilitumia mfumo wa ushindani wa zabuni katika kupata mshauri na mhandisi. Upembuzi yakinifu ulifanywa na kampuni ya Meta consultancy ili kubaini athari za kimazingira na kuandaa michoro na gharama za ujenzi wa kituo cha mabasi cha Misuna. Taarifa ya upembuzi yakinifu iliwasilishwa kwenye kamati ya fedha na baadae ikapitishwa na Baraza la Madiwani.

Ujenzi wa kituo; Mkandarasi aitwaye Hari Singh & Sons limited alishinda zabuni na kutekeleza shughuli za ujenzi wa kituo chini ya ushauri wa kampuni ya Luptan. Halmashauri ilitumia mfumo shirikishi ambapo vibarua walitoka katika Kata ya Misuna kulingana na makubaliano yalivyofikiwa wakati wa kutwaa ardhi. Kituo cha mabasi kilikamilika na kukabidhiwa tarehe 1 Julai, 2017.



***Kituo kipya cha Mabasi eneo la Misuna***

## 5.0 RASILIMALI

Kupitia ushirikiano baina ya Serikali Kuu na Manispaa ya Singida, eneo la Misuna liliboreshwa na kuwa kituo cha mabasi cha kisasa cha kutolea huduma bora na kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato na hatimaye kuboresha huduma zitolewazo na Halmashauri. Rasilimali fedha zililizotumika katika jitihada hii zimeainishwa katika jedwali Na. 1.

**Jedwali Na 1: Rasilimali Fedha**

| Na. | Shughuli | Kiasi (TZS) | Chanzo cha fedha |
|---|---|---|---|
| 1. | Ujenzi wa vibanda 20 | 157,000,000 | Wafanyabiashara |
| 2. | Ujenzi wa vizimba vya mapato, uzio, usawazishaji, barabara za waenda kwa miguu, taa za nishati ya jua | 2,700,000,000 | Serikali Kuu |

Rasilimali watu ni pamoja na watumishi wa Halmashauri ambao walisimamia shughuli za ujenzi, Timu ya Menejimenti ya Manispaa, Madiwani na Mkuu wa Mkoa ambaye aliefuatilia utekelezaji wa jitihada hii. Mradi ulitekelezwa kuanzia Machi, 2016 hadi Julai, 2017 ambapo mkandarasi alikabidhi rasmi.

## 6.0 MATOKEO

Manispaa ya Singida imepata matokeo mbalimbali kutokana na uhusiano thabiti baina yake na Serikali Kuu. Matokeo hayo ni pamoja na;

Uwepo wa kituo cha mabasi ambacho kinafanya kazi; Halmashauri imeweza kujenga kituo cha mabasi cha kisasa ambacho kina huduma zote kama sehemu ya kuegesha magari, vyoo, vizimba vya mapato, kituo cha polisi na vibanda 20.

Ongezeko la mapato; Halmashauri imeshuhudia ongezeko la mapato yatokanayo na kituo cha mabasi kwa 300%. Kabla ya utekelezaji wa jitihada hii, kiasi cha TZS 350,000 kilikusanywa kwa siku sawa na TZS 125,750,000 kwa mwaka. Hadi mwaka 2019, makusanyo yameongezeka kufikia wastani wa TZS 1,300,000 kwa siku sawa na TZS 474,500,000 kwa mwaka. Kuongezeka kwa mapato kumetokana na kuongezeka kwa mabasi yanayotumia kituo cha Misuna, tozo ya TZS 200 kwa watu wanaoingia eneo la kituo na ushuru wa migahawa, vyoo na bafu.

Kuanzishwa kwa mfumo wa ukusanyaji mapato wa kielektroniki; Halmashauri imeanzisha mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji mapato kwa kutumia Mfumo wa Ukusanyaji Mapato wa Serikali za Mitaa ambao hubaini miamala yote inayofanywa na mawakala. Kituo cha mabasi cha Misuna kama chanzo muhimu cha mapato kinatumia mfumo huu katika ukusanyaji wa mapato.

Fursa za ajira; Kituo cha mabasi cha Misuna kimetoa fursa za ajira kwa wajasiriamali ambao huuza bidhaa zao ndani na kuzunguka eneo la kituo. Ndani ya kituo kuna biashara rasmi na zisizo rasmi. Halmashauri imeajiri wakusanyaji wa mapato 18, askari mgambo 11 na wafanya usafi 10.

Kuboresha utoaji wa huduma; Manispaa imeongeza uwezo wa kuanzisha na kutoa huduma kutokana na kuimarika kwa mapato ambayo yanakidhi mahitaji ya kawaida na ya maendeleo. Kutokana na mapato hayo, Halmashauri imeweza kuboresha miundombinu ya kituo cha afya na shule ya msingi.



***Njia za kutembelea katika Kituo cha Afya cha Sokoine***

Ukarabati wa miundombinu ya shule; Halmashauri imeweza kutumia fedha zilizokusanywa kutokana na kituo cha mabasi kukarabati madarasa ya Shule ya Msingi Mtamaa na kutengeneza madawati kwa ajili ya watoto.



***Madarasa yaliyokarabatiwa katika shule ya msingi Mtamaa***

Kuimarika kwa shughuli za kuchumi; shughuli za kiuchumi kuzunguka Kituo cha mabasi cha Misuna zimetengeneza fursa za ajira kwa wadau mbalimbali. Ajira zaidi ya 100 za mawakala wa mabasi, 20 za wapakiaji mizigo na wauzaji wa chakula zimepatikana. Katika eneo la Misuna kumekuwepo na ongezeko la nyumba za wageni ambazo pia zinatoa ajira kwa wananchi na Halmashauri inakusanya ushuru.

Kuimarisha vyanzo vingine vya mapato; Halmashauri inabuni na kuboresha vyanzo vingine vya mapato kwa kutumia fedha zilizotokana na kituo cha mabasi. Hii ni pamoja na kuweka uzio katika soko la Singida la vitunguu kudhibiti ukusanyaji wa mapato. Hali kadhalika, fedha zilizotokana na kituo cha mabasi zimetumika kuboresha maeneo ya minada Kata za Mtamaa na Manga ili kuongeza wigo wa ukusanyaji mapato kutoka maeneo hayo.

## 7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU;

Manispaa imeanzisha mikakati ya kuifanya jitihada hii kuwa endelevu na kuhakikisha ukusanyaji wa mapato unaongezeka na kuiwezesha Halmashauri kuendelea kutoa huduma za kiuchumi na kijamii. Mikakati hii ni pamoja na;

Matumizi endelevu ya Mfumo wa Kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato; risiti zinatolewa na mfumo kutokana na mashine za POS ambazo zinatumiwa na wakusanyaji wa mapato. Mfumo huu unawezesha Halmashauri kutambua makusanyo yote ya mapato. Halmashauri inapanga kuweka CCTV kamera kudhibiti makusanyo kutoka kituo cha mabasi na soko la vitunguu.



***Mashine ya POS***

Halmashauri inakusudia kujenga jengo la maduka ndani ya Kituo cha Misuna litakalo toa nafasi za maduka makubwa na migahawa ya kisasa vitakavyoongeza uwezo wa kukusanya mapato.

## 8.0 SIRI YA MAFANIKO

Manispaa ya Singida imefanikiwa kuongeza mapato na kutoa huduma mbalimbali. Hii ni kutokana na uwezeshi wa Serikali Kuu, ushiriki wa wadau, kufanya kazi kama timu na usimamizi thabiti wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa. Uwepo wa eneo la wazi katika eneo la Misuna na utayari wa wananchi kuachia maeneo yao kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha mabasi ni siri nyingine ya mafanikio.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA IRAMBA

**UBORESHAJI WA HUDUMA ZA AFYA KWA WAJAWAZITO**



***Uzoefu wa H/W Iramba***

**1.0 UTANGULIZI**

H/W ya Iramba ni moja kati ya Halmashauri 7 za Mkoa wa Singida iliyopo kati ya Latitudo $4^0$ na $4^0.3'$ Kusini na Longitudo $34^0$ na 35° Mashariki. Halmashauri inapakana na H/W za Meatu kwa upande wa Kaskazini, Mkalama upande wa Mashariki, Singida upande wa Kusini na Igunga upande wa Magharibi. Mwinuko wa ardhi ni kati ya 1,000m hadi 1,500m kutoka usawa wa bahari.

Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012, H/W ya Iramba ina idadi ya watu 236,282, kati yao 116,997 ni wanaume na 119,285 ni wanawake na idadi ya watu kwa eneo ni 52 kwa $Km^2$. Makabila makuu ya asili ni Wanyiramba na Wasukuma. Makabila mengine ni wataturu na wabarbaig. H/W ya Iramba imegawanywa katika Tarafa 4, Kata 20, Vijiji 70 na Vitongoji 392. Shughuli kuu za kiuchumi ni kilimo, ufugaji, uvuvi, uchimbaji wa madini na upasuaji mbao. Mazao ya chakula ni mahindi, mtama, mpunga, maharage, muhogo na viazi vitamu wakati mazao ya biashara ni alizeti, pamba, vitunguu na karanga. Mifugo iliyopo ni ng'ombe,mbuzi, kondoo, punda na kuku.

H/W ya Iramba ilifanikiwa kuboresha vituo vya kutolea huduma za afya kupitia Mpango wa Uboreshaji wa Sekta ya Afya. Mpango huu, ulilenga kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi katika kutoa huduma za afya na kuhamasisha ushiriki wa jamii katika kuchangia gharama za huduma za afya. Aidha, mpango huu ulilenga kuhamasisha uanzishaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii katika vijiji mbalimbali na kupanua wigo wa upatikanaji wa huduma za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya. Maendeleo ya sekta ya afya kwa H/W ya Iramba yamejikita katika ya sekta ya umma na ushiriki mdogo wa sekta binafsi ambapo kuna vituo vya kutolea huduma 41; hospitali 1, vituo vya afya 3 na zahanati 37 (31 za umma na 6 za kibinafsi).

**2.0 TATIZO**

Hadi mwaka 2015, uwiano wa vifo vya wajawazito wakati wa kujifungua ndani ya H/W ya Iramba ulikuwa 100 kwa kila 100,000. Tatizo hili lilitokana na sababu mbalimbali ambazo ni elimu duni ya afya na mfumo dhaifu wa rufaa na mawasiliano kati ya zahanati, vituo vya afya na hospitali ya wilaya. Baadhi ya wajawazito walitegemea huduma za wakunga wa jadi katika kujifungua. Kati ya mwaka 2013 na 2016 idadi ya wanawake 1,322 walijifungua kwa msaada wa wakunga wa jadi ambapo baadhi yao walipoteza maisha na watoto wao. Hapakuwa na huduma ya gari la wagonjwa kwa ajili ya kutoa usaidizi kwa wajawazito kutoka vijijini kufikia huduma za afya. Vilevile, baadhi ya wahudumu wa afya hawakuwa na ujuzi stahiki wa kutoa huduma za uzazi katika baadhi ya vituo vya kutolea huduma. Vifaa vya mawasiliano kama simu ambavyo ni muhimu katika kurahisisha mawasiliano kati ya vituo vya kutolea huduma za afya havikuwepo hivyo kuleta ugumu wa mawasiliano na hospitali ya wilaya pale inapotokea dharura.

**3.0 LENGO**

MSM zimepewa jukumu la utoaji wa huduma na huwajibika kuhakikisha uwepo wa utoaji bora huduma za elimu, maji safi na salama, umeme na afya. H/W ya Iramba baada ya kubaini matukio ya vifo vya wajawazito iliweka lengo la kuimarisha huduma za afya na kutokomeza vifo vya wajawazito. Malengo mahususi ya jitihada hii ni pamoja na;

(i) Kuhakikisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.
(ii) Kuongeza na kuimarisha stadi na ujuzi wa wahudumu wa afya.
(iii) Kukarabati jengo la mama ngojea la hospitali ya wilaya.
(iv) Kutoa elimu ya afya kwa wajawazito.
(v) Kuboresha mfumo wa mawasiliano na rufaa kati ya zahanati, vituo vya afya na Hospitali ya Wilaya

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Halmashauri kwa kushirikiana na wadau ilibuni mikakati mbalimbali ili kufikia malengo. Mikakakati hiyo ni pamoja na;

Uundaji wa kikosi kazi; kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama Taasisi zisizo za Kiserikali (CMT, SEMA, WORLD VISON, AMREF, Marie Stopes, na Engender Health) Halmashauri ilianzisha kikosi kazi kubaini matatizo ya mfumo wa huduma za afya na kuweka mikakati ya kutatua changamoto hizo. Mikutano kadhaa ilifanyika ambapo iliamuliwa kufanyike uboreshaji wa miundombinu ya hospitali, utoaji wa elimu ya afya kwa wajawazito na uboreshaji wa huduma za rufaa.

Ukarabati wa jengo la mama ngojea; jengo lililokuwepo katika hospitali ya wilaya kwa ajili ya mama ngojea lilikuwa chakavu na halikuwa na vifaa stahiki kama vitanda na magodoro suala lililazimu hatua za uboreshaji. Halmashauri ilishirikiana na SEMA kukamilisha uboreshaji wa jengo la mama ngojea ambapo SEMA ilitoa fedha za ukarabati na vifaa na Halmashauri ilichangia utaalamu na usimamizi..

Uboreshaji wa mfumo wa rufaa; ili kuboresha mfumo wa rufaa, Halmashauri ilipeleka magari ya wagonjwa 2 kwenye vituo vya afya vya Mgongo na Ndago na kutenga bajeti ya mafuta ili kurahisisha huduma za dharura. Vilevile, Halimashauri iliboresha mfumo wa mawasiliano kwa kuwapatia simu za mkononi na muda wa maongezi maafisa wafawidhi 33 wa vituo vya kutolea huduma za afya ili kurahisha mawasiliano na hospitali ya wilaya pale inapotokea dharura inayohitaji rufaa. Namba za simu za wajumbe wa Timu ya Usimamizi wa Afya ya Halmashauri ziliwekwa bayana katika kila kituo cha kutolea huduma za afya ili mawasiliano.

Kuteua walezi wa vituo vya kutolea huduma za afya; kila mjumbe wa Timu ya Usimamizi wa Afya ya Halmashauri alipewa jukumu la kusimamia angalau kituo kimoja cha kutolea huduma za afya. Majukumu waliyopewa ni pamoja na kutoa ushauri, kubaini matatizo na kutafuta suluhisho. Aidha, walezi hawa huwajibika kuwasilisha taarifa kwa Halmashauri juu ya changamoto zinazokabili vituo wanavyohudumia.

Kukuza uelewa na kutoa elimu ya afya ya uzazi; wahudumu wa afya jamii wakishirikana na wataalamu wa afya waliendesha mafunzo ya kukuza uelewa juu ya uzazi salama. Wakunga wa jadi walielekezwa kuhusu uzazi salama na kushauriwa kuwa jukumu lao pekee ni kusadia wajawazito kufika katika vituo vya afya. Wauguzi katika vituo vya afya walipewa mafunzo kuhusu huduma za msingi za mama na mtoto na kukumbushwa kuhusu namna ya kuzuia vifo vya wajawazito kwa kutumia vifaa tiba stahiki wakati wa kutoa huduma za mama na mtoto wakati na baada ya kujifungua.

Ununuzi wa dawa na vifaa tiba; Halmashauri ilihakikisha uwepo wa dawa na vifaa tiba ikiwa ni pamoja na vifaa maalumu kwa ajili ya wajawazito. Vifaa hivi vilinunuliwa na kusambazwa kwenye vituo vyote vya afya na baadhi ya zahanati.

**5.0 RASILIMALI**

Utekelezaji wa jitihada hii ulitumia rasilimali mbalimbali. Rasilimali fedha zipatazo TZS 323,750,000 zilitumika katika ukarabati wa jengo la mama ngojea na ununuzi wa dawa na vifaa tiba kama inavyofafanuliwa kwenye jedwali 1. Vituo vya kutolea huduma za afya 33 vilipatiwa simu za mkononi na muda wa maongezi wa thamani ya TZS 30,000 kwa mwezi (TZS 11,880,000 kwa mwaka). Rasilimali watu ni pamoja na wajumbe wa Timu ya Usimamizi wa Afya ya Halmashauri, wauguzi na wahudumu wa afya jamii ambao walitoa elimu ya afya na kujenga uelewa wa jamii kuhusu huduma za mama na mtoto.

Rasilimali nyingine ni ushirikiano kati ya Halmashauri na asasi zisizo za kiserikali (SEMA, Engender Health, MARIE STOPES, WORLD VISON na AMREF) zinazohusika na masuala ya afya.

**Jedwali 1: Rasilimali Fedha**

| NA | SHUGHULI/ KAZI | KIASI TZS | CHANZO | MWAKA |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Ukarabati wa jengo la mama ngojea | 45,000,000 | Water AID/SEMA | 2015/16 |
| 2 | Mafunzo ya wahudumu wa afya jamii na wauguzi | 14,125,000<br>18,350,000 | MARIE STOPES<br>WORLD VISION | 2016 |
| 3 | Kukuza uelewa wa jamii | 6,750,000 | Halmashauri | 2016 |
| | **Ununuzi wa vifaa tiba na vinginevyo** | | | |
| 4 | Vifaa vya kujifungulia | 56,000,000 | Serikali<br>AMREF | 2016/2017 |
| 5 | Vitanda vya kujifungulia | 87,500,000 | | |
| 6 | Vifaa vya kushtua baada ya kuzimia | 96,000,000 | | |
| | **Jumla** | **323,750,000** | | |

## 6.0 MATOKEO

Utekelezaji wa jitihada hii umeleta matokeo yafuatayo;

(i) H/W ya Iramba imefanikiwa kukamilisha ukarabati wa jengo la mama ngojea likiwa na vifaa vya tiba na miundombinu muhimu. Jengo hili lipo karibu na wodi ya wazazi likiwa na vitanda, shuka na jiko ili kuwezesha wajawazito kujiandalia chakula.



***Wajawazito wakiwa ndani ya jengo la mama ngojea***

(ii) Elimu ya afya hutolewa mara kwa mara; wahudumu wa afya hutoa elimu ya afya jamii katika Kata zote.

(iii) Hamasa ya wahudumu wa afya imeongezeka baada ya kuanzishwa kwa huduma ya mawasiliano kwa simu za mkononi na posho ya muda wa maongezi kila mwezi.

(iv) Idadi ya wajawazito kujifungua katika vituo vya kutolea huduma za afya imeongezeka. Aidha, idadi ya wajawazito wanaotumia jengo la mama ngojea imeongezeka kutoka 28 mwaka 2016 hadi 54 mwaka 2018.

(v) Vifo vya wajawazito vimepungua kutoka 100/100,000 mwaka 2017 hadi 39/100,000 mwaka 2018.

(vi) Idadi ya wajawazito wanaohudumiwa na wakunga wa jadi imepungua kutoka 1,056 mwaka 2013 hadi 7 mwaka 2018.

(vii) Mfumo wa rufaa umeboreshwa kwa uwepo wa huduma za magari ya wagonjwa katika vituo vya afya na kuboreshwa kwa mawasiliano kati ya zahanati, vituo vya afya na hospitali ya Wilaya.

(viii) Mafuzo ya kuimarisha ujuzi kwa wahudumu wa afya yanatolewa mara kwa mara kwa ushirikiano kati ya Halmashauri na wadau wa maendeleo (USAID na World Vision).

(ix) Kumekuwepo na ongezeko la Kaya kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii kutokana na kuongezeka kwa uelewa. Zaidi ya 58% ya Kaya ndani ya H/W ya Iramba zinanufaika na huduma za mfuko wa afya ya jamii.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Ili kuwepo kwa uendelevu wa jitihada hii, Halmashauri kwa kushiriiana na wadau inaendelea kutenga fedha za kuboresha huduma za afya. Mikakati mingine ni pamoja na;

(i) Halmashauri inaendelea kuwezesha wakuu wa vituo vya afya na zahanati kupata muda wa maongezi ili kurahisisha mawasiliano panapotokea dharura.
(ii) Ukarabati na matengenezo ya mara kwa mara wa magari ya wagonjwa na kuhakikisha uwepo wa mafuta ya magari hayo.
(iii) Halmashauri inaendelea kushirikiana na wadau wa maendeleo wa sekta ya afya kuboresha utoaji wa huduma za afya.
(iv) Kuendelea kutoa mafuzo ya kuimarisha ujuzi kwa watoa huduma za afya.
(v) Halmashauri ina mpango wa kujenga na kukarabati vituo vya afya 2 vya Ndago na Kinampanda ili kupunguza msongamano katika hospitali ya wilaya.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Siri ya mafanikio ya jitihada hii inatokana na utayari wa jamii katika kupokea elimu ya afya na kutumia maarifa kubadilika. Utayari wa Timu ya Usimamizi wa Afya ya Halmashauri katika kutoa rasilimali za ukarabati wa jengo la mama ngojea na vituo vya afya, ununuzi wa magari ya wagojwa na kuboresha mawasiliano ya simu na kutoa muda wamaongezi kwa kila kituo cha kutolea huduma ni siri nyingine ya mafanikio. Uwepo wa wadau wa maendeleo wanaosaidia sekta ya afya na utayari wao kushirikiana na Halmashauri umefanya jitihada hii ifanikiwe. Mafuzo ya uimarishaji ujuzi yanayotolewa mara kwa mara kwa watoa hudumu za afya jamii yanaongeza motisha na ari ya utendaji. Kuteua walezi wa vituo vya kutolea huduma za afya kumechangia kubaini changamoto kwa wakati na hivyo kuwezesha kuchukua hatua stahiki mapema.

# SEKRETARIETI YA MKOA WA SHINYANGA

## UPUNGUZAJI WA VIFO VYA WAJAWAZITO NA WATOTO










*Uzoefu wa Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga*

**1.0 UTANGULIZI**

Mkoa wa Shinyanga upo kati ya Latitudo $3^0 15''$ na $4^0 30''$ Kusini na Longitudo $31^0$ 30" na $34^0$ 15" Mashariki ukiwa na eneo la 18,555 $km^2$. Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012 idadi ya watu katika Mkoa ni 1,534,808 na ongezeko la watu ni 2.1% kwa mwaka. Makabila makuu ya asili ni Wasukuma, Wanyamwezi na Wanyiramba. Makabila mengine ambao ni Wataturu na Wasumbwa.

Mkoa umegawanyika katika Wilaya 3 ambazo ni Kahama, Kishapu na Shinyanga. Idadi ya Halmashauri ni 6 ambazo ni Manispaa ya Shinyanga, Mji wa Kahama na H/W za Kishapu, Shinyanga, Msalala na Ushetu. Mkoa una Tarafa 15, Kata 130, Vijiji 511, Mitaa 87 na Vitongoji 2,760.




***Ramani ya Mkoa wa Shinyanga***

Shughuli za kiuchumi ni kilimo na ufugaji, uchimbaji madini na biashara. Wastani wa kipato katika Mkoa ni TZS 1,596,344. Idadi ya watu katika mkoa imegawanywa katika makundi ya wanaoishi mjini na vijijini idadi kubwa ikiwa ni wafugaji na wakulima. Zaidi ya watu 1.3 milioni wanaishi vijijini.

Mkoa una vituo vya kutolea huduma za afya 222 ambapo 194 ni zahanati, 22 ni vituo vya afya na 6 ni hospitali (3 za serikali na 3 za binafsi). Kila Wilaya ina Hospitali ya Serikali. Vilevile kuna ujenzi unaendelea wa hospitali katika Manispaa ya Shinyanga, H/W za Ushetu na Shinyanga.

**2.0 TATIZO**

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga ilikumbwa na ongezeko la vifo vya wajawazito na watoto sababu kuu ikiwa kukosekana kwa huduma ya damu salama wakati wa dharura. Hali hii ilisababisha vifo vya wajawazito kufikia vifo 76 mwaka 2016 na 73 mwaka 2017. Uongozi wa Hospitali ulilazimika kuwalelekeza ndugu wa wagonjwa kuchangia damu wagonjwa wao inapotakiwa dharura. Hata hivyo baadhi walioneka kuwa na damu ambayo haiendani na damu ya mgonjwa. Hali hii, ilisababisha kuchelewa kuwapatia wagonjwa huduma jambo ambalo lilisababisha vifo. Mchakato wa kupata damu, kuifanyia vipimo na kumuwekea mgonjwa ulichukua muda mrefu (Siku 3 hadi 5). Wajawazito ambao hubainika kuwa na upungufu wa damu na ambao hujifungua kwa njia ya upasuaji huhutaji huduma ya haraka ya kuongezewa damu. Kwa ujumla, upungufu wa damu ulisababisha vifo vya wajawazito wenye dharura wakati wa kujifungua ikiwa ni pamoja na watoto waliozaliwa na upungufu wa damu.

Vifo vingi vya wajawazito ambao walionesha dalili za hatari vilisababishwa na umbali kutoka nyumbani hadi kituo cha kutolea huduma za afya. Kwa mfano kijiji cha Mwakitolyo kipo umbali wa 120km kutoka Shinyanga Mjini. Wakati mwingine wajawazito walipata magonjwa mengine kama fistula kutokana na kuchelewa kujifungua kulikosababishwa na umbali kufika kituo cha kutolea huduma za afya. Sababu kubwa zinazochangia matatizo katika ujauzito ni kupoteza damu, maambukizo katika mfumo wa uzazi na kufanya kazi ngumu wakati wa ujauzito. Kwa kiasi kikubwa vifo vingi vinaweza kuepukika endapo

huduma za dharura zitapatikana kwa wakati, uwepo wa watalamu wenye sifa na vifaa muhimu wakati wa kujifungua.

Vilevile, upungufu wa maji tiba kwa ajili ya wagonjwa wenye uhitaji ulichangia kuongezeka kwa vifo vya mama na mtoto. Mahitaji ya maji tiba katika Hospitali ya Rufaa ya Shinyanga ni lita 240 kwa siku ambapo katika hali ya kawaida maji hayo yalikuwa yakinunuliwa kutoka Bohari ya Dawa ambapo mara kadhaa hayakupatikana kwa wakati.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la Sekretarieti ya Mkoa na Timu ya Mkoa ya Usimamizi wa Afya lilikuwa kuimarisha huduma za afya na kupunguza vifo vya mama na mtoto. Jitihada hii ilikuwa na malkengo mahususi yafuatayo;

(i) Kupunguza vifo vya wajawazito na watoto wachanga vinavyosababishwa na ukosefu wa damu salama kwa kuhakikisha damu salama inakuwepo.
(ii) Kupunguza vifo vya wajawazito wenye viashiria vya hatari ambavyo vilisababishwa na kusafiri umbali mrefu hadi kituo cha kutolea huduma za afya kwa kujenga jengo la mama ngojea.
(iii) Kupunguza vifo vinavyosababishwa na ukosefu wa maji tiba kwa kuanzisha kiwanda cha maji tiba ili kuwepo na maji tiba muda wote.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Kubaini tatizo; mikutano ya Menejimenti ya Mkoa wa Shinyanga inayofanyika kila wiki kujadili shughuli za utekelezaji katika Mkoa, ilipokea taarifa na kujadili tatizo la vifo vya wajawazito na watoto ambavyo vilisababishwa na upungufu wa damu salama katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Taarifa ilionesha kuwa vifo vya wajawazito vilifikia 74 mwaka 2016 na 73 mwaka 2017 na sababu zilikuwa ni umbali kufika katika vituo vya kutolea huduma za afya na upungufu wa maji tiba.

Maamuzi ya sekretarieti ya Mkoa; Mwaka 2017, mkutano wa Menejimenti ya Mkoa ukiongozwa na Katibu Tawala wa Mkoa Bw. Albert G. Msovela, uliazimia kutokomeza changamoto hizo. Suala kubwa lilikuwa kupata rasilimali za utekelezaji hivyo ililazimu kushirikisha wadau wa maendeleo. Baadhi ya wadau hao ni Umoja wa Mataifa, Population Fund (UNFPA), Touch Foundation na Saint Luke.

Kuanzisha benki ya damu; UNFPA ilionesha nia ya kujenga jengo kwa ajili ya kuhifadhi damu salama. Serikali iliombwa kununua vifaa maalumu vya kukusanya,kupima na kuhifadhi damu. Mwaka 2016/2017, tathmini ya gharama za ujenzi wa jengo la damu salama na ununuzi wa vifaa vinavyohitajika ilifanyika na kubaini kuwa TZS 33,435,000 zitahitajika. Baada ya kupata fedha mchakato wa zabuni ulifanyika na mkandarasi M/S Fau Construction Company Limited alipewa zabuni ya ujenzi. Vifaa vya kuhifadhi damu salama vilinunuliwa na Sekretarieti ya Mkoa. Benki ya damu iliyojengwa ina uwezo wa kukusanya na kuhifadhi lita 1,401 kwa mwaka.




***Benki ya damu ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga***

Uchangiaji wa damu salama; jambo la msingi kabisa kwa benki ya damu ni kuhifadhi damu salama ya kutosha na kupatikana kwa wakati. Hospitali ya Rufaa huhakikisha zoezi la uchangiaji damu ni salama kwa anayetoa na anayepokea na huandaa watu waliotayari kuchangia damu kwa ridhaa yao bila malipo na kuwa tayari kwa vipimo. Kuhakikisha upatikanaji wa damu salama, utambuzi wa watu wenye damu salama ni wa msingi. Ilikufikia azma hii, benki ya damu inafuata misingi ifuatayo:

(i) Damu itakubaliwa endapo imetolewa kwa ridhaa ya mtu mwenyewe bila kudai malipo na damu iwe salama.

(ii) Kuwepo kwa jitihada za kuwa na idadi ya kutosha ya watu wenye damu salama na kuendelea kuwatambua na kuwathamini.

(iii) Taarifa za damu ni siri.

Kampeni za uchangiaji wa damu; uhamasishaji kwa wachangiaji wa damu ulifanywa na watumishi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa kwa kutumia mbinu mbalimbali za mawsiliano kushawishi wachangiaji wa damu kufika na kuchangia damu katika benki. Wachangiaji wa mwanzo walihamasishwa kuwa na ari na tabia ya kuchangia damu mara kwa mara. Asasi za kijamii na mashirika yasiyo ya kiserikali yalishiriki vyema katika kujenga uelewa na hamasa katika kuchangia damu.

Kuanzisha jengo la mama ngojea; katika kupunguza vifo vya wajawazito wenye viashiria vya hatari, Menejiment ya Sekretarieti ya Mkoa iliamua kujenga jengo la mama ngojea karibu na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa. Wazo hili liliungwa mkono na Touch Foundation ambayo ilitoa TZS 70,000,000 zilizotumika kufanya ukarabati wa jengo la awali na ujenzi wa vyumba vingine vya ziada. Ujenzi ulifanyika chini ya usimamizi wa Touch Foundation.



***Jengo la Mama Ngojea***

Kuwapatia Mama ngojea vifaa vya malazi; baada ya kukamilika kwa ujenzi, Hospitali ya Mkoa ilitoa vitanda, magodoro na vyandarua. Vilivile kitengo hiki kilipatiwa simu ya mkononi ilyounganishwa kwenye mtandao wa Vodacom Tanzania Limited na gharama za muda wa maongezi hulipwa na shirika lisilo la kiserikali la Pathfinder. Jengo la mama ngojea lina uwezo wa kuchukua wajawazito 40 kwa mara moja.

Huduma kwa wajawazito; wajawazito hushauriwa kuhudhuria kliniki na wanapogundulika kuwa na viashiria vya hatari hushauriwa kutumia mama ngojea ili kuwa karibu na huduma. Jengo la mama ngojea linatumika sio tu kwa wajawazito wenye viashiria vya hatari bali hata kwa wajawazito ambao makazi yao ni mbali na hospitali. Wajawazito wote wana haki ya kutumia jengo la mama ngojea lakini wanaopewa vipaumbele ni wale wenye viashiria vya hatari kama vile umri chini ya miaka 16 na zaidi ya miaka 40, uzazi wa kwanza na zaidi ya uzazi wa sita. Msimamizi wa jengo la mama ngojea huwasiliana na vituo vya afya kuhusu wajawazito wenye viashiria vya hatari ambapo gari la wagonjwa na teksi za jamii zilizotambuliwa na Pathfinder hutumika kuwaleta katika jengo la mama ngojea.

Kuanzisha kiwanda cha maji tiba; katika hitaji la kupunguza vifo vitokanavyo na upungufu wa maji tiba Menejimenti ya Hospitali iliandaa andiko la kuanzisha kiwanda cha maji tiba hospitalini. Wazo hili liliungwa mkono na Taasisi ya Saint Luke inayojihusisha na afya ya mama na mototo. Taasisi hii ilitoa teknolojia, kusimika vifaa na kufanya ufuatiliaji wa ubora wa vifaa baada ya kusimikwa. Serikali ilitoa TZS 97,000,000 kwa ajili ya mradi huu. Baada ya kukamilika kwa kiwanda, taasisi ya Saint Luke ili wapatia mafunzo watumishi wa kuendesha kiwanda hicho. Kiwanda kina uwezo wa kuzalisha lita 120 za maji tiba kwa siku. Jengo la kiwanda lilikarabatiwa kuruhusu uendeshaji wa shughuli za uzalishaji na uhifadhi wa maji tiba. Ukarabati ulisimamiwa na Mhandisi wa ujenzi wa Mkoa.



***Kiwanda cha kuzalisha maji tiba***

**5.0 RASILIMALI**

Rasilimali kwa ajili ya kuimarisha huduma za afya zilipatikana kutoka Serikalini pamoja na wadau wa maendeleo. Rasilimali fedha kwa ajili ya kuanzisha benki ya damu salama zilipatikana kutoka UNFPA na Serikali. Rasilimali watu katika vitengo hivi ni watumishi wa Serikali. Kwa upande wa jengo la mama ngojea, ujenzi uligharamiwa na Touch Foundation. Mahitaji mengine katika jengo la mama ngojea kama vitanda na magodoro yalitolewa na serikali. Usimamizi wa kila siku wa mama ngojea hufanywa na watumishi wa serikali kutoka Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Shinyanga. Mawasiliano ya simu yanawezeshwa na Pathfinder International kwa kushirikiana na Timu za Usimamizi za Afya za Mkoa, Hospitali na Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga.

Uanzishaji wa kiwanda cha maji tiba uligharamiwa na Taasisi ya Saint Luke ambayo pia hufuatilia ubora wa maji tiba yanayozalishwa. Usimamimizi wa kiwanda wa kila siku hufanywa na watumishi wa hospitali ambao wamepatiwa mafunzo.

**6.0 MATOKEO**

Uwepo wa benki ya damu; jengo la benki ya damu lenye vifaa vyote vya kuhifadhi damu salama limejengwa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na linafanya kazi. Benki ya damu inakusanya lita 1,401 za damu kwa mwaka ambazo ni sawa na 39% ya mahitaji ya damu katika hospitali ambazo ni lita 3,600 kwa mwaka.

Uwepo wa jengo la mama ngojea; jengo hili limeanza kufanya kazi tangu Februari, 2016 ambapo zaidi ya wajawazito 40 hupata huduma kwa wakati mmoja. Idadi ya wajawazito ambao wamepata huduma za jengo la mama ngojea ni 181 (2016), 163 (2017) na 114 (2018). Jengo la Mama ngoje lina huduma za mawasiliano na vifaa vya kutunza kumbukumbu kama simu, kompyuta na rejesta.

Kupungua kwa vifo vya wajawazito; Mkoa wa Shinyanga umefanikiwa kupunguza vifo kutoka 74 mwaka 2016 hadi 54 mwaka 2018. Uwepo wa huduma za mama ngojea umesaidia kupunguza idadi ya vifo kutokana na wajawazito wengi kupata fursa ya huduma za afya kwa urahisi na kwa wakati.

Uhakika wa kupata maji tiba; uapatianaji wa maji tiba umekuwa wa uhakika tangu kuanzishwa kwa kiwanda ambapo lita 120 huzalishwa kati ya mahitaji ya lita 240 kwa siku. Gharama za kununua maji tiba zimepungua kutoka TZS 1,500 hadi TZS 676 kwa 500m.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga ikishirikiana na Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na wadu wa maendeleo imeweka mikakati mbalimbali katika kuhakikisha jitihada hii inakuwa endelevu. Mikakati hiyo ni;

(i) Kuendelea kuhamasisha jamii ili kushiriki katika zoezi la hiari la kuchangia damu.
(ii) Kuanzisha mfuko wa uchangiaji damu.
(iii) Kuhakikisha bajeti za shughuli za uchangiaji wa damu zinaingizwa katika mipango ya Mkoa na Halmashauri.
(iv) Kuanzisha timu ya ukusanyaji wa damu katika ngazi ya Mkoa.
(v) Kuhusisha wadau mbalimbali katika kusaidia benki ya damu kwa kuchangia fedha na damu.
(vi) Kutoa motisha kwa timu ya kukusanya damu salama.
(vii) Kutoa mafunzo kwa wajawazito na waume zao kuhusu virutubisho anavyopaswa kutumia mjamzito ili kuondoa tatizo la kupungua kwa damu na kuwapatia vyandarua ili kuwakinga na malaria.
(viii) Kuendelea kuboresha huduma za mama ngojea.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga, Hospitali ya Rufaa ya Mkoa na wadau wa maendeleo walifikia mafanikio haya ya kuanzisha benki ya damu, kiwanda cha kuzalisha maji tiba na ujenzi wa jengo la mama ngojea kutokana na ubunifu wa Timu ya Menejimenti ya Mkoa na ushirikiano wa karibu na wadau wa maendeleo.

# HALMASHAURI YA MJI WA KONDOA


**UTHIBITI SHIRIKISHI WA TAKA NGUMU**



***Uzoefu wa H/Mji wa Kondoa***

## 1.0 UTANGULIZI

H/Mji wa Kondoa ni moja kati ya Halmashauri 8 za Mkoa wa Dodoma iliyoanzishwa Julai, 2015. Halmashauri hii inapatikana kati ya Latitudo 4 $^0$5 na 4'05 Kusini na Longitudo 35$^o$46'60 Mashariki ikiwa na eneo la 936.13km$^2$. Halmashauri inapakana na H/W ya Chemba upande wa Kusini, H/W ya Kondoa upande wa Kaskazini, Magharibi na Mashariki. Hali ya hewa ni ya ukame na joto ni kati ya 16$^o$C na 29$^o$C na wastani wa mvua ni kati ya 600mm na 900mm kwa mwaka. Kuna misimu miwili ambayo ni kiangazi (Juni hadi Novemba) na kipindi cha masika (Desemba hadi Mei). Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012, idadi ya watu ni 59,022 (29,177 wanawake na 29,845 wanaume) na wastani wa idadi ya watu katika Kaya ni 4.8. Halmashauri ina Tarafa 2, Kata 8, Mitaa 36 na Vitongoji 89.




***Ramani ya Mji wa Kondoa***

Shughuli za kiuchumi na kijamii zinatofautiana kutokana na eneo, Kata husika na namna wakazi wanavyoingia na kutoka katika eneo ya mji. Wakazi wanaoishi eneo la mji ni wafanyabiashara na wajasiariamali na wale wanaoishi maeneo ya pembezoni (Vijijini) ni wakulima na na wafugaji. Shughuli za kiuchumi katika maeneo ya Mji ni pamoja na masoko, useremala, maduka, viwanda vya kuchakata alizeti, karakana za magari, migahawa na nyumba za kulala wageni. Idadi kubwa ya wakazi wa Mji ni wajasiriamali na 0.2% ni waajiriwa katika sekta za umma na binafsi. Katika maeneo ya pembezoni wakazi hujishughulisha na uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara kama mahindi, alizeti, mtama, muhogo na uwele. Mifugo ni pamoja na ng'ombe, mbuzi na punda.

## 2.0 TATIZO

Halimashauri ilikumbwa na tatizo la ongezeko la taka ngumu kutoka 47.45T hadi 59.22T kwa siku kutokana na ongezeko la watu kutoka 28,337 mwaka 2002 hadi 59,022 mwaka 2012. Udhibiti wa taka ngumu haukuwa shirikishi. Kulikuwa na vizimba vya taka 12 tu katika maeneo ya soko, stendi ya mabasi, Darajani, Iboni, Nyalashi, Ghorofani na Uwanja wa Puma na katika maeneo mengine taka ngumu zilitupwa holela. Vizimba 12 havikuwa na uwezo wa kukusanya taka zote zilizozalishwa katika maeneo ya makazi, viwanda, maduka, nyumba za kulala wageni na vyanzo vingine. Taka zilizosambaa katika maeneo ya makazi zilisababisha uchafuzi wa mazingira na kueneza magonjwa mbalimbali kama kipindupindu, kuhara na homa ya matumbo. Jedwali Na. 1 linaonesha milipuko ya magonjwa.

**Jedwali Na 1: Mlipuko wa Magonjwa**

| Na | Ugonjwa | 2016 | 2017 | 2018 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Kipindupindu | 46 | 0 | 0 |
| 2 | Homa ya matumbo | 123 | 23 | 10 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 3 | Maumivu ya tumbo | 121 | 10 | 0 |
| 4 | Kuhara damu | 97 | 21 | 0 |
| 5 | Kuharisha | 65 | 0 | 0 |

Mbali na magonjwa, kusambaa kwa taka ngumu kuliharibu taswira ya mji. Baadhi ya barabara hazikupitika kutokana na mlundikano wa taka ngumu uliosababishwa na mfumo duni wa ukusanyaji na usafirishaji. Baadhi ya Kaya zillikuwa na tabia ya kukusanya taka ngumu na kuzitupa katika mifereji ya maji ya mbua na kusababisha kuziba na hatimaye mafuriko ya mara kwa mara. Halmashauri iliingia gharama ya TZS 11,940,000 kwa mwezi kugharamia uzoaji wa taka ikiwa ni pamoja na matengenezo ya lori, ununuzi wa dizeli, kulipa vibarua na dereva. Picha ifuatayo inaonesha hali halisi ya uchafu wa mazingira kabla ya jitihada hii.



***Taka ngumu katika eneo la Mnarani na Lori la Halmashauri***

**3.0 LENGO**

Juni 2017, Halmashauri ya Mji Kondoa iliweka lengo la kuboresha udhibiti wa taka ngumu na kupunguza mlipuko wa magonjwa yanayotokana na uchafuzi wa mazingira kwa 100% kufikia mwaka 2018. Malengo mahususi yalikuwa;

(i) Kugatua shughuli za udhibiti wa taka ngumu katika ngazi ya Mtaa kwa 100% kufikia Juni, 2018.
(ii) Kujenga uelewa kwa jamii kuhusu udhibiti wa taka ngumu katika Mitaa 36 kufikia Desemba, 2018.
(iii) Kuanzisha Kamati za Mazingira za udhibiti wa taka ngumu.
(iv) Kuongeza chanzo cha mapato ya Halmashauri kutokana na ada ya ukusanyaji wa taka ngumu.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Jitihada ya H/M Kondoa juu ya udhibiti wa taka ngumu inaenda sambamba na Sheria ya Utunzaji Mazingira ya mwaka 2004 pamoja na Sera ya mazingira ambayo hutoa mfumo wa kisheria na kitaasisi kwa ajili ya utunzaji wa mazingira endelevu. Sera hii pia inaeleza wajibu wa MSM katika usimamizi wa mazingira ambapo baadhi ya wajibu huo ni pamoja na udhibiti wa taka ngumu. Ili kufikia matakwa ya kisera na Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004, H/Mji wa Kondoa ilitekeleza mikakati ifuatayo.

Kufanya kwa maamuzi; Septemba 2016, Afisa Mazingira na Usafi alitoa wazo kwenye Timu ya Menejimenti ya Halmashauri kuhusu ugatuaji wa shughuli za udhibiti wa taka ngumu kwa jamii. Lengo lilikuwa kujadili na kupata suluhu ya namna ya kudhibiti taka ngumu pasipo kuhusisha Halmashauri. Menejimenti ilipokea wazo na kuridhia juu ya ugatuaji wa uthibiti wa taka ngumu kwa jamii na kuamua lifikishwe mbele ya Kamati ya Mipango Miji na Mazingira, Kamati ya Mipango na Fedha na Baraza la Madiwani ilikupata baraka za utekelezaji.

Uhamasishaji wa Madiwani; pendekezo lilijadiliwa katika vikao vya Kamati na mikutano ya kisheria ya Baraza. Baada ya majadiliano Madiwani walikubali pendekezo hilo na kushauri ugatuaji wa udhibiti wa taka ngumu kwa jamii utekelezwe kuanzia Jumamosi ya mwisho ya Julai, 2017 ambayo ilikuwa ni siku ya usafi na jamii kwa ujumla hushiriki zoezi hilo.

Uhamasishaji wa kufanya usafi na uanzishaji wa ada ya ukusanyaji taka; siku ya usafi wa mazingira ambayo hufanyika kila mwezi, Afisa wa Halmashauri alishiriki zoezi hilo pamoja na jamii na kutumia fursa hiyo kuielimisha jamii kuhusu mbinu mpya ya udhibiti wa taka ngumu. Vilevile mikutano ya hadhara ilitumika katika kuelimisha na kuhamasisha jamii. Baada ya uhamasishaji, jamii ilikubali na kupitisha azimio la kuchangia TZS 500 kwa wiki kwa ajili ya ada ya ukusanyaji wa taka ngumu. Kaya zilishauriwa kutunza taka katika ndoo na vifungashio na kuhifadhi sehemu ambayo zitakusanywa na kusafirishwa moja kwa moja hadi eneo la dampo. Wajumbe wa kamati walikusanya ada kwa kutumia mfumo wa kieletroniki kwa kila kaya na wafanyabiashara katika mitaa. Mfumo huu uliwezesha udhibiti wa mapato na matumizi. Kutokana na ada zinazokusanywa, jamii hukodi lori kwa ajili ya ukusanyaji na usafirishaji wa taka hadi eneo la dampo.



***Upakiaji wa taka ngumu katika Kaya***

Uundaji wa Kamati ya Mazingira ya Mtaa; viongozi wa Mitaa waliitisha mikutano ya wananchi kwa lengo la kuunda Kamati za Mazingira. Kamati 36 zilianzishwa zenye wajumbe 10 kwa kila Kamati kuratibu shughuli za usimamizi na uthibiti wa taka ngumu. Kamati zina jukumu la kuhakikisha usafi kwa ujumla, kulinda mazingira, kukusanya taka ngumu katika maeneo ya umma na kuhamasisha utekelezaji wa sheria kwa kushirikiana na Maafisa Watendaji wa Mitaa. Vilevile, Kamati ina wajibu wa kukusanya ada za usafi na kuandaa taarifa juu ya hali ya usafi na utunzaji wa mazingira ambapo taarifa hiyo huwasilishwa kwa Mtendaji wa Mtaa.

Usimamizi shirikishi wa utekelezaji wa sheria ndogo; Juni 2017, H/Mji wa Kondoa ilianza rasmi usafi wa mazingira kwa kutumia sheria ndogo ambazo ziliundwa na H/W ya Kondoa mwaka 2010 pamoja na maboresho yake yaliyofanyika chini ya kifungu Na 160 cha Sheria ndogo ya mazingira ya Mamlaka ya Mji Mdogo wa Kondoa. Sheria ndogo ziliundwa kutokana na sheria mama "Sheria za Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya)". Sheria ndogo zinaelekeza kwamba mtu yeyote atakayevunja sheria ya udhibiti wa taka ngumu atalipa faini ya TZS 50,000 papo kwa papo. Tozo nyingine ambazo usimamizi wake umegatuliwa kwa Watendaji wa Mitaa na Kamati za Mazingira za Mitaa zimeainishwa katika Jedwali Na 2.

**Jedwali Na 2: Tozo zilizogatuliwa kwa Mitaa**

| Na. | Aina ya biashara | Kiwango cha Tozo kwa mwezi | Kiwango cha Tozo kwa Mwaka |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Vileo vya Asili | 1,000 | 12,000 |
| 2 | Maduka ya rejareja | 2,000 | 24,000 |
| 3 | Mama Lishe | 1,000 | 12,000 |
| 4 | Maeneo ya kuuza mbao | 2,000 | 24,000 |
| 5 | Migahawa | 2,000 | 24,000 |
| 6 | Maduka ya Jumla | 5,000 | 60,000 |
| 7 | Nyumba za kulala wageni | 5,000 | 60,000 |
| 8 | Viwanda vya kuchakata vyakula | 4,000 | 48,000 |
| 9 | Viwanda vya kuoka mikate | 3,000 | 36,000 |
| 10 | Karakana za mbao | 4,000 | 48,000 |
| 11 | Baa | 5,000 | 60,000 |
| 12 | Ofisi | 2,000 | 24,000 |
| 13 | Saluni | 2,000 | 24,000 |
| 14 | Duka la nyama | 3,000 | 36,000 |
| 15 | Karakana za magari | 5,000 | 60,000 |
| 16 | Karakana za uchomeleaji | 5,000 | 60,000 |

Matumizi ya ada za ukusanyaji wa taka; Kamati za Mitaa zina mamlaka ya kutumia ada/tozo zilizokusanywa kwenye shughuli zote za usafi ikiwa ni pamoja na kulipa vibarua wa kupakia na kupakua taka, kukodi malori, kununua dizeli na kulipa posho kwa wajumbe wa kamati.

Kuweka vibao vya matangazo ya onyo katika vizimba vya taka vilivyofungwa; mabango ya kuonesha sheria ndogo zilizotungwa na adhabu zake yaliwekwa katika vizimba vya taka vilivyofungwa ili kuufahamisha umma. Lengo ni kuzuia jamii isiendelee kukusanya taka ngumu katika vizimba hivyo na badala yake watunze taka hizo hadi zinapokusanywa na kupelekwa dampo.

**5.0 RASILIMALI**

Rasilimali watu; watumishi wa Halmashauri na wajumbe wa kamati walishiriki kikamilifu katika hatua zote za kujenga uelewa kwa jamii na kusimamia utekelezaji wa jitihada hii. Rasilimali fedha imehusisha TZS 555,000 ambazo zilitolewa awali kama fedha ya kianzio.

**6.0 MATOKEO**

Baada ya kugatua shughuli za udhibiti wa taka ngumu, H/Mji wa Kondoa imeshuhudia matokeo yafuatayo;

(i) Kuongezeka kwa uelewa kuhusu usafi wa mazingira; kutokana na jitihada hii, jamii imebadilika na kuwa na wajibu wa kuhakikisha mitaa yao ni misafi na taka ngumu zinadhibitiwa. Kila mwanajamii huhakikisha usafi wa mazingira yanayomzunguka. Hali hii imepunguza matumizi ya nguvu na adhabu zinazotolewa na Kamati na watendaji wa Kata na Mitaa.

(ii) Kupungua kwa magonjwa ya mlipuko; ugonjwa wa homa ya matumbo umepungua kutoka wagonjwa 123 mwaka 2016 hadi 10 mwana 2018. H/Mji wa Kondoa imefanikiwa kutokomeza magojwa ya mlipuko yatokanayo na taka ngumu.

(iii) Ugatuaji wa usimamizi na udhibiti wa taka ngumu; kabla ya utekelezaji wa jitihada hii, Halmashauri iliwajibika moja kwa moja kushughulikia masuala yote yanayohusu udhibiti wa taka ngumu kama ukarabati wa lori la kubeba taka, usimamizi wa vizimba vya taka, kukusanya ada za usafi, kuajiri vibarua na kukodi malori ya kubeba taka. Baada ya jitihada hii, shughuli zote za udhibiti wa taka ngumu zinafanywa na jamii na kusimamiwa na Halmashauri.

(iv) Kukuza ajira; wajumbe wa Kamati za Mitaa, vibarua na askari wa mgambo wanalipwa posho kutokana na ada za uzoaji wa taka; hii imekuza ajira kwa kundi hili.

(v) Vizimba vya taka ambavyo awali vilitumika kukusanyia taka sasa vimeondolewa na maeneo hayo kupangiwa matumizi mengine.



***Sehemu ya kizimba iliyobadilishwa matumizi***

(vi) Mifereji ya kupitisha maji kipindi cha mvua imekuwa misafi; utekelezaji wa jitihada hii umeondoa tatizo la kutupa taka katika mifereji ambayo iliziba na kuzuia maji kipindi cha mvua.
(vii) Tuzo ya ushindi; mwaka 2018, H/Mji wa Kondoa ilipata tuzo ya mshindi wa kwanza katika mashindano ya usafi wa mazingira ya Mkoa.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Ili kuhakikisha matokeo ya jitihada hii ni endelevu, Halmashauri ilibuni mikakati mbali mbali;

(i) Halmashauri inaendelea kusimamia utekelezaji wa shughuli za usafi wa mazingira katika ngazi za Mitaa.
(ii) Mara kwa mara jamii hujengewa uelewa juu ya umuhimu wa kulipa ada zakukusanya uchafu kwa muda muafaka na juu ya wajibu wao kuhusu usafi wa mazingira.
(iii) Kuendelea kusimamia sheria ndogo za usafi wa mazingira.
(iv) Kuendelea kushirikisha Wenyeviti wa Mitaa katika zoezi la kuelimisha jamii.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Halmashauri ya Mji wa Kondoa imefanikiwa kuleta mabadiliko chanya kwenye usafi wa mazingira na udhibiti wa taka ngumu. Siri ya mafanikio ni;

(i) Kufanya kazi kama timu baina ya maafisa wa Halmashauri na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya katika kusimamia usafi wa mazingira kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi.
(ii) Utayari wa jamii katika kukubali ugatuaji wa mfumo wa usimamiaji na udhibiti wa taka ngumu.

# Sura ya Nne

# Maendeleo ya Jamii Kiuchumi

Sura ya Nne inahusu jitihada za wananchi kujiletea maendeleo ya kiuchumi kupitia dhana mpya ya *"Kijiji Kimoja Zao Moja"*. Dhana hii husisitiza maendeleo yanayotokana na jamii yenyewe kwa kuibua miradi yenye upekee na vijiji vingine. *"Kijiji kimoja zao moja"* ni harakati zilizoanza miaka ya 1970 katika Mkoa wa Oita nchini Japani malengo yakiwa kuinua uchumi vijijini. Lengo mahususi la dhana hii lilikuwa ni kuhamasisha kila kijiji cha Oita kuchagua mradi wa uzalishaji ambao una utofauti wa aina fulani katika mkoa na kuzalisha kwa viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa.

Dhana ya *"Kijiji Kimoja Zao Moja"* inalenga kuinua maendeleo ya jamii na uchumi katika mkoa kupitia kujitolea kuinua uwezo wa wananchi wa ngazi ya chini. Kabla ya kuanzisha harakati hizi katika eneo la Oita, waanzilishi walipata ushirikiano mkubwa wa jamii kupitia mashindano ya mpira na walikuwa na ushirikiano na miji rafiki ya nchi za nje. Mbinu hizi ziliwaweka watu pamoja, ziliwajengea uwezo wa kimaendeleo, na walishirikishana ujuzi waliopata. Mikakati mingine iliyofuata ilikuwa ni kuanzisha sera za jamii kuongeza zaidi thamani ya bidhaa, kuboresha mifumo, kuanzisha zao jipya au la kipekee, ufundi wa kuchakata mazao ya kilimo, utalii, na mtazamo juu ya hali ya jamii.

Dhana ya *"Kijiji Kimoja Zao Moja"* inaonekana kuwa ni njia ya kuimarisha ujasiriamali wa watu wa vijijini kwa kutumia rasilimali, elimu na uzoefu, kufanya kazi zinazoongeza thamani kwa kuzipa utofauti bidhaa zao na kujenga uwezo wa rasilimali watu katika shughuli za uchumi kijijini. Kutumia ujuzi na rasilimali zilizopo bila kuathiri mazingira ni jambo linalotiliwa mkazo sana katika shughuli za dhana hii. Hii ina uhusiano na dhana ya maendeleo yanayotokana na jamii yenyewe. Katika harakati za *Kijiji Kimoja Zao Moja*, kuna msemo maarufu usemao "Fikiri kimataifa lakini tenda kulingana na Mazingira". Sura hii inawasilisha Mbinu Bora kutoka Halmashauri za Wilaya za Kiteto, Simanjiro, Mbulu, Singida na Shinyanga.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Kiteto inahusu Uzalishaji wa Maziwa na Uongezaji wa Thamani. Kabla ya utekelezaji wa jitihada hii, uzalishaji wa maziwa ulikuwa kati ya pakiti 48 na 65 za ujazo wa 500ml na kupata kipato kidogo kati ya TZS 30,000 na TZS 68,000 kwa siku. Bidhaa hizi ziliuzwa kwa TZS 800 kwa pakiti ya maziwa na zilisafirishwa kutoka kiwandani hadi kwa wauzaji wa rejareja kwa kutumia vyombo vya plastiki vya ujazo wa 0.5 lita ambavyo havikuwa na nembo ya utambulisho wala alama ya Shirika la Viwango au Mamlaka ya Chakula na Dawa katika kuonesha ubora wa bidhaa. Hali hii ililazimu kuchukua hatua za kuboresha ufugaji ili kuchochea uchumi na kupunguza umasikini kwa kuongeza thamani ya mazao ya mifugo. Mbinu zilizotumika ni kukuza uelewa, kuanzisha kiwanda cha maziwa, kujenga uwezo, kuongeza mtaji na kuimarsha ubora wa bidhaa za maziwa. Matokeo ya jitihada hii ni uwepo wa kiwanda cha maziwa, kuongezeka kwa uzalishaji na uongezaji wa thamani ya maziwa, uwepo wa soko la ukahika la maziwa na jamii kunufaika na bidhaa bora za maziwa. Mafanikio ya jitihada hii yanatokana na hali ya hewa ya Kiteto inayostawisha mifugo, uwepo wa ardhi ya kutosha kwa ajili ya malisho na uongozi imara wa wajumbe wa bodi ya ushirika.

Mbinu bora ya Halmashauri ya Simanjiro inahusu kuboresha maisha kwa uongezaji wa thamani ya ngozi. Awali ngozi za wanyama zilionekana kutokuwa na faida yeyote hivyo zilitupwa. Wastani wa ngozi za

ng'ombe 50 na za mbuzi 130 zilizalishwa kwa wiki na hazikuwa na soko. Hakukuwa na kiwanda cha kuchakata ngozi na kuzalisha bidhaa kama viatu, mikanda na pochi. Hali hii iliwanyima fursa za ajira watu wa Simanjiro katika kutengeneza bidhaa za ngozi. Jitihada hii ililenga kuboresha maisha ya watu wa Simanjiro kwa kuanzisha kiwanda cha ngozi, kuanzisha vikundi vya uchakataji wa ngozi, kujenga uwezo kwa vikundi, kuwezesha mitaji na kujenga miundombinu ya uchakataji wa ngozi. Matokeo ya Jitihada hii ni kuanzishwa kwa kiwanda kidogo cha uchakataji wa bidhaa za ngozi katika eneo la Mirerani, upatikanaji wa bidhaa za ngozi zenye ubora kwa bei nafuu, kuanzishwa kwa soko la ngozi na kuongezeka kwa fursa za ajira. Matokeo haya yanatokana na ushirikiano baina ya Halmashauri na wadau na wanachama wa MILEPROMA, upatikanaji wa ngozi ghafi kwa bei nafuu, utayari wa Afisa Maendeleo ya Jamii na Afisa mifugo katika kuhamasisha jamii, uwazi na kuaminiana kati ya wanachama wa kikundi.

Jitihada ya H/W ya Mbulu imelenga katika uzalishaji wa iitunguu swaumu na uongezaji wa thamani, ambayo imetekelezwa na Ushirika wa DIDIHAMA katika Kata ya Bashay. Kabla ya mwaka 2003 shughuli za uzalishaji na uuzaji wa vitunguu swaumu zilifanya kienyeji na wakulima wadogo. Wakulima walizoea kupata mavuno kidogo kwa ekari, ukosefu wa huduma za ugani, mbinu duni za uzalishaji, bei ndogo na mfumo mbovu wa masoko. Halmashauri ilitumia mbinu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuunganisha wakulima, kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji, kujenga maghala na barabara, kuanzisha Ushirika wa Wakulima, kuongeza thamani ya mazao, kujenga uwezo wa wakulima na kuboresha bei ya vitunguu swaumu. Jitihada hii iliwaunganisha wakulima, ikaimarisha uzalishaji na masoko na kuongeza kipato cha kaya. Mafanikio haya yametokana na kufanya kazi kwa bidii kwa watumishi wa Halmashauri, Baraza la Madiwani, utayari na uchapakazi wa jamii ya kabila la Wairaqw, hali ya hewa na mazingira yanayoruhusu kustawi kwa zao hili.

Mbinu bora ya Singida inahusu udhibiti wa ugonjwa wa kideri ili kuboresha uzalishaji wa kuku. Ufugaji wa kuku katika H/W ya Singida ni shughuli ya jamii za watu maskini wa vijijini wanaotumia mbinu ya ufugaji wa holela. Kulikuwa na uzalishaji duni kutokana na kushamiri kwa magonjwa ya kuku hasa ugonjwa wa kideri ambao ulizababisha vifo vya kuku kwa zaidi ya 50% hadi 90% kila mwaka. Hali hii ililazimu Halmashauri kuanzisha jitihada hii ili kuwa na uhakika wa chakula na kuondoa umasikini. Mikakati ya utekelezaji ni kujenga uelewa kwa jamii kupitia mafunzo, kujenga jengo la ututoleshaji wa vifaranga, kuunda vikundi vya ufugaji kuku na benki za ushirika za vijijini (*VICOBA*), kuchagua watoa chanjo kutoka ndani ya jamii na kuendesha zoezi la chanjo. Jitihada hii imejenga uelewa wa jamii kuhusu magonjwa ya kuku, kutibu na kuzuia, kuongezeka kwa uzalishaji wa kuku, kipato na kutengeneza fursa za ajira. Mafanikio yalitokana na ushirikiano baina ya Halmashauri na jamii.

Jitihada ya H/W ya Shinyanga inahusu Uimarishaji Shirikishi wa Miundombinu ya Skimu ya Umwagiliaji ya Nyida. Wakulima katika Kijiji cha Nyida walipata mavuno kidogo kutokana na ubovu wa miundombinu ya umwagiliaji hivyo kusababisha kipato duni. Halmashauri iliamua kuboresha miundombinu ya umwagilaji kupitia mradi wa TANCAID II. Jitihada hii ilitumia mbinu mbalimbali ikiwemo kujenga uelewa, utafiti shirikishi wa kubaini changamoto, upangaji mipango na bajeti shirikishi na uundaji wa kamati ya mradi. Baada ya utekelezaji wa jitihada hii, wakulima waliweza kuongeza eneo la uzalishaji na uzalishaji wa mpunga. Jitihada hii ilifanikiwa kwa sababu mradi ulikuwa hitaji halisi la wakulima. Sababu nyingine ni uongozi imara wa Umoja wa Umwagiliaji, ubunifu wa afisa wa Halmasahuri na uwepo wa mtaalamu kutoka JICA ambaye alifanya kazi kwa ukaribu na wakulima.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA KITETO

**UZALISHAJI NA UONGEZAJI WA THAMANI YA MAZIWA**




*Uzoefu wa Ushirika wa Uzalishaji Maziwa Kibaya*

**1.0 UTANGULIZI**

H/W ya Kiteto ni mojawapo ya Halmashauri 8 za Mkoa wa Manyara, iliyoanzishwa mwaka 1984 ikiwa 220km kutoka makao makuu ya Mkoa wa Manyara - Babati. Halmashauri hii inapakana H/W za Simanjiro upande wa Kaskazini, Kilindi upande wa Mashariki, Gairo na Kongwa upande wa Kusini na Chamwino na Chemba upande wa Magharibi. Halmashauri ipo kwenye Latitudo $40^{0}31'$ na $60^{0}3'$ Kusini na Longitudo $36^{0}15'$ na $37^{0}25'$ Mashariki ikiwa na eneo la 16,685km$^2$ ambalo 3,800km$^2$ hutumika kwa shughuli za kilimo, 12,322km$^2$ kwa mifugo na wanyama wa porini, 560km$^2$ ni misitu na 203km$^2$ maji.

Halmashauri ina eneo lenye ukame wa wastani. Hali ya joto ina wastani wa 22°C huwa na joto miezi ya Julai, Agosti, Septemba, Oktoba na Novemba na baridi miezi ya Machi, Aprili, Mei na Juni. Pamoja na kuwepo kwa mabadiliko katika unyevu wa hewa, Halmashauri hupata wastani wa mvua kati 350mm - 700mm kwa mwaka. Kuna msimu mmoja tu wa mvua ambao huanza Januari hadi Mei.

Kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012, H/W ya Kiteto ina watu 244,669, kati yao 120,233 ni wanaume na 124,436 ni wanawake na ongezeko la 3.2% kwa mwaka. Makabila makuu ni Wamasai (32%), Wagogo (27%), Warangi (18%) na Wanguu (2.6%). Makabila mengine yanaunda 20.4% ya watu wote. Halmashauri imegawanyika katika Tarafa 7, Kata 23 na Vijiji 63.

Shughuli kuu za kiuchumi ni kilimo na ufugaji. Takribani 90% ya wakazi hushughulika na ufugaji na 10% hufanya shughuli nyingine za kiuchumi kama biashara, viwanda vidogo na ufugaji nyuki. H/W ya Kiteto ndiyo yenye mifugo mingi zaidi mkoani Manyara. Jumla ya 247,576.4ha za ardhi zimetengwa kwa ajili ya malisho.

**Jedwali 1: Idadi ya Mifugo katika H/W ya Kiteto**

| S/N | Kata | Aina ya Mifugo | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Ng'ombe | Mbuzi | Kondoo | Nguruwe | Punda | Kuku |
| 1 | Chapakazi | 6,547 | 4,475 | 1,996 | 220 | 226 | 6,159 |
| 2 | Bwagamoyo | 1,242 | 631 | 465 | 3,026 | 42 | 3,026 |
| 3 | Makame | 28,019 | 20,847 | 15,277 | 0 | 616 | 4,405 |
| 4 | Ndirigishi | 8,480 | 11,250 | 2,996 | 284 | 51 | 4,350 |
| 5 | Kibaya | 99 | 97 | 5 | 97 | 0 | 1,345 |
| 6 | Ndedo | 12,200 | 22,345 | 6,960 | 0 | 974 | 1,352 |
| 7 | Kaloleni | 391 | 984 | 196 | 135 | 10 | 3,491 |
| 8 | Matui | 2,967 | 2,079 | 841 | 521 | 120 | 1,606 |
| 9 | Lengatei | 33,064 | 35,323 | 16,000 | 0 | 561 | 7,086 |
| 10 | Engusero | 10,816 | 13,434 | 2,809 | 162 | 251 | 10,961 |
| 11 | Dosidosi | 3,137 | 2,944 | 1,235 | 2 | 31 | 2,737 |
| 12 | Laiseri | 33,286 | 12,531 | 4,848 | 28 | 191 | 10,112 |
| 13 | Bwawani | 1,926 | 1,043 | 253 | 8 | 0 | 1,742 |
| 14 | Njoro | 21,101 | 30,075 | 11,687 | 0 | 1,076 | 20,558 |
| 15 | Loolera | 19,731 | 13,681 | 5,772 | 0 | 1,077 | 8,605 |
| 16 | Kijungu | 5,554 | 9,520 | 7,849 | 25 | 229 | 2,866 |
| 17 | Dongo | 5,208 | 3,103 | 865 | 26 | 31 | 3,412 |
| 18 | Namelock | 24,605 | 37,351 | 6,077 | 0 | 263 | 7,720 |
| 19 | Olbolot | 9,974 | 7,337 | 4,055 | 0 | 371 | 5,398 |
| 20 | Magungu | 8,322 | 5,062 | 1,264 | 42 | 51 | 5,272 |
| 21 | Partimbo | 61,067 | 43,766 | 18,019 | 92 | 1,786 | 8,436 |
| 22 | Sunya | 35,658 | 23,173 | 16,136 | 237 | 1,052 | 12,825 |
| 23 | Songambele | 4,545 | 2,076 | 305 | 72 | 123 | 16,147 |
| Jumla | | 337,939 | 303,127 | 303,127 | 1,993 | 9,122 | 149,611 |

Miundombinu ya kuhudumia idadi hii kubwa ya mifugo haitoshelezi; kuna mabwawa 23 tu yanayotoa huduma kati ya 46 na majosho 27 ya kuhudumia ng'ombe 940,000. Upungufu wa miundombinu ya

kustawisha mifugo husababisha ongezeko la vifo vya mifugo. Changamoto nyingine ni magonjwa kama ndigana (75%), kwato na midomo (20%) na minyoo (5%).

Mbali na nyama kama zao la mifugo, ngozi na maziwa ni mazao mengine yenye thamani kubwa. Uzalishaji wa maziwa katika Halmashauri ni kati ya lita 100,000 na 120,000 kwa siku wakati wa masika na hupungua kufika nusu wakati wa miezi ya kiangazi. Wastani wa uzalishaji wa maziwa kwa ng'ombe ni lita 1 hadi 1.5 kwa siku.

**2.0 TATIZO**
Ufugaji wa ng'ombe ni moja ya shughuli kuu za kiuchumi kwa wakazi wa H/W ya Kiteto; kabila la Wamasai likiongoza. Hali ya hewa na mazingira kuruhusu mifugo kustawi vyema. H/W ya Kiteto ina eneo kubwa la malisho ambalo linaruhusu ufugaji katika Kata zote kama ilivyoneshwa kwenye jedwali Na. 1.

Kuanzishwa kwa kikundi cha wazalishaji wa maziwa mwaka 2012 katika Mji wa Kibaya, kulilenga kukusanya, kuchakata na kuuza mazao yatokanayo na maziwa. Wakati wa kuanza kwa jitihada hii mwaka 2012, uzalishaji ulijikita katika kuzalisha maziwa na mtindi. Uzalishaji ulikuwa mdogo kati ya paketi 48 na 65 za 500ml mauzo yakiwa kati ya TZS 30,000 na 68,000 kwa siku. Maziwa yaliuzwa kwa TZS 800 kwa paketi. Bidhaa hizi ziliuzwa na kusafirishwa kutoka kiwandani hadi kwa wachuuzi wa rejareja katika vifungashio vya nusu lita ambavyo havikubandikwa nembo za utambulisho wala ya kuonesha ubora kutoka Shirika la Viwango au Mamlaka ya Chakula na Dawa.

Vyombo vya kutunzia maziwa ambavyo vilitumika katika uzalishaji havikuwa na kiwango kinachotakiwa. Wazalishaji wa maziwa walitumia ndoo za plastiki na za chuma badala ya kutumia vifaa vya aluminium ambavyo vinapendekezwa katika kuhifadhi maziwa. Hii ilisababisha changamoto katika usafirishaji wa maziwa kwa wauzaji wa rejareja. Japokuwa bidhaa mbalimbali zingeweza kuzalishwa kutokana na maziwa, ushirika ulijikita katika kuzalisha maziwa na mtindi tu. Mazao kama siagi na jibini hayakuzalishwa.

**3.0 LENGO**
Lengo kuu la Halmashauri na Ushirika wa Maziwa Kibaya katika jitihada hii ni kuongeza tija katika ufugaji ili kuimarisha uchumi na kupunguza umasikini. Malengo mahususi ni pamoja na;

(i) Kuanzisha ushirika wa wazalishaji wa maziwa.
(ii) Kuimarisha kipato cha wanachama wa ushirika na wafugaji.
(iii) Kuongeza fursa za ajira.
(iv) Kuongeza mnyororo wa thamani wa mazao ya mifugo.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**
Jitihada ya Ushirika wa Maziwa Kibaya inatokana na kutekelezwa kwa mikakati mabalimbali tangu mwaka 2012 kikundi cha wazalishaji wa maziwa kilipoanzishwa. Mikakati iliyotumiwa na ushirika huu imejadiliwa hapa chini.

Kufanya maamuzi ya awali; mwanzoni mwa mwaka 2012 wafugaji kwa kushirikiana na Afisa Mifugo walianzisha kikundi cha uzalishaji maziwa. Baadaye Afisa Ushirika alifanya juhudi ya kuanzisha na kusajili ushirika. Mwaka 2016, H/W ya Kiteto ilitoa usaidizi kwa Kikundi cha wazalishaji maziwa Kibaya cha awali kuunda Ushirika wenye nguvu. Usaidizi huu ulihusu kuandaa katiba, kuuza hisa za ushirika, kuitisha mkutano mkuu wa mwaka na kufanya uchaguzi wa uongozi; Mwenyekiti wa Bodi ya Ushirika, Mweka hazina na wajumbe 7 wa bodi.

Kukuza uelewa na kuanzisha kiwanda; Halmashauri ilifanya mikutano mbalimbali na jamii kuhusu uzalishaji na uchakataji wa maziwa na kuunda mfumo wa kuunganisha wafugaji na ushirika. Vilevile ushawishi ulifanywa kwa wafugaji kutoka vijiji jirani ili kujiunga na ushirika. Hatua hii ilichochea ujenzi wa kiwanda cha uchakataji wa maziwa na kuanzisha vituo vya kukusanyia maziwa. Ili kufanya kiwanda kuwa na ufanisi, ushirika ulinunua genereta ya dharura, pikipiki na kuanzisha vituo vya mauzo katika vijiji vya Mrijo na Njoro.

Usaidizi na usimamizi kutoka H/W ya Kiteto; Halmashauri ilitoa ardhi na kujenga jengo linalotumiwa na ushirika. Ujenzi wa jengo la ushirika ulitokana na andiko liliandaliwa na Afisa Mifugo na Uvuvi ambalo liliwasilishwa katika kikao cha Timu ya Menejimenti ya Halmashauri na hatimaye kwenye Kamati ya Fedha na kupata ridhaa ya Baraza. Idara ya Mifugo iliendelea kutoa usaidizi kwa wanachama wa ushirika kuhusu ufugaji na uzalishaji bora wa maziwa. Idara ilitoa mafunzo ya kuongeza maarifa na ujuzi juu ya ufugaji wa kisasa kama kudhibiti magojwa, chanjo, matumizi sahihi ya madawa na maboresho ya malisho.



***Jengo la uchakataji wa maziwa la Ushirika wa Kibaya***

Utambulisho wa bidhaa za maziwa; Halmashauri ilitoa usaidizi katika kupata na kusajili nembo ya utambulisho kutoka Shirika la Viwango na Mamlaka ya Chakula na Dawa na kupata vyeti vya uthibitisho juu ya ubora wa bidha kwa matumizi ya binadamu.

Kujenga uwezo na ufadhili; shirika lisilo la kiserikali la TRIAS linalojihusha na ujenzi wa uwezo wafugaji juu ya ufugaji bora lilitoa usaidizi kwa Ushirika kwa kuendesha mafunzo. Halmashauri iliunganisha Ushirika na vyama vya ushirika vya Ufaransa (SOLIDAL na AFD) ambavyo vilitoa TZS 204 milioni kwa ajili ya mtaji wa kuanzisha Ushirika wa Maziwa Kibaya. Fedha hizi zilitumika kununua aina za ng'ombe wenye uzalishaji mkubwa wa maziwa na kuendesha mafunzo kwa wafugaji kuhusu uchakataji wa maziwa.

Udhibiti wa ubora; uendeshaji wa Ushirika wa Maziwa Kibaya unasimamiwa na Afisa Ushirika wa Halmashauri na Maafisa Mifugo. Kuhusu utawala na usimamizi wa fedha, Shirika la Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika husimamia uendeshaji wa Ushirika kwa kufanya ukaguzi wa mahesabu kila mwaka na kutoa taarifa kwa mujibu wa sheria ya ushirika.

## 5.0 RASILIMALI

Uanzishaji na uendeshaji wa ushirika umefanikiwa kutokana na matumizi ya rasilimali mbalimbali ambazo ni rasilimali watu, fedha na vifaa. Maafisa wa Halmashauri, wanachama wa ushirika na wafugaji wamehusika kwa kiasi kikubwa katika utekelezaji wa jitihada hii. Rasilimali nyingine zimeainishwa kwenye jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2 : Rasilimali za Ushirika wa Maziwa Kibaya**

| S/N | Rasilimali | Idadi | Thamani |
|---|---|---|---|
| 1 | Vifaa vya uchakataji | 1 | 20,000,000 |
| 2 | Pikipiki | 1 | 5,000,000 |
| 3 | Pikipiki | 1 | 4,500,000 |
| 4 | Ndoo za kuhifadhi maziwa | 6 | 1,600,000 |
| 5 | Mtambo wa kuchemsha maziwa | 1 | 4,000,000 |
| 6 | Mtambo wa kuchemsha maziwa | 1 | 2,000,000 |
| 5 | Wafanyakazi | 4 | 650,000 |
| 6 | Mtambo wa kufungasha | 1 | 800,000 |
| 7 | Jokofu | 1 | 2,000,000 |
| 8 | Jokofu | 1 | 1,200,000 |

## 6.0 MATOKEO

H/W ya Kiteto imeshuhudia matokeo mbalimbali ambayo yametokana na uwepo wa Ushirika. Matokeo haya ni kama ifuatavyo.

Uwepo wa kiwanda cha uchakataji wa maziwa; ushirika una mali mbalimbali zinazorahisisha uchakataji. Hii ni pamoja na jengo, mitambo ya uchakataji, uhifadhi na ufungashaji wa maziwa, pikipiki 2 zinatumika kusambaza bidhaa kwa wauzaji wa rejareja mjini Kiteto na vijiji jirani vya Mrijo, Njoro na Mbigiri. Vilevile Ushirika unamiliki jenereta inayowezesha kiwanda kufanya kazi umeme wa gridi unapokatika na tangi la kuhifadhi maji kwa matumizi wakati wa upungufu.



***Jenereta, pikipiki 2 na tangi la maji***

Kuongezeka kwa uzalishaji wa maziwa na uchakataji; uwepo wa ushirika umechochea kuongezeka kwa uzalishaji wa maziwa kutoka lita 50 kwa siku mwaka 2002 hadi kufikia lita 250 - 300 mwaka 2018 kwa siku. Mauzo kwa siku yameongezeka kutoka TZS 100,000 hadi TZS 300,000 kwa siku. Kutokana na uwepo wa ushirika, wafugaji wamepata uhakika wa kuuza maziwa yanayokidhi vigezo. Kiwanda kina uwezo wa kuchakata hadi lita 3,000 kwa siku; kiwango ambacho ni kikubwa kuliko maziwa yanayozalishwa.

**Jedwali 3: Mauzo kabla na baada ya kuimarishwa Ushirika**

| Kabla | | Baada | |
|---|---|---|---|
| **Mwezi (Mwaka 2012)** | Mauzo | **Mwezi( Mwaka 2018)** | Mauzo |
| Desemba | 1,560,000.00 | Desemba | 13,294,336.00 |
| Oktoba | 1,464,000.00 | Novemba | 20,168,836.83 |
| Septemba | 1,200,000.00 | Oktoba | 15,735,437.42 |
| Agosti | 1,392,000.00 | Septemba | 18,455,537.42 |
| Julai | 1,152,000.00 | Agosti | 12,394,938.00 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Juni | 1,680,000.00 | Julai | 12,890,162.52 |

Uhakika wa soko la maziwa kwa wafugaji; uwepo wa kiwanda cha uchakataji imekuwa fursa kwa wazalishaji wa maziwa katika H/W ya Kiteto hususani eneo la Kibaya. Kabla ya jitihada hii ziada ya maziwa yaliyozalishwa iliharibika kutokana na kukosa soko na bei kuwa chini. Kuwepo kwa kiwanda, kumesaidia maziwa kununuliwa, kuhifadhiwa na kuuzwa katika mfumo wa bidhaa mbalimbali. Utengenezaji wa bidhaa mchangajiko kutokana za maziwa (Maziwa mabichi, Mtindi, Jibini na siagi) umeongeza soko la maziwa.

Upatikanaji wa bidhaa bora za maziwa; wakazi wa mji wa Kibaya wanapata bidhaa za maziwa zenye ubora. Udhibiti wa ubora wa maziwa unaanza kwa kuzingatia mbinu bora za ufugaji, kuyapima katika maabara mara baada ya kupokelewa kutoka kwa wafugaji na kuzingatia kanuni za usafi wakati wa uchakataji.



***Bidhaa za maziwa; Jibini, Maziwa mabichi na Mtindi***

Kupanuka kwa soko; Ushirika umepanua wigo wa soko la bidhaa zake katika miji ya Morogoro, Arusha na Dodoma. Soko la awali lilikuwa kwa vijiji vya H/W ya Kiteto (Njoro na Mrijo) ambavyo vipo mbali na kijiji cha Kibaya uchakataji unapofanyika.

Idadi ya wanachama katika Ushirika imeongezeka; Ushirika ulianza na wanachama 20 mwaka 2012 na kufikia wanachama 100 mwaka 2018. Ongezeko la wanachama limechangia kuongezeka kwa mtaji kutokana na ada ya kiingilio, ununuzi wa hisa na riba ya mikopo inayotolewa kwa wanachama.

Kupatikana kwa fursa za ajira; kuanzishwa kwa ushirika kumechochea fursa za ajira kwa jamii ya watu wa kikiji cha Kibaya. Mwaka 2018 watu 4 wameajiriwa (wanaume 3 na mwanamke 1) ambao wanalipwa mshahara. Wajumbe 10 wa bodi ni waajiriwa wa muda. Fursa nyingine zisizo za moja kwa moja ni pamoja na vijana na wanawake wanaokusanya maziwa kutoka kwa wafugaji na kuyauza kiwandani.



***Waajiriwa katika ushirika wa kibaya***

Tuzo; Ushirika wa Kibaya umekuwa kati ya wazalishaji bora wa maziwa Tanzania. Katika mashindano ya kitaifa yaliyofanyika mwaka 2018 Jijini Dodoma yakihusisha wazalishaji wa bidhaa za maziwa, Ushirika wa Kibaya ulipata tuzo ya mshindi wa tatu.



***Tuzo ya ushirika wa Kibaya***

## 7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU

Ushirika wa Maziwa Kibaya umekuwepo kwa zaidi ya miaka 15. Uendelevu wa ushirika unatokana na michango ya wanachama, kununua na kuuza hisa na fedha zinazotokana na uuzaji wa bidhaa za maziwa. Kutokana na kuzalisha bidhaa mchanganyiko zitokanazo na maziwa uhakika wa soko la bidhaa hizo umekuwepo. Ushirika una mipango ya kupanua wigo wa uzalishaji kwa kuwafikia wazalishaji wengi wa maziwa na kupanua kiwanda cha uchakataji. Halmashauri ina mpango wa kutafuta wadau kuwezesha ushirika, ufugaji na kuongeza thamani kwa mazao ya mifugo.

## 8.0 SIRI YA MAFANIKIO

Mafanikio ya Halmashauri na Ushirika wa Kibaya yanatokana na sababu mbalimbali. Hali ya hewa ya H/W ya Kiteto ni nzuri kwa uzalishaji wa maziwa. Siri ya mafanikio ni uwepo wa ardhi ya kutosha kwa ajili ya malisho, Halmashauri kutoa ardhi bure kwa ajili ya ujenzi wa kiwanda cha maziwa na uongozi thabiti wa bodi ya wadhamini ya ushirika.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA SIMANJIRO


**UONGEZAJI WA THAMANI YA NGOZI NA UBORESHAJI WA MAISHA**



*Uzoefu wa Kikundi cha MILEPROMA*

## 1.0 UTANGULIZI

H/W ya Simanjiro ni moja kati ya Halmashauri 8 za Mkoa wa Manyara, inayopatika kati ya Latitudo $3^0$ 45" na $5^0$ 15" Kusini na Longitudo $3^0$ 15" na $38^0$ Mashariki. Halmashauri ipo katika mwinuko wa kati ya 560m hadi 2,123.04m kutoka usawa wa bahari na inapakana na H/W ya Arumeru upande wa Kaskazini, H/W za Hai na Moshi upande wa Kusini, Kiteto na Kondoa upande wa Magharibi na Mwanga, Same, Handeni, Kilindi na Korogwe upande wa Mashariki. Halmashauri ina Tarafa 6, Kata 18, Vijiji 57 na Vitongoji 281. Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012, H/W ya Simanjiro ina watu 178,693 kati yao 89,718 wanawake na 88,975 wanaume.




***Ramani ya Mkoa wa Manyara***

Eneo la Halmashauri ni 20,591km$^2$; 600km$^2$ ni eneo linalofaa kwa kilimo, 12,682km$^2$ ni pori tengefu, 75km$^2$ vyanzo vya maji na sehemu nyingine iliyobaki ni milima na makazi. Shughuli kuu za kiuchumi ni ufugaji, kilimo, madini, uwindaji wa kitalii na ufugaji nyuki. Wananchi wengi (80%) ni wafugaji wa ng'ombe, kondoo, mbuzi, kuku, punda, ngamia na nguruwe. Inakadiriwa kwamba Halmashauri ina ng'ombe 437,925, kondoo 225,003, mbuzi 396,452, nguruwe 896, kuku 94,429, punda 21,867 na ngamia 55. Mazao yanayolimwa ni mahindi, maharage, mbaazi, alizeti, vitunguu maji, vitungu swaumu, mpunga na mtama. Halmashauri ina madini mbalimbali kama *Tanzanite, ruby, green garnet, green tourmaline* na *rhodelite*. Madini haya huchimbwa katika maeneo ya Mirerani, Kangala, Landanai, Komolo, Namalulu, Kitwai na Naberera. Utalii wa tamaduni za Wamasai na Akie (Ndorobo), uwindaji wa wanyama na utalii wa picha huchangia katika shughuli za kiuchumi.

## 2.0 TATIZO

H/W ya Simanjiro ni moja ya Halmashauri zenye idadi kubwa ya mifugo. Mazao yatokanayo na mifugo ni mengi; nyama, maziwa, mbolea na ngozi. Uhitaji wa bidhaa hizi, matumizi yake na bei zake vinatofautiana kwa kiasi kikubwa. Hata hivyo, ngozi za mifugo hazikuwa na faida yeyote hivyo kutekelezwa katika maeneo ya machinjio au kutupwa. Wastani wa ngozi 50 za ng'ombe na 130 za mbuzi zilizalishwa kwa wiki na hazikuwa na soko. Ngozi ambazo zilitelekezwa katika maeno ya machinjio zilisababisha harufu mbaya kwa wakazi wanaozunguka eneo hilo. Halmashauri iliingia gharama ya kuzoa ngozi zilizotelekezwa ambapo TZS 35,000 zilitumika kwa wiki. Pamoja na kuwepo kwa malighafi ngozi,

hapakuwa na viwanda vya kuchakata na kutengeneza bidhaa mbalimbali za ngozi kama viatu, mikanda, na pochi. Hali hii iliwanyima wananchi wa Simanjiro fursa za ajira.

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuboresha maisha ya wananchi kwa kuongeza thamani ya ngozi katika H/W ya Simanjiro. Malengo mahususi ni pamoja na;

(i) Kuongeza uelewa kwa jamii kuhusu faida za ngozi.
(ii) Kuongeza bei ya ngozi ghafi kutoka TZS 0 hadi kifikia angalau TZS 1,000.
(iii) Kujenga kiwanda cha kuchakata na kuzalisha bidhaa za ngozi.
(iv) Kuongeza fursa za ajira kupitia uchakataji wa ngozi kutoka 0 hadi 300.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Mwaka 2010, shirika lisilo la kiserikali la World Vision lilibaini kuwa ngozi hazikuwa na thamani yeyote katika Halmashauri ya Simanjiro na zilitelekezwa badala ya kuchukuliwa kama rasilimali. World Vision iliona kuna umuhimu wa kujenga uelewa kwa jamii kutambua kwamba ngozi zinaweza kutumika kama fursa ya kujipatia kipato. Katika kufikia malengo haya, mikakati mbalimbali ilibuniwa na imechambuliwa hapa chini.

Uhamasishaji wa jamii; mwaka 2010 maofisa wa World Vision na wanachama wa UVIMASHA walihudhuria maonesho ya JuaKali nchini Kenya na kujifunza mbinu za kutengeneza bidhaa za ngozi. Baada ya kurejea walianzisha mchakato wa kuchakata ngozi katika Kata ya Mirerani. Jamii ilishirikishwa katika mchakato huu na kuvutiwa kujifunza kutumia ngozi katika kutengeneza bidhaa mbalimbali. World Vision ilihamasisha kuanzisha vikundi katika kutekeleza jitihada hii.

Uundaji wa vikundi; mwaka 2010, watu 27 walijiunga na kutengeneza kikundi cha uchakataji na utengenezaji wa bidhaa za ngozi kilichofahamika kwa jina la *Mirerani Leather Processing & Product Manufacturing (MILEPROMA).* Kikundi hiki kilisajiliwa na Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni *(BRELA)* kwa namba ya usajili Na. 432759 ya tarehe 14. 07. 2017. Wanachama wa kikundi walipata usaidizi wa World Vision kuhudhuria mafunzo juu ya uchakataji ngozi-ghafi yalitolewa na Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO).

Kukuza uwezo wa wanachama; wanachama walipatiwa ziara ya mafuzo ya kuongeza maarifa na ujuzi wa kutengeneza bidhaa za ngozi. Mwaka 2010, wanachama 27 walihudhuria mafunzo kuhusu uundaji na uendeshaji wa vikundi. Mwaka 2011 wanachama hawa walipatiwa TZS 250,000 kwa ajili ya kununua ngozi ili kuendesha mafunzo kwa vitendo kuhusu uchakataji na utengenezaji wa bidhaa za ngozi kama pochi, mikanda na viatu. Mafunzo haya yalifadhiliwa na World Vision na UVIMASHA.

Mwaka 2012, wanachama 110 waliendelea kupata mafuzo ya ziada kuhusu uundaji wa vikundi, ujasiriamali, uchakataji wa ngozi, utengenezaji wa bidhaa za ngozi (viatu, mikoba, kofia). Mafunzo haya yaligharamiwa na Halmashauri, SIDO na shirika lisilokuwa la kiserikali la FAIR TRADE. Mafunzo haya yalifanyika katika ofisi za World Vision zilizopo Kata za Endiamtu na Loibosoit. Mwaka 2013, Mafunzo kuhusu uchakataji wa ngozi yalitolewa kwa wanachama wengine 70. Mafunzo haya yalilenga kujenga uwezo kuhusu hatua za awali za uchakataji wa ngozi na yalifanyika baada ya kusimika miundombinu ya uchakataji.



**Miundombinu ya uchakataji**

Kati ya mwaka 2013 na 2014, mafunzo mengine yalifanyika kwa wajumbe 120 (kutoka vikundi 4). Mafunzo yalihusu uchakataji wa ngozi, matumizi ya mashine za kutengeneza bidhaa za ngozi, masoko na mbinu za ujasiriamali.  Mafunzo yaligharimiwa na Halmashauri, SIDO, MUVI. Vilevile, wajumbe 4 walipelekwa Chuo cha Teknolojia cha Dar es Salaam tawi la Mwanza  kwa mafunzo ya mwezi mmoja kuhusu uchakataji wa ngozi na utengenezaji wa viatu.  Wanachama wengine 12 walihudhuria maonesho ya Sabasaba Dar es Salaam, Nanenane Arusha, Maonesho ya bidhaa za ngozi Kilimanjaro, na Maonesho ya SIDO Kigoma kwa lengo la kujifunza mbinu mbalimbali za uchakataji ngozi. Ziara hizi za mafuzo zirigharamiwa na Halmashauri na MUVI.

Upatikanaji wa mtaji; mwaka 2014 Halmashauri ilitoa mkopo wa TZS 12,000,000 kwa kikundi cha MILEPROMA. Mkopo huu ulitolewa baada ya wanachama kupatiwa mafunzo kuhusu uwekezaji na usimamizi wa biashara.

Ujenzi wa miundombinu ya uchakataji wa ngozi; mwaka 2014, World Vision na UVIMASHA walikipatia kikundi TZS 25,000,000 kwa ajili ya kujenga miundombinu ya uchakataji wa ngozi. Miundominu hii ni pamoja na jengo ambalo lina matangi ya kulowanisha ngozi na mashine za uchakataji.  Mwaka 2015 World Vision na UVIMASHA walijenga miundombinu ya ziada  kuongeza uzalishaji kutoka ngozi 12 (wakati wa kutumia vyombo vya plastiki) hadi 40 kwa kutumia miundombinu ya kisasa . Mwaka huohuo, SIDO ilitoa usaidiza wa mashine 6 za kukata, kugandamiza, kushona,  kulainisha na kupunguza unene wa ngozi ili kuongeza ubora wa bidhaa. Mwaka 2017, Halmashauri ilitoa kemikali ambayo ni bora zaidi kwa kuloweka ngozi hivyo kupunguza muda wa ulowekaji kutoka siku 10 hadi siku 3. Baada ya maboresho haya kiwanda kina uwezo wa kuzalisha viatu vya shule jozi 20 kutoka jozi 5 kwa siku.



***Miundombinu ya uchakataji iliyoboreshwa***

Utafutaji wa masoko ya bidhaa za ngozi; ili kupata masoko, matangazo juu ya bidhaa zinazozalishwa yalifanywa katika maonesho kama Nanenae Arusha mwaka 2017, Sabasaba Dar es Salaam 2018, SIDO kigoma 2017 na Maonesho ya biashara ndogo na za kati (SMEs) Kilimanjaro mwaka 2017. Vilevile Halmashauri iliunganisha kikundi hiki na shule za umma na za binafsi katika kuongeza mauzo ya bidhaa za ngozi ambapo shule 7 za msingi na 2 za sekondari katika Mji mdogo wa Mirerani zilinunua viatu jozi 600.

Kuendesha mafunzo kwa wafugaji kuhusu ubora wa ngozi; ubora wa bidhaa za ngozi hutegemea ubora wa ngozi ghafi. Mwaka 2015 na 2018 wafugaji 500 walipatiwa mafunzo kuhusu ufugaji bora na udhibiti wa kupe ambao huharibu ngozi. Mwaka 2016, wahudumu 24 wa machinjio kutoka Kata za Mirerani na Orkesumet walipatiwa mafunzo kuhusu namna bora za kuchuna ngozi na kupatiwa visu maalumu visivyo na ncha kali vya kuchuna ngozi. Hii ilisaidia kupata ngozi zenye ubora wa daraja 2 kutoka daraja la 3 na 4 wa awali.



***Ngozi zilizoboreshwa***

**5.0 RASILIMALI**

Utekelezaji wa jitihada hii umetumia rasilimali mbalimbali ikiwa ni pamoja na fedha, watu na vifaa. Rasilimali fedha zimebainishwa kwenye jedwali hapa chini.

**Jedwali Na 1: Rasilimali fedha**

| S/N | SHUGHULI | KIASI TZS | CHANZO |
|---|---|---|---|
| 1. | Kuandaa Katiba na usajili wa MILEPROMA (2015) | 2,700,000 | Wanachama wa MILEPROMA |
| 2. | Ununuzi wa mashine 6 (2017) | 20,000,000 | SIDO na MUVI |
| | Mafunzo ya ya kutumia mashine (2016 na 2017) | | |
| | Usajili wa MILEPROMA BRELA | | |
| | Ziara za Mafunzo Moshi, Dar Es Salamu na Kigoma (2017 na 2018) | | |
| 3. | Mafunzo kuhusu uchakataji wa ngozi (2015 hadi 2017) | 12,000,000 | Halmashauri |
| | Ununuzi wa Kemikali ya uchakataji wa Ngozi (2017) | | |
| | Ununuzi wa vitendea kazi ( 2017) | | |
| | Ukarabati wa mifumo ya ulowekaji wa ngozi (2017) | | |
| 4. | Ujenzi wa miundombinu ya uchakataji | 25,000,000 | World Vision na UVIMASHA |
| | Mafunzo ya uchakataji na utengenezaji wa bidhaa za ngozi | | |
| | **JUMLA** | **59,700,000** | |

Rasilimali watu ni pamoja na wanachama na uongozi wa MILEPROMA. Wanachama wamegawanyika katika vitengo 4; kitengo cha uzalishaji (Uchakataji wa ngozi), utengenezaji wa bidhaa za ngozi na kushonea shanga, utengenezaji wa viatu vya shule, mikanda na pochi. Afisa Maendeleo ya Jamii na Afisa Mifugo walishiriki kikamilifu kutoa utaalamu na ushauri. Rasilimali nyingine ni majengo 2 yenye thamani ya TZS 25,000,000 na mashine 6 zenye thamani ya TZS 10,000,000 zinazotumika kuchakata na kutengeneza bidhaa za ngozi.

**6.0 MATOKEO**

Utekelezaji wa Jitihada hii umeleta matokeo yaliyojadiliwa hapa chini.

(i) Uwepo wa kiwanda kidogo cha uchakataji wa bidhaa za ngozi katika Mji mdogo wa Mirerani. Kiwanda hiki kinafanya kazi na kina vifaa na mashine mbalimbali za uzalishaji wa bidhaa za ngozi.



***Wanachama wakiwa kiwandani***

(ii) Upatikanaji wa bidhaa za ngozi kwa gharama nafuu katika soko la Mirerani; mipira imara ya michezo, viatu, vishikio vya fungo, mikanda na pochi.



***Bidhaa bora za ngozi***

(iii) Soko la ngozi ghafi limeanzishwa; awali ngozi za wanyama hazikuwa na thamani yeyote. Baada ya jitihada hii, ngozi inauzwa kati ya TZS 3,000 na TZS 10,000 kulingana na hali ya soko, ubora na ukubwa.

(iv) Fursa za ajira; jitihada hii imetoa fursa za ajira kwa wanachama 14 wanaojihusisha na uchakataji, uzalishaji wa bidhaa za ngozi na utafutaji wa masoko.



***Wafanyakazi katika kiwanda cha bidhaa za ngozi***

(v) Bidhaa zinaitangaza H/W ya Simanjiro; bidhaa zinazotengenezawa zina nembo ya MILEPROMA – Simanjiro na hutangazwa katika maonesho mbalimbal ndani na nje ya nchi.

(vi) Ongezeko la kipato cha wanachama wa MILEPROMA; ajira katika kiwanda cha uchakataji wa bidhaa za ngozi kwa wanachama wa kikundi imeongeza kipato kwa wanachama ambao hujilipa TZS 300,000 kwa mwezi kutoka kwenye mauzo ya bidhaa wanazozalisha.



***Duka la MELEPROMA***

(vii) Kikundi kimekuwa kituo cha kujifunzia; Watu na vikundi kutoka maeneo mbalimbali kama Msitu wa Tembo na Orkesumet (Simanjiro) na kutoka Halmashauri nyingine kama Hanang na Karatu wametembelea MILEPROMA kwa ajili ya kujifunza utengenezaji wa bidhaa za ngozi. Vilevile, wanachama 2 wa MILEPROMA walialikwa Zanzibar kwenda kutoa mafunzo kwa vikundi mbalimbali kuhusu uchakataji wa bidhaa za ngozi.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Ili kuhakikisha matokeo ya jitihada hii yanakuwa endelevu, mikakati ifuatayo imetekelezwa.

(i) Halmashauri inaendelea kutoa usaidizi kwa MILEPROMA kutafuta soko la bidhaa za ngozi ndani na nje ya Halmashauri na kuwaunganisha na wazalishaji wa bidhaa na masoko.

(ii) Mafunzo ya kujenga uwezo kuhusu utengenezaji wa bidhaa nyingi zaidi yanaendelea kutolewa kupitia ziara za mafunzo na maonesho ya Nanenane, Sabasaba na SIDO.

(iii) Halmashauri ina mpango wa kuifanya MILEPROMA kuwa kituo cha kujifunzia kwa kuitangaza kwa Halmashauri za Mikoa jirani na kuiwezesha kuanzisha matawi sehemu nyingine.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Jitihada hii ilifanikiwa kutokana na sababu zifuatazo;

(i) Upatikanaji wa ngozi ghafi kwa bei nafuu.

(ii) Ushirikano imara baina ya Halmashauri, wadau na wanachama wa MILEPROMA.


(iii) Utayari wa Afisa Maendeleo ya Jamii, Afisa mifugo na uongozi wa MILEPROMA.

(iv) Uwazi, utendaji kazi bora na kuaminiana baina ya wanachama wa MILEPROMA.

(v) Jitihada hii inatekelezwa katika eneo la kimkakati (lenye utalii) karibu na Jiji la Arusha na Manispaa ya Moshi ambapo kuna soko kubwa la bidhaa za ngozi.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU

**UZALISHAJI NA UONGEZAJI THAMANI WA VITUNGUU SWAUMU**





***Uzoefu wa Ushirika wa DIDIHAMA – Kata ya Bashay***

## 1.0 UTANGULIZI

H/W ya Mbulu ni moja kati ya Halmashauri 7 za Mkoa wa Manyara iliyopo kati ya Latitudo $3^0$ na $4^0$ Kusini na Longitudo $34^0$ na $35^0$ Mashariki na kupakana na H/W za Karatu upande wa Kaskazini, Babati upande wa Mashariki, Hanang upande wa Kusini na Iramba upande wa Mashariki ikiwa na eneo la 4,350 $km^2$. Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012 Halmashauri ina watu 191,570 kati yao 96,481 ni wanaume na 95,089 ni wanawake. Wastani wa ongezeko la watu ni 3.8 % ukiwa juu ya wastani wa kitaifa wa 2.8% na wastani wa watu katika kaya ni 6.3. Halmashauri ina Kata 18, Vijiji 76 na Vitongoji 362.

Halmashauri ipo katika mwinuko wa kati ya 1,000m (Magharibi) hadi 2,400m (Mashariki) kutoka usawa wa bahari na hali ya hewa ni ya baridi. Kiwango cha mvua ni kati ya 400mm ukanda wa Magharibi na zaidi 1,200mm ukanda wa Mashariki. Wastani wa mvua ni 600mm kwa mwaka; kiwango hiki hakitoshi kuendesha shughuli za kilimo kwa mwaka mzima. Kiwango cha joto kwa mwaka ni kati ya $15^o$ C hadi $24^o$C.




***Ramani ya Mkoa wa Manyara na ya H/W ya Mbulu***

Shughuli kuu za kiuchumi za wakazi wa H/W ya Mbulu ni kilimo na ufugaji zinazochangia 90% ya uchumi wa Halmashauri na huajiri 96% ya nguvukazi; 4% ya nguvukazi ipo kwenye ajira za sekta nyingine. Mazao makuu yanayozalishwa ni mahindi, maharage, mtama, alizeti, vitunguu swaumu, pareto, viazi na choroko. Eneo la 54,000Ha linafaa kwa kilimo, hatahivyo ni 47,834Ha zinatumika kwa kilimo.

## 2.0 TATIZO

Vitunguu swaumu huzalishwa katika bonde la Bashay. Zao hili huhitaji hali ya hewa ya ubaridi na mwanga wa kutosha ili kustawi na kupata mazao yenye ubora. Kilimo cha vitunguu swaumu huhitaji uzimamizi wa karibu, umwagilaji wa mara kwa mara, mtaji na nguvukazi ya kutosha ili kupata mavuno mengi. Hata hivyo, maji kwa ajili ya umwagiliaji hayakutosheleza kutokana na uchache wa vyanzo vya maji na miundombinu duni ya umwagiliaji iliyochangia kupotea kwa 30% ya maji. Vilevile, uhaba wa maji ulitokana na mfumo mbovu wa usimamizi wa ratiba ya kugawa maji ya umwagiliaji.

Kabla ya mwaka 2003, uzalishaji wa vitunguu swaumu na mfumo wa masoko uliendeshwa na wakulima wadogo kwa kutumia njia za asili. Chanzo cha maji ya uwagiliaji kilikuwa Mto Yaeda. 930Ha zilitumika katika uzalishaji wa vitunguu swaumu kwa njia za asili, maji kwa ajili ya umwagiliaji hayakutosheleza mahitaji na hakukuwa na mfumo rasmi wa kugawa maji jambo ambalo lilileta migogoro ya kugawa maji.

Japokuwa Vitunguu Swaumu ni moja ya zao muhimu la biashara la H/W ya Mbulu, wakulima walikumbana na changamoto mbalimbali za uzalishaji na masoko kama ifuatavyo;

(i) Uzalishaji mdogo kwa hekta ukilinganisha na ongezeko la mahitaji. Uzalishaji kwa hekta ulikuwa 3-5T ambapo wastani wa uzalishaji kwa hekta moja ni 8-10T.
(ii) Uhaba wa huduma za ugani; bonde la Bashay halikuwa na Afisa Ugani.
(iii) Teknolojia duni ya uzalishaji; wakulima wengi walitumia jembe la mkono au la kukokotwa na ng'ombe.
(iv) Matumizi hafifu ya pembejeo za kilimo (Mbegu, mbolea za viwandani na kemikali).
(v) Bei ndogo ya vitunguu swaumu (150,000 – 200,000) kwa gunia.
(vi) Miundombinu mibovu ya soko kutokana na ubovu wa barabara na ghala.
(vii) Kukosekana kwa vipimo maalumu vya kupima vitunguu swaumu, kulikuwa na mizani 3 tu ndani ya ghala.
(viii) Upotevu mkubwa wa vitunguu swaumu baada ya mavuno (uharibifu wa 30% ya mavuno).

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la uzalishaji na uongezaji wa thamani ya vitunguu swaumu katika Bonde la Bashay ni kuboresha shughuli za kilimo na maisha ya watu. Malengo mahususi ni pamoja na;

(i) Kuongeza uzalishaji wa vitunguu swaumu kutoka 3T hadi 8T kwa hekta.
(ii) Kupunguza upotevu wa vitunguu swaumu baada ya mavuno.
(iii) Kuanzisha kiwanda cha kuchakata vitunguu swaumu na kupata nembo ya ubora kutoka Shirika la Viwango na Mamlaka ya Chakula na Dawa.
(iv) Kuimarisha vikundi 4 vya wakulima (Busara, Hekima, Amani and Chonde), Vyama 2 vya kuweka na kukopa (SACCOS) na Ushirika wa Wakulima wa DIDIHAMA (AMCOS) katika Kata ya Bashay.
(v) Kuanzisha maghala 2 na kukarabati mengine 2 ya vitunguu swaumu katika Kata za Bashay na Dinamu.
(vi) Kukarabati daraja la Dirim, barabara ya mlisho ya 28km na kalavati 30.
(vii) Kutumia vipimo sahihi wakati wa kuuza na kununua vitunguu swaumu.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Kuunganisha wakulima katika skimu za umwagiliaji; kutokana na uhaba wa maji ya umwagiliaji, mwaka 2003 vikundi vya wakulima vililazimika kujiunga katika skimu 4. Skimu hizo ni Mangisa, Diyomat, Harsha na Dirim ambazo zinatumia chanzo kimoja cha maji ya Mto Yaeda (mto wa msimu). Skimu hizi 4 ziliweza kugawana maji kwa usawa kwa njia ya mserereko. Skimu hizi kwa pamoja zilijiunga na kuanzisha umoja wa umwagiliaji. Mwaka 2004, Timu ya utaalamu ya Halmashauri ilitoa usaidizi kwa vikundi hivi na kusajiliwa kama SACCOS.

Kuboresha miundombinu ya umwagiliaji; mwaka 2005, kupitia Programu ya Maendeleo ya Umwagiliaji Shirikishi (PIDP) uliofadhiliwa na IFAD, bwawa la maji la Mangisa lenye ujazo wa 500,000$m^3$ lilijengwa ili kuhifadhi kiasi kikubwa cha maji ya umwagiliaji. Jitihada hizi za ujenzi wa bwawa na miundombinu mingine ya umwagiliaji ziliongeza uzalishaji kutokana na kuongezeka kwa eneo la uzalishaji kutoka hekta 930 (2002) hadi hekta 1200 (2005) na uzalishaji kwa hekta uliongezeka kutoka 279T (2002) hadi 6,000T (2005).

Ujenzi wa ghala na barabara za mlisho; mwaka 2005, H/W ya Mbulu ikishirikiana na Programu ya Maendeleo ya Kilimo na Mifumo ya Masoko (AMSDP) ilijenga ghala la kuhifadhi vitungu swaumu. Lengo kuu la mradi huu lilikuwa kuwezesha wakulima kuhifadhi mazao baada ya kuvuna wakisubiri bei nzuri. Lengo jingine la ujenzi wa ghala llikuwa kuondoa madalali waliowalaghai wakulima kwa bei ndogo au kuwashawishi kuuza mazao yakiwa shambani. Halmashauri ilitoa uzaidizi katika kujenga miundombinu ya kilimo na masoko kama barabara ya mlisho ya 28km, kalavat 30, daraja 1, maghala 2 na kununua

mtambo wa uchakataji wa vitunguu swaumu. Vilevile, Halmashauri ilitoa mizani kwa ajili ya kuwezesha vipimo sahihi vya mazao na kuunganisha vikundi 3 vya VICOBA na taasisi za fedha (Benki ya Posta, NMB na CRDB).



***Mizani***

Kuanzisha AMCOS; mwaka 2011, AMCOS iitwayo DIDIHAMA ilianzishwa ikiwa na wanachama 50 kutoka kwenye ushirika. DIDIHAMA inatoa huduma za uzalishaji na utafutaji wa masoko. Baadhi ya huduma zinaotolewa na DIDIHAMA ni kutafuta masoko kwa ajili ya mazao, kuratibu upatikanaji wa pembejeo na kusimamia huduma  za ghala la Bashay.



***Ghala na vichanja vya kuhifadhia vitunguu swaumu***

Kuongeza mnyororo wa thamani; mwaka 2013, H/W ya Mbulu kwa kushirikiana na Programu ya Miundombinu ya Masoko, Kuongeza Thamani na Mitaji  Vijijini (MIVARF) ilitoa usaidizi kwenye jitihada ya wakulima  katika kuongeza thamani ya vitunguu swaumu kuanzia teknolojia ya uzalishaji, masoko na uchakataji.  Vilvile, Halmashauri ilitoa pembejeo za kilimo kwa ajili ya uzalishaji wa vitunguu swaumu katika Kata ya Bashay. Vikundi 15 vinatumia vifungashio vya kisasa vilivyopatikana kutoka kiwanda cha PPTL, Tanga.  Vikundi pia vimeunganishwa na huduma za ugani kama TAHA na Mafisa Ugani wa Vijiji, hivyo kuongeza uzalishaji kutoka 3T hadi 5T kwa ekari. Vikundi 5 vimeunganishwa na JB Agrovet na Kisusi Agrovet kwa ajili ya kupata pembejeo. Vilevile, MIVARF ilichangia gharama za ununuzi wa mtambo wa kuchakata vitunguu swaumu  wenye thamani ya TZS 70,850,000 ambapo MIVARF ilichangia 58% (TZS41,250,000), Halmashauri 10%  (TZS 6,750,000) na Jamii 32% (TZS 22,850,000).

Kujenga uwezo na kuboresha bei za soko; MIVARF na SIDO walitoa mafunzo kwa wakulima 30 kuhusu uchakataji wa vitunguu swaumu na kuunganisha vikundi 4, SACCOS 2, na AMCOS 1 na masoko. Vikundi 22 viliunganishwa na wanunuzi kupitia Shirika la Masoko la Kariakoo (KMC) na kuingia makubaliano ya kuhakikisha wakulima wanapata bei nzuri ya TZS 5,500 hadi 6,000 kwa kilo kwa wanunuzi wa rejareaja na TZS 300,000 hadi 330,000 kwa kilo 100 kwa wanunuzi wa jumla. Vilevile, vikundi hivi viliunganishwa na wanunuzi kutoka Msumbiji kupitia KMC ambapo jumla ya 20T zilinunuliwa kwa msimu kupitia Kampuni ya MESULA na 2SEEDS NETWORKS.



***Mafunzo ya uchakataji wa vitunguu swaumu***

Kuongeza mtandao wa masoko; vikundi 7 viliunganishwa na kusajiliwa na TAHA kwa lengo la kupata huduma za ugani, pembejeo na kupata taarifa za masoko. Vikundi hivi viliunganishwa na gazeti la MKULIMA MBUNIFU na kila kikundi hupata nakala zaidi ya 20 za MKULIMA MBUNIFU. Gazeti hili hutoa taarifa mbalimbali ikiwemo taarifa za masoko na mbinu bora za kilimo. Vikundi vyote 22 vinapata taarifa za masoko kupitia mikutano, mbao za matangazo zilizotundikwa katika maeneo ya uzalishaji (Bashay and Diyomat) na vituo vya masoko vilivyopo Bashay.

Kuhakikisha shughuli zote zinafanyika kwa ufanisi, H/W ya Mbulu kwa kushirikiana na SIDO, MVIWATA, MIVARF, JICA, IRDP, MDC, 4CCP, FARM AFRICA, RUDI, TOA, OR-TAMISEMI, DMDD ilitumia mbinu mbalimbali za uhamasishaji wa jamii, upangaji mipango shirikishi wa Fursa na Vikwazo kwa Maendelo (O&OD), usimamizi wa utekelezaji wa sheria ndogo, na ushirikiano na wadau.

**5.0 RASILIMALI**

Utekelezaji wa jitihada ya kukuza uzalishaji na kupanua wigo wa masoko ya vitunguu swaumu katika kata ya Bashay, H/W ya Mbulu, Serikali Kuu na wadau maendeleo walitumia rasilimali mbalimbali katika kila hatua ya utekelezaji.

Hatua 1: Ujenzi wa ghala Kata ya Bashay. Ghala la vitunguu swaumu lilijengwa mwaka 2008 kwa kutumia fedha za AMSDP na H/W ya Mbulu ambapo jumla ya TZS 360,000,000 zilitumika; Halmashauri ilichangia TZS 18,000,000 (5%), jamii TZS 36,000,000 (10%) na AMSDP TZS 306,000,000 (85%).

Hatua 2: Ujenzi wa kiwanda cha uchakataji wa vitungu swaumu katika Kata ya Bashay kwa gharama ya TZS 70,850,000 ambapo MIVARF ilitoa TZS 41,250,000 (85%), H/W ya Mbulu TZS 6,750,000 (5%) na jamii TZS 22,850,000 (10%).

Rasilimali watu ni pamoja na wajumbe wa Timu ya Menejimenti ya Halmashauri, maafisa ugani, uongozi wa AMCOS, SACCOS na vikundi vya wakulima. Rasilimali nyingine ni ardhi ya uzalishaji wa vitunguu swaumu 1,260Ha inayomilikiwa na wakulima na sehemu lilipojengwa ghala na kusimikwa mtambo wa uchakataji yenye 3Ha zinazomilikiwa na DIDIHAMA.

**6.0 MATOKEO**

Mbinu za utekelezaji wa jitihada hii ambazo zilitumiwa na H/W ya Mbulu, wadau mbalimbali na wakulima wa vitunguu swaumu zimeleta matokeo chanya yaliyobainishwa hapa chini;

Uwepo wa umoja thabiti wa wakulima; vikundi nufaika 22 (19 wazalishaji, 2 wachakataji na 1 utafutaji wa masoko) vimeanzishwa na vimesajiliwa na Halmashauri kwa mujibu wa sheria; vikundi vingine 4 vimesajiliwa BRELA. Vilevile, vikundi 102 vya wakulima vimepatiwa mafunzo na kuhamasishwa kuhifadhi mazao yao katika maghala pamoja na kupewa ujuzi wa kuchambua, kupanga katika madaraja na

kufungasha vitunguu swaumu. Wawakilishi wa vikundi wamehudhuria maonesho mbalimbali ya kilimo. Wakulima 73 kutoka AMCOS ya DIDIHAMA wamefuzu katika uchakataji na usindikaji wa vitunguu swaumu.

Uwepo wa miundombinu bora; daraja la Dirim limejengwa kuruhusu usafirishaji na mawasiliano kati ya vijiji na mashamba pamoja na barabara yenye urefu wa 28km na kalavati 30 kuwezesha usafirishaji kipindi chote cha mwaka.

Kuimarika kwa uzalishaji na mauzo; uzalishaji wa vitunguu swaumu umeongezeka kutoka 3T kwa hekta mwaka 2013/2014 hadi kufikia 8T mwaka 2018/2019. Halmashauri imehakikisha kwamba vikundi 102 vya wakulima vinaunganishwa na taasisi za fedha na vikundi 7 vimewezeshwa kujiunga na kusajiliwa TAHA kwa ajili ya kupatiwa huduma za ugani, pembejeo na taarifa za masoko. Mchakato wa soko la vitunguu swaumu unasaidiwa na mfumo wa ghala lililojengwa katika Kata ya Bashay lenye wezo wa kuhifadhi 500,000T na mtambo wa kuchakata vitungu swaumu wenye uwezo wa kuchakata 3.8T kwa siku. Miundombinu mingine ni pamoja na skimu ya umwagiliaji ya Mangisa iliyojengwa na JICA na daraja 1 katika kijiji cha Diyomat lililojengwa na MIVARF. Mtambo wa kuchakata vitunguu swaumu umepunguza upotevu wa mazao baada ya kuvunwa kutoka 30% hadi chini ya 20%.

Kuongezeka kwa pato la kaya; uchakataji wa vitunguu swaumu umeongeza pato la kaya kutokana na mauzo ambapo gunia la vitunguu swaumu ghafi la kilo 100 huuzwa kwa bei kati ya TZS 150,000 hadi TZS 200,000 wakati vitunguu swaumu vilivyochakatwa vya uzito wa kilo 100 huuzwa kati ya TZS 600,000 hadi TZS 640,000. Mizani na vipimo vimewezesha kuongeza kipato katika kaya kutoka TZS 600,000 hadi TZS 5,000,000 kwa mwaka. Ongezeko hili limechochea kuimarika kwa uchumi wa Halmashauri. Ghala la Bashay linatoa fursa kwa wakulima kuongeza thamani ya vitunguu swaumu kwa kukausha kabla ya kuhifadhi (kusafisha, kuchambua, kupanga madaraja na kufungasha).



***Bidha za vitunguu swaumu***

Wakulima wa Vitunguu swaumu wameshuhudia mabadiliko chanya katika kumudu huduma za kijamii na kiuchumi. Kutokana na kuimarika kwa uzalishaji wa vitunguu swaumu, uchakataji na kuboreshwa kwa miundombinu kumewezesha kuunganisha mashamba na huduma za ghala. Ongezeko la uzalishaji na pato la kaya limewezesha wakulima kujenga nyumba bora na uhitaji wa kuunganishwa na huduma za maji na umeme umeongezeka.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

H/W ya Mbulu na wakulima wa vitungu swaumu wamejitolea kuhakikisha jitihada hii inakuwa endelevu. Halmashauri kwa kushirikiana na wadau wote katika myororo wa thamani wa zao la vitunguu swaumu, imeweka mikakati mbalimbali ya uendelevu ambayo ni pamoja na;

(i) Kuboresha mipango na bajeti katika uzalishaji, uchakataji na uuzaji wa vitunguu swaumu kutoka Kata ya Bashay.

(ii) Kuboresha miundombinu ya uzalishaji, uchakataji na uuzaji wa bidhaa za vitunguu swaumu.
(iii) Kuendelea kutafuta rasilimali kwa ajili ya uzalishaji, uchakataji na uuzaji wa bidhaa za vitunguu swaumu.
(iv) Kuimarisha uhusiano wa kimasoko baina ya mkulima, SACCOS na AMCOS na taasisi za masoko ya nje na taasisi za fedha na kupata uhakika wa kupata mikopo ya kilimo.
(v) Kuendelea kutoa mafunzo kwa wakulima juu ya utunzaji, uchakataji, ufungashaji na uuzaji wa vitunguu swaumu.
(vi) Kuendelea kutumia wadau wa ndani na nje katika uzalishaji, uchakataji na uuzaji wa vitunguu swaumu.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Lengo la H/W ya Mbulu lilikuwa kuimarsha shughuli za kilimo na maisha kupitia uzalishaji wa vitunguu swaumu na kuongeza thamani ya zao hilo katika Bonde la Bashay. Mafanikio ya jitihada hii yanatokana na sababu zifuatazo;

(i) Utayari na juhudi za H/W ya Mbulu.
(ii) Juhudi na utayari wa wakulima wa vitunguu swauma wa kabila la Wairaqw.
(iii) Uwepo wa mazingira na rasilimali za asili zinazoruhusu uzalishaji wa vitunguu swaumu.
(iv) Kukubali kutumia mfumo wa ghala na vipimo vinavyokubalika katika uuzaji wa bidhaa za vitunguu swaumu.
(v) Utayari wa vikundi vya wakulima wa vitunguu swaumu kukubali kuchakata na kuongeza thamani.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA SINGIDA

**UDHIBITI WA KIDERI KUBORESHA UZALISHAJI WA KUKU**




***Uzoefu wa H/W ya Singida***

## 1.0 UTANGULIZI

H/W ya Singida ni moja kati ya Halmashauri 7 za Mkoa wa Singida iliyopo kati ya Latitudo 3° na 7° Kusini na Longitudo 33° na 35° Mashariki. H/W ya Singida inapakana na H/W za Mkalama upande wa Kaskazini, Hanang upande wa Mashariki na Ikungi upande wa Kusini. Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012, Halmashauri ina watu 225,521, kati yao 111,772 ni wanaume na 113,749 ni wanawake na wastani wa watu kwa Kaya ni 5.4. Halmashauri imegawanyika katika Tarafa 3, Kata 21, Vijiji 84 na Vitongoji 433.

Halmashauri ina eneo la 6,053km$^2$ ambazo 4,031.8km$^2$ hutumika kwa kilimo, 1,423.2km$^2$ malisho, 517km$^2$ misitu, 77km$^2$ ni eneo lenye maji na 4km$^2$ ni machimbo ya madini na milima. Halmashauri ina hali ya ukame na hupata kiasi kidogo cha mvua kwa mwaka na wastani wa mvua kwa mwaka ni kati ya 600mm hadi 700mm. Kuna misimu miwili; kipindi kifupi cha mvua (masika) katika miezi ya Desemba hadi Machi na kiangazi kati ya Aprili hadi Novemba.




***Ramani ya Mkoa wa Singida***

Shughuli kuu za kiuchumi katika Halmashauri hii ni kilimo na ufugaji ambavyo huajiri 85% ya wananchi. Mazao ya biashara ni alizeti, vitunguu, karanga, mtama, mikunde, dengu, ufuta na pamba na mazao ya chakula ni mahindi, mtama, uwele, maharage, muhugo na viazi vitamu. Ufugaji ni shughuli ya kiuchumi inayochukua nafasi ya pili baada ya kilimo ambapo ufugaji wa kuku huchuka 58%. Shughuli nyingine za kiuchumi ni uvuvi, biashara ndogondogo, uchimbaji wa madini na viwanda vidogo kwa pamoja huunda 15%.

## 2.0 TATIZO

Katika sekta ya mifugo, kuku wa kienyeji ndio viumbe wanaongoza kufugwa. Mara nyingi hufugwa na watu wenye uchumi mdogo katika ngazi ya kaya hasa wanawake na watoto. Ufugaji wa kuku wa kienyeji ni moja ya shughuli ya kiuchumi ambayo haijapewa kipaumbele katika maeneo ya vijijini. Endapo ufugaji wa kuku wa kienyeji katika mazingira ya vijijini ungepata kipaumbele katika mipango na bajeti ya Halmashauri, ungechangia kwa kiasi kikubwa maendeleo ya watu wenye vipato vidogo vijijini.

Katika H/W ya Singida , ufugaji wa kuku wa kienyeji unatekelezwa zaidi na watu maskini na wenye vipato duni na mara nyingi ni ufugaji holela ambapo kuku hujitafutia chakula wenyewe. Kutokana na milipuko ya magonjwa ukiwemo ugonjwa wa kideri, wafugaji wengi wamekuwa wakiathirika kwa kupata mavuno duni ya kuku. Ugonjwa wa Kideri umekuwa ukisababisha vifo vya kuku kati ya 50% hadi 90% kila

mwaka. Idadi ya kuku katika kaya imekuwa ikibadilika kila mwaka kutokana na ugonjwa wa kideri. Idadi ya kuku katika kaya ni kati ya 10 hadi 20 kipindi cha Juni/Julai wakati kuna chakula cha kutosha na hupungua kufikia 0 hadi 3 wakati wa kiangazi na baada ya mlipuko wa ugojwa wa kideri katika miezi ya Oktoba na Novemba. Mlipuko wa ugonjwa wa kideri wa mara kwa mara, ulisababisha wakulima kupata hasara za kiuchumi na kuathiri pato lao hivyo kushindwa kumudu huduma za msingi kama ada za shule, gharama za afya na ujenzi wa makazi bora.

**3.0 LENGO**

Jitihada ya kudhibiti ugojwa wa kideri ilitekelezwa baada ya kutambua kwamba kuku ndio viumbe wanaofugwa kwa kiasi kikubwa, ni chanzo kikubwa cha protini na kipato kwa jamii za vijijini. Lengo kuu la jitihada hii lilikuwa kuimarisha uhakika wa chakula na kuondoa umasikini vijijini. Jitihada hii likuwa na malengo mahususi yafuatayo;

(i) Kuongeza idadi ya kuku kwa kutokomeza mlipuko wa ugonjwa wa kideri.
(ii) Kuongeza maarifa kuhusu ugonjwa wa kideri na namna ya kuudhibiti.
(iii) Kuimarisha hali ya uchumi kwa wananchi wa vijijini.
(iv) Kupunguza athari za kijamii na kiuchumi zinazotokana na ugonjwa wa kideri katika ngazi ya Kaya, kijiji na Halmashauri.

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Jitihada hii imetekelezwa kwa kutumia mbinu mbalimbali. Utekelezaji ulianza kwa Programu ya Jamii ya Kudhibiti na Kukinga Ugonjwa wa Kideri iliyohusu kushauri wafugaji juu ya mbinu rahisi na za kudumu, kuboresha afya ya kuku, kuongeza uzalishaji na kujenga uelewa kwa baadhi ya wafugaji kuhusu faida zitokanazo na ufugaji wa kuku. Programu hii ilikuwa shirikishi. Katika kuhakikisha jamii inakubali na kushiriki katika utekelezaji wa jitihada hii, Vijiji 5 vya mfano (Mughanga, Mwakiti, Nkuninkana, Musungua na Unyangwe) kutoka Kata za Mtinko, Ilongero, Ihanja na Sepuka vilichaguliwa na mafunzo yalitolewa katika ngazi zote za maamuzi (Kata, Vijiji na Vitongoji).

Mafunzo kwa viongozi wa jamii; mwaka 2010 mafunzo ya awali yalitolewa kwa viongozi wa jamii wenye uhusiano wa moja kwa moja na maendeleo ya jamii na afya za mifugo. Viongozi hao ni Madiwani na Wenyeviti wa Vijiji na Vitongiji na wataalamu kutoka Halmashauri. Mafunzo haya yalilenga kutambulisha proramu kwa viongozi wa jamii ilikupata ridhaa katika kuanzisha mpango wa utoaji chanjo ya kideri na elimu ya ufugaji wa kuku katika vijiji, kupanga bajeti na kuweka sheria ndogo ili kuifanya programu hii kuwa endelevu. Warsha ya mafunzo ya siku moja kuhusu faida za kiuchumi na kijamii kutokana na ufugaji wa kuku ilitolewa. Mfano kuhusu idadi ya kuku wanaosafirishwa kila mwezi kwenda maeneo mbalimbali ya miji ulitolewa kushawishi washiriki kuamini kwamba ufugaji wa kuku unaweza kuondoa umasikini. Vilevile, mafunzo yaliainisha mbinu bora za utunzaji wa kuku wa kienyeji ikiwa ni pamoja utunzaji wa mayai, ulishaji wa kuku, ujenzi wa vibanda vya kufugia kuku na masoko ya kuku.

Mafunzo pia yalifafanua magonjwa yanayoathiri kuku na udhibiti wake;usambazaji wa virusi vya ugonjwa wa kideri, kinga, namna ya utambuzi wa ugonjwa na mbinu za kudhibiti magonjwa ya kuku. Wakati wa kutoa mafunzo katika ngazi ya kijiji, kikundi cha sanaa kilicheza igizo kuhusu utunzaji wa kuku, afya ya kuku na uuzaji wa kuku. Wakati wa mafunzo washiriki walipewa fursa ya kutoa uzoefu wao na changamoto wanazokutana nazo katika ufugaji. Uzoefu wa washiriki ulileta tija katika programu hii. Kabla ya kumaliza mafunzo washiriki waliaswa kuwasilisha mpango kazi wa namna watakavyo tekeleza mpango wa kuzuia ugonjwa wa kideri. Mipango kazi hiyo ilijadiliwa na kuboreshwa.

Uteuzi wa watoa chanjo; baada ya mafunzo Wenyeviti wa Vitongoji walitakiwa kupendekeza majina ya watu ambao wataweza kuendesha zoezi la kuchanja kuku katika Vitingoji. Uchaguzi wa watoa chanjo ulifanyika katika mikutano ya Vitongoji iliyowajulisha wananchi kuhusu mpango wa chanjo. Kulingana na ukubwa wa Kitongoji watoa chanjo waliteuliwa kati ya 1 hadi 3 kutoka kila Kitongoji wakijumuisha wanawake na wanaume.

Mafunzo kwa watoa chanjo wa jamii; watoa chanjo wa jamii walipatiwa mafunzo na maafisa kutoka Halmashauri kuhusu uchanjaji wa kuku, mawasiliano na ushirikishwaji wa wakulima kwenye zoezi la kuchanja kuku. Vilevile, watoa chanjo wa jamii walipewa mafunzo ya uelemishaji wa jamii kuhusu umuhimu wa kuchanja kuku. Hali kadhalika walipewa mafunzo ya kuchukua na kuhifadhi taarifa za idadi ya kuku wakati wa kutoa chanjo, idadi ya kuku waliochanjwa na sababu za kutochanja baadhi ya kuku.

Usambazaji wa chanjo ya Kideri; zoezi la chanjo kwa mara ya kwanza lilifanywa na watoachanjo wa jamii pamoja na wataalamu wa Halmashauri. Takwimu za kijamii na kiuchumi zilikusanywa wakati zoezi la kuchanja kuku likiendelea. Watoa chanjo wa jamii walipatiwa chanjo za kideri kwa mizunguko mitatu ya kwanza na baada ya hapo walielekezwa kununua kutoka kwa Afisa Ugani wa Kilimo na Mifugo wa Kata ambaye alikabidhiwa chanjo hizo. Kazi za Afisa Ugani ni kusimamia ugawaji wa chanjo na kusimamia zoezi la uchanjaji wa kuku, kutatua migogoro kati ya wafugaji, kuhakikisha chanjo iliyotolewa imetumika kama ilivyokusudiwa na kupima utendaji kazi wa mtoa chanjo wa jamii. Afisa Ugani alihusika kukusanya takwimu na taarifa za zoezi la utoaji chanjo na kuzihifadhi kabla ya kuwasilisha kwa maratibu wa Halmashauri. Afisa Ugani alikuwa na jukumu la kuhakikisha malipo ya chanjo yanafanyika kabla ya kutoa chanjo nyingine. Afisa Mtendaji Kata, Afisa Maendeleo ya Jamii, Watendaji wa Vijiji na Wenyeviti wa Vitongoji walitoa usaidizi kwa Afisa Ugani wakati wa utekelezaji wa kampeni za chanjo.

Kupanga ratiba ya kampeni ya chanjo; baada ya kuchanja kuku, kinga haijengeki ndani ya muda huo, wiki moja hadi mbili zinahitajika ili matokeo ya chanjo yaweze kuonekana. Kuku wanapaswa kuchanjwa angalau mwezi moja kabla ya kutokea kwa mlipuko wa ugonjwa, hivyo wafugaji wa kuku walishirikiswa kutoa uzoefu wao kuhusu kipindi gani ugonjwa wa kideri hutokea katika kijiji chao. Lengo lilikuwa kutambua kipindi muafaka wa kuchanja kuku na njia ya uchanjaji. Kampeni shirikishi ilianzishwa wakati wa kuchanja kuku na wakati wa kurudia chanjo na kubaini njia bora ya kuchanja kuku. Njia ya kudondosha tone la chanjo kwenye jicho la kuku ni ya uhakika zaidi kuliko njia ya kuchanganya chanjo na maji ya kunywesha kuku kwani inahitaji kuongeza chanjo nyingine baada ya wiki 2 au 4 kila baada ya miezi 3. Kuchanja kuku kila baada ya miezi 3 hadi 4 ni mojawapo ya njia za kulinda vifaranga vilivyototolewa.



***Mtoa chanjo wa jamii akitoa huduma***

Kuanzisha vikundi vya ufugaji kuku na VICOBA; ili kuongeza uzalishaji wa kuku Afisa Maendeleo ya Jamii alifanya kampeni za uhamasishaji kwa jamii kujiunga katika vikundi kuwezesha kupata mikopo na ujuzi kutoka Halmashauri. Jamii ziliunda VICOBA kwa lengo la kusaidiana na kuwezeshana mitaji kwa lengo la kuboresha ufugaji wa kuku.

Ujenzi wa majengo ya kutotolesha vifaranga, utengenezaji wa chakula na soko la kuku; baada ya kutambua umuhimu wa ufugaji wa kuku, Halmashauri ilitoa usaidizi wa ujenzi wa jengo la kufunga mashine ya kutotolesha vifaranga, utengenezaji wa chakula cha kuku na soko la kuuzia kuku. Ujenzi na ununuzi wa mashine ya kutotolesha vifaranga na mashine ya kusaga chakula cha kuku ulifanyika kupitia fedha za Mpango wa Maendeleo wa Sekta ya Kilimo (ASDP).



***Soko la kuku***



***jengo la mashine ya kusaga chakula cha kuku***



***jengo la mashine ya kutotolesha***

## 5.0 RASILIMALI

Utekelezaji wa jitihada hii ulihusisha matumizi ya rasilimali mbalimbali ambazo ni watu, fedha na vifaa. Rasilmali watu ni wakufunzi 4 kutoka Wiazara Kilimo na Maendeleo ya Mifugo ambao walishiriki kuandaa na kutoa mafunzo kwa vijiji 5 vya mfano. Wengine ni wataalamu kutoka makao makuu ya Halmashauri, Kata na Vijiji pamoja na watoa chanjo wa jamii. Rasilimali fedha zilijumuisha fedha za kugharamia mafunzo na ununuzi wa chanjo kama ilivyobainishwa kwenye jedwali 1 na 2 hapa chini.

**Jedwali Na 1: Gharama za mafunzo na chanjo katika Vijiji 5**

| | Idadi ya washiriki | Idadi ya siku | Kiasi | Jumla TZS |
|---|---|---|---|---|
| Watoa chanjo wa jamii | 23 | 3 | 60,000 | 4,140,000 |
| Wenyeviti wa Vijiji | 5 | 3 | 60,000 | 900,000 |
| Watendaji wa Vijiji | 5 | 3 | 60,000 | 900,000 |
| Watendaji wa Kata | 4 | 3 | 60,000 | 720,000 |
| Maafisa Ugani wa Kata | 4 | 3 | 60,000 | 720,000 |
| Afisa Maendeleo wa Jamii wa Halmashari | 1 | 3 | 60,000 | 180,000 |
| Afisa Kilimo na Mifugo wa Halmashauri | 1 | 3 | 60,000 | 180,000 |
| Maafisa mifugo (ngazi ya Halmashauri) | 4 | 3 | 60,000 | 720,000 |
| Afisa Ugani wa Halmashauri (DAEO) | 1 | 3 | 60,000 | 180,000 |
| Wawezeshaji kutoka Wizara ya Kilimo na Mifugo | 4 | 3 | 120,000 | 1,440,000 |
| Chanjo | 48 | 1 | 6,000 | 288,000 |
| Viburudisho kwa washiriki | 48 | 3 | 6,000 | 864,000 |
| Gharama za ukumbi | 1 | 3 | 150,000 | 450,000 |
| Shajala | 48 | 1 | 10,000 | 480,000 |
| Jumla | | | | 12,162,000 |

**Jedwali Na 2: Gharama za mafunzo kwa Kata 28**

| | Idadi ya washiriki | Idadi ya siku | Kiasi TZS | Jumla TZS |
|---|---|---|---|---|
| Watoa chacho wa jamii | 330 | 1 | 20,000 | 6,600,000 |
| Watendaji wa Kata | 24 | 1 | 20,000 | 480,000 |
| Afisa Ugani wa Kata | 24 | 1 | 20,000 | 480,000 |
| Afisa Maendeleo ya Jamii wa Kata | 24 | 1 | 20,000 | 480,000 |
| Wawezeshaji kutoka ngazi ya Halmashauri | 28 | 1 | 45,000 | 1,260,000 |
| Chanjo | 500 | 1 | 6,000 | 3,000,000 |
| Viburudisho kwa washiriki | 390 | 3 | 6,000 | 7,020,000 |
| Shajala | 390 | 1 | 5,000 | 1,950,000 |
| Jumla | | | | 21,270,000 |

**6.0 MATOKEO**

Kampeni ya Kwanza ya utoaji wa chanjo ilifanyika mwezi Januari 2011 kwa kutumia chanjo aina ya *I-2 thermo-tolerant vaccine* kwa vijiji 5 vya mfano na baadaye Halmashauri iliamua kushirikisha Kata zote. Kutokana na kampeni hii ya utoaji chanjo, yafuatayo ni matokeo ya jitihada hii.

Kuongezeka kwa uelewa kuhusu magonjwa ya kuku; mafunzo kwa viongozi wa jamii na baadhi ya wajumbe kutoka kwenye jamii yameongeza uelewa wa wafugaji kuhusu magonjwa ya kuku, namna ya kutibu na kinga. Uelewa huu unadhihirishwa na uwepo wa watoa chanjo wa jamii na kuongezeka kwa mahitaji ya chanjo.

Kuongezeka kwa uzalishaji wa kuku katika kaya; idadi ya kuku katika kaya imeongezeka kutoka wastani wa kuku 8 hadi kufikia wastani wa kuku 20 kwa kila kaya na idadi ya wafugaji wa kuku imeongezeka. Wastani wa kuku 1 na mayai 8 huuzwa na wastani wa kuku 1 na mayai 3 hutumika kama kitoweo katika kaya kwa kila mwezi. Ugonjwa wa kideri ambao ulikuwa tishio kwa kupoteza kuku zaidi ya 80% kila mwaka umedhibitiwa kikamilifu.



***Usafirishaji wa kuku kwenda sokoni***

Kuongezeka kwa kipato cha familia; jitihada hii imesababisha kuongezeka kwa kipato kwa baadhi ya watu katika jamii. Hali hii inadhihirishwa na ujenzi wa nyumba bora, kuongezeka kwa uwezo wa kukidhi mahitaji ya msingi kama kulipa ada, huduma za afya, umiliki wa pikipiki na magari kwa baadhi ya wana jamii na uwezo wa kushiriki katika vyama vya akiba na mikopo.



***Uuzaji wa kuku***

Ushiriki wa wanawake katika ufugaji wa kuku umeongezeka; kutokana na jitihada hii, ushiriki wa wanawake katika shughuli za ufugaji wa kuku kibiashara umeongezeka sambamba na uwezeshaji wa wanawake kiuchumi.



***Wafugaji wa kuku wakiwemo wanawake***

Fursa za ajira; zoezi la kuchanja kuku ni gumu na linahitaji muda mwingi hivyo linahitaji kufanywa na watu wenye ari ya kujitoa. Mara nyingi wachanja kuku hupata malipo kutoka kwa wakulima ikiwa ni pamoja na gharama za chanjo na huduma. Malipo haya yanaongeza ari kwa wachanja kuku katika kuhudumia eneo kubwa zaidi.

Kuongezeka kwa utaalamu wa ufugaji wa kuku; ujuzi wa ufugaji wa kuku umeongezeka katika ulishaji, chanjo na utotoleshaji wa vifaranga kwa kutumia mbinu za kisasa. Wakulima wachache wanajihusisha na utengenezaji wa chakula cha kuku na utotoleshaji wa vifaranga kibiashara.

Ushiriki wa watoa chanjo wa jamii; programu ya utoaji chanjo ya kideri kwa kutumia wajumbe kutoka kwenye jamii hupunguza gharama na kuongeza wigo wa kufikia maeneo mengi zaidi. Ushiriki huu wa watoa chanjo wa jamii katika zoezi unachangia kufanya programu hii kuwa endelevu kwa kuwa watoa chanjo ni sehemu ya jamii.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Katika kuhakikisha ugonjwa wa kideri na magonjwa mengine yanadhibitiwa kikamilifu, mikakati mbalimbali imewekwa.

(i) Uhamasishaji endelevu na kujenga uwezo wa jamii kuhusu magonjwa ya kuku na namna ya kudhibiti.
(ii) Kuendeleza ushirikiano kati ya Mafisa Ugani na jamii kupitia mfumo wa Halmashauri wa kutoa zawadi kwa Afisa Ugani anayefanya kazi kwa ufanisi.
(iii) Halmashauri imeweka mipango ya kuanzisha maabara ya kuchunguza magonjwa ya kuku.

(iv) Soko la kuku limeanzishwa katika Kata ya Mtinko ili kuchochea wakulima kuendelea kuzalisha kuku kwa wingi.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Mafanikio ya jitihada hii yamechangiwa na sababu zifuatazo;

(i) Kwa asili, jamii ya Wanyaturu inapenda ufugaji wa kuku hivyo kuwa uzoefu na maarifa ya ufugaji huo.

(ii) Uwepo wa kalenda ya msimu ya kilimo ambayo inaonesha kipindi ambacho wakulima wana fursa ya kutumia muda wao kushiriki katika zoezi la kuchanja kuku.

(iii) Uhakika wa kurejesha gharama za chanjo; idadi kubwa ya wakulima wana utayari wa kulipa gharama za chanjo kutokana na uhakika wa kupata soko la kuku.

(iv) Utayari wa watumishi wa Halmashauri, Viongozi wa Jamii na watoa chanjo katika kuendesha zoezi la chanjo.

# HALMASHAURI YA WILAYA YA SHINYANGA


**UBORESHAJI SHIRIKISHI WA SKIMU YA UMWAGILIAJI YA NYIDA**



*Uzoefu wa H/W ya  Shinyanga*

**1.0 UTANGULIZI**

H/W ya Shinyanga ni moja kati ya Halmashauri 6 za Mkoa wa Shinyanga iliyopo kati ya Latitudo $3^0$.20' na $3^0$.95' Kusini na Longitudo $32^0$.30' na $33^0$.30' Mashariki na inapakana na Halmashauri ya Kishapu na Manispaa ya Shinyanga upande wa Mashariki, Halmashauri ya Mji wa Kahama na H/W ya Geita upande wa Magharibi, H/W ya Kwimba upande wa Kaskazini na H/W ya Nzega upande wa Kusini. Halmashauri ina eneo la 4,212$km^2$ na imegawangika katika Tarafa 3, Kata 26, Vijiji 126 na Vitongoji 856. Kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012, Halmashauri ina watu 378,928; wanaume 184,695 na wanawake 194,232. Kuna kaya 23,872 zenye wastani wa watu 6.3 na idadi ya watu kwa kilometa ya mraba ni 88.




***Ramani ya H/W ya Shinyanga***

Kijiji cha Nyida kipo Kata ya Nyida Tarafa ya Itwangi, 68km Magharibi mwa Mji wa Shinyanga. Kijiji kinasifika kwa uzalishaji wa mpunga katika Skimu ya Umwagiliaji ya Nyida. Skimu ina eneo la 700Ha. Skimu ya umwagiliaji ilianzishwa mwaka 1998 na kujengwa kati ya mwaka 2002 na 2004 chini ya Programu ya Uendelezaji Shirikishi wa Skimu za Umwagiliaji (PIDP) iliofadhiliwa na IFAD. Skimu ilisajiliwa mwaka 2003 kwa Namba ya usajili SO. No 11882 chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani na mwaka 2018 ilisajiliwa chini ya Kamisheni ya Taifa ya Umwagiliaji kwa namba ya usajili No.075. Skimu ina wanachama 386; 290 wanaume na 96 wanawake. Chanzo cha maji ya umwagiliaji Mto Manonga na Mto Puni ambayo ni ya msimu.

**2.0 TATIZO**

H/W ya Shinyanga ina hali ya hewa ya ukame na hupokea kiasi kidogo cha mvua kwa mwaka. Wastani wa mvua ni kati ya 450mm – 990mm na hunyesha kipindi cha Oktoba hadi Mei. Kiwango hiki cha mvua kingetosheleza kwa kilimo endapo mvua zingekuwa za uhakika lakini mvua hazinyeshi mfululizo hivyo kusababisha changamoto katika uzalishaji wa mazao. Kutokana na hali hii Halmashauri inaendeleza jitihada za kushawishi wakulima kuzalisha mazao ambayo ni himilivu kwa ukame. Wakulima vilevile, hupata changamoto ya malisho na maji kwa ajili ya mifugo.

Kati ya Mwaka 1986 na 2000 wakulima wa mpunga katika Kijiji cha Nyida waliathirika katika uzalishaji kutokana na upungufu wa mvua. Uzalishaji ulikuwa mdogo wa wastani wa gunia 8 kwa ekari ukilinganisha na wastani wa gunia 25 hadi 30 za mpunga endapo kuna mvua za kutosha. Uzalishaji mdogo pia ulisababishwa na ubovu wa miundombinu ya skimu ya umwagiliaji kutokana mifereji mibovu na kukosekana kwa uthibiti wa mifugo katika eneo la skimu. Tatizo lilidumu kwa zaidi ya miaka


10 kabla ya jitihada za kujinasua. Hali hii ilisababisha uzalishaji duni na kuzorota kwa maendeleo ya watu wa Nyida. Picha zifuatazo zinaonesha hali halisi kabla ya jitihada hii.



***Hali halisi ya mifereji ya umwagiliaji kabla ya matengenezo***

**3.0 LENGO**

Lengo kuu la jitihada hii ni kuboresha Skimu ya Umwagiliaji ya Nyida na maisha ya watu kwa kuongeza kiwango cha uzalishaji. Malengo mahususi ya jitihada hii ni pamoja na kujenga bwawa la hifadhi ya maji na kukarabati mifereji ya umwagiliaji ya urefu wa 380m.




***Ramani ya skimu ya Umwagiliaji ya Nyida.***

**4.0 MIKAKATI YA UTEKELEZAJI**

Utekelezaji wa jitihada hii umehusisha Serikali, wafadhili na jamii. Jitihada hii ilitekelezwa kwa ushirikiano kati ya Tanzania na Japani (JICA) chini ya TANCAID II. Lengo la ushirikiano huu lilikuwa kuboresha miundombinu ya umwagiliaji na kujenga uwezo wa Maafisa Umwagiliaji kutumia mwongozo kabambe wa umwagiliaji, kuimarisha wakulima katika kusimamizi na ufuatiliaji wa miundombinu ya umwagiliaji na hatimaye kuhakikisha ujenzi bora wa miundombinu. Matumizi ya Mwongozo huu kwa vitendo kwa mara ya kwanza yalifanyika katika ujenzi wa mifereji yenye urefu wa 380m katika Skimu ya Nyida kabla ya kusambazwa maeneo mengine. Mwongozo una maeneo 4 ambayo yanahusisha Uandaaji, Utekelezaji, Uendeshaji, Matengenezo na Mafunzo. Katika Skimu ya Umwagiliaji ya Nyida Mwongozo ulijikita katika Uandaaji na Utekelezaji, hivyo hatua zilizotekelezwa ni kuendesha kampeni za kukuza uelewa juu ya skimu, Uandaaji wa Mipango shirikishi, Utafiti Shirikishi, Upembuzi yakinifu, Makubaliano ya utekelezaji wa mradi, usanifu, kutoa zabuni, kuandaa mikataba na hatimaye kutekeleza ujenzi. Maelezo ya kila hatua yamefafanuliwa hapa chini.

Kuendesha kampeni za kukuza uelewa kuhusu skimu; Mikutano ya jamii iliendeshwa kati ya Agosti 2017 na Septemba 2017. Awali mikutano hii ilianzishwa na umoja wa umwagilaji kujadili umuhimu wa skimu

ya umwagilaji. Wakulima waliamini kwamba umwagiliaji ndio uti wa mgongo kwa maendeleo ya uchumi. Katika mikutano hii, Mtaalamu wa umwagiliaji na Afisa Maendeleo ya Jamii walihudhuria na kufanya uhamasishaji kwa wakulima kuunganisha juhudi zao katika kukarabati miundombinu ya umwagiliaji.



***Mikutano ya Uhamasishaji***

Utafiti shirikishi; Juni mwaka 2017, wakulima walishiriki kikamilifu katika kutathimini mradi kabla ya zoezi la ukarabati. Wanachama wa Umoja wa Umwagiliaji walishirikishwa kwenye utafiti shirikishi kubaini matatizo na kuyapanga kulingana na uzito wake. Utafiti na upangaji bajeti shirikishi; kupanga kiwango cha uchangiaji katika gharama za uendeshaji na matengenezo, aina ya vifaa vya ujenzi, rasilimali na michango ya kifedha kutoka kwa wakulima. Mkutano uliendeshwa katika ngazi ya kijiji ambapo uliandaliwa na Umoja wa umwagiliaji. Wakati wa utekelezaji wa zoezi hili la utafiti shirikishi, wakulima walibainisha maeneo mengi yanayohitaji kufanyiwa matengenezo wakati wa ukarabati. Wakulima pia walisafisha eneo lote la mfereji kwa kuondoa majani na vichaka. Matokeo ya utafiti shirikishi yamebainishwa katika jedwali Na 1.


**Jedwali 1. Matokeo ya Utafiti Shirikishi**

| UTAFITI SHIRIKISHI NA VIPAUMBELE | | | | |
|---|---|---|---|---|
| Na. | **Tatizo** | **Chanzo cha tatizo** | **Suluhisho** | **Nafasi** |
| 1 | Upotevu wa maji katika mfereji mkuu | Mifereji mibovu (1,324m) | Kupanua na kujengea mifereji mikuu | 1 |
| 2 | Uhaba wa maji ya umwagilaji | Kukosekana kwa bwawa la kuhifadhi maji | Kujenga bwawa | 2 |
| 3 | Upotevu wa maji katika mifereji 5 kutoka mfereji mkuu | Mifereji mibovu (1,543 meters) | Kujenga mifereji | 1 |
| 4 | Upotevu wa maji katika mifereji 5 | Mifereji mibovu | Kujenga mifereji | 1 |
| 5 | Ubovu wa barabara katika skimu | Mmomonyoko wa udongo | Ukarabati wa barabara | 3 |



***Zoezi la kupima na tathimini shirikishi***

Upangaji mipango shirikishi; Wakulima walikubali kupanga mipango ya utekelezaji kwa kubainisha shughuli mbalimbali za utekelezaji katika kipindi chote cha ukarabati wa mifereji. Wakulima walishiriki katika kuaandaa ramani ya skimu na kuorodhesha shughuli zitakazotekelezwa. Picha ifuatayo inaonesha wakulima wakishiriki katika uandaaji wa ramani ya skimu.



***Wakulima wakianda ramani ya skimu***

Kuunda kamati ya mradi; kamati ya mradi ya wajumbe 10 (6 wanaume na 4 wanawake) iliundwa kusimamia utekelezaji wa mradi. Wajumbe wa kamati walipatiwa mafunzo kuhusu usimamizi wa kazi za ujenzi na kupatiwa orodha ya kazi zitakazotekelezwa ili kurahisisha ufuatiliaji. Orodha hiyo iliandaliwa na Afisa wa Halmashauri kwa lugha ya Kiswahili ili kusimamia ubora katika ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji. Kiambatanisho 1 kinaonesha orodha ya kazi iliyotumika katika ufuatiliaji na usimamizi wa mradi.

Kutoa zabuni na kuandaa mikataba ya ujenzi; zabuni na utoaji wa mkataba wa ujenzi ulifanyika kwa kutumia akaunti maalumu maarufu kama "*force account".* Timu ya ujenzi ilianzishwa Septemba 2017 na

shughuli zote za ujenzi zilikuwa chini ya maelekezo ya wataalamu kutoka JICA, Ofisi ya Umwagilaji ya Kanda, Mhandisi wa Umwagiliaji kutoka Halmashauri, na wajumbe wa kamati ya mradi kutoka Umoja wa Umwagiliaji. Kamati ya Mradi ilisimamia ujenzi kwa kushirikiana na mtaalamu kutoka Halmashauri. Mafundi kutoka kwenye jamii na wakulima walitumika kikamilifu wakati wa shughuli za ujenzi. Wakulima pia walishiriki katika kukusanya vifaa vya ujenzi kama mawe, kokoto na mchanga. Zoezi liliandaliwa vema na Umoja wa Umwagiliaji na lilishirikisha wakulima 250 ambao ni wanufaika wa moja kwa moja wa mradi.



***Ujenzi wa mifereji***

**5.0 RASILIMALI**

Utekelezaji wa jitihada hii ulitumia TZS 1,078,594,981.82 kukamilisha mradi; jamii ilichangia 20% ya fedha zote na Serikali kuu na JICA 80%. Jedwali Na.2 linaonesha rasilimali fedha zilizotumika.

**Jedwali: Na 2 Rasilimali fedha**

| S/N | MWAKA | KAZI ZILIZOTEKELEZWA | KIASI(TZS) | CHANZO |
|---|---|---|---|---|
| 01 | 2002-2005 | Ujenzi wa bwawa la maji, barabara za kuhudumia mashamba | 480,000,000 | Mradi wa PIDP |
| 02 | 2012 | Ukarabati wa bwawa na mfereji mkuu mita 80 | 32,000,000 | TASAF |
| 03 | 2017 | Ujenzi wa mifereji midogo (380m) | 100,000,000 | JICA-TANCAID II |
| 04 | 2018-2019 | Ujenzi wa mfereji mkuu 1,324m | 466,594,981.82 | JICA (SSIDP) |
| | | **Jumla** | **1,078,594,981.82** | |

Rasilimali watu ni pamoja na wataalamu kutoka JICA, Halmashauri na wanachama wa Umoja wa Umwagiliaji ambao walishiriki kikamilifu katika shughuli za ukarabati.

**6.0 MATOKEO**

Ukarabati wa Skimu ya Umwagilaji ya Nyida umeleta matokeo makubwa yenye faida kwa jamii na Halmashauri. Jumla ya meta 380 ya mifereji ilikarabatiwa, njia 2 za kupita katika eneo la skimu zimejengwa, tatizo la upotevu wa maji limetatuliwa na upitishaji wa mifugo katika eneo la skimu umedhibitiwa.





***Miundombinu ya Skimu baada ya kuboreshwa***

Ongezeko la uzalishai wa mpunga; mavuno yameongezeka kutoka gunia 8 kwa ekari hadi gunia 25 kwa ekari na kuchochea kuongezeka kwa kipato cha mkulima kutoka TZS 520,000 hadi 1,625,000 kwa ekari mwaka 2018. Ongezeko la kipato kwa mkulima limeongeza uwezo wa kukidhi mahitaji mbalimbali kama vile kumudu kununua vyombo vya usafiri kama pikipiki, kuanzisha biashara, kununua ng'ombe, kujenga nyumba bora na kuweza kulipia huduma mbalimbali.

Kuongezeka kwa eneo la uzalishaji; Eneo la uzalishaji limeongezeka kutokana na ukarabati wa skimu ya umwagiliaji ambao umechochea wakulima kuongeza mashamba. Eneo limeongezeka kutoka 394Ha za awali hadi kufikia 421Ha.



***Mashamba ya Mpunga***

Skimu ya umwagilaji ya Nyida imekuwa kituo cha kujifunzia; Juhudi zilizofanywa na wanachama wa umoja wa umwagiliaji wa Nyida zimevutia Wizara ya Maji na Umwagiliaji kutambua Skimu ya Nyida kama skimu ya mfano kwa ajili ya skimu nyingine kujifunza. Mwaka 2018 H/W za Misenyi, Bariadi, Karagwe na Namtumbo zilitembelea Skimu ya Umwagiliaji ya Nyida kwa lengo la Kujifunza.

**7.0 MIKAKATI YA UENDELEVU**

Ili kuhakikisha matokeo ya jitihada hii yanakuwa endelevu, mikakati ifuatayo imewekwa;

(i) Kutumika kwa mafundi wa jamii na ushiriki wa jamii katika utekelezaji wa mradi kunatoa taswira ya uendelevu wa mradi kwani jamii yenyewe inaweza kufanya matengenezo ya mara kwa mara.

(ii) Kuna makubaliano kwa wakulima kutenga 5% ya mazao ya mpunga kwa ajili ya uendeshaji na matengenezo ya Skimu.

(iii) Kuna sheria ndogo za kuzuia mifugo na kuchunga katika eneo kuzunguka Skimu na sheria hizi zinafuatwa.

**8.0 SIRI YA MAFANIKIO**

Mafaniko ya Jitihada hii ya H/W ya Shinyanga yanatokana na sababu zifuatazo;

(i) Skimu ilikuwa ni hitaji halisi la jamii hivyo jamii ilikuwa na ari ya kushiriki kikamilifu katika hatua zote za uboreshaji.
(ii) Uongozi imara wa Umoja wa Umwagiliaji.
(iii) Ubunifu wa Afisa Umwagiliaji wa Halmashauri katika kuandaa orodha kwa wakulima katika kusimamia utekelezaji wa mradi.
(iv) Utayari kutoka kwa maafisa wa Halmashauri.
(v) Uwepo wa mtaalamu kutoka JICA ambaye amefanya kazi kwa ukaribu na jamii kungoza, kulekeza na kuhamasisha wakulima.

**(Mradi wa Maendeleo ya Umwagiliaji kwa Skimu Ndogo)**
**(Fomu iliyorahisishwa Kwa ajili ya usimamizi wa kazi za ujenzi kamati za miradi)**

Kanda:__________________________________Wilaya:

Kamati ya Mradi:

Jina la mradi:

Imehakikiwa Na:________________________________Tarehe:

| **Namba** | | **Kuangalia Vifaa** | **Tathmini** | |
|---|---|---|---|---|
| **(1)** | **Kazi za Udongo** | | | |
| | (a) | Huondoaji wa vizuizi vyote visivyohitajika katika eneo litakalo chimbwa/Jazwa | Ndio | Hapana |
| | (b) | Kina cha uondoaji ni kati ya sm 20  | Ndio | Hapana |
| | (c) | Mpaka wa uchimbaji umekatwa na kuchongwa kama ilivyoonyeshwa kwenye mchoro | Ndio | Hapana |
| | (d) | Udongo uliochimbwa umehifadhiwa sehemu husika | Ndio | Hapana |
| | (e) | Udongo unaotengeneza tuta siyo mkavu/haujatawanyika | Ndio | Hapana |
| | (f) | Udongo unaotengeneza tuta siyo chepechepe | Ndio | Hapana |
| | (g) | Uwekaji/Utawanyaji wa udongo wa tuta  umefanyika vizuri,kama sm 20 hivi | Ndio | Hapana |
| | (h) | Udongo wa juu (mimea,majani,magugu n.k) haupo katika tuta  | Ndio | Hapana |
| | (i) | Hakuna udongo uliobakia/kutawanyika kwenye tuta | Ndio | Hapana |
| | (i) | Hakuna nafasi/mashimo kwenye tuta baada ya ushindiliaji | Ndio | Hapana |
| | (k) | Sm 10 mpaka 20 za ziada zimeachwa kwa ajili ya kingo za mfereji | Ndio | Hapana |
| | (l) | Ushindiliaji umefanyika zaidi ya mara 6 kwa kutumia shindilia | Ndio | Hapana |
| | (l) | Kama kuna matatizoyoyote katika kazi ya udongo ainisha hapa chini | | |
| **(2)** | **Kazi ya Zege** | | | |
| | (a) | Maji kwa ajili ya uchanganyaji wa zege ni masafi | Ndio | Hapana |
| | (b) | Mchanga,Kokoto kwa ajili ya zege zimehifadhiwa tofauti | Ndio | Hapana |
| | (c) | Mchanga,Kokoto kwa ajili ya zege hazina organic material(Mimea,majani,magugu n.k) | Ndio | Hapana |
| | (d) | Mchanga,Kokoto kwa ajili ya zege  zimehifadhiwa sehemu nzuri | Ndio | Hapana |
| | (e) | Saruji inafaa | Ndio | Hapana |
| | (f) | Saruji haikuifadhiwa juu ya ardhi/chini | Ndio | Hapana |

| Namba | | Kuangalia Vifaa | Tathmini | |
|---|---|---|---|---|
| | (g) | Saruji imehifadhiwa sehemu yenye mwanga  | Ndio | Hapana |
| | (h) | Uchangaji wa zege haujafanyika juu ya ardhi/chini  | Ndio | Hapana |
| | (i) | Uchanganyaji wa zege haujatumia maji yaliyotumika | Ndio | Hapana |
| | (j) | Ndani ya 'form work' ni kusafi | Ndio | Hapana |
| | (k) | Ushindiliaji wa kutosha umefanyika kwenye zege | Ndio | Hapana |
| | (l) | Hakuna nafasi wala matundu kwenye zege lililojengwa  | Ndio | Hapana |
| | (m) | Hakuna 'Udongo wa juu'(mimea,majani,magugu n.k) kwenye zege  | Ndio | Hapana |
| | (n) | Nondo hazina matope,mafuta au mchanganyo wowote | Ndio | Hapana |
| | (o) | Muda wa kutosha umetengwa kwa ajili ya wa kumwagilia zege | Ndio | Hapana |
| | (p) | Zege lililojengwa linamwagiliwa ipasavyo ili likomae | Ndio | Hapana |
| | (q) | Kama kuna matatizo yoyote katika kazi ya ujenzi wa zege ainisha hapa chini | | |
| **(3)** | | **Kazi ya ujenzi wa mawe** | | |
| | (a) | Mawe hayana mipasuko | Ndio | Hapana |
| | (b) | Kiwango cha mawe ni sm 30 mpaka 50 na2/3 ya unene wa ukut.  | Ndio | Hapana |
| | (c) | Mawe husafishwa kabla ya kutumika/kujengea | Ndio | Hapana |
| | (d) | Maji kwa ajili ya mota ni masafi | Ndio | Hapana |
| | (e) | Mchanga umechekechwa kabla ya matumizi | Ndio | Hapana |
| | (f) | Mchanga unafaa hauna mchanganyiko wowote | Ndio | Hapana |
| | (g) | Saruji inafaa | Ndio | Hapana |

| Namba | | Kuangalia Vifaa | Tathmini | |
|---|---|---|---|---|
| | (h) | Nafasi kati ya jiwe na jiwe zimejazwa  vizuri na mota) | Ndio | Hapana |
| | (i) | Kama kuna matatizoyoyote katika kazi ya ujenzi wa mawe ainisha hapa chini | | |
| **(4)** | | **Kazi nyingine** | | |
| | (a) | Urefu wa geti unatosha kwa ajili ya kutumia | Ndio | Hapana |
| | (b) | Geti linafunga na kufungua vizuri | Ndio | Hapana |
| | (c) | Hakuna hitilafu yoyote kwenye geti | Ndio | Hapana |
| | (d) | Geti limepakwa vizuri kuzuia kutu | Ndio | Hapana |
| | (e) | Vibanio vikokwenye hali nzuri  | Ndio | Hapana |
| | (f) | Ukubwa wa mawe ya gabioni n ism 30 mpaka 40  | Ndio | Hapana |
| | (g) | Mawe kwa ajili ya gabioni yamepangwa vizuri kwenye waya | Ndio | Hapana |
| | (h) | Kama kuna matatizoyoyote katika kazi nyingine ainisha hapa chini | | |

# REJEA

*Abiona, A. I. and Bello, W. N. (2013). Grassroots Participation in Decision-Making Process and Development Programmes as Correlate of Sustainability of Community Development Programmes in Nigeria, Journal of Sustainable Development; Vol. 6 (3):47-57. Canadian Centre of Science and Education, [www.ccsenet.org/jsd] site visited on 19 /03/ 2013.*

Apolo, Kansiime (2013). The Impact of Public Procurement Reforms on Service Delivery in Uganda; Bishop Stuart University.

Chibehe, M.M. (2004). Factors Affecting Sustainability of Farmer Groups: the case of Twikinde Malimbichi Cooperative Society. MA Dissertation, SUA, Unpublished, 90pp.

Helene Bie Lielleor and Ulrik Lund-Sorensen (2013). FARMERS' CHOICE evaluating an approach to agricultural technology and adoption in Tanzania, Rockwool Foundation research Unit, PRACTICAL ACTION Publishing, pp. 154.

Helmsing, A. H. J. (1995). *Local Government Central Finance.*An Introduction: NewYork USA

Howlett. D and J. Nagu. (1997). *Agricultural Project Planning in Tanzania, A handbook on cycles and sequences, participation, identification, planning and design, economic and financial analysis, and environmental assessment of agricultural projects.* ISBN 1898828261. pp 89.

Kusago, Takayoshi. (2008). *Sustainable Livelihood and Happy Generation in Minamata-City Japan*: A Model for Endogenous Community Development.

Makonda, K.S.C. (2003). Partnership and sustainability of water supply systems in Bukombe District, Tanzania. *MA Dissertation*, Sokoine University of Agriculture, Morogoro, Tanzania. Unpublished. pp.154

Mwanga, J.N. (2011). Empowerment of Local Society in Tanzania –the Nucleus for Development- With Experience from Indonesia and Japan, *Rare Series Policy Paper*, Local Government Training Institute, Dodoma Tanzania. 100 pp.

Ohama, Y. (2002). Basic Framework and viewpoints of Participatory Local Social Development (PLSD) and construction of its evaluation framework.

Porter, Michael E. (1998). *Competitive Advantage: Creating and Sustaining Superior Performance*, 397

pp, Amazon.

Pretty, J.N. (1995). Participatory learning for sustainable agriculture. *World Development* 23(8): 1247-1263.

Scoones, I. and John Thompson (1994). *BEYOND FARMER FIRST: Rural people's knowledge, agricultural research and extension practice*. Intermediate Technology Publications LTD, London, UK, pp.301.

Sharma, P.N. and Ohama, Y. (2007*). Participatory Local Social Development-An Emerging Discipline*, Bharat Book Centre Publishers & Distributors, Lucknow India. pp. 467.

Shikuku, O.M. (2012). Community related Variables influencing sustainability of water projects in Nyando District a case. *MA Dissertation*, University of Nairobi, Digital Repository

URT (1998). Local Government Reform Agenda

URT, (2010). Public private partnership (PPP) *Act*, no 18 of 2010, pp 21

URT (2011). Millennium Development Goals, Tanzania country report. Ministry of Finance and Economic Affairs, Dar es Salaam – Tanzania.

Zadeh, B.S. and Nobaya, A. (2010). Participation and Community Development. *Current Research Journal of Social Sciences* 2(1): 13-14, 2010. [http://maxwellsci.com/print/crjss/v2-13-14.pdf] site visited on 22/07/2014.